*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA MOJA

### Kikao cha Thelathini na Saba – Tarehe 25 Mei, 2018

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Tukae.

Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

### HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

Na. 312

**Kupeleka Umeme kwenye Vijiji na Zahanati**

**MHE. TUNZA I. MALAPO (K.n.y. MHE. CECIL D. MWAMBE)** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mikakati gani ya haraka kuhakikisha Vijiji vya Mumburu, Mkwera na Nanditi vinapata huduma za umeme kwani vipo karibu na nguzo kubwa za umeme?

(b) Je, Serikali itapeleka lini umeme kwenye Zahanati za Chikundi, Mbemba na Kituo cha Afya cha Chiwale?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cecil David Mwambe, Mbunge wa Ndanda, lenye kipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, nia ya Serikali ni kuvipatia umeme vijiji vyote Tanzania Bara visivyokuwa na miundombinu ya umeme ifikapo mwezi Juni, 2021. Ili kutimiza azma hiyo, Serikali imeanza kutekeleza Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza na jumla ya vijiji vitano vimeingizwa kwenye mradi huu unaotekelezwa na Mkandarasi aitwaye *JV RADI Services, Njarita Contractors and Aguila Contractors.* Vijiji hivyo ni Mwambao, Mji Mwema, Nanganga B, Tuungane na Nanditi. Wigo wa kazi katika eneo hilo ni ujenzi wa kilometa 7.16 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 33 na kilometa 14 za njia ya umeme wa msongo wa kilovoti 0.4/0.23, ufungaji wa transfoma saba na

kuunganisha wateja wa awali 184. Gharama za kazi hizo ni shilingi milioni 683.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji vya Mumburu na Mkwera ni miongoni mwa vijiji 36 visivyokuwa na umeme kati ya vijiji 64 katika Jimbo la Ndanda vitakavyopatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu, mzunguko wa pili utakaotekelezwa kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi mwezi Juni, 2021.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Zahanati ya Chikundi ina umeme tangu tarehe 25, Aprili, 2017. Aidha, Kituo cha Afya cha Chiwale kina umeme baada ya kuunganishwa wakati wa utekelezaji wa Mradi wa *REA* Awamu ya Pili. Vilevile Zahanati ya Mbemba itapatiwa umeme kupitia Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza unaoendelea kutekelezwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Kwa niaba ya Mheshimiwa Mwambe.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Mwambe nina maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, kuna taarifa kwamba mkandarasi ambaye amepewa kazi ya kukamilisha miradi hii ya *REA* katika Mkoa wa Mtwara, hasa Wilaya ya Masasi yenye Jimbo la Ndanda pamoja na Nanyumbu ana matatizo ya kiusajili.

Je, Serikali haioni ni wakati mwafaka wa kuachana na mkandarasi huyu na kumtafuta mwingine ambaye atakamilisha kazi hii kwa wakati? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, umeme ni huduma, lakini pia umeme ni biashara. Inakuaje mji mpya unapoanzishwa watu wamekaa wanahitaji huduma ya umeme lakini hawaipati kwa wakati? Serikali mnahujumu shirika hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza kwa niaba ya Mheshimiwa Cecil Mwambe na swali lake la kwanza limejielekeza kwa Mkandarasi anayefanya Mradi huu wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza ambaye kwa mujibu wa jibu langu la msingi nimemtaja, *JV RADI Services.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya Mheshimiwa Mbunge, nataka nimthibitishie kwamba mkandarasi huyu siyo kwamba ana tatizo la usajili, ni utaratibu wa kawaida wa kuhakiki ambao upo ndani ya Serikali. Kuna jumla ya Wakandarasi sita katika Mradi huu wa *REA* Awamu ya Tatu mzunguko wa kwanza ambao uhakiki wao unaendelea kwa vyombo mbalimbali.

MheshimiwaMwenyekiti, kwa hiyo, naomba wakazi wa Mtwara wavute subira kwamba hivi karibuni tu uhakiki huo utakamilika na ataendelea na kazi. Sambamba na hilo, pamoja na uhakiki huo, huyu mkandarasi alipewa mkataba kwa mujibu wa taratibu, lakini pia ameanza kazi. Kuna vijiji kama vitatu Mtwara Vijijini amewasha umeme, anaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, kwa maeneo ya miji ambayo inakua, Mheshimiwa Mbunge ameeleza kwamba upatikanaji wa umeme au uunganishwaji wa miundombinu ya umeme unakuwa ni shida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge na kama ambavyo tumewasilisha bajeti yetu jana, kuna miradi mbalimbali ambayo Serikali imeona ianze kutekeleza ili kukidhi mahitaji ya umeme katika miji inayokua. Mfano, kuna mradi unaokuja *peri-urban* Awamu ya Kwanza utakaoanza mwaka wa fedha 2018/2019. Pia hata *densification* ya awamu ya pili ambayo ni kwa mikoa 11 ikiwemo Mtwara, Dodoma, Kagera, Singida, Lindi, Kilimanjaro, itaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, Serikali imeliona hilo kwa kuwa kazi ni nyingi na tumeona tuisaidie hilo liweze kuendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Qambalo, Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Profesa Haule.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kusisitiza kwamba Awamu ya Tatu ya *REA* ni awamu ya kuwasha Tanzania nzima na kwamba umeme utakapokwenda vijijini hakuna hata kaya itarukwa. Ni ukweli kwamba usambazaji huu unapofanyika vipo vitongoji au vijiji *coverage* inakuwa ni ndogo sana. Mfano Kijiji cha Gwangali kule Karatu, kati ya vitongoji vitano, ni vitongoji viwili tu ndiyo umeme umevifikia. Nini kauli ya Serikali juu ya wakandarasi hawa ambao hawazingatii maelekezo ya Serikali?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana. Ni lini tu anataka kujua.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Karatu, ambaye ameuliza nini kauli ya Serikali?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu jana kupitia hotuba ya bajeti yetu ya Wizara ya Nishati, tumesema kinagaubaga kwamba mkakati wa Serikali ni kuhakikisha vijiji na vitongoji vinafikiwa na huduma ya umeme. Kwa hiyo, tumetoa rai kwa wakandarasi. Kwa mujibu wa hotuba yetu, tumesema kutokana na mpango huo na ndiyo maana kuna vijiji vya nyongeza 1,541 ambavyo tunavifanyia uhakiki. Kwa hiyo, naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge, nia ya Serikali ni kufikisha umeme kadri inavyowezekana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Haule, Mheshimiwa Nape na Mheshimiwa Catherine.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Pamoja na kazi nzuri ambayo inafanywa na Wizara ya Nishati katika kusambaza umeme vijijini, lakini zipo taarifana hali halisi ndivyo ilivyo kwamba *REA* Awamu ya Tatu inasuasua sana kwa madai kwamba wakandarasi hawajalipwa pesa zao. Sasa ni lini Serikali itawalipa pesa zao ili wakandarasi hawa waongeze kasi ya kusambaza umeme kama ambavyo Serikali imeahidi hapa ndani ya Bunge?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu. Kwa mujibu wa kanuni swali hili muda wake umekwisha. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na napenda nimthibitishie Mheshimiwa Nape kwamba wiki mbili zilizopita Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Benki Kuu ilifungua *Letter of Credit* kwa makampuni zaidi ya 18 kiasi cha shilingi bilioni 260. Naomba nilithibitishie Bunge lako tukufu kwamba kuanzia sasa miradi ile itashika kasi kwa sababu tatizo la ufunguaji wa *Letter of Credit* limekwisha na Benki Kuu imefanya kazi yake na ninapenda niishukuru sana. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Haule, halafu Mheshimiwa Catherine.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Mikumi ni Jimbo la kitalii na kuna wawekezaji wengi sana wamejenga mahoteli kule katika Jimbo la Mikumi katika maeneo ya Kikwalaza, Tambukareli pamoja na kule Msimba, lakini mpaka leo wanatumia majenereta na hawana umeme. Je, Serikali

haioni umuhimu wa kupeleka umeme maeneo hayo ili kuwawezesha wawekezaji wetu waweze kuwekeza katika sekta hii muhimu ya utalii?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa hii, kama ambavyo nakumbuka naye Mheshimiwa Haule anakumbuka, Bunge lako hili hili aliuliza swali la msingi kuhusu upelekaji wa umeme katika Jimbo lake. Napenda nimthibitishie kwamba majibu tuliyotoa ya upelekaji wa umeme wa Awamu ya Tatu na kwa maeneo aliyotaja ambayo yanahusiana na masuala ya utalii, Serikali ya Awamu ya Tano italifanyia kazi. Namwomba aiunge mkono bajeti yetu leo, tuendelee kufanya kazi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Catherine.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Nishati alifanya ziara katika Jiji la Arusha tarehe 18 Machi na alifanya mkutano wa hadhara na wananchi wa Mkonoo, Kata ya Terat na kuwaahidi hadi kufikia mwezi Aprili, umeme wa *REA* utakuwa umeshaanza kushughulikiwa, lakini sasa ni Mei hakuna chochote kinachoendelea, je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake kwa wananchi hawa wa Mkonoo, Kata ya Terat? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa, ni kweli Mheshimiwa Waziri alifanya ziara katika Kata hiyo ya Terat na kwa kuwa Mkoa wa Arusha Mkandarasi wake *NIPO* ambaye anafanya kazi vizuri alitoa maelekezo hayo na kwa kuwa mkandarasi *NIPO*

ni mmojawapo wa Wakandarasi ambao wamefunguliwa *Letter of Credit* na ameagiza vifaa, ninaamini kwamba kazi itafanyika. Kwa hiyo, napenda nimwagize Mkandarasi *NIPO* wa Mkoa wa Arusha atekeleze agizo la Mheshimiwa Waziri na kwamba mwezi huu wa tano unaoendelea mpaka mwezi wa sita umeme uwe umewaka katika maeneo haya ambayo yameainishwa. Nampongeza sana Mheshimiwa Catherine. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara hiyo hiyo, Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia.

Na. 313

**Kuvusha Umeme Chini ya Bahari Kwenda Kilindoni**

**MHE. MBARAKA K. DAU** aliuliza:-

Kisiwa cha Mafia kinapata umeme kutoka kwenye jenereta kubwa ya *TANESCO* ambayo nayo inatumia mafuta mengi yenye gharama kubwa.

Je, ni lini Serikali itavusha umeme chini ya bahari *(submarine cables)* kutoka Nyamisati kwenda Kilindoni takribani kilometa 50?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaraka Kitwana Dau, Mbunge wa Mafia, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* imefanya tafiti za awali za kuona njia bora ya kuipatia Wilaya ya Mafia umeme wa uhakika na wa bei nafuu. Tafiti za awali zilizofanyika ni kuvusha umeme chini ya bahari *(submarine cables)* kutoka Nyamisati hadi Kilindoni na utafiti wa pili ni kuzalisha umeme kwa kutumia

vyanzo mchanganyiko *(hybrid)* vya umeme jua, upepo na mafuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti hizi za awali zimeonesha kuwa gharama za kuzalisha umeme kwa kutumia vyanzo mchanganyiko ni nafuu zaidi na hivyo hatua za awali za utekelezaji wa mradi huu zimeshaanza. Uwezo wa mitambo hii ya kuzalisha umeme itakapokamilika inatarajiwa kuwa na megawati saba ikilinganishwa na uwezo wa megawati 3.68 zilizopo kwa sasa (megawati 2.18 zinamilikiwa na *TANESCO* na megawati 1.5 zinamilikiwa na kampuni binafsi ya Ng'omeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa tayari *TANESCO* imeshapata eneo la mradi Wilayani Mafia kwa ajili ya kujenga mitambo ya kuzalisha umeme na inakamilisha taratibu za kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu utakaoainisha gharama halisi za utekelezaji wa mradi huo ambapo unatarajiwa kuanza kazi mwezi Juni, 2018 na kukamilika ndani ya miezi saba. Aidha, Benki ya Maendeleo ya Ufaransa imeonesha nia ya kufadhili mradi huo mara upembuzi yakinifu utakapokamilika.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dau halafu Mheshimiwa Mayenga ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri, lakini nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, Mheshimiwa Naibu Waziri anasema mshauri elekezi ataanza kazi mwezi Julai na itachukua kama miezi saba. Sasa nataka atuhakikishie watu wa Mafia, baada ya miezi saba ya mshauri kumaliza kazi, je, ujenzi rasmi wa hizi *hybrid* utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa sasa hivi kuna tatizo kubwa sana Mafia la kukatikakatika umeme na vyanzo ni vya mafuta, hivyo vimekuwa havitoshelezi na kwa kuwa Mikoa ya Lindi na Mtwara imeshaingizwa kwenye

Gridi ya Taifa na kuna majenereta pale kama manane hivi ya *two megawatts,* je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni sasa kwa kipindi hiki cha mpito wakati tukisubiri hizo jitihada nyingine kuwa tayari, tupatiwe angalau majenereta mawili yale ya Lindi na Mtwara?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa. Mheshimiwa Mbaraka Dau, swali lake la kwanza ameuliza baada ya upembuzi yakinifu kuanza na kukamilika, nimthibitishie kwamba ni kweli mradi huo utaanza ndani ya hiyo miezi saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumweleza Mheshimiwa Dau kwamba kwa mujibu wa swali langu la msingi tumesema kabisa kwamba Benki ya Maendeleo ya Ufaransa imeonesha nia ya kufadhili mradi huu na kinachosubiriwa ni upembuzi yakinifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa eneo tumelipata na kazi itaanza mwezi wa saba, naomba nimthibitishie kwamba kwa kudra za Mwenyezi Mungu kwa kipindi cha miezi saba hiyo na kwa kuwa tunayo benki tayari imeonesha nia, kazi hiyo itaanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili, ameuliza kwamba sasa baada ya mafanikio makubwa ya kuunganisha Mikoa ya Mtwara na Lindi kwenye Gridi ya Taifa, amewasilisha ombi kwa niaba ya wananchi wake na naomba nimpongeze, ni lini kwamba tunaweza tukapeleka yale majenereta?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kama Serikali tumelipokea hilo jambo lake na linazungumzika, lakini kwa sasa tunajaribu kwa sababu uzinduzi wenyewe wa kuunganisha umeme wa gridi umefanyika tu juzi, tunajaribu kuangalia upatikaji wa umeme baada ya kuunganisha mikoa hii kwenye gridi, lakini hapo baadaye tutakapoona umeme

umetulia unapatikana kwa ukamilifu, basi nalo linazungumzika na tutalipokea. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mayenga hayupo. Mheshimiwa Vullu.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusu umeme kupelekwa Mafia, naomba kujua nini harakati na mkakati wa Serikali wa kupeleka umeme katika Visiwa vya Jibondo, Chole na Jiwani huko huko Mafia? Kwa sababu Jibondo, Chole na Jiwani vyote hivyo ni visiwa ndani ya Kisiwa kikuu cha Mafia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa, kwa kuwa *REA* kupitia miradi ya kupeleka umeme vijijini upo mradi wa kupeleka umeme katika maeneo ya *off-grid* ikiwemo visiwa; visiwa alivyovitaja Jibondo, Jiwani na Chole vipo katika mkakati huo na kama miezi minne iliyopita *REA* ilifanya tathmini katika maeneo mbalimbali ya visiwa vikiwemo Visiwa vya Kibiti, Mkiongoroni, Mbuchi, Salale, Saninga, Koma na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka nimthibitishie mradi huo upo na bahati nzuri wafadhili ambao ni Serikali ya Norway pamoja na Sweden wapo ku-*support* maeneo yote ya visiwa ikiwemo hata Visiwa vya Ukerewe na maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilithibitishie Bunge lako tukufu kwamba mradi huo upo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa majibu mazuri.

Waheshimiwa Wabunge, tumwache akaandae majibu ya bajeti leo. Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Bulaya.

Na. 314

## Kutokunufaika kwa Vijiji Vinavyopakana na Hifadhi ya Serengeti

**MHE. ESTER A. BULAYA** aliuliza:-

Vijiji vya Tamau, Nyantwali, Serengeti, Mcharo, Kanzugu, Bukore na Mihale Wilaya ya Bunda vinapakana na Hifadhi ya Serengeti lakini havinufaiki na chochote kutoka katika hifadhi husika.

Je, ni utaratibu gani umeandaliwa na Mamlaka ya Hifadhi ya Wanyamapori ili kusaidia vijana wanaozunguka hifadhi kupatiwa ajira ili kunufaika na hifadhi husika kama njia mojawapo ya kudumisha ujirani mwema?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ester Amos Bulaya, Mbunge wa Bunda Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Hifadhi ya Taifa ya Serengeti inapakana na Wilaya nane ambazo ni Ngorongoro, Meatu, Itilima, Bariadi, Busega, Tarime, Bunda na Serengeti. Aidha, Wilaya ya Bunda ina vijiji sita vinavyopakana moja kwa moja na hifadhi ambavyo ni Serengeti, Nyatwali, Tamau, Balili, Kuzungu na Bukore. Aidha, vijiji vya Mihale na Bukore vinapakana na pori la Akiba la Ikorongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2017/2018 hifadhi imetenga jumla ya shilingi 32,233,180 kuchangia ujenzi wa madarasa mawili katika shule ya msingi Bunyunyi, Kijiji cha Hunywari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Halmashauri ya Wilaya ya Bunda inaendelea kukusanya tozo za huduma yaani *hotel levy* kwenye hoteli na *lodges* katika hifadhi zilizopo kwenye eneo la utawala la Wilaya hiyo. Mchango wa hifadhi

katika Wilaya ya Bunda kutoka mwaka 2004/2005 hadi mwaka 2017/2018 ni shilingi 276,720,630 ambazo zimetumika kutekeleza jumla ya miradi tisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na miradi ya ujirani mwema, Wizara imekuwa ikichangia katika Halmashauri ya Wilaya ya Bunda asilimia 25 ya mapato yanayotokana na ada ya shughuli za uwindaji wa kitalii zinazofanyika katika mapori ya Akiba ya Ikorongo na Gurumeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha mwaka 2004/2005 hadi 2014/2015 Halmashauri wa Wilaya ya Bunda ilipokea jumla ya shilingi 156,200,125.87. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017 na 2017/2018 yaani kuanzia juni mwaka 2017 hadi Januari 2018 Halmashauri ya Wilaya ya Bunda imepokea jumla ya shilingi 77,559,441.84.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri mambo mengi wamekuongopea humu, siyo Wilaya wala Halmashauri ya Mji ambayo imewahi kunufaika na chochote kutokana na Mbuga ya Serengeti. *The way* walivyokujibu kama Bunda, kuna Halmashauri moja. Hivi vijiji vyote viko kwenye Halmashauri ya Mji na asubuhi nimetoka kuongea na Mkurugenzi na Mhasibu hatujawahi kupata hata shilingi moja. Ni lini sasa tutapata hii asilimia 25 ya tozo za uwindaji? Swali la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi wanaozunguka Mbuga ya Serengeti katika Jimbo langu wamekuwa wakipata tatizo kubwa sana la tembo kuharibu mali zao na Mheshimiwa Jenista ameshajionea uharibifu huu. Takribani wananchi 880…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester uliza swali.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** ...kati ya hao waliolipwa ni 330 tu, bado watu 550 hawajalipwa kifuta jacho japo kidogo. Ni lini sasa watalipwa? *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Mheshimiwa Waziri majibu. Swali kama hili labda ungemwambia tu mkutane baadae mmalizane, myajibu, maana itakuwa ni vizuri zaidi. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme kwamba ni kweli kabisa Wilaya ya Bunda ina Halmashauri mbili na haya majibu sisi tunayoyatoa tunatoa katika Wilaya, siyo katika Halmashauri. Tunatoa katika Wilaya nzima, tunazungumzia Wilaya. Kama ingekuwa kwamba labda inatakiwa tuangalie kwenye Halmashauri, basi majibu hayo yengefanana. Hayo majibu niliyoyasema na hizo fedha ambazo nimezisema ni zile zilizoletwa katika Wilaya nzima ya Bunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa nijibu maswali yake kama ifuatavyo; kwa asilimia 25 na kwa kuwa Halmashauri yake ya Mji ina vijiji vinavyopakana na haya Mapori ya Akiba na hizi fedha nilizosema zimeshapelekwa, kama bahati mbaya Halmashauri yake haijapata mgao, basi tukitoka hapa nitafuatilia kuhakikisha ule mgawanyo unakwenda katika vijiji vyote vinavyohusika. Kwa hiyo, hilo nitalifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba nirekebishe kidogo takwimu, kwa takwimu sisi tulizonazo Mheshimiwa Mbunge, katika Wilaya ya Bunda, kifuta jasho kilicholipwa ni kwa wahanga 1,127 ambao jumla ya shilingi 186,333,350 zimelipwa kama kifuta jasho. Shilingi milioni moja zililipwa kama pole kwa mhanga mmoja ambaye alipoteza maisha.

Kwa hiyo, suala la kusema kwamba hazijatolewa, zimetolewa na katika *list* niliyonayo mpaka sasa hivi nimeangalia kama Bunda kuna wahanga ambao wanadai, bado sinayo. Kwa hiyo, kama wapo ambao bado wanadai, naomba hiyo *list* tuipate ili tuweze kuifanyia kazi kusudi waweze kulipwa mara moja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Komanya, halafu Mheshimiwa Mbatia.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu inapaswa kunufaika na miradi ya maendeleo inayotokana na ujirani mwema, *Outreach Department* kutokana na *Serengeti National Park* na *Ngorongoro Conservation;* lakini ni zaidi ya miaka kumi haujawahi kutekelezwa mradi wowote.

Je, ni lini sasa Halmashauri ya Meatu italetewa miradi ya maendeleo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa majibu kwa kifupi sana, muda wetu umekwenda.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa kwamba taasisi zetu zote zinazohusika na masuala ya uhifadhi zinao mpango madhubuti kabisa wa kuhakikisha kwamba zinachangia katika miradi mbalimbali ya vijiji vile vinavyozunguka katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Wilaya ya Meatu nina uhakika kabisa kwamba imetengewa kiasi cha fedha ambazo zitatekeleza miradi mbalimbali ya vile vijiji vinavyozunguka katika maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, tumekuwa tukifanya hivyo, kwa mfano, takribani kuanzia mwaka 2004 mpaka 2016 jumla ya shilingi bilioni 17.2 zimetumika katika kutekeleza miradi mbalimbali ya vijiji vinavyozunguka hifadhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nina uhakika na Wilaya ya Meatu ni mojawapo ambayo imefaidika na itaendelea kufaidika. Na mimi naomba tuwasiliane baadae

ili tuone kwamba imetengewa kiasi gani katika mwaka unaofuata.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mbatia. Waheshimiwa Muda wetu ni mdogo, naomba radhi sana.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Mkoa wa Kilimanjaro umezungukwa na vijiji 88 ambavyo ni vya ujirani mwema, lakini kwa miaka kumi iliyopita mapato ya mlima huu ilikuwa ni shilingi bilioni 471.5 lakini vijiji vinavyozunguka vimepata shilingi bilioni 2.28 tu ambayo ni chini ya asilimia 0.48 wakati sera ni asilimia 7.5.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haioni umuhimu ili vijiji hivi vipate haki yake badala ya kupata shilingi bilioni 2.6 kwa mwaka, wapate shilingi bilioni 40, *TANAPA* waweze kukaa na Halmashauri husika za Rombo, Moshi na Hai ili waweke utaratibu ili waweze kupata haki yao inavyostahili? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa vijiji vingi vinapakana kabisa na ile hifadhi yetu ya Mlima Kilimanjaro na niseme tu kwamba katika utaratibu wa sera ya ujirani mwema, tunachokifanya sisi katika bajeti nzima ile ya *TANAPA* tunatenga kati ya asilimia tano mpaka asilimia saba kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali ile ya ujirani mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukusema kwamba basi hizi zote asilimia saba ndiyo ziende katika vile vijiji, katika lile eneo husika. Maadam Mheshimiwa Mbatia ameleta haya mapedekezo, tutakaa chini, tutayaangalia na nitaiagiza *TANAPA* wakae na hizo Halmashauri ili kuona namna gani wanaweza kufaidi zaidi katika huo mradi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwenyewe amefurahi, amekupigia makofi.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Mifugo. Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo.

Na. 315

**Kuboresha Miundombinu ya Malambo Tarafa ya Umba na Mkomazi**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI** aliuliza:-

Eneo la tambarare la Tarafa ya Umba na Mkomazi hususan Vijiji vya Mkundi - Mbaru, Mkundi - Mtae lina miundombinu ya majosho ya mifugo na malambo ya kunyweshea mifugo iliyo chakavu.

(a) Je, ni lini sasa Serikali itaboresha miundombinu hii ili ipunguze adha ya wafugaji kuhangaika?

(b) Kwa kuwa eneo hili ni la wafugaji tangu mwaka 1954, je, ni lini sasa Serikali italiwekea mpaka rasmi ili kupunguza migogoro isiyokwisha ya wafugaji na wakulima?

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza uniruhusu nikutakie heri ya siku yako ya kuzaliwa hii leo na baada ya kukutakia heri ya siku yako ya kuzaliwa, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mbunge wa Mlalo, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto ilijenga birika la maji la kunywea mifugo katika Kijiji cha Kamba kupitia miradi ya maji ya kunywa vijijini. Pia mwaka 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto kwa kushirikiana na wafugaji ilikarabati josho na birika la kunywea mifugo katika Kijiji cha Kivingo kwa gharama ya shilingi milioni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 kiasi cha shilingi milioni 4.8 zilimetengwa kwa ajili ya kukarabati majosho mawili katika Vijiji vya Mkundi-Mtae na Kiwanja ili kupunguza adha ya wafugaji kuhangaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka 2018/2019 Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto imetenga shilingi milioni kumi kutekeleza mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Vijiji vya Mkundi - Mtae, Mkundi - Mbaru na Kivingo. Aidha, utekelezaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi utahusisha uwekaji wa alama za kudumu kwa maana *(beacon)* pamoja na uendelezaji wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya malisho kwa kuweka miundombinu muhimu ya mifugo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe wito kwa Halmashauri zote nchini kuweka mipango ya matumizi bora ya ardhi ili kupunguza migogoro kati ya wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

(a) Pamoja na majibu ya Serikali ambayo kwa kweli hayaridhishi sana na hayaendani hata na swali lilivyoulizwa, naomba tu sasa nipate kuuliza kulingana na majibu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shilingi milioni 4.8 alizotenga kwa ajili ya majosho katika vijiji vya Mkundi - Mtae na Kiwanja, haoni kwamba ni fedha chache sana kulinganisha na hizi shilingi milioni 12 zilizotengwa kwa ajili ya Vijiji vya Kamba na Kivingo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huo, Serikali haioni kwamba haina dhamira ya kweli ya kuondoa kero kwa wafugaji?

(b) Kwa kuwa hakuna maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maeneo ya malisho, hili nalizungumza mwezi wa

Ramadhani nikiwa na uhakika; hizi *beacon* Serikali inazotaka kwenda kuweka, inaenda kuziweka katika maeneo gani? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi kwa namna ambavyo anawapigania wananchi wake hasa kundi hili muhimu la wafugaji katika Jimbo lake. Swali lake la kwanza anataka kujua juu ya dhamira ya dhati ya Serikali katika kuwasaidia wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimhakikishie kwamba Serikali inayo dhamira ya dhati ya kuwasaidia wafugaji na ndiyo maana katika bajeti yetu ya mwaka huu 2018/2019 ziko pesa tulizozitenga kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunatengeneza miundombinu ya mifugo na kwa upande wa swali la pili, anasema wapi tunakwenda kuweka hizo *beacon?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mipango ya matumizi bora ya ardhi ipo katika Halmashauri na ardhi za vijiji zipo kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Sheria ya Ardhi na Sheria Na. 6 ya Matumizi ya Ardhi. Kwa hiyo, namna ya kupanga na namna ya kutumia bado ipo katika mamlaka ya Serikali za Mitaa wao wenyewe ikiwa Mbunge yeye ni mmojawapo katika Madiwani ambao wanapaswa kwenda kusimamia na kushiriki katika upangaji wa matumizi bora ya ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimwambie kwamba kwa upande kama Serikali Kuu tunayo sheria inayolinda maeneo hayo hasa ya malisho, Sheria Na. 13 ya mwaka 2010 inayohusu malisho ya mifugo. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba sisi kama Serikali tuna nia dhahiri na ya dhati kabisa ya kuwasaidia wafugaji.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Kiruswa.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa asilimia 95 ya wakazi wa Longido ni wafugaji na ndicho wanachokitegemea kwa uchumi wao; na kwa kuwa mvua kubwa za mwaka huu zimeharibu miundombinu ya mabwawa likiwemo bwawa la Kimokolwa lililopasuka, Emuriatata na Sinoniki; na kwa kuwa mabwawa mengine matatu yanayotegemewa...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa ulizwa swali, kwa kuwa zimekuwa nyingi.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri ana mpango gani au ametutengea fedha kiasi gani kurekebisha miundombinu hiyo iliyoharibika?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Kiruswa anataka kujua ni kiasi gani tumewatengea? Tunayo hela ambayo tumeitenga kwa ajili ya kuweza kuwasaidia wananchi wa Longido kwenda kurekebisha miundombinu yao ya mifugo ikiwa ni pamoja na mnada wa mifugo wa pale Longido.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili la miundombinu iliyopasuka kutokana na mvua nyingi zilizonyesha nchini, naomba mimi na yeye Mheshimiwa Mbunge tuweze kukutana na kuweza kulijadili na kuona ni namna gani tutaweza tukatoka kwenda kuwasaidia wananchi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Ameshakuelewa. Mheshimiwa Julius Kwa kifupi sana.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kuuliza swali kwamba kwa kuwa tatizo

kubwa la nchi yetu katika wafugaji ni suala la upatikanaji wa maeneo ya malisho na sheria ya mwaka 2010 ya Nyanda za Malisho Serikali ilishayaridhia.

Je, ni mkakati gani ya Serikali kuhakikisha kwamba kwa kutekeleza sheria hiyo inatenga maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Unajibu vizuri sana maswali, isipokuwa usirudie swali lake.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na nashukuru kwa kunipongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sheria Na. 13 ya mwaka 2010 inatekeleza sheria mama za ardhi Sheria Na. 4 na Sheria Na. 5 ya mwaka 1999, lakini inatekeleza pia Sheria Na. 6 ya Matumizi ya Ardhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi zote zinataja kwamba umuhimu wa Serikali za vijiji kutambua wadau wanaokwenda kutumia ardhi zile na kuwatengea na kuwapimia na kuwamilikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado inabaki kuwa ni kazi ya Halmashauri yenyewe, kisha kazi ya kutambua na kuwapa idhini ya kwamba hili ni eneo la malisho ni yetu sisi kwa kulingana na sheria yetu Na. 13 ya mwaka 2010.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaomba Waheshimiwa Wabunge wote....

**MWENYEKITI:** Ameshakuelewa, ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaelekea Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso.

Na. 316

**Hitaji la Kibali cha Kilima Pamba - Wilaya ya Tanganyika**

**MHE. MOSHI S. KAKOSO** aliuliza:-

Wakulima wa Vijiji vya Vikonge, Bugwe, Majalila na Kupanga wako tayari kulima kilimo cha pamba katika Wilaya ya Tanganyika, tatizo lililopo ni Serikali kutoa kibali cha idhini ya kulima kilimo hicho.

Je, ni lini Serikali itatoa kibali hicho ili wananchi waanze shughuli za kilimo cha pamba?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba niwatakie Waislamu wote nchini Ramadhan Kareem. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Moshi Selemani Kakoso, Mbunge wa Mpanda Vijijini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali iliweka marufuku ya kilimo cha pamba katika badhi ya maeneo ikiwemo Mkoa wa Katavi ili kuzuia kuenea kwa mdudu anayeitwa funza mwekundu. Zuio hilo ni mojawapo ya utekelezaji wa makubaliano ya kimataifa ya kuzuia kuenea kwa wadudu ambao hawako kwenye maeneo mapya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali ilipokea taarifa iliyotolewa na Mheshimiwa Kakoso kuhusu uwepo wa wakulima wa pamba katika Wilaya ya Tanganyika. Kutokana na taarifa hiyo, timu ya wataalam kutoka Chuo cha Utafiti cha Ilonga na Bodi ya Pamba ilitumwa kwenda Wilayani Tanganyika na Mpanda ili kupata uthibitisho kuhusu uwepo wa wakulima wa pamba na kufanya tathimini ya mwenendo wa funza mwekundu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa iliyoandaliwa na wataalam hao imeainishwa kwamba mdudu huyo hayupo katika maeneo ya Mkoa wa Katavi yanayokaliwa na watu. Aidha, taarifa ilibainisha kwamba Wilaya za Tanganyika na Mpanda hazipatikani na eneo lenye zuio na kupendekeza Wilaya hiyo na Wilaya zote hizo ziruhusiwe kulima pamba.

Kutokana na taarifa hiyo, Serikali kwa msimu wa mwaka 2017/2018 imetoa kibali cha kuruhusu zao la pamba lizalishwe katika Wilaya ya Tanganyika na Wilaya ya Mpanda Mkoani Katavi na uzalishaji umeanza katika Wilaya hiyo. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo, mwenye swali ni Mheshimiwa Kakoso, subiri kwanza.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Kwanza naipongeze Serikali kwa jitihada ambazo walizifanya na kutoa ushirikiano kwangu na kuwawezesha wakulima hawa waweze kulima zao hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la msingi, kwa kuwa wakulima wamelima pamba kwenye maeneo ya Wilaya ya Mpanda Tanganyika na wamelima kupitia mfumo usiokuwa na ushirika, je, hawaoni sasa ni wakati muafaka kwa wakulima hawa ambao wamelima zao hili waruhusiwe kununuliwa zao lao kupitia makampuni binafsi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Halmashari za Manispaa ya Mpanda na Halmashauri ya Wilaya ya Tanganyika watanufaika vipi na zao hilo hasa kupitia *cess* ambayo Halmashauri wanatakiwa waipate? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, kuna tukio muhimu sana lipo ndani ya Bunge na haijawahi kutokea katika Mabunge yote Duniani. Tanzania itakuwa ni ya kwanza.

Naomba kumtambua Jaji Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye yuko na mwenyeji wake Mheshimiwa Spika wa Bunge la Tanzania. *(Makofi)*

Naamini watu wa *camera* mmpata picha nzuri na tukio hili litaingia kwenye *Guinness Book of Wonders* kwa sababu haijawahi kutokea. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza naomba nichukue fursa hii kumpongeza kabisa Mheshimiwa Kakoso kwa sababu amekuwa ni *champion* kwa uanzishwaji wa zao la pamba katika Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye maswali yake mawili ya nyongeza; la kwanza ni kuhusu mazao yale ya *cess.* Naomba nitoe rai kwa Halmashauri zote nchini, ushuru wa mazao wanatakiwa wajipange na kufanya mikakati thabiti kuhakikisha kwamba mazao ndiyo yanayoingizia Hamlashauri mapato. Kwa hiyo, natoa rai kwa Halmashauri zote nchini zihakikishe kwamba zinatilia mkazo katika ushuru wa mazao ambao ni ule tunaita *cess*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine naomba nitoe rai kwamba wakulima wote nchini wajiunge kwenye *AMCOS* (Vyama vya Msingi vya Ushirika) na ndivyo ambavyo sisi kama Serikali sasa hivi tunaimarisha katika kuleta mapinduzi ya vyama vya ushirika. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndassa, ajiandae Mheshimiwa Chegeni halafu Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilikuwa naomba kumwuliza Mheshimiwa Waziri,

je, anajua kwamba mpaka sasa Bodi ya Pamba haijatoa leseni kwa wanunuzi wa pamba na sababu ni nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, swali fupi majibu mafupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Ndassa kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo swali lake moja dogo la nyongeza kuhusu Bodi ya Pamba kutotoa leseni mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba sasa hivi tuko kwenye mchakato wa kuhakikisha kwamba Bodi ya Pamba inatolewa leseni na haitazidi mwezi ujao leseni itakuwa imetolewa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Chegeni, swali fupi.

**MHE. DKT. RAPHAEL M. CHEGENI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. Je, Mheshimiwa Waziri anafahamu kwamba Vyama vya Ushirika vimeshakufa muda mrefu na kwamba sasa wakulima wanalazimishwa wauze pamba kupitia Vyama vya Ushirika. Je, nini tamko la Serikali kuwasaidia wakulima wa pamba?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi. Jiandae Mheshimiwa Mulugo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kama nilivyosema ni kwamba tumeamua kufanya *total transformation* kwenye Vyama vya Ushirika ili tuweze kuimarisha na kuboresha. Kwa maana hiyo, Serikali tumejipanga kuhakikisha kwamba wakulima wote kupitia Vyama vya Ushirika tutakuwa tunahakikisha wanapouza mazao yao wanalipwa pesa zao pale pale bila kungoja kupitia kule Benki. Nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mulugo.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipatia na mimi nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Songwe au Wilaya ya Songwe kwa ujumla hatuna zao la biashara zaidi ya zao la Pamba ambalo tulikuwa tunalima mwaka 1995 wakati sisi tunasoma mpaka leo. Wananchi wa Songwe hawana zao la biashara kabisa.

Sasa naiuliza Serikali, je, toka mwaka huo wanafanya utafiti wa huyo mdudu mwekundu lakini maeneo haya ya Tanganyika kama alivyosema Mheshimiwa Kakoso na Katavi yote ni Ukanda ule ule wa kwangu Mbeya, Songwe na alikotokea Mheshimiwa Naibu Waziri.

**MWENYEKITI:** Swali, swali.

**MHE. PHILLIPO A. MULUGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itaruhusu sasa Bonde la Songwe tuweze kulima pamba kama ambavyo leo ametoa kibali kwa Wilaya ya Tanganyika? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi. Anataka kujua ni lini tu, nanyi mnakaa *block* moja huko.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu langu la msingi nimesema Mkoa wa Katavi Serikali tumeruhusu baada ya utafiti wa kina kufanyika kwamba zao la pamba liweze kulimwa kwenye Mkoa wa Katavi. Kwenye jibu langu la msingi nilisema, maeneo yale yanayopakana na Mkoa wa Katavi ikiwemo kwenye Jimbo la Mheshimiwa Mulugo kule Songwe, ni kwamba utafiti unaonyesha kwamba bado funza mwekundu yupo katika eneo lile la Mheshimiwa Mbunge.

Kwa hiyo, naomba atoe subira kwa Serikali ili utafiti wa kina ufanyike kwamba funza mwekundu ameshaondoka katika eneo hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mipata.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Wilaya ya Nkasi hatuna kabisa zao la biashara, na kwa kuwa Wilaya ya Tanganyika inapakana na Wilaya ya Nkasi, naiomba Serikali, je, iko tayari kwenda kufanya utafiti ili wananchi wa Wilaya ya Nkasi wapate kuruhusiwa kulima zao la pamba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye jibu la swali la nyongeza la Mheshimiwa Mulugo na katika swali la nyongeza la Mheshimiwa Mipata, hayo maeneo yote yanapakana na Jimbo la Mpanda pamoja na lile la Katavi. Kama nilivyosema ni suala la utafiti katika Wizara yetu ya Kilimo ili tujiridhishe kwamba funza mwekundu bado yuko kwenye maeneo hayo au ameshaondoka? Kwa hiyo, tunaomba muda tumalize kufanya utafiti wa kina na wa haraka ili tuweze kuwapatia majibu ya msingi na ya uhakika. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani.

Na. 317

**Malipo kwa Mawakala wa Pembejeo za Kilimo**

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itawalipa Mawakala wa Pembejeo za Kilimo fedha zao ambazo walikopesha Serikali tangu mwaka 2014/2015?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, wifi yangu kama ifuatavyo:-

Mhesimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2014/2015 Serikali ilitoa ruzuku ya pembejeo kupitia vikundi vya wakulima na benki jamii badala ya utaratibu wa vocha za pembejeo uliokuwa unatumika awali. Utaratibu huu ulitumika kwa lengo la kuwajengea uwezo wakulima kuweza kukopa na kujipatia pembejeo wao wenyewe. Serikali ilitakiwa kuchangia asilimia 20 ya gharama za pembejeo zinazotosheleza ekari moja tu. Utaratibu huu ulikuwa utumike nchi nzima, lakini Mikoa iliyotekeleza ilikuwa ni Morogoro, Njombe, Iringa, Manyara, Mbeya, Ruvuma, Rukwa na Tabora tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yangu ilipokea na kupitia nyaraka mbalimbali za Makampuni na Mawakala wa Pembejeo 23 zenye madai ya jumla ya shilingi 7,180,914,669 waliofanya kazi ya kusambaza pembejeo zenye ruzuku msimu ule wa kilimo 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhakiki wa awali umefanyika kwenye mikoa kumi. Kupitia uhakiki huo wa awali imejiridhisha pasipo shaka uwepo wa upungufu kwa baadhi ya Makampuni na Mawakala kwa madai waliyowasilisha ikiwemo kukosekana kwa nyaraka za manunuzi, kutokuwepo kwa mikataba ya kazi, kukosekana kwa orodha ya wakulima wanufaika katika vijiji husika na kukiukwa kwa taratibu za utoaji wa pembejeo kwa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na matokeo ya uhakiki huo wa awali kuwa na upungufu mkubwa katika madai hayo, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kufanya uhakiki wa kina katika Mikoa yote na kwa Mawakala wote ili kubaini uhalali wa madai hayo ili madeni halali yaweze kulipwa. Taarifa rasmi ya uhakiki huo itatolewa mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa pembejeo zilizogawiwa kwa msimu wa mwaka 2016/2017 ambapo Kampuni ya Mbolea Tanzania *(TFC)* ilipewa jukumu la kusambaza mbolea na baadhi ya Kampuni na Mawakala wa Mbegu walisambaza mbegu bora, uhakiki pamoja na

ukaguzi wa mahesabu unaendelea. Uhakiki huu utakapokamilika, taarifa itatolewa mapema. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ngonyani.

**MHE. JACQULINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasikitishwa sana na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jambo kubwa hili la Mawakala wa Pembejeo. Pamoja na majibu hayo, naomba niulize swali moja dogo la nyongeza lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokuwalipa Mawakala kwa wakati kwa kisingizio cha uhakiki kwa kipindi cha miaka minne ambapo Mawakala hao wamekuwa wakiishi kwa shida, wamekuwa wakifilisiwa mali zao na wengine wamekuwa wakipoteza maisha, naomba sasa *commitment* ya Serikali, ni lini Serikali itawalipa mawakala hao?

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inachelewesha malipo ya mawakala kwa zaidi ya miaka mitatu na thamani ya fedha kwa huduma waliyotoa haitalingana na thamani hiyo endapo wangelipwa kwa wakati. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwalipa mawakala hawa fedha zao ikiwa ni pamoja na riba ya asilimia tano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ninaelewa *concern* ya Mheshimiwa Mbunge, ninaamini pia na Wabunge wengi na hata katika bajeti yetu ya Wizara ya Kilimo alitoa na machozi, nampa pole katika hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi kabisa ni kwamba Serikali ya Awamu ya Tano ina nia njema na *intention* yake siyo kwamba haitaki kuwalipa mawakala hawa wa pembejeo, lakini kwenye jibu langu la msingi kama nilivyosema ni kwamba uhakiki unaendelea na uhakiki huu ni wa kina; na mara utakapofanyika sisi kama Serikali tutatoa

taarifa na vilevile kama Wizara ya Kilimo wale wahusika wote ambao walikuwa chini yetu watumishi wa Serikali, tumeshawafukuza kazi.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, muda wetu mdogo. Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini.

Na. 318

**Korosho Zilizochanganywa na Mawe**

**MHE. HAWA A. GHASIA** aliuliza:-

Je, Serikali imechukua hatua gani kwa walioruhusu korosho zilizochanganywa na mawe kusafirishwa nje ya nchi bila kuchanguliwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Soko la Korosho ghafi katika msimu wa 2017/2018 lilikuwa zuri hususan kutokana na kupanda kwa bei ya korosho na kuuzwa kuanzia shilingi 3,500 hadi shilingi 4,000 kwa kilo. Bei ilipanda kutokana na Serikali kuimarisha minada ya korosho na kuwahamasisha wanunuzi kutoka nchini Vietnam kuja kununua korosho moja kwa moja Tanzania badala ya kupata korosho hizo kupitia India kama ilivyokuwa imezoeleka kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na hali hiyo, baadhi ya watu wasio waaminifu katika tasnia ya korosho wameanza kuchanganya korosho na vitu visivyokuwa korosho yakiwepo mawe na kokoto au kuchanganya korosho nzuri na mbovu kwa lengo la kuharibu Soko la korosho nje ya nchi. Suala hili lilibainika baada ya makontena

mawili ya korosho ghafi kutoka Tanzania kugundulika kuwa zimechanganywa na kokoto huko Vietnam. Timu ya uchunguzi iliyoundwa na Serikali imebaini kuwa korosho hizo zilitoka Tanzania na zilipitia katika Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zilizochukuliwa na Serikali ni pamoja na kuwafanyia uchunguzi wa kina wale wote walioripotiwa katika taarifa ya timu ya uchunguzi iliyoundwa na Serikali ili hatua stahiki zichukuliwe kwa watakaobainika kuwa waliruhusu korosho zilizochanganywa na kokoto kusafirishwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua nyingine ni pamoja na kuitaka Bodi ya Korosho Tanzania, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi ya Ghala, Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Mamlaka za Serikali za Mitaa kushirikiana katika kuimarisha usimamizi wa ubora wa korosho katika mnyororo wake wote kudhibiti uhalifu huo. Pia kusimamia kikamilifu na kuhakikisha kwamba korosho zinazosafirishwa nje ya nchi zinakuwa na ubora unaostahili na kuweka nembo ya utambulisho kwa maana ya kuzi-*brand* na mfumo wa kuzitambua korosho zake nje ya nchi na hivyo kulinda soko lake na kuzitaka kampuni za ndani na nje ya nchi kuwasilisha malalamiko yao Serikalini pindi yanapotokea matatizo katika biashara zao kabla ya kuzisambaza kwenye mitandao ya kijamii na kwenye vyombo vya habari kwa kuwa huchafua jina la biashara ya korosho za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchunguzi unaofanywa sasa na vyombo vyetu vya dola umeshapelekea watuhumiwa kadhaa kukamatwa na kwa manufaa ya uchunguzi huo Serikali itatoa kauli mara itakapokuwa tayari kufanya hivyo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ghasia, halafu ajiandae Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa korosho ambazo zimegundulika kuwa zimechanganywa na mawe zilipitia Bandari ya Dar es Salaam

na tatizo hilo halipo katika Bandari ya Mtwara: Kwa nini Serikali isitoe kauli kwamba kwa korosho za Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma ni marufuku kupitishwa katika Bandari ya Dar es Salaam?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, huu uchunguzi unaonekana umechukua muda mrefu sana na swali langu niliuliza walioruhusu, ni rahisi sana kukamata walioruhusu korosho hizo ziende kwa sababu kulikuwa na uwezekano kabisa kuzigundua kabla hazijasafirishwa kwenda nje ya nchi. Kwa nini Serikali inasita kuwataja waliohusika ili iwe fundisho kwa wengine katika msimu ujao? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi na haya makontena yote yanapita kwenye *scanners*, kwa nini *scanners* hazikuona mawe?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza uhalifu hauna *destination* lakini sisi Kama Serikali hilo tumelipokea, tutalifanyia tathmini na tuangalie jinsi gani Bandari ya Mtwara inaweza ikatumika pia badala ya ile ya Dar es Salaam ingawa pia hao watu wabeba mizigo hata meli unakuta wakati mwingine anataka apeleke mzigo mahali ambapo pia anaweza akarudi na mzigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika swali lake la pili, Serikali sisi sio kwamba tunapata kigugumizi. Tume ya kitaalam ilimaliza kazi yake na tumeshawasilisha hili jambo kwenye vyombo vya dola, inafanyia kazi na mara tu ule uchunguzi wa kina na wa uhakika utakapofanyika wote waliohusika watatajwa na hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yao. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Nakuona umekaa na kitambaa kwenye meza hapo. Mheshimiwa Kuchauka.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Baada ya tasnia ya korosho mwaka 2017 kufanya vizuri sana msimu uliopita, mwaka huu kumekuwa na matatizo ya

mgogoro katika Mkoa wa Lindi kati ya Chama cha Ushirika cha Runali na Bodi ya Korosho. Jambo hili limefanya mpaka sasa hivi *sulphur* iwe bado haijafika katika Mkoa wa Lindi jambo ambapo limefanya sasa hivi mfuko mmoja wa *sulphur* kufika shilingi 70,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itoe tamko, ni lini mtatuletea *sulphur* ili kupunguza bei ya *sulphur* ambayo imepanda baada ya kuwa na mgogoro kati ya Runali na Bodi ya Korosho?

**MWENYEKITI:** Ahsante. Swali jipya kabisa, lakini Mheshimiwa Waziri lijibu, na ajiandae Mheshimiwa Chikota.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna tatizo la kuchelewa kwa *sulphur,* lakini kutokana na swali lake alilouliza, mpaka sasa hivi ni kwamba Chama kile cha Runali kimeshaagiza tani 128 za *sulphur*, zimeshafika na zimeshasambazwa. Vilevile kwa faida ya wengine hata *TANECU* wameshaagiza tani 1,100 na tayari zimeshasambazwa na zinauzwa kwa shilingi 32,000. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba mkulima mdogo wa korosho hawezi kufanya hujuma hizi na hujuma hizi zinafanywa na makampuni makubwa na msimu wa korosho unatarajia kuanza mwezi wa tisa.

Kwa nini Serikali inakuwa na kigugumizi cha kuwataja makampuni hayo ili msimu ujao wasiingie katika soko la korosho? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati najibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dada Hawa Ghasia, nimesema kwamba Serikali hatuoni na hatujapata kigugumizi chochote, ni kwamba tayari tume ya wataalam tumeshawasilisha ile taarifa ya uchunguzi kwenye vyombo vya dola, vinalifanyia kazi na mara tu ule uchunguzi wa uhakiki utakapofanyika na wa kina basi wote watatajwa na hatua kali za kisheria dhidi yao zitachukuliwa. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji. Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki.

Na. 319

**Ujenzi wa Mabwawa ya Maji Wilaya ya Mkalama Mkoani Singida**

**MHE. ALLAN J. KIULA** aliuliza:-

Wilaya ya Mkalama iliyoko Mkoani Singida hupata mvua chini ya wastani na maji yote ya mvua hutiririka na kupotea.

(a) Je, Serikali inachukua hatua zipi kutoa kipaumbele kwa Wilaya ya Mkalama kujengewa mabwawa makubwa hasa ikizingatiwa kuwa fedha za ndani *(own sorce)* za Halmashauri haziwezi kutosheleza ujenzi wa huduma hii?

(b) Je, ni lini Serikali itafanya utafiti kuona kiwango cha maji kinachopotea wakati wa mvua na kutoa ushauri wenye tija?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Jimbo la Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji imeziagiza Halmashauri zote nchini kuainisha maeneo yanayoweza kujengwa mabwawa na kutenga fedha kwenye bajeti zao kwa ajili kujenga angalau bwawa moja kwa mwaka. Katika mwaka 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama imeendelea na kazi ya kuainisha maeneo kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ambapo hadi sasa Vijiji vya Kitumbili, Nkito, Malaja, Nkalankala, Lyelembo na Nduguti kazi hii imekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti wa maji hufanyika linapofanyika zoezi la kuyatambua maeneo yanayofaa kujengwa mabwawa ili kujua kiasi cha maji kinachoweza kuhifadhiwa katika mabwawa hayo ikilinganishwa na mahitaji. Hivyo, kazi hii ya utafiti ya maji yanayopotea kipindi cha mvua yanaweza kufanyika sambamba na zoezi la kuainisha maeneo yanayofaa kwa kujengwa mabwawa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiula halafu Mheshimiwa Dkt. Sware na Halima Bulembo wajiandae.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza, kwa sababu *catch line* ni kwamba Halmashauri haina uwezo wa kujenga mabwawa, Serikali ipo tayari kutoa pesa hata bwawa moja moja kujenga mabwawa Mkalama katika maeneo yaliyotajwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa sababu ni ukweli usiopingika kwamba Halmashauri hazina uwezo wa kufanya utafiti, Serikali iko tayari kunipa watafiti nikaondoka nao kwenda kufanya utafiti na mimi nitakuwa nao huko?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, muda wetu umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa namna anavyowapigania wananchi wake. Kwa kutambua changamoto kubwa sana ya maji katika Jimbo la Mkalama, Mheshimiwa Waziri wangu aliona haja ya kumsaidia Mheshimiwa Mbunge, akaagiza Mamlaka kwa Wakala wa Uchimbaji Visima *(DCCA)* kumchimbia visima 20 katika Jimbo lake katika kutatua tatizo la maji. Namwomba Mheshimiwa Mbunge wakati Serikali ikiangalia namna ya kumchimbia mabwawa, asimamie visima hivi ili wananchi wake wapunguze adha ya maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kumpatia watalaam, sisi kama Wizara ya Maji hatutokuwa na kikwazo chochote kumpatia watalaam aende nao katika kuhakikisha wanafanya utafiti, wananchi wake waendele kupata maji. *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Ahsante. Mheshimiwa Halima halafu Mheshimiwa Dkt. Sware.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru. Ukiachilia mbali Mkoa wa Kagera uko karibu zaidi na Ziwa Victoria, lakini Mkoa wa Kagera una uhaba mkubwa wa maji. Ni lini sasa Wizara itaamua kubuni mradi mkubwa wa maji kama ule unaotoa maji Ziwa Victoria kwenda Tabora, ukizingatia Mkoa wa Kagera uko karibu zaidi na Ziwa Victoria? *(Makofi)*

**MWENYEKTI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi sana, muda wetu mdogo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutambua maji ni uhai nasi kama Wizara ya Maji jukumu letu ni kuhakikisha tunawapatia wananchi maji. Tumefanya jitihada mbalimbali wananchi ambao ni wakazi wanaoishi pembezoni na maziwa kuhakikisha wanapata maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mkurugenzi wa eneo husika aandae mradi ambao sisi kama Wizara tutaangalia namna ya ku-*support* kwa haraka wananchi wake waweze kupata maji kwa haraka safi, salama na yenye kuwatosheleza.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Sware. Waheshimiwa muda wetu ni mdogo.

**MHE. DKT. IMMACULATA S. SEMESI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Jimbo la Kondoa la Vijijini pia lina uhaba wa mkubwa wa mabwawa na yale yaliyopo yanahitaji ukarabati mkubwa hususan katika bwawa la Kisaki ambalo linahudumia mifugo na wanadamu.

Sasa Serikali ina mpango gani pia wa kuweka jicho la ziada katika Halmashauri ya Wilaya ya Kondoa Vijijini? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu ya Maji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, imekuwa ikichimba mabwawa na hata visima virefu katika maeneo yenye ukame mkubwa sana. Labda nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwa kuendelea kushirikiana na wafadhili wetu, tutaangalia namna ya kuweza kuondoa tatizo hilo na kuwachimbia mabwawa. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, muda wetu ni mdogo. Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili.

Na. 320

**Tofauti za Mitaala kwa Shule za Serikali na Shule Binafsi**

**MHE. NURU A. BAFADHILI** aliuliza:-

Shule za Serikali na shule binafsi zina mitaala tofauti, je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka wa kuwa na mfumo mmoja wa mitaala?

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nuru Awadhi Bafadhili, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtaala hutolewa kwa lengo la kuweka mwongozo mpana wa viwango vya utoaji elimu kwa kuzingatia idadi ya masomo yatakayofundishwa, umahiri utakaojengeka, njia za ufundishaji na kujifunzia, vifaa vya ufundishaji, upimaji, ufuatiliaji na tathmini za mtalaa husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtalaa unaotumika katika shule za Serikali na shule binafsi ni mmoja na wanafunzi wote wanaosoma shule hizo hupata umahiri unaofanana. Aidha, mtalaa ambao ni tofauti ni ile mtu inayotumika katika shule chache za kimataifa *(international schools)* zilizopo nchini. Mitalaa hii ya kimataifa imeruhusiwa ili kukidhi mahitaji ya raia wa kigeni wanaoishi hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bafadhili.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Takwimu ya ufaulu zinaonesha kuwa wanafunzi wa Serikali wanapata idadi ndogo ya ufaulu kuliko *private*. Hiyo inasababisha kupata nafasi ndogo ya udahili katika vyuo na inasababisha kupata watalaam wachache kutokana na uchache wa nafasi zao ya udahili.

Je, Serikali haioni kwamba inaweza ikapoteza watalaam kutokana na uchache wa wanaodahiliwa kwa kuwa wanafunzi wengi wa *private* wanaachwa kwa dhana

kwamba wana uwezo wa kulipia ada za vyuo kutokana na uwezo wao uliokithiri wa kusoma katika shule hizo za *private? (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, miaka ya nyuma shule zilikuwa za sekondari na msingi zikifundisha masomo ya ufundi mbalimbali; uhonaji, useremala na kadhalika, je, Serikali ina mpango gani ya kuhakikisha inarudisha tena masomo haya ya ushonaji, ufundi mbalimbali kwa vitendo ili kuweza kuwawezesha wanafunzi wanapomaliza masomo yao wajiajiri? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Nuru swali lake la kwanza amezungumzia habari ya takwimu ya wanafunzi wanaomaliza kwenye *private school* na wale wanaomaliza kwenye shule za Serikali. Naomba nimhakikishie kwamba hili suala ni la kitakwimu na anachokisema sidhani kama ana uhakika kwamba wa *private* ni wengi kuliko wale wa shule za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ni swali la kitakwimu, basi tutalichukua ili tuweze kuleta takwimu sahihi kulingana na alichokizungumza. Kwa imani natambua ya kwamba hakuna ambapo shule za Serikali zimekuwa nyuma sana ukilinganisha na za *private* kitakwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali lake la pili linazungumzia habari ya wanaomaliza ni namna gani wataweza kuendelezwa akirejea kwamba zamani mitaala ilikuwepo ya kufundisha useremala na mambo mengine. Naomba nimhakikishie kwamba Shule zetu au vyuo vyetu vya *VETA* zinafanya kazi hiyo ya kuweza kufundisha wanafunzi wanaoishia *form four* au darasa la saba mambo ya ufundi, lakini vile vile tuna vyuo 55 ambavyo vilikuwa ni Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na sasa hivi kati yake karibu vyuo 20

vinakarabatiwa ili kuweza kufundisha ufundi stadi kwa wanafunzi wale ambao wanakuwa wameshindwa kuendelea na masomo ya sekondari aidha kwa *A' level* au kwa *form one.*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Issaay, halafu Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. Hivi sasa nchi nzima hatuna vitabu vya elimu ya msingi kwa darasa la nne hasa mitalaa mpya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa wanafunzi hawa wanatarajia kufanya Mitihani ya Taifa hivi punde mwisho wa mwaka huu, Serikali ina utaratibu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama majibu ya Serikali hayatatosheleza kwa umma wa Watanzania na sisi Wabunge, basi tuahirishe mjadala ulioko mezani tukajadili jambo hili kwa manufaa mapana ya nchi yetu. Naomba majibu ya Serikali.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, anachokizungumza Mheshimiwa Mbunge sidhani kama ni sahihi, kwa sababu ni karibu wiki mbili au tatu zimepita Wizara imesambaza vitabu vya darasa la kwanza mpaka darasa la nne kwa Halmashauri zote nchini. Sasa kwa hali hiyo, nina imani kwamba vitabu vipo katika mashule na hapana huo upungufu anaozungumza kwa sasa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri kwamba mtalaa wa shule binafsi na

Serikali ni mmoja, lakini kwa zaidi ya miaka kumi shule za binafsi zimekuwa zikiongoza katika ufaulu.

Je, Serikali pamoja na kwamba inasema ina wajibu wa kusimamia kiwango cha ubora elimu nchini, haioni sasa ni wakati muafaka kujifunza kwa watu binafsi ni kwa namna gani wanafundisha watoto wao wanafaulu katika shule zao; badala ya kwamba Serikali inayosimamia ubora lakini shule zake zimekuwa zikifanya vibaya? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda tu nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, siyo kweli kwamba shule za binafsi zinafanya vizuri zaidi ya kuliko shule za Serikali. Ninachotaka kumhakikishia ni kwamba...

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI**: Sikilizeni majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y. WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia idadi ya wanafunzi wanaokwenda kwenye shule za *private* ni wachache kuliko wanaokwenda kwenye shule za Serikali. Kwa hiyo, kwa vyovyote unapofanya *rating* ya wanafunzi, lazima pia uzingatie na wingi wa wanafunzi. Kwa hiyo, asilimia kumi ya wanafunzi 20 huwezi kulinganisha na asilimia kumi ya wanafunzi 1,000 kwa maana ya kwamba idadi inakuwa tofauti. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, kipindi cha maswali kimekwisha na muda wetu umekwisha.

Wageni wa Mheshimiwa Spika waliopo kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika ni wafuatao, Mheshimiwa Fuya

Kimbita, Mbunge Mstaafu, karibu Bungeni, Ndugu Hadija Ahmed Abdallah, karibu Bungeni na Ndugu Ahmed Gwebe, karibuni sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni waliopo Jukwaa la Spika, wageni 21 wa Mheshimiwa Subira Mgalu Naibu Waziri wa Nishati ambao ni Wenyeviti wa UWT na Makatibu wa Wilaya zote za Mkoa wa Pwani na Kamati ya Utekelezaji ya Mkoa wakiongozwa na Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Pwani, Mheshimiwa Farida Mgomi na Katibu Mkoa Ndugu Sophia Masawe. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Mheshimiwa Subira Mgalu, Naibu Waziri, ni ndugu zake watano kutoka Mkoa wa Pwani wakiongozwa na Ndugu Kurwa Mgalu, mdogo wake. *(Makofi)*

Wageni wengine wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 25 wa Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab ambao ni viongozi wa Chama cha Mapinduzi kutoka Wilaya ya Muheza Mkoani Tanga wakiongozwa na Ndugu Laiyak Guru, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Muheza, karibuni sana. *(Makofi)*

Pia kuna wageni 15 wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni makada wa CCM Jimbo la Ukonga kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 16 wa Mheshimiwa Oran Njeza ambao ni viongozi wanne wa Kamati ya Maendeleo za Kata kutoka mkoani Mbeya na wanafunzi 12 wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Mbeya Vijijini, Mkoani Mbeya, wakiongozwa na Ndugu Upendo John. *(Makofi)*

Vilevile tunao wageni 84 wa Mheshimiwa Zuberi Kuchauka Mbunge ambao ni wanafunzi kutoka shule ya msingi Nkuhungu iliyopo Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni kumi wa Mheshimiwa Emmanuel Papian ambao ni walimu wa shule ya sekondari ya Eco kutoka Kiteto, Mkoani manyara. *(Makofi)*

Wengine ni wageni 20 wa Mheshimiwa Rashid Ajali ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma, wanaotokea Newala Vijijini, Mkoa Mtwara. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Abdallah Mtolea, ambaye ni Mwenyekiti wa *Makangarawe Youth Development Association* Ndugu Vincent Ngoholai. *(Makofi)*

Pia tunaye mgeni wa Mheshimiwa Victor Mwambalaswa ambaye ni mjomba wake kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Gervas Mwakyoma, karibu. *(Makofi)*

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Omary Mgumba ambao ni watoto wake kutoka Jijini Dar es Salaam Ndugu Dimoso Mgumba na Ndugu Juma Suwapanga. *(Makofi)*

Pia yupo mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi, ambaye ni mtoto wa kaka yake kutoka Kihesa, Mkoa wa Iringa, Ndugu Jackson Chumi. *(Makofi)*

Pia tunao wageni 10 wa Mheshimiwa Mariam Ditopile ambao ni wanafunzi wenzake wanaosomea Shahada ya Uzamili kutoka Chuo cha Biashara *(CBE)* kilichopo Jijini Dodoma, karibuni. *(Makofi)*

Wapo wageni wanne wa Mheshimiwa Martin Msuha, ambao ni Viongozi wa CCM Kata za Ubungo Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Pia tunao wageni watano wa Mheshimiwa Constatine Kanyasu, ambao ni Waheshimiwa Madiwani kutoka Halmashauri ya Mji Geita wakiongozwa na Mheshimiwa Morand Constantine ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Geita, Karibuni. *(Makofi)*

Wengine ni wageni wanne wa Mheshimiwa Alex Gashaza ambao ni Makatibu wa Ofisi ya Mbunge kutoka Ngara Mkoani Kagera wakiongozwa na Mkuu wa Makatibu Ofisi ya Mbunge Ndugu Fadhili Rusange. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Wabunge wote kuwa Katibu aliwapatia madodoso kutoka MKURABITA na kuwaomba wajaze na kuyarejesha. Hivyo tunakumbusha wajaze na kuwapatia wahudumu wa ukumbini. Suala hili ni muhimu kwani takwimu zitakazopatikana ni kwa manufaa ya wananchi katika Majimbo ya maeneo ya uwakilishi.

Mheshimiwa Ngeleja, Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club* anaomba kuwatangazia Wabunge wote kuwa siku ya Jumamosi na Jumapili kutakuwa na Mechi ya Kirafiki siku ya Jumamosi *Ndugai Boys Versus* Kombania ya Jeshi, kwa mchezo wa *football, netball, volleyball* na *basketball*.

Aidha siku ya Jumapili *Ndugai Boys* watacheza na Chuo cha St. John kwa mchezo wa *football* na *netball*. Michezo yote itafanyikia kwenye Uwanja wa Jamhuri kuanzia saa 9.00 alasiri. Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi, mnakaribishwa. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Hoja za Serikali.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu ni mdogo na bajeti hii mnajua ina umuhimu kupitishwa haraka. Tukianza miongozo tutakosa wachangiaji wengi.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Hapana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Katibu.

**MHE. SAED A. KUBENEA:** Hoja ya kuahirisha mjalada.

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 - Wizara ya Nishati**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaanza na uchangiaji. Mheshimiwa David Silinde dakika kumi na Mheshimiwa Nape dakika tano.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati. Nina mambo kama sita hivi ya kuzungumza. Jambo la kwanza ambalo nataka nilizungumzie ni kampuni ya *TANESCO* kugharamia wananchi wetu wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi *TANESCO* inahitaji wateja, lakini pamoja na kwamba *TANESCO* inahitaji wateja kule vijijini kwenye hii miradi ya *REA* wananchi wetu wa vijijini wamekuwa wakitakiwa ambalo ni jambo jema kabisa kulipa shilingi 27,000 na kwingine mpaka sasa hivi mradi ukishakuwa umepita wanalipa zaidi ya shilingi 100,000 na kitu.

Natoa ushauri kwa *TANESCO* kwenye hili, endapo *TANESCO* inahitaji wateja wengi, namba moja inahitaji wakati wa Mradi wa *REA* Vijijini unapita wale wananchi waunganishiwe umeme bure kwenye vijiji vyote. Zile gharama ambazo mwananchi anahitaji kugharamia huu umeme atalipishwa kwenye ile mita au matumizi ya umeme kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili nimelitoa kwa sababu, kwa sasa hivi ukienda vijiji unakuta mradi umepita kwenye kijiji kimoja, wenye umeme ni watu 10 au 15. Sasa tuangalie hali halisi. Hili mkilipokea nafikiri litaweza kuongeza idadi ya wateja, wananchi wetu watalipa na watatushukuru sana kwa kufanya hivyo, hilo ni jambo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Wizara ya Nishati kumekuwa na uagizaji wa mafuta kwa kupitia mfumo wa *bulk procurement*. Mfumo huu tuliupitisha hapa Bungeni kwa lengo moja kwamba mafuta yaagizwe nchini ili bei ishuke, lakini mpaka sasa hivi, pamoja na mfumo huu wa *bulk procurement* kila siku tunaona bei za mafuta zikipanda kadri siku zinavyokwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nazungumzia mfumo huu, mfumo huu sasa hivi umekuwa ni *monopoly* na umekuwa ni kama vile unatukandamiza sisi watumiaji wa mafuta nchini. Kwa hiyo, ombi langu kwenu Serikali na *TANESCO* kwenye huu mfumo tufanye jambo moja kama tutakubaliana sio jambo baya kuwa na mfumo wa *bulk procurement,* lakini kama kuna watu wana uwezo wa kuagiza mafuta kwa kiwango ambacho kinaweza kikaletwa na hiyo meli moja, muwaruhusu walete nchini ili kuwepo na *competitiveness* kwenye soko huria, sio kama sasa hivi mnavyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ninaisema kwa sababu moja, mfumo huu wanafanya kwa kutumia tenda sasa hawa watu ambao wanachukua kwa mfano mnapata labda PUMA anapewa jukumu la kuleta mafuta nchini kwa mwezi huo anakwenda abidi bei ya juu tofauti na bei ya kwenye soko la dunia, unakuta bei kule labda kwa pipa moja ni dola 50 lakini yeye ana-*bid* pipa moja kwa dola 70. Kwa hiyo, matokeo yake watu wanaoumia ni wananchi wetu wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu, hali ya upatikanaji wa umeme hapa nchini. Ukisoma hotuba ya Mheshimiwa Waziri ameandika hapa kwamba kufikia mwaka 2020 umeme utakuwa megawati 5000 na mwaka 2025 megawati za umeme zitakuwa 10000. Nimepitia miradi yote hapa, nikagundua kabisa kwamba kuna kitu Serikali inatudanyanya ni kuweka hizi takwimu za uongo. Kwa miaka 50 mpaka leo hii, megawati ninavyozungumzia leo ni 1,517 ni takwimu ambazo zipo kwenye kitabu chake yeye mwenyewe. Sasa anatakiwa ndani ya miezi 16 iliyobakia

kumaliza awamu hii hapa maana yake tumebakiza kama miezi 16 anatakiwa amalizie megawati 3500. Sasa ukija ukipitia utekelezaji wa miradi, miradi mingi inategemea mikopo ambayo hatuna uhakika wa kupata hizo fedha, lakini jambo la pili, wanataka kuanzisha miradi ya gesi ambayo ukisoma kitabu cha mpango, hakuna mahali popote tumezungumzia hii miradi ya gesi namna ambavyo itakwenda kutekelezeka na hakuna fedha yoyote ambayo imetengwa katika mpango wa mwaka ambao ulisomwa huku ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la gesi najua Serikali ni kama hili jambo tumeamua kuliacha ama kulipuuza kidogo, gesi ukiangalia kwa sasa hivi nchini, tuna-*reserve* ya karibu trilioni 57 *cubic feet.* Tunasahau kabisa wenzetu wa Msumbiji, Msumbiji hapa jirani zetu, ujazo wao uliothibitika wana karibu trilioni *cubic feet* 200 sisi tuna 57 na hawa watu kwenye miradi ya gesi kule Msumbiji wameendelea kuifanya. Sasa ukisoma kwenye kitabu cha Waziri utagundua kabisa hakuna mpango wa wowote wa utekelezaji wa hili jambo kwenye kuwekeza kwenye vitalu vya gesi na utafutaji wa gesi nchini. Kwa hiyo, tunahitaji na haya vilevile Mheshimiwa Waziri utakavyokuja utupatie maelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, nataka nizungumzie ufisadi wa Kampuni ya Shell. Kampuni ya Shell, ni moja ya Kampuni kubwa, zinazodili na mafuta na gesi duniani. Kampuni hii Serikali imekaa kimya na Serikali inajua juu ya huu ufisadi, Kampuni ya Shell mwaka 2016 kipindi hiki, hiki cha Awamu ya Tano ilinunua vitalu vya Kampuni ya *BG (British Gas)* vya gesi lakini pamoja na kununua vitalu hivi, Sheria, ukisoma *The Finance Act,* hii hapa tulinayo nayo hapa, kampuni inaponunua vitalu au inapohamisha *share* kutoka kampuni moja kwenda kampuni nyingine, kabla ya kuhamisha hizo *share*, inatakiwa jambo la kwanza ilipe *capital gain tax* kwa Serikali. Lakini jambo hili limefanyika hii sheria tumepitisha mwaka 2012 jambo hili limefanyika Kampuni ya Shell haijalipa hiyo *captal gain tax* yenye thamani ya dola milioni 500 sawa sawa na shilingi trilioni 1.1 ya Kitanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalizungumza hili nikiwa na uthibitisho Kampuni ya Shell sasa hivi ninavyozungumza Nigeria imefanya tukio hili hili walilofanya Tanzania, Nigeria kule walifanya walikuwa wananunua Kampuni ya *OPL* 245 inayomiliki visima vya mafuta walifanya ufisadi huu wakahonga maafisa wa Nigeria, ufisadi wake ulikuwa una thamani ya dola bilioni 1.1 sawa sawa na shilingi trilioni 2.45.

Sasa Kampuni ya Shell kumbe imekuwa na tabia ya kuhonga wafanyakazi pamoja na Serikali kufanya haya mambo ambayo wameyafanya Tanzania. Sasa *capital gain tax* kwa Taifa letu ndio mapato ya ndani kwenye Taifa. Lakini Serikali imekaa kimya na *TRA* wameidhinisha hili jambo la Kampuni ya Shell kutokulipa *capital gain tax* ambayo ni mali ya Watanzania, hii ni mapato kwa Watanzania. Sasa tunakimbizana na walipa kodi huku unaenda leo umewasajili Wamachinga mwaka jana 8000, unakuja leo na hoja kwamba tuwapige kodi Wamachinga wakati kuna ufisadi mkubwa makampuni makubwa yanafanya katika nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya haya hayakubaliki na Mheshimiwa Waziri unajua, dunia nzima inajua, Sheli ina kesi sasa hivi kule Italy, Bilan kwenye ufisadi wa Nigeria, na ufisadi wa aina hiyo, hiyo, wamefanya Tanzania. Sasa tunahitaji majibu ya Serikali kwenye hili jambo tunataka kujua hii *capital gain tax* ambayo Shell hawakulipa kwa kununua vitalu vya *BG* inapatikana lini katika hili Bunge, tunataka iwe moja ya vyanzo vya mapato, maana yake ninaamini kabisa ukichukua fedha hizi, hizi shilingi trilioni 1.1 tatizo la maji nchini litakuwa limetatuliwa. Lakini tukiendelea kuacha *unless otherwise* mtuambie watu wamehongwa na wanashindwa kulisema hili jambo. Lakini kama kweli, watu tuna uzalendo, hizi hela lazima zirudi, na Bunge tutalipigia kelele mpaka zitapatikana katika hili Bunge, hatutakubali kwenye hili jambo liendelee namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kama Bunge litakubali baada ya Bunge kuwisha iundwe kamati maalum kufuatilia juu ya ufisadi wa shilingi trilioni 1.1

ulioufanya Kampuni ya Shell mwaka 2016 uliopelekea Taifa letu likose mapato.

Kwa hiyo, hilo nilisema ni lazima niliseme, ili Taifa lijue, na lisikie kwamba ufisadi kwenye hii nchi bado umeendelea kuwa tabia haujaisha pamoja na jitihada zote ambazo zimekuwa zikifanyika. Kwa hiyo, hilo nimeamua niliweke sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna Mradi wa *Stiegler's Gorge,* tumeambiwa kwamba bwawa la *Stiegler's Gorge* litakuwa na urefu wa kilometa 100; lakini bwawa hilo hilo, litakuwa na *square meter* karibu za kilometa 914. Tunahitaji Serikali itueleze bwawa hilo ili liweze litatumia muda gani litatumia kutumia uwezo wa kuzalisha megawati...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, kengele yako ya pili, Mheshimiwa Nape, ajiandae Mheshimiwa Adadi, ajiandae Mheshimiwa Hawa Ghasia.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie kwenye mapendekezo haya ya bajeti ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, toka tupate Uhuru Mikoa ya Kusini Lindi na Mtwara, tumekuwa na tatizo kubwa sana la upatikanaji wa umeme wa uhakika. Lakini hivi karibuni, juzi hapa, Mikoa ya Lindi na Mtwara imeunganishwa kwenye Gridi ya Taifa, nataka nichukue nafasi hii kuipongeza sana Serikali kwa uamuzi huu mzuri, uamuzi wa kijasiri wa kuikomboa Mikoa ya Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kwamba baada ya kuiunganisha Lindi na Mtwara, Mikoa ya Kusini kwenye Gridi ya Taifa, tatizo ambalo tumehangaika nalo toka tupate Uhuru sasa litakuwa limefikia mwisho. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri umeweka historia nzuri kwetu,

tumeteseka, tumepata tabu uwekezaji ulikuwa tabu kusini lakini uamuzi huu wa busara wa Serikali wa kutuunganisha na Gridi ya Taifa tunaamini utakuwa umemaliza tatizo la umeme kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu kwenu sasa, la kwanza, nadhani ni vizuri tukaboresha ile miundombinu pale ya kusambaza umeme, imekuwa ya muda mrefu. Moja ya tatizo kubwa linatokea Kusini mvua ikinyesha kwa dakika tano miundombinu yenu inakuwa hoi kabisa. Kwa hiyo, ninaamini kutuunganisha na Gridi ya Taifa ni hatua moja kubwa ya maendeleo kwa mikoa ya Lindi na Mtwara na kwa niaba ya wananchi wangu naomba nipongeze. Lakini ni vizuri sasa tukabadilisha ile miundombinu pale na hasa ile ambayo imekaa muda mrefu, tuibadilishe ili iweze kubeba huu mzigo mkubwa wa umeme ambao mmetuletea kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Naamini jambo hili sasa litafungua fursa ya uwekezaji na kukua kwa uchumi kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, nimpongeze Mheshimiwa Waziri Kalemani, bila kumung'unya maneno huwa sipendi kusifia watu lakini Mheshimiwa Kalemani, ni katika Mawaziri wasikivu. Ukimfuata anakusikiliza, Mheshimiwa Kalemani na Naibu wake ni Mawaziri wanyenyekevu, na mimi nadhani Mawaziri wengine waige mfano wa huyu bwana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika siasa ni vizuri kusikiliza na hata yale tusiyopenda kuyasikia. Mheshimiwa Kalemani ni katika Mawaziri wako tayari kusikiliza hata lile asilolipenda kusikia. *(Makofi)*

Kwa hiyo, kwa kweli nina heshima kubwa kumpongeza Kalemani na mimi nadhani akiendelea hivi, atakwenda vizuri, msikivu anasikiliza, ukimshauri anafanya. Maboresho aliyoyafanya katika Mkoa wa Lindi ametuletea Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa, msikivu sana, lakini ni kwa sababu tulimfuata, tukazungumza naye, akatuelewa na akatusikiliza, wito wangu kwa Mawaziri wengine tuigeni

mfano wa Mhesimiwa Kalemani, ukiambiwa jambo usilolipenda wewe ndio kiongozi jalala kubali, sikiliza. Naamini Mheshimiwa Kalemani atakwenda vizuri, ziko changamoto kwenye Wizara yako, lakini ninaamini ukiendelea kuwa msikivu yale ambayo yako juu ya uwezo wako, najua hayo watu watakusamehe, lakini yale ambayo yako ndani ya uwezo wako ukiyasikiliza, ukayatekeleza, tutakuunga mkono na huu ni mfano mzuri mambo yakienda vizuri tutapongeza, yakienda vibaya tutasema. Hata Naibu wake ni msikivu sana, sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nadhani umefika wakati Serikali ikalitazama suala la kuligawa Shirika la Umeme la *TANESCO* ili tuwe na maeneo mawili, upande mmoja wa usambazaji, upande mwingine wa uzalishaji na kwenye hili la kuzalisha umeme, Serikali tufungue milango kwa sekta binafsi kwenda kuzalisha hata kama tutaingia nao ubia kwa sababu siamini kama tunao mtaji wa kutosha wa kuzalisha umeme. Ninaamini tukiruhusu sekta binafsi iende ishirikiane na Serikali kwenye kuzalisha umeme mambo yetu yatakwenda vizuri ndio maana hata kwenye bajeti mwanzoni tulipokuwa tukizungumza hata wale wanaozungumza suala la *Stiegler's* sidhani kama kuna watu... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Nape. Mheshimiwa Hawa Ghasia, ajiandae Mheshimiwa Adadi kwa dakika tano tano.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kupata fursa ya kuweza kuchangia bajeti hii. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi kubwa wanayoifanya, pia kwa kuwasikiliza Wabunge na kuweza kutembea karibu kila Wilaya kwenda kufuatilia utekelezaji wa miradi ya *REA* na miradi ya umeme kwa ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Mbunge wa kutoka Mtwara napenda pia kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa ujumla kwa kutuunganisha katika Gridi ya Taifa. Ni matumaini yangu sasa uwekezaji katika mikoa ya Lindi na Mtwara itawezekana kwa sababu mwanzo kwa megawati 18 za umeme wa kukatikakatika nadhani wawekezaji kila mmoja alikuwa anasita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze pia Serikali *REA* Awamu ya Tatu tayari, katika Wilaya yangu kuna vijiji Mheshimiwa Waziri tayari kashaniwashia na nina imani vilivyobaki atahakikisha vinapata umeme kwa wakati. Nilitaka nishauri mambo matatu haraka haraka kwa sababu dakika tano zenyewe ndio hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kwanza ni kuhusu *service levy,* Wilaya yangu Manispaa ya Mtwara pamoja na Kilwa na maeneo yale ambayo yanapitiwa na bomba la gesi tulikuwa tunanufaika kupata kodi ya huduma kutokana na masuala mazima ya gesi katika Wilaya zetu na pesa hizi zilikuwa zinasaidia sana katika kuchangia maendeleo ya wananchi katika maeneo yale. Lakini cha kusikitisha tumeletewa barua na *TRA* kwamba kuanzia Julai mosi *service levy* ya gesi itachukuliwa na *TRA* kwa maana kwenda Mfuko Mkuu. Niiombe Serikali yangu ilifikirie suala hili mara mbili mbili na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na uamuzi huo na niiombe Serikali yangu uamuzi huo hebu iusitishe kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ni kuhusu gesi ya majumbani. Niipongeze Serikali nimesikia kwamba sasa hivi inataka kuanza kuiweka gesi majumbani Dar es Salaam na Mtwara. Sasa mara nyingi ukisikia Dar es Salaam na Mtwara ujue wataanzia Dar es Salaam, nikuombe Mheshimiwa Waziri katika hili naomba uanzie Mtwara, Mji wa Mtwara ni miongoni mwa miji iliyopangwa vizuri na hiyo kazi yako ya kuingiza gesi katika majumba itakuwa rahisi pia italeta amani na utulivu katika Mkoa wa Mtwara kwa sababu wananchi watayaona matunda ya moja kwa moja ya gesi katika maisha yao ya kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri pia niiombe Serikali na niiombe *TANESCO* waangalie vigezo vyao vya kujua ni megawati ngapi zinatumika katika mkoa au katika Wilaya. Mara nyingi tumekuwa tukisikia kwamba Mkoa wa Mtwara na Lindi mahitaji yao ni megawati 18, lakini kiwanda kimoja tu cha Dangote kinahitaji zaidi ya megawati 44. Sasa nataka kuiuliza *TANESCO* hivi mnavyoweka mahitaji ya mkoa au ya Wilaya mnaangalia umeme wa majumbani tu? Suala la umeme wa viwandani hamliweki na kama mlikuwa mnaangalia umeme wa majumbani tu niwaombe *TANESCO* hebu rudini upya mkaangalie mahitaji halisi kwa sababu kusema Mtwara megawati zetu ni 18 nadhani lilikuwa ni kosa la kiufundi kwa sababu viwanda vingi vinavyokuja kila kiwanda unakisikia kinataka megawati 10, megawati 15, megawati 20. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama yale mahitaji viwanda mnaviweka pembeni nadhani sidhani kama inakuwa ni sahihi kukadiria umeme kwamba utumike majumbani tu. Nina imani kabisa umeme wa viwandani ndio utakaoleta maendeleo kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI**: Ahsante. Mheshimiwa Adadi ajiandae, Mheshimiwa Flatei jiandae Mheshimiwa Lwenge.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kushukuru sana kupata nafasi hii kuchangia hoja hii ambayo ni muhimu sana ya umeme.

Kwanza napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani pamoja na Naibu wake kwa kweli kama alivyosema Mheshimiwa Nape ni Mawaziri ambao wanatakiwa kupongezwa sana ni wasikivu. Mimi kwenye jimbo langu nina kata 37 na vijiji 135 wakati vitongoji ni 522, ni jimbo moja ambalo ni kubwa sana. Lakini tumeathirika sana kwenye mgao wa *REA* kwa sababu ni nusu tu ya vijiji vyote hivyo ambavyo vimeweza kupata mgao wa *REA* wa

umeme. Sasa nawashukuru sana ndio maana nimesema namshukuru sana Dkt. Kalemani kwa sababu awamu hii ya *REA* tumepangwa kufanyiwa vijiji karibu 19 lakini kwa hisia zake na usikilizaji wake ameweza kuongeza karibu vijiji vingine vingi tu akishirikiana na Naibu Waziri pamoja na Mkurugenzi wa *REA* na Mkurugenzi Msofe, nawasifu sana hawa watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachoshangazwa kwamba mkandarasi yupo *site* muda mrefu lakini mpaka sasa hajawasha hata kijiji kimoja, sasa nimejaribu kumshauri aweke vikundi karibu hata vitatu kwa sababu vijiji vyangu ni vingi lakini bado anasita. Mheshimiwa Waziri naomba agizo lako apewe huyu mkandarasi *RADI* ili aweze kuweka kuongeza vikundi ili kazi hii iweze kwenda katika *speed* ambayo inatakikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni hii *densification* mradi huu umekuja na kijiji kimoja tuu ambacho kimefanyika kule Mgome, lakini bado haujaanza kufanyika kwa ukamilifu. Sasa ningeomba suala hili lifanyiwe mkakati mzuri ili iweze kufanyika kwa bidii sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa kulizungumzia ni mradi wa Bomba la Mafuta wa Hoima kutoka kule Uganda mpaka Tanga tunashukuru sana. Tunapongeza sana mradi huu, mradi huu ambao umepokelewa Mkoa wa Tanga kwa hisia kubwa sana tukitegemea kwamba uchumi wetu mkoa mzima wa Tanga utafaidika. Mradi huu umepita kwenye jimbo langu, na umepita hasa mpaka kwenye shamba langu. Lakini Mheshimiwa Waziri kitu ambacho tunakuomba ni kwamba najua kwenye takwimu inaonekana kwamba tumekwenda zaidi ya asilimia 90 ukilinganisha na wenzetu zaidi ya asilimia 20.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini suala la fidia ni muhimu sana lianze kufanyiwa mikakati saa hizi ili fidia hiyo iweze kulipwa mapema na wakati utakapoanza ujenzi basi kusiwe na hayo matatizo na la pili ni suala la kazi, kazi ambazo

tunategema kwamba zile kazi ambazo sio za kitaalam, sasa mradi huu kwa mfano unapita Mkanyageni, Rusanga, Bagamoyo, Ngomeni, Kilapula tunategemea wakazi wa sehemu hizi wapate hizo kazi ambazo sio za kitaalam. Nitashangaa sana kama wataalam wa kazi hizi wote watatoka Bukoba au Singida kuja kufanya kazi Tanga. Mheshimiwa Waziri hilo angalia lisijekutokea kwa sababu wananchi wa Tanga, wananchi wa Muheza wamejitaarisha sana kufanya kazi kwenye mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ningependa tu ku-*comment* kwenye mradi mkubwa huu wa *Stiegler's Gorge* au Mradi wa Rufiji, ambao umepangiwa karibu shilingi bilioni 700. Mradi huu ni mkubwa najua kuna upinzani mwingine ambao unasema kwamba mradi huu usifanyike kwa mambo kadha wa kadha. Lakini historia ya nchi hii, miradi yote mikubwa ni lazima inapingwa tu, inapingwa nikianzia kwenye mahoteli haya ya Serena, mahoteli mengi tu ya Kilimanjaro yalipoanza ujenzi tu yanapingwa, hapa tumeleta Bombardier zinapingwa, *SGR* inapingwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi mradi mkubwa huu ambao unataka kuleta megawati 2100 unapingwa. Sasa ni vizuri tu wenzetu wakaelewa kwamba wale wanaopinga pale watoe *support* kwenye mradi huu ambao ni mkubwa, kwanza Selous yenyewe ni kubwa *54,000 square metres* ni kubwa sana. Naamini wataalam walifanya kazi yao vizuri wakaishauri Serikali kwamba mradi huu ufanye kazi. Kwa hiyo, naamini kwamba mradi utakuwa na manufaa sana ya nchi.

Mheshimiwa Mwenekiti, baada ya kusema hayo naunga hoja mkono, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Flatei, atafuatiwa na Mheshimiwa Lwenge, ajiandae Mheshimiwa Julius Kalanga.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nikushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwanza nianze tu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri

ndugu yangu Kalemani na Naibu wake kwa kweli wanafanya kazi nzuri. Huwa ukimpongeza mtu unaangalia nini amefanya, Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwanza umefika katika jimbo langu la Mbulu Vijijini ambako hakujafikiwa kwa muda mrefu sana. Jimbo hili limeanza muda mrefu nashukuru sana umefika na umeangalia vijiji vyangu ambavyo havina umeme. Kwa hiyo, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sio hilo tuu nikupongeze sana kwa kuwa msikivu, umekuwa msikivu kwa sisi Wabunge kwa kweli hongera sana na ukiendelea namna hii naamini Mungu atakubariki sana na atakubariki kwa sababu unasikia kero na shida za umeme ambazo tunazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja sasa na pongezi hizi, unajua kwa nini nakupongeza Mheshimiwa Waziri? Ukianglia kwenye sala ya baba yetu kwa sisi tunaosali, inaanza kabisa pale na kusema baba yetu uliye mbinguni unamsifu huyu Mungu, lakini unaendelea tena na jina lako litukuzwe unamsifu huyu Mungu, lakini unaendelea pia ufalme wako ufike unamsifu huyu Mungu, unafika mahali unamwambia mapenzi yako yatimize unamsifu huyu Mungu. Lakini baadae pale unapomsifu Mungu, kuna ombi unachomeka kwenye sala ile ya baba yetu unamwambia hivi utupe leo riziki zetu kwa sisi wakatoliki lakini watu waprostentanti wanasema utupe leo mkate wetu. Kwa hiyo, hayo yote ni maombi. *(Makofi)*

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri ujue pamoja na sifa zote nilizokupa sasa naleta ombi kwako, kama sala ya baba yetu ilivyo, na baba yetu wa mbinguni anakuballi mara nyingi unapomsifu halafu unaongezea kitu kinachoitwa ombi.

Sasa naweka ombi hapa baada ya kusifu kwa masifu yote haya na Wabunge wamekusifu, sasa naomba niongezee sifa nyingine, pia ulifanyakazi usiku umekimbia vijiji vyote umefika Babati, umefika Mbulu, umefika Mjini, umefika kila mahali tunakutembeza usiku saa nne, hongera kwa ajili ya hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimwombe ndugu yangu, umeme wa Mbulu unahitajika sana nina vijiji 76, vinne tu vina umeme na wewe umeviona mwenyewe. Niombe basi kwa kuwa Mbulu Mjini kuna *substation* na Katesh kuna *substation* umeme wa pale Mbulu kwenye *substation* ile unatumika si zaidi ya asilimia 30. Kwa hiyo, kuna *hostage* kubwa ya umeme uliopo pale, tupelekee kwenye vijiji ambavyo nimekuomba na nimekuletea. Vijiji 41, vijiji 21umenipa na umeniahidi mwenyewe mbele ya wananachi wangu nikuombe kabisa vijiji hivi kwa kweli uviweke. Mimi naomba natumia muda huu kutaja hizi kata ili walau uzikumbuke na naamini utakumbuka. Kuna kata za Masyeda, Endagchani, Bashai, Dinamu, Maletadu, Haideleli, Hendamecha, Hendamilai, Gilihimu, Moradi, Tumatii, Labai, Magajuu, Yaendachini, Yaendaampa, Yaendanshikesh, Galababi, Geteleli na Meoda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeamua kusema haya makusudi kwa sababu jimbo langu halina umeme na kama hauna umeme hauwezi kufanya chochote. Jimbo la muda mrefu limeanza mwaka 1905 kukosa umeme ni jambo la hatari sana.

Kwa hiyo, niombe sasa umeme upo Haydom pale kwenye Hospitali kubwa ya Rufaa. Umeme ule ni wa muda urefu una miaka 28, unazimika mara tano kutwa yaani siku moja unazimika mara tano. Hospitali ile ni kubwa, naomba basi usaidie pale umeme wa haraka ufanye marekebisho makubwa ili Hospitali ya Haydom wagonjwa wanaopelekwa pale kwenye kile chumba cha *operation* wasiwe na wasiwasi kwa sababu umeme utazimika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hospitali ile inatumia madaramu 100 kwa mwezi, kwa ajili ya jenereta. Niombe sana Mheshimiwa Waziri ukipeleka pale umeme utaipatia Taifa fedha na Serikali itapata fedha, lakini pia utakuwa umeondoa adha ya umeme pale Haydom. Ni ukweli usiopingika ni kwamba Mheshimiwa Waziri baada ya kufika pale, kwa sasa nguzo zimefika, zimefika Maretaduu. Sasa nikuombe ndugu yangu, msimwambie mkandarasi aanzie

Mbulu Vijijini ili walau kazi ile iweze kwenda na basi kwakuwa wewe umefika umeahidi umeme utawaka mwezi ujao, niombe kabisa ile ahadi ishukie palepale umeme uwake kadri tulivyokuomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine naomba nichangie kitaifa sasa, pale nilikuwa nakwambia Mheshimiwa Waziri jimboni kwangu, maana kwanza jimbo halafu baadae tunakutana na Taifa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Lwenge.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuweza kuchangia bajeti ya Wizara ya Nishati. Nianze kwa kumpongeza Waziri na Naibu pamoja na wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Awamu ya Tano ni awamu ya viwanda tunataka uchumi wa viwanda, sasa ili tuweze kufanikiwa ni lazima kwamba tuunge mkono mipango iliyoletwa kwenye kitabu hiki ambacho tutapata uzalishaji wa megawati 5000 ikifika mwaka 2020, naomba sana tukubaliane naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi wanapinga Mradi wa Rufiji, mradi huu ulishafanyiwa upembuzi yakinifu, katika kufanya upembuzi yakinifu masuala ya mazingira huwa yanazingatiwa, ndiyo mradi unakuwa *viable* baada ya kuzingatia namna gani mtashughulikia masuala ya mazingira. Sasa jambo hili lilishafanyika na sasa hivi wamefikia hatua ya kupata makandarasi, kwa hiyo, wapo mbele hawarudi nyuma tena. Usanifu wa kina ulishafanyika tayari ili tuweze kupata megawati 2100 na tuweze kusambaza umeme nchi nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea sisi sote tuunge mkono juhudi hizi za Serikali, tumpongeze sana Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kufanya uamuzi mgumu kwa miaka mingi huu mradi umekuwa unawekwa danadana. Lakini tumeamua sasa kutekeleza na mwaka huu wa bajeti shilingi bilioni 700 zinatengwa kwa fedha za ndani kwa hiyo, lazima tushukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri tu kwamba katika uzalishaji wa Nishati mradi huu ni muhimu lakini pia nipongeze kwa mradi wa Ruhuji ambao unatumia maji ya maporomoko kutoka Njombe. Wananchi wa Njombe ni watunzaji wazuri sana wa vyanzo vya maji. Maana miradi hata pamoja na Rufiji ili uweze kuwa endelevu lazima tuweke mkazo katika kutunza vyanzo vya maji ili kuwe na maji ya uhakika na tuweze kupata Nishati ya bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la utekelezaji wa usambazaji wa umeme Awamu ya II, niipongeze sana Serikali tumepeleka umeme kwenye vijiji vingi. Nilitaka nitoe ushauri kujenga miundombinu ya umeme ni moja, lakini kufanya uendelevu miundombinu ile ili iendelee kutoa huduma ni jambo lingine. Sasa nilikuwa nataka nikushauri Waziri tunakwenda kupeleka umeme katika vijiji 12,000 lakini kama hatuna mpango mkakati wa kufanya *maintenance* (matengenezo) ya miundombinu hii utakuta wakati haiwi endelevu. Kwa hiyo, niishauri kwamba tuwe na kitengo ambacho kina nguvu ya kusimamia na kutekeleza hii *maintenance* ya hii miundombinu ambayo imejengwa kwa fedha za ndani za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikichukua kwa upande wa jimbo langu la Wanging'ombe nashukuru, Awamu ya Pili mmepeleka umeme kwenye vijiji takribani 40 ni kazi kubwa tunashukuru sana na katika Awamu ya Pili kuna tatizo kidogo limejitokeza, mkandarasi yule aliyekuwa ameteuliwa katika Jimbo la Wanging'ombe Mkoa mzima wa Njombe alipewa mkandarasi mmoja anaitwa *Lucky Export*. Huyo mkandarasi aliagiza vifaa toka India, hivi sasa majenereta yale aliyoleta toka India karibu 30 yameungua. Katika muda wa miaka

miwili, *life span* ya transfoma ni zaidi ya miaka 20 lakini ndani ya miaka miwili transfoma zaidi ya 30 zimeungua. Sasa mimi nataka kuuliza watu wako ambao hawaendani na kasi yako hivi walifanya *due dilligence* ya mkandarasi yule? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pili yale matransfoma waliangalia ubora wake? Kwa sababu nina mashaka. Hivi sasa hivi nimekushirikisha Waziri nina vijiji 14 toka Disemba havina umeme kwa sababu ya transfoma na sasa hivi matransfoma wanachukua *TANALEC* toka kiwanda chetu cha ndani, hilo pia...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahasante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Kalanga, ajiandae Mheshimiwa Sokombi.

**MHE. JULIUS K. LAZIER:** Mheshimwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii na kwa kweli kama Wabunge wengi wanavyosema, wengi hatuna mashaka kabisa na kazi ya Waziri huyu wa Nishati. Kweli ni msikivu kama watu wanavyosema na anasikiliza watu, lakini tatizo letu kwenye nchi si kusikiliza, tatizo kubwa tulilonalo ni kutekeleza yale tunayokubaliana kutekeleza. Na nchi hii haijawahi kuwa na tatizo la mipango, tatizo kubwa kubwa la nchi yetu ni kutekeleza kile tunachopanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hii miradi mingi ina kwashakoo kama alivyo mtu wa kawaida. Ina kwashokoo kwa sababu haina fedha, miradi yetu imedumaa, hata nia yako iwe kubwa kiasi gani kama hupewi fedha itakuwa ni bure tu. Nataka nikuhakikishie utaishia kuwa na mipango bora na mizuri lakini kwa Serikali hii ambayo haikupi fedha hautatekeleza miradi hiyo na hili ndilo tatizo ambalo ni kubwa kwenye nchi, na kama Bunge hili lina nia njema ya kusaidia watanzania lazima hili lipate suluhu ya kudumu. Haiwezekani tupange za *REA* shilingi 50 kwenye mafuta na asilimia tatu kwenye LUKU, halafu fedha zinatumiwa, halafu Bunge linakuja

hapa linapiga makofi kama vile kilichofanyika ni sahihi. *(Makofi)*

Mheshmiwa Mwenyekiti, tunataka Waziri utuambie fedha zetu tulizotenga kwenye mafuta na kwenye LUKU ziko wapi na ni shilingi ngapi na kwanini hamuwalipi wakandarasi ambao wameshindwa kutekeleza miradi kwa sababu hawapewi fedha. Kama Serikali inakula hata fedha za wananchi ya wanyonge ambao wamechanga wao hiyo Serikali mnasema ni ya wanyonge kwa kuwasaidia au kwa kuwanyonga. Miradi yenu imedumaa kwa sababu imekosa lishe kwa sababu hampeleki fedha, na hamuwezi kutekeleza. Ndio maana mnatulazimisha tuwasifu kwa kupanga na sisi tunataka kuwasifu kwa kufanya. Fanyeni tuone mlivyofanya tuweze kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili suala la *Stieglers,* naamini hakuna Mbunge hata mmoja mwenye akili timamu anaweza akapinga mradi huu. Naupongeza ni mradi mzuri, lakini kazi ya Serikali ya tuondoleeni shaka wenye mashaka, kwa nini hamtaki kutuambia hiyo *Environmental Impact Assestment* imefanyika na imeleta majibu gani? Kwa nini mnatafuta kichaka cha uzalendo sisi tukihoji? Kazi ya raia yeyote aliyeko huru ni kuhoji, na kazi ya Serikali ni kutoa majibu. Tupeni majibu ya mashaka yetu juu ya *Stieglers Gorge.* Wabunge wa Morogoro wamesema kwamba kuna wananchi wao wataenda kuathirika na mradi huu wapeni majibu. Kwa nini ninyi mnataka wanyamaze, tunataka mtupe na mtuondolee mashaka kwa takwimu za kisayansi na za kisomi sio siasa za Wabunge humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni mzuri kama tu mtatuondolea mashaka ya Watanzania. Maana nchi hii haiishi kwa miaka mitano tu ya Serikali hii, itaishi miaka mia moja ijayo na miaka mingi ijayo. Tuondoleeni mashaka msitubeze, tunataka mtuambie *Impact Assessment* mlizofanya kwa ajili ya mradi huu hiyo wazi kila Mtanzania ajadili na aridhike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio imeisha? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Endelea!

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante dakika tano, Mheshimiwa Sokombi dakika tano.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI.** Mheshimiwa Mwenyekiti,...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kalanga dakika tano zimekwisha na ulisema una msiba unakwenda kuzika, bora utangulie sasa uende. *(Kicheko)*

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI.** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kupata nafasi hii na mimi nichangie kwenye Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua fika kwamba umeme ni kichocheo kikubwa cha kuleta maendeleo hapa nchini kwetu Tanzania na inatokana na vyanzo mbalimbali kwa mfano, tuna jua, tuna upepo na tuna maji. Tunajua pia fika kwamba asilimia kubwa ya wananchi wa Tanzania wanaishi vijijini, lakini wananchi hao wanaishi vijijini lakini Serikali inaangalia tuu upande wa mjini kuliko watu wa vijijini wanaotuletea maendeleo hapa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini Serikali isione umuhimu wa kupeleka umeme wa kutosha kwa hawa wananchi wa vjijijini? Umeme unaopelekwa vijijini ni umeme kidogo sana, haukidhi haja ya wananchi waishio vijijini. Transfoma pia zilizofungwa ni transforma ambazo hazikidhi vigezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, transfoma zinazofungwa vijijini hazina uwezo hata kidogo wa kuweza hata kufunga hata *bulb* tano. Unakuta mtu ana nyumba kuna *bulb* sita, lakini umeme unaotumika pale unaweza kuwasha *bulb* mbili au tatu. Kwa hiyo, basi naomba Serikali ione jambo muhimu sana kuweza kupeleka umeme wa kutosha vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekti, tumeona *REA Phase I* tumeona *REA Phase II* lakini kuna vijiji ambavyo havijafikiwa hata kidogo na umeme huu wa *REA*. Kwa mfano Musoma Vijijini tuna Kangetutya, Rwabu, Kabulabula, Kanderema, Saragana, Nyambono na Nyambinilila lakini hao watu hivyo vijiji vyote havina umeme. Pia tuna Bunda Vijijini ambako tuna Nyang'aranga, Tingirima, Manchimwelu, Rakana, Salakwa, Nyasiloli, Tingati, Nyaburundu. Hivi vijiji vyote havina umeme*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimshauri Waziri aone umuhimu wa kuweza kupeleka umeme wa uhakika kabla hatujaenda kwenye kupeleka umeme wa uhakika. Kabla hatujaenda kwenye miradi mikubwa kwa mfano wa *Stiegler's Gorge,* tungeangalia kwanza tatizo lililoko katika *REA Phase I* na *Phase II* tukaziba mashimo kwa nini hawakuweza kufikia malengo asilimia 100 halafu pia ndiyo tungetoka kwenda kwenye mradi mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumejaaliwa kuwa na upepo wa kutosha sana hasa Singida na Same. Kwa nini tusione umeme wa kutumia upepo, kwa mfano nchi za Uholanzi na Ujerumani pia wanatumia umeme wa upepo, kwa nini Tanzania isione umuhimu wa kuwatafuta wataalam wakaja hapa kufundisha wataalam wetu ili na sisi tutumie umeme wa upepo nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu tunaona umeme wa upepo ni umeme ambao utatukwamua sana wananchi wa Tanzania kuliko kukaa kuwazia miradi mikubwa mikubwa ambayo itakuja kuharibu mazingira na kukata mingi sana nchini kwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano mdogo tu, Kijiji cha Nyabange kiko Butiama, ni nyumba nne tu zilizofungwa umeme, yaani fikiria kijiji chote ni nyumba nne tu! Hebu niambie, na tayari mkandarasi alishamaliza kazi na alishakabidhi, Je, hizo nyumba nne ina maana kwamba ziliwekwa kwa mfano au ni vipi? Serikali ituambie, ni umeme huu kweli umelenga kuwakomboa wananchi...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**TAARIFA**

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa!

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umekwisha. Ulivyoita ulikuwa unazungumza nyuma na umetumia muda mwingi sana kwenye upepo, ahsante. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Kiza, ajiandae Mheshimiwa Katani.

**MHE. KIZA H. MAYEYE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya niweze kuchangia asubuhi hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni-*declare interest* kama Mjumbe wa Kamati ya Nishati na Madini. Niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, kaka yangu Kalemani na Naibu Waziri dada yangu Subira, kiukweli mnafanya kazi na tunaiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na jitihada ambazo wanazifanya Serikali, bado kuna changamoto zipo katika suala la nishati. Nianze na suala la *REA,* katika Mkoa wangu wa Kigoma *REA II* bado kuna vijiji ambavyo havikupata umeme na kuna changamoto kwamba umeme umepita katika kijiji "A" lakini kijiji "B" hakijapata umeme. Niombe sana Mheshimiwa Waziri tunapokwenda katika *REA III* mhakikishe kwamba vijiji hivi ambavyo havikupata umeme vinaweza kupata umeme. Ninashukuru kwamba sasa tunakwenda kuzindua *REA III.* Ninaelewa Kigoma tulichelewa kwa sababu ya kesi ya mkandarasi, niombe sana pesa ziende kwa wakati, wakandarasi wale wa *REA III* wafanye kazi na tumalize kwa wakati na vijiji vile tuweze kupata umeme ndani ya mkoa wangu wa Kigoma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie tena suala la *TANESCO* ndani ya Mkoa wa Kigoma. Kigoma tunatumia umeme wa *TANESCO* ambao unagharimu sana Seriakli yetu. Tunatumia pesa nyingi kwa kutumia mafuta haya ya dizeli. Ndani ya Mkoa wa Kigoma tuna mwekezaji katika eneo la Kisezi ambaye anazalisha megawati tano mpaka sasa za umeme wa jua. Ninaomba majibu Mheshimiwa Waziri, niliwahi kukuuliza, mna mkakati gani kuunganisha umeme huu wa jua katika mkoa wa Kigoma, kwa sababu wananchi wa Kigoma tunahitaji nishati ya umeme. *(Makofi)*

Kwa hiyo, ninaamini kama tutaunganisha na kwa sababu tunakwenda kwenye Gridi ya Taifa, mkituunganishia na umeme huu ninaamini Kigoma tutakuwa na umeme wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Mkoa wa Kigoma ni mkoa *potential* sana. Ni Mkoa ambao ninaamini tukipata umeme wa kutosha tutaweza kupata wawekezaji wa viwanda vingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee tena kwa kupongeza mradi huu wa Mto Malagarasi. Nimeona katika kitabu cha Mheshimiwa Waziri, mmeanza sasa na kuna megawati 45 kutoka Mto Malagarasi kwenda Kidahwe – Kigoma, niwapongeze sana lakini niombe sasa wakandarasi wafanye kazi, pesa ziende kwa wakati na mradi huu uweze kumalizika kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee tena suala la ulipaji wa fidia. Kumekuwa na migogoro mingi na manung'uniko mengi kwa wananchi. Wanapisha miradi hii lakini Serikali inachelewesha kuwapatia fidia zao. Inasikitisha sana kwamba mtu amepisha, ni kweli wananchi wanaunga mkono Serikali yao kwa miradi ambayo inafanyika basi muwasaidie wananchi hawa waweze kupewa fidia zao kwa wakati. Kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, watu hawa ambao wamepisha mradi huu wa Malagarasi basi muweze kuwapatia fidia zao kwa wakati. Lakini hata miradi mingine kwa mfano bomba la gesi kule Tanga ambalo

linapita kwenda Uganda, muweze kuwapatia wananchi hawa fidia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niongelee tena suala la Gridi ya Taifa, Kigoma na Katavi mpaka sasa hatujaingia katika Gridi ya Taifa, ninaelewa mpo katika mchakato, ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri tuingie katika Gridi ya Taifa ndani ya Mkoa wa Kigoma kwa haraka. Nimeona Wabunge wa Mtwara wamewapongeza kwa sababu mmewafanyia vizuri wameingia katika Gridi ya Taifa. Ninaomba sasa na Kigoma tukirudi hapa mwakani tuwapongeze kwa kumaliza Gridi ya Taifa ndani ya Mkoa wa Kigoma kwa haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, niseme ahsante na ninawapongeza tena, ahsanteni. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa, Katani.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru, lakini na mimi niungane na Wabunge wanaotoka Lindi na Mtwara kukupongeza Mheshimiwa Dkt. Kalemani kwa kazi mliyoifanya majuzi ya kutuunganisha kwenye Gridi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pamoja na kazi hizi nzuri ambazo unazifanya, kwangu kule Tandahimba tuna tatizo la mkandarasi na nilishakuambia. Nilishakuambia lakini mpaka leo hakuna kinachoendelea juu ya mkandarasi yule na sijui kwa nini mlimuondoa mkandarasi wa mwanzo *NAMIS* ambaye amefanya kazi nzuri sana kwa maeneo ya Kusini. Sijui mlikuwa na *interest* gani kwenye jambo hili na hata kabla ya kumuondoa niliwahi kukuambia kwamba mkandarasi huyo ndiyo anatufaa kwa maeneo ya Lindi na Mtwara. Lakini umetupa mkandarasi ambaye hafanyi kazi vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nafuatilia nilipata kuzungumza na wewe lakini nikazungumza na mkandarasi mwenyewe kumbe wakati mwingine tatizo sio mkandarasi,

tatizo ni fedha! Hamjapeleka fedha kwa mkandarasi yule na matatizo haya ya fedha yanafanywa makusudi. Bunge linakaa linapitisha sheria, tunakusanya fedha kwenye mafuta, lakini Wizara ya Fedha hawawapi fedha hizo na ninyi mnakaa kimya, mnakuja hapa tunapanga mipango mingi ambayo haitekelezwi kwa tatizo la Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui Wizara ya Fedha tufanye jambo gani maana sio miradi hii tu ya *REA* ipo miradi mingi, umeona kwenye bajeti ya kilimo kwenye korosho fedha zimechukuliwa, kwenye *REA* fedha zimechukuliwa, sasa sijui kuna jini gani Wizara ya Fedha, sijui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwangu kule Tandahimba lakini na Taifa kwa ujumla kuna tatizo kwenye miradi hii ya *REA,* sijajua kama *TANESCO* wanafanya biashara hii ya umeme kwa biashara au namna gani? Unakwenda kwenye kata ambazo kuna watu wengi, haziendi umeme lakini umeme unakwenda kwenye kitongoji ambacho kinakaa watu 15 ukaacha sehemu ambayo kuna watu zaidi ya 10,000. Hili ukienda kwangu ndiyo liko hivyo, ukienda Kata ya Mdimba ambayo ina zaidi ya watu 16,000, ukienda Kata ya Mkoleha ina zaidi ya watu 12,000, ukienda Kata ya Mihambwe ina zaidi ya watu 15,000, ukienda Michenjele kuna zaidi ya watu 9,000, ukienda Chaume kuna zaidi ya watu 12,000 lakini maeneo haya mpaka leo hayajafikiwa na umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sijui *criteria* mnayoitumia kupeleka umeme huu wa *REA* maana huo umeme unapokwenda ni nguzo tatu kutoka barabarani ndiyo zinaenda ndani. Kwa hiyo, hata unaposema kwamba *REA* inaenda vijijini sijajua tafsiri ya vijiji ni ipi maana unakwenda kwenye kitongoji, nguzo tatu tu zinaingia ndani, eneo kubwa la wanavijiji wanakuwa hawapati umeme. Sasa nadhani Mheshimiwa Waziri kuna namna ya kufanya ili mambo yenu yaende sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nirudi sasa kwenye mradi wetu wa gesi. Mimi ni miongoni mwa wahanga wakubwa, wakati tunatetea rasilimali ya gesi Mtwara nimekaa jela sana,

nimekaa jela sana kwenye jambo hili na leo kuna mambo yananiumiza sana. Kwenye mradi wa bomba la gesi tunaouzungumza ambao tulikuwa na *LNG* ambayo najua Mheshimiwa Waziri huna mamlaka nayo, hakuna huu mradi wa *LNG* haupo tena. Wala usitudanganye danganye ukatupa chenga, *LNG* tena haipo! Ndiyo maana mmeanza na mamiradi mengine makubwa ya *Stiegler's Gorge* na wenzangu wamesema na mara nyingi wenzetu wa upande wa upande wa pili mmekuwa mkitoa tafsiri tofauti kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna mpinzani anapingana na mradi huu wa Rufiji, hakuna! Hayupo mpinzani anapingana na mradi huu lakini watu mkisimama mnasema wapinzani sio wazalendo, sisi sote ni wazalendo na tunalipenda Taifa letu. Tunachosema ni tathmini, tathmini hiyo ya kitaalam ifanywe. Bahati njema kwenye Baraza lenu la Mawaziri, zipo *Ph.D holders* zaidi ya 15 sijui huko! Sasa sijui kwenye kuangalia mambo haya mnayaangalia kwa namna gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wanawashauri kwa nia njema ya Taifa hili lakini mnageuza mnadhani kwamba wapinzani sio wazalendo. Mimi naomba mjue sana kwamba Watanzania sisi viongozi tuliokuwepo humu ndani wote ni wazalendo. Mtumie hekima za pamoja kama Mheshimiwa Dkt. Kalemani amezungumza ndugu yangu pale Mheshimiwa Nape, Mawaziri msikilize yanayosemwa! Mpate muda wa kuwasikiliza watu wanasema kitu gani, hata msiyoyapenda, myasikilize, kama haya mnayoambiwa kwenye *Stiegler's Gorge* hamjafanya utafiti wa kimazingira mkubali! Mlishasema, anasimama mtu hapa anasema walifanya utafiti lakini ukweli ni kwamba utafiti haujafanywa! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli ni kwamba utafiti haujafanywa. Tuangalie, mradi huu tunaozungumza gharama yake ni trilioni tano, lakini Mheshimiwa Waziri wewe unajua kwamba mradi wa umeme huu wa upepo unahitaji shilingi trilioni 2.5 na tunapata megawati 3500, unajua! Lakini kwanini tujibebeshe mzigo yaani una mzigo wa kilo kumi

umekushinda, unasema unataka ubebe wa kilo 50, ndiyo Serikali ya CCM tunaenda nayo hii. Kwenye gesi una miradi mingi, *Kinyerezi I, Kinyerezi II,* una mradi ule wa Somangafungo una ule wa Mtwara, una megawati zaidi ya 1,055 haijakamilika tunakwenda kwenye dubwana hili kubwa, mnaambiwa kwa kushauriwa vizuri, zifanywe tafiti za uhakika za kimazingira athari za watu wale lakini watu wanageuza maneno haya, wanasema watu sio wazalendo, watu sio namna gani, nawaambia wapinzani ni wazalendo kweli kweli ndiyo maana mengi yaliyozungumzwa na wapinzani Rais Magufuli anayatekeleza, yaliyozungumzwa na wapinzani kwa kuhakikisha kwamba Wapinzani ni wazalendo, yapo mengi sana yamezungumzwa, lakini tunazungumza mambo mengi kwa sababu Serikali haifuati utaratibu kwa mara nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka mfanye mambo kwa kufuata utaratibu, myalete Bungeni tuyajadili, mlete ukweli wa mambo mnayoyafanya, lakini mkiambiwa mnadhani wapinzani mara zote hawana uzalendo na Taifa hili. Wapinzani hawa wana uzalendo na Taifa hili kwa kiasi kikubwa sana. Niwaombe sana, tunapochangia, hakuna mtu mwenye nia mbaya na ninyi Mawaziri, lakini tunataka Taifa liende mbele. Tusichukue miradi mingi ambayo hatuwezi kuitekeleza kwa maslahi ya watu fulani. Kama kuna miradi ilianzwa mwaka 2015 na Rais aliyepita, ninyi mnaoingia mmalizie ile miradi muanzishe mingine wakati mingine imekamilika. Matokeo yake *policy* yenu ni mbovu, kila anayeingia madarakani anaanzisha *project* mpya, nchi sijui imekuwaje hii! Hii nchi sijui inakwendaje hii! Na tunaposhauri haya tunashauri kwa nia njema ndugu zangu, hatuna tatizo sisi na CCM, tuna tatizo na utendaji wenu mbovu wa CCM ndiyo tunashauri mjirekebishe. Lakini tukizungumza hapa mnadhani wapinzani wanapiga ngonjera tu. Tuna malengo ya dhati ya kuwasaidia ili Taifa liende mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumezungumza, tulivyozungumza suala la *REA* fedha zake ambazo tunazisema narudia, tunazisema, zimechukuliwa na Wizara ya Fedha na miradi haitekelezwi. Sisi kama Bunge ambao

tumepitisha fedha hizi tunatoa tamko gani, tunafanya jambo gani ili fedha ziende kwenye Wizara? Mheshimiwa Kalemani anayesifiwa afanye mambo yake vizuri, tunapitisha mambo kama Bunge tunadharauliwa na Serikali wakati Bunge kazi yetu ni kuisimamia na kuishauri Serikali lakini Serikali inatudharau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufanye maamuzi magumu ya kufanya jambo ambalo watajua kwamba Bunge ni chombo ambacho kinaweza kuisimamia Serikali. Nikushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Chikota, ajiandae Mheshimiwa Kakoso, ajiandae Mheshimiwa Hamida Abdallah, ajiandae Mheshimiwa Gulamali na ajiandae Mheshimiwa Zacharia Issaay.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nianze kuungana na Wabunge wenzangu kumpongeza Waziri na Naibu Waziri kwa utendaji wake uliotukuka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Kalemani na Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgalu wanapaswa kuigwa na kwa sisi Wanamtwara tunawashukuru sana kwa sababu wakati tupo kwenye kipindi cha mtafaruku, wakati ile mitambo ya kufua umeme, mashine tisa zilivyopata hitilafu, hawa walikuwa wanakuja usiku na mchana na sasa hivi tunafurahi kwamba tatizo lile limekwisha. Tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee naipongeza Wizara hii na *TANESCO* kwa mambo manne makubwa waliyotufanyia sisi wana Mtwara, la kwanza kama walivyosema Wabunge kutoka Mtwara kutuunganisha Mkoa wa Lindi na Mtwara kwenye Gridi ya Taifa, hilo hatutalisahau na Mheshimiwa Kalemani na Mheshimiwa Subira mmeandikwa kwenye vitabu vya Mtwara kwamba ninyi ni akina nani kwa maendeleo ya Mtwara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni kukamilika kwa ukarabati wa ile mitambo ambayo ilipata hitilafu lakini zaidi mmetuongezea mitambo miwili mipya ambayo juzi, Jumatatu ya wiki hii Mheshimiwa Waziri Mkuu alizindua pale Mtwara, tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, ni kukamilisha kwa kile kituo cha Maumbika, kile kituo kina maana sana kwa sisi wana Mtwara na Lindi. Kwanza, kulikuwa na ujenzi wa *line* ya msongo mkubwa kilovoti 132 kutoka Mtwara hadi Maumbika, umbali wa kilometa 80; lakini pili ndiyo mahali ambapo sasa Mtwara na Lindi tunaungwa kwenye Gridi ya Taifa; lakini tatu, badala ya kutarajia njia moja kwa Wilaya zote za Kusini, Mtwara na Lindi, sasa Ruangwa, Nachingwea na maeneo mengine wana *line* ya kwao. Kwa hiyo, Mtwara ukikatika umeme, Nachingwea na Ruangwa wanaweza kupata umeme bila kutegemea *line* moja kama ilivyokuwa zamani, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la nne na la mwisho, kesho kiwanda cha Dangote kinaanza uzalishaji wa saruji kwa kutumia gesi asilia kwa maelekezo ya Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli. Lakini baada ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kuelekeza Wizara yako chini ya wewe Mheshimiwa Kalemani na Mheshimiwa Subira Mgalu mlisimamia kuhakikisha hilo linatekelezwa na kesho Kiwanda cha Dangote kinatumia nishati ya gesi asilia katika kuzalisha saruji. Hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo nina machache ya kushauri kuhusu Mradi wa *REA.* Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wanafahamu historia ya Mikoa ya Mtwara na Lindi, huko nyuma tulikuwa na kampuni moja ya *ATMAS Group* ambao walipewa kazi ya ku-*supply* umeme Mtwara na Lindi, lakini baada ya kushindwana na Serikali katika makubaliano fulani *ATMAS Group* walivunja yale makubaliano. Kwa hiyo, *REA I* na *REA II* Mikoa ya Mtwara na Lindi haikufaidika sana na tunatarajia kwamba *REA III* ndiyo tufaidike sana na mradi huu lakini kama walivyosema Wabunge wa Mtwara, kuna changamoto ya mkandarasi.

Mkandarasi bado anasuasua, vijiji ambavyo viempatiwa umeme ni vichache, mimi jimboni kwangu bado sijamuona na hajafanya chochote licha ya ile *survey* aliyoifanya ni kwa dada yangu Mheshimiwa Ghasia nasikia amewasha vijiji vitatu lakini kwa kweli kasi si ya kuridhisha. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Kalemani kwa usikivu wako basi fuatilia utendaji wa mkandarasi huyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine Mheshimiwa Kalemani nakumbuka baada ya kutoka ile orodha nilikuambia kuna changamoto katika jimbo langu. Jimbo langu huko nyuma lilikuwa sehemu ya Mtwara Vijijini kwa hiyo vijiji vingi vinavyosomwa vya Nanyamba sio vya Nanyamba ni Mtwara Vijijini na kwa usikivu wako ulisema unalifanyia kazi. Hili natarajia bado liko mezani kwako, utalifanyia kazi ili kurekebisha ile idadi ya vijiji katika Jimbo la Nanyamba na nina matumaini makubwa sana na hata wana Nanyamba wanaponiulza nitoe idadi ya vijiji sitoi, natarajia kwamba ukitoa ile *approval* ya vijiji vingine basi niwaambie kwamba vijiji vitakavyofaidika na mradi wa *REA III* ni vijiji moja, mbili, tatu.

Kwa hiyo Mheshimiwa Kalemani nakuomba sana hili ulisimamie kwa karibu na Mheshimiwa Subira ulisimamie kwa karibu nakuomba sana hili ulisimamie kwa karibu na Mheshimiwa Subira ulisimamie kwa karibu ili tupate ile orodha mpya ya vijiji ambavyo vitafaidika na *REA Phase III* kwa Jimbo la Nanyamba. Lakini nakuomba sasa Waziri uhakikishe kwamba *densification* katika Mkoa wetu wa Mtwara inaanza mapema.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Kakoso ajiandae Mheshimiwa Hamida.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru sana kunipa nafasi nipate kuchangia awali ya yote nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya kwa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Dkt. Kalemani anakumbukwa kwenye eneo la Jimbo la Mpanda Vijijini pale ambapo tulifanya ziara ya kushtukiza karibu maeneo yote tuliyotembea umeme umewaka. Nakupongeza sana, tunachokuomba Mheshimiwa Waziri umeme *REA III* upande wa Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma tulichelewa sana, hatukupata kwa sababu ya matatizo ambayo wewe Mheshimiwa Waziri unajua kulikuwa na ugomvi wa kugombania *tender* ambazo zilitufanya sisi tubaki nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba sana Mheshimiwa Waziri tupe upendeleo wa karibu sana Mikoa hii ambayo ilibaki nyuma katika utekelezaji wa Mradi wa *REA III*. Mheshimiwa Waziri vipo vijiji ambavyo havikupata mradi huu kwa muda mrefu, eneo la Mishamo tuna vijiji zaidi ya 16 ambavyo havikupata, ninaomba kwenye mradi huu wa sasa pale ambapo tutakuwa tumempata Mkandarasi tuvipe kipaumbele ili viweze kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme huo wa *REA* tunategemea kuwa utaenda kwenye eneo la Ukanda wa Ziwa Tanganyika ambako tuna vijiji vya Karema, Ikola, Kapalamsenga na vijiji ambavyo vitapitiwa kwa maana ya Kasekese, Kaseganyama, Sibwesa tunaomba sana vijiji hivi mvipatie umeme kwa wakati. Tunajua kuchelewa kupatikana kwa fedha za kuendesha mradi huu ambako tulikuwa na mkwamo wa kukosekana kwa mkandarasi, tunaomba Mheshimiwa Waziri pale ambapo tutapata fedha zipelekwe haraka zaidi ili ziweze zikatekeleze mradi huu wa *REA III*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Kigoma, Rukwa ni mikoa ambayo haina umeme wa Gridi ya Taifa tunaomba sana Waziri ufanye jitihada za makusudi kuhakikisha hii mikoa nayo inaunganishwa ipate umeme wa

uhakika. Kwani bado umeme ambao tunautegemea ni umeme ambao unatumia mafuta ambao una gharama kubwa sana. Nikuombe Mheshimiwa Waziri kwenye bajeti ya kitabu chako hatujaona kabisa kwamba kuna jitihada ambazo zimepangwa kwa ajili ya kuuweka Mkoa wa Katavi na Rukwa kwenye Gridi ya Taifa bado tunahitaji na sisi tupate umeme huu utasaidia na kukua na kuchochea uchumi wa Taifa letu hasa kwa mikoa ambayo ilisahaulika, mikoa ya pembezoni kwa maana ya Mkoa wa Rukwa, Katavi na Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tunajua wewe ni mchapa kazi, wewe ni msikivu, wewe unajali wananchi, tunaomba sana maeneo ambayo tulitembea wote kuna umeme ambao haujawafikia wananchi na wewe uliwaahidi kwamba utafika kila eneo naomba kwenye maeneo ya Kijiji cha Majalila, Kijiji cha Ifukutwa, Kijiji cha Mchakamchaka, Kabungu na kule Gerezani, Kalilankurunkuru ambako tulifika wote, nii baadhi ya maeneo tu ndiyo yamepata umeme. Kwa hiyo, eneo la vijiji tunahitaji sasa umeme uweze kusambazwa na uwafikie wananchi. Nina matumaini kwenye maeneo hayo Mheshimiwa Waziri ninayokwambia unayatambua vizuri na wananchi walikupokea kwa shangwe na furaha baada ya kufika kwako na ulishaandika historia kwenye eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba uweke kipaumbele tuweze kupata umeme na uongeze vijiji ambavyo vinahitajika ili na wao wananchi waweze kunufaika kama maeneo mengine walivyonufaika. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Hamida, wajiandae Mheshimiwa Gulamali, Mheshimiwa Issaay, Mheshimiwa Bukwimba na Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi niweze kuchangia. Lakini nianze kwa dhati kabisa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya na

nimefanya nao kazi kwa kipindi cha miezi minne nimeona kazi ambazo wanazifanya na wanakwenda kwa kasi ya Hapa Kazi Tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendelee kuwatakia kila la kheri katika bajeti hii ambayo iko mezani leo, Mwenyezi Mungu awajaalie na fedha zipatikane ili waweze kutekeleza mipango ambayo imo katika kitabu chao ambacho kipo hapa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na niishukuru Serikali kiujumla kwa kutuunganisha umeme wa gridi kwa mikoa hii miwili ya Lindi na Mtwara na Wabunge wote tumefarijika sana wa mikoa hii ya Lindi na Mtwara. Nilikuwa kule tarehe 21 siku ya uzinduzi wa umeme huu wa Gridi ya Taifa nimeshuhudia nimeona. Kwa hiyo, natoa shukrani zangu za dhati kwa Serikali kwa kuona umuhimu mkubwa sasa kuona kwamba Lindi inahitaji maendeleo na tuweze kwenda kwa kasi ya Hapa Kazi Tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tumeona kwamba umeme ndiyo mkombozi wa uchumi katika nchi yetu, lakini ni mkombozi pia wa kutengeneza ajira kwa Taifa letu. Kwa hiyo, umeme huu wa *REA* ndiyo mkombozi wa mkubwa katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu. Tumeona changamoto mbalimbali nimebahatika kutembea katika mikoa karibu tano/sita kwenda kukagua miradi hii ya *REA*.

Kwa hiyo, tunayo changamoto kubwa sana, Waheshimiwa Wabunge wameongea kwamba eneo la kijiji utakuta nyumba tatu/nne ndiyo zinapata umeme. Mimi sitoi lawama kwa Wakala wa Umeme Vijijini yawezekana mikataba ambayo wamesaini imewaelekeza kufanya hivi, lakini naishauri Serikali kufanya *review* ya kuangalia ni maeneo gani yamesahaulika ambayo yanahitaji kupelekewa huduma hii ya umeme ili kazi ya ziada iwafikie hawa mawakala wa usambazaji wa umeme ili maeneo yote yaliyosahaulika kule vijijini yaweze kuwafikia umeme na wao waweze kwenda na kasi hii ambayo tunaenda nayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 83 umezungumzia suala la Mradi wa *LNG* Mradi huu ni wa muda mrefu, kabla ya Bunge hili ulianza huu Mradi na Waheshimiwa Wabunge wote waliunga mkono na kuona sasa Tanzania tunaondoka hapa tulipo tunakwenda mbele. Kwa hiyo, ninachotaka kusema kwamba isionekane mradi huu wa *LNG* basi unaweza ukaathiri Mradi *Stiegler's Gorge* ninaomba ieleweka kwamba miradi hii yote miwili iweze kwenda ili nchi yetu iweze kufaidika na miradi hii.

Kwa hiyo, ninaiunga mkono miradi hii na kuishauri Serikali kwamba imalize mazungumzo ya mradi huu wa *LNG* ili watu waingine kazini kuendelea na mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini mradi wa *LNG*, nikiwa Diwani na Naibu Meya pale Lindi Manispaa nilishuhudia kupitisha michoro hii ya eneo ambalo mradi unaenda kujengwa na tulishapitisha tulitoa hatimiliki ya eneo hili. Kwa hiyo eneo lile wananchi wanakaa lakini si la kwao tena, kwa sababu hati tayari imekabidhiwa kwa Serikali. Nilichokuwa naomba na ninasisitiza sana wananchi hawa wapewe fidia zao kwa haraka kwa sababu ni kipindi kirefu sasa inafika miaka mitano kila bajeti inayokuja tunapitisha, bajeti tunamaliza mwaka pesa haziendi na wananchi wanaendelea kukaa pale wanashindwa kujiendeleza kimaendeleo.

Kwa hiyo, ninamuomba sana ndugu yangu Dkt. Kalemani asimamie suala la kuwapa fidia wananchi wa eneo lile ili waweze kuondoka wapishe eneo la mradi mpaka hapo Serikali itakapoamua kumaliza mazungumzo hata kama ikiwa miaka mitano/sita/kumi lakini tukiamini kwamba wananchi hawa wameondoka na wamepewa fidia zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado kuna eneo ambalo wanapishwa wahamie hawa waathirika wa eneo hili, wananchi hawanahitaji huduma za elimu, wanahitaji huduma za afya na wanahitaji huduma muhimu sana. Kwa hiyo, eneo ambalo wanahamishiwa basi Serikali ihakikishe

kwamba kunaboreshwa na kunajengwa shule, zahanati na huduma zingine muhimu kama za maji, dawa na kadhalika. Kwa hiyo, hayo ni mambo muhimu sana kwa wananchi wa Kata hii ya Mbanja eneo hili la Likong'o na wanakohamia ni pale Kijiji cha Kikwetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni vizuri Serikali…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Gulamali, ajiandae Mheshimiwa Zacharia.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi leo kuchangia katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nipende kuitumia nafasi hii kuwapongega Waziri pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani na Mheshimiwa Subira Mgalu hongereni sana kwa kazi nzuri ambazo mnazozifanya. Kwa kweli binafsi niseme kwa kupongeza huku ni kwa sababu ya kazi kubwa mnayoifanya katika kuhakikisha kwamba nchi inapata mwanga kuondokana na giza totoro ambalo lilikuwepo siku za nyuma hasa katika maeneo ya vijijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hongereni sana na mnafanya kazi nzuri na niseme tu asiyekupongeza ama asiyewapongezeni huyo tunaweza tukamuita mchawi maana yake kwa jitihada kubwa mnazozifanya kwa kweli hata kule kwangu kule katika Wilaya yetu ya Igunga tunajionea mabadiliko makubwa sana katika sekta ya umeme vijijini na niseme tu katika Wilaya ya Igunga katika kata ambazo tunazo 35, nilikuwa katika Jimbo langu la Manonga tulikuwa na Kata karibu kumi hazina umeme kabisa

na kiza totoro lakini kwa jitihada kubwa ambayo mnaifanya Wizara yenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ulikuja kule kijijini kwetu ulitembea Kata ya Mwashiku ulijionea mwenyewe na ukawaahidi wananchi wale wa Kata ile ya Mwashiku watapata umeme. Ni kweli tayari wakandarasi wako *site* na katika upatikanaji wa umeme katika Kata za Mwashiku, Ngulu, Mwashiku na Ntobo watapata umeme. Kwa hiyo, mtaondoa adha ambayo walikuwa nayo siku za nyuma na sasa hivi Mheshimiwa Waziri nikwambie tu tayari wanakijiji wa zile kata tayari wameashaanza kuwekeza katika viwanda vidogo vidogo. Wameshaanza ujenzi wa mashine za kukoboa, kusaga wameshaanza kuleta majenereta kwa ajili ya kufanya kazi za Madini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hizi ni kwa sababu umepeleka umeme katika yale maeneo, na ninaamini baada ya zile kata kuna kata ambazo zimebakia za Igoweko, Uswaya, Tambalale, Mwamala, Ugaka pamoja na Kitangiri watapata na wao umeme kama ambavyo Kata zingine ambazo zinapata sasa hivi. Kwa kweli Mheshimiwa Waziri nakupongeza sana kwa kazi kubwa mnayoifanya. Lakini usambazaji huu wa umeme mnaousambaza mahitaji ya *megawatt* yanaitajika sana na ndiyo ili kuja kuondoa tatizo la umeme siku za usoni mmekuja na mradi mkubwa wa *Stiegler's Gorge* ambao utazalisha umeme karibu megawati 2100. Mheshimiwa Waziri mradi huu ni muhimu sana kwa Taifa letu na binafsi naunga mkono hoja Mradi huu utekelezwe na sizani kama kuna mtu ambaye anaupinga na hasa katika utekelezaji wake Mheshimiwa wamezungumzia juu *environmental assessment its okay*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini Mheshimiwa Waziri katika hekta 54,000 tunaenda kuchukua hekta 1400 *it means* tuna zaidi ya hekta 52,400 zinazobaki. Kwa hiyo, hata kama ni mazingira bado haya mazingira yatabaki salama na niombe tu mradi huu uende haraka kwa sababu mahitaji ya umeme kwa sasa hivi ni makubwa sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuongezea tu Mheshimiwa watu wengi sana wanazungumzia juu ya upatikanaji wa umeme na tayari tumeshakuwa na *hydro* ambayo tunaenda kuitekeleza hivi karibuni na mpaka ukamilishaji wake tutakuwa tunapata zaidi ya megawati 5000 mpaka kufikia mwaka 2020 kutokana na utekelezaji ambao mnawekeza. Mheshimiwa Waziri katika kupata umeme huu tunaoupata katika maeneo mbalimbali na tumezungumzia hasa katika ukurasa wako nilikuwa naangalia hapa ukurasa wa 72 na 73 pia umegusia juu ya upatikanaji wa umeme, mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri natambua juhudi zako katika kuhakikisha kwamba unaboresha huduma hii katika nchi yetu. Nikuombe sasa Mheshimiwa Waziri kuna makampuni umeyataja hapa katika ukurasa huu wa 73 ambayo yanawekeza katika utafutaji wa mafuta na gesi. Nikuombe katika haya Makampuni yapo makampuni pia yanahitaji yapate *extension* kwa ajili ya ufanyaji kazi wake ili yawe na uhakika wa uwekezaji, kwa mfano yapo makampuni yanataka kuwekeza katika utafutaji wa gesi karibu zaidi ya dola 250, dola zote hizi mtu hawezi kuwekeza kama hana *assurance* ya kufanya kazi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu natambua Mheshimiwa Waziri wewe ni msikivu sana na ninaamini katika utendaji kazi wako nakuomba sasa hebu kuwa karibu pia na hawa wawekezaji wakubwa wanaowekeza katika gesi ili kurahisisha hii kazi ambayo kila mmoja anazungumzia mradi wa gesi. Naamini ukiwa nao karibu hawa wawekezaji, gesi ikizalishwa maana yake itapunguza hiyo adha kubwa ambayo tuliyonayo lakini itasaidia nchi yetu kupiga hatua kutoka tulipo sasa na kwenda sehemu nyingine zaidi ya mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri suala la gesi ni suala la muhimu sana katika Taifa letu nikuombe ulitilie mkazo wa kipekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache Mheshimiwa Waziri nakuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako mzuri. Mheshimiwa Zacharia, wajiandae Mheshimiwa Lolesia, Mheshimiwa Lusinde na Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na kabla sijachangia naomba hata kama siyo muda wake niseme kwamba yule Waziri aliyenijibu hakunitendea vyema. Hakuna vitabu vya darasa la Nne kule Halmashauri ya Mji wa Mbulu, ninaomba Serikali ipeleke kwa kuwa wale watoto baadae wataenda kufanya mtihani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miongozo tunayoomba hapa yana sababu zake lakini na maswali tunayojibiwa na Mawaziri ni vizuri wao wangesema tujiridhishe kama Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niseme tu kwamba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuwepo kwetu hapa Bungeni kwa muda wote, Mwenyezi Mungu ameendelea kutukrimu na kutulinda. Lakini pia nichukue nafasi kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano, imefanya kazi kubwa sana, hasa upande wa Wizara hii ya Nishati na Madini na hasa Nishati kwa nchi nzima. Yapo maeneo hayakutarajiwa kupata umeme hata kule Mbulu kwenye Jimbo letu na hata Wilaya ya Mbulu, hivi sasa walau kuna muelekeo wa kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mambo machache la pili, jambo lingine ambalo napenda kuishauri Serikali ni kwamba nipongeze Wizara, Waziri na timu yake wamefanya ziara mara mbili wamekuja Mbulu, wameona hali halisi wajitahidi kuona ni namna gani mapungufu yale ya *REA* ya Awamu ya Kwanza na Awamu ya Pili umeme ulikuwa umepelekwa kwenye kaya kama 10/20 ukaendelea pengine kitongoji kimoja tu. Kwa hiyo, kwenye mpango ule wa maboresho wa usambazaji wa umeme vijijini ninaomba sana Serikali ifanye tathmini upya na iweze kufanya marejeo. Hivi

sasa Waziri ameenda amesema tutapeleka umeme kila kijiji na kila nyumba, lakini hali hii inaweza kuwa mwiba wa mchongoma kwa wachaguliwa kwa sababu uchaguzi uko usoni na umeme usipoenda wananchi wataona kama vile hatujawatendea haki na kutekeleza kile ambacho Serikali inakusudia juu yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine tunapiga kelele sana humu Bungeni kuhusu fedha hizi za *REA* jinsi ambavyo hawapati pesa, juzi tulikuwa tunamuuliza mkandarasi ambaye Waziri alikuja akazindua umeme tukamwambia mbona umekaa kimya hujaendelea tena baada ya Waziri kuondoka akasema nasubiri hela. Nilikuwa nafikiri tuone utaratibu wa namna gani fedha tunapeleka kwa wakati na kadri ambavyo inaombwa kwenye bajeti. Tutapiga kelele kwa Waziri lakini kama fedha hazitaenda basi Waziri atakuwa anagombana na sisi, lakini sababu zenyewe hazitoshi za mkanganyiko wa sisi kugombana na kubishana. Nilikuwa nafikiri kama itawezekana Serikali itoe fedha zile za kwenye bajeti na kama itashindikana iangalie vipaumbele vingine au vyanzo vingine ambavyo vitatusaidia kupata fedha zaidi ili mradi huu ambao ni chachu kwa watanzania upate kufanikiwa na tuweze kupata umeme kwenye vijiji na kwenye mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kama ulivyokuja Mbulu ulikwenda kuzindua umeme chini ya kilometa moja kutoka katikati ya mji, maana yake ni kwamba tuna vijiji kama 34 havina umeme na orodha unayo. Tunaomba basi wewe kwa niaba yako wewe na Wizara na watendaji, nia yenu ile njema ya kuja Mbulu na kuzungumza vizuri na wananchi wa Mbulu ipate kutekelezwa ili wananchi wale wapate ahadi yako na waweze kupelekewa umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla kuna athari zinatokea katika utekelezaji wa mradi huu wa *REA* Awamu ya Kwanza, Awamu ya Pili na Awamu ya Tatu katika maeneo ambayo mradi unatekelezwa zaidi kwenye rasilimali za wananchi ikiwemo mashamba ya miti, mashamba ya mazao.

Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba kama itawezekana kufanyike vikao vya majadiliano wale mameneja wa kwenye Wilaya watumie lugha nzuri, ya kwamba huu mradi ni wa kitaifa hauna fidia lakini pale ambapo kuna athari kubwa yule mlengwa anakutwa na hiyo athari basi tuone ni namna gani tunakaa naye mezani ili tuone na yeye asiathirike kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni kwamba, ulikuja Mheshimiwa Waziri kule Mbulu, ukaja na chombo cha umeme kitakachoweza kutoa umeme kwenye baadhi ya kaya, wananchi sasa wanataka kile chombo kwa wingi na tumeingia kwenye mgogoro. Mimi nadhani kama *Mobisol* walishapeleka umeme kwenye baadhi ya majengo wakawa wanawa-*charge* wananchi wetu, Serikali ione umuhimu sasa wa kutafuta kile chombo kwa yale majengo/makazi ambayo yako mbali na *line* kubwa na yana gharama kubwa ni vizuri tukapeleka kile chombo tukatafuta utaratibu wa wale wananchi kulipia hata kwa gharama ile ya bili, lakini kwa kiwango cha kuendana na mahitaji yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayasema haya kwa sababu, hata kile chombo kikipelekwa wananchi wengi vijijini asilimia kubwa wao hawahitaji umeme wa friji, hawahitaji umeme wa *tv,* hawahitaji umeme wa pasi, wanahitaji mwanga, ku-*charge* simu na mambo mengine madogo madogo. Kwa hiyo, tukipeleka kile chombo...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji )*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri, muda wako umekwisha, unajua ukichangia vizuri muda unakwenda sana. Mheshimiwa Lolesia, ajiandae Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Nishati. Kwanza nianze kwa kumpongeza

Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya katika Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati ni Wizara muhimu sana na ni nyeti kwa ajili ya uchumi wa Taifa. Kwa hiyo, niombe Serikali iwekeze fedha nyingi kwenye Wizara hii kwa sababu ni kwa kipindi kirefu mpango wa Serikali wa miaka mitano kuhakikisha kwamba kila kijiji katika Taifa la Tanzania kinafikiwa na umeme. Sasa haiwezekani kuweza kufikia vijiji vyote kama tusipopeleka fedha ya kutosha kwenye Wizara hii ili kuwezesha basi utekelezaji wa upelekaji wa umeme vijijini. Kwa sababu katika Mkoa wetu wa Geita tangu walipozindua umeme mwaka jana mpaka sasa ni kijiji kimoja tu cha Izunya ndicho ambacho kimepata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzinduzi ulifanyika katika Wilaya ya Nyang'hwale, lakini katika Wilaya ya Nyang'hwale tumewasha kijiji kimoja cha Izunya, Wilaya nyingine za Geita, Mbogwe na sehemu nyingine zote hata Chato bado umeme huu haujaweza kuwashwa. Kwa hiyo, naomba Serikali sasa iwekeze fedha nyingi za kutosha kwenye *REA* ili utekelezaji wa umeme huu *REA* Awamu ya Tatu uweze kuwafikia wananchi, hasa waishio vijijini. Ninasema hivyo, mimi tu kwenye Jimbo langu kati ya vijiji 84 vijiji Tisa tu ndiyo vimefikiwa na umeme, vijiji 74 bado mpaka sasa havijapata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa sababu niliendа kumtembelea ofisini nikaomba kwamba awamu ya kwanza ya kupelekewa vijiji, vinapelekewa vijiji 12 tu ni vichache mno kati ya vijiji 74. Kwa hiyo, niombe basi vile vijiji 30 nilivyoomba viongezeke kwenye ile awamu ya kwanza, ninaomba suala hili Mheshimiwa Waziri mlizingatie, ili wananchi hasa kwenye kata ambazo zilikuwa hazijafikiwa kabisa na umeme ziweze kupatiwa umeme huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika Mkoa wa Geita tuna miradi ya umeme ya kupeleka mradi wa njia za umeme

ambazo ni kutoka Bulyanhulu mpaka Geita na vijiji nane vitaweza kufikiwa na umeme kupitia mradi huo. Niombe pia, utekelezaji wa mradi huu uweze kuanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kuna mradi wa kusafirisha umeme kilovoti 220 kutoka Geita kuelekea Nyakanazi ambapo vijiji 32 pia vya Mkoa wa Geita, vitaweza kupatiwa umeme. Naomba pia utekelezaji wa mradi huu uweze kuanza mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapenda kuipongeza pia Serikali kwa mradi mkubwa wa umeme wa Rufiji ambao utawezesha kuweza kupata kilovoti 2100 na umeme huu utaweza kuongeza kwenye changamoto ya umeme iliyokuwepo kwa muda mrefu. Sehemu nyingi tulikuwa hatupati umeme wa uhakika, lakini mradi huu wa Rufiji ukikamilika tuna imani tutaweza kuongeza uwezo wa kufikiwa na umeme watu wengi zaidi katika nchi ya Tanzania na hatimaye tutaweza kufikia uwezo wa kuweza kufikia malengo ya Awamu ya Tano ya viwanda kwa sababu bila ya umeme hatuwezi kuanzisha viwanda.

Kwa hiyo, niombe Serikali iwekeze sasa kwenye mradi huo, tena ninashukuru kwamba, inawekeza mradi huu kupitia fedha za ndani, kwa hiyo, tuna uhakika kabisa mradi huu utaweza kutekelezeka kwa sababu tunatekeleza kwa kupitia fedha za ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaomba Wizara iweze kuangalia uwezekano wa kuleta nishati mbadala kwa sababu, kwa sasa hivi wananchi walio wengi, hasa vijijini, wanatumia mkaa na kuni, mazingira yanaangamia. Tukiangalia maeneo mengi, hata ukitokea tu hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam njiani siku za nyuma kulikuwa na miti ya kutosha, lakini sasa hivi mazingira yanaharibika kila siku.

Kwa hiyo, niombe Wizara iweze kuweka mpango mkakati maalum kuweza kupeleka nishati mbadala vijijini ili tuweze kupunguza utuamiaji wa miti kwa sababu miti mingi inatumika kuchoma mikaa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Lusinde, wajiandae Mheshimiwa Rashid Abdallah Shangazi, Mheshimiwa Goodluck Mlinga na Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nimshukuru Mungu sana kwa ajili ya kutupa zawadi ya uhai ili tuweze kuchangia Wizara hii.

Kwanza na mimi niungane na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Waziri Mheshimiwa Dkt. Medard Matongolo Chanancha Kalemani, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Subira Mgalu, Katibu Mkuu Ndugu Khamis Mwinyimvua na timu nzima ya watu wanaowasaidia katika Wizara hiyo kufanya kazi pamoja na *DG* wa *REA* kwa kweli wanafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mambo ambayo Wabunge tuna kazi ya kuishauri Serikali, ili Serikali ikiyafanyia kazi kulingana na ushauri tunaoutoa maendeleo katika vijiji vyetu, wale Wabunge wa vijijini na wale wa mijini kwa kweli yatakuwa ya haraka na shirikishi. Mheshimiwa Waziri umekuwa ukisema mara nyingi vizuri sana sina hakika kwamba, Makandarasi pamoja na watendaji wako wanakusikiliza na kukuelewa. Kwa mfano, suala la umeme shirikishi umelisema sana, lakini ukienda *site* kuna baadhi wanafuata shirikishi kuna baadhi hawafuati. Sasa sielewi wale ambao hawafuati wanapokea maelekezo kwa nani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme shirikishi maana yake Mwenyekiti wa Kijiji, Diwani wa eneo lile, Mbunge wa Jimbo lile washirikishwe kushauri uanzie wapi uishie wapi maana wao ndiyo wakazi wa maeneo yale. Wakati mwingine mnaruka *centre* ya kijiji kikubwa wanakwenda kwenye kitongoji ndani, huku pembeni wanaacha malalamimko makubwa kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tulikuwa tunataka tushauri Mheshimiwa Waziri, unaposema umeme shirikishi basi fuatilia na kule nyuma ambao wanakiuka agizo lako, maana

wewe unaagiza hiki wengine wanafanya kinyume na unavyoagiza wewe. Wakiambiwa na Wenyeviti wa Vijiji wanasema acheni siasa, wakiambiwa na Madiwani wanasema acheni siasa, aah! sasa siasa ni ipi na utendaji ni upi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilifikiri Mheshimiwa Waziri utusaidie, kwa mfano, umefika wewe mwenyewe Kijiji cha Muungano katika Kata ya Muungano, ukasema umeme utakwenda kijiji kwa kijiji, klitongoji kwa kitongoji, lakini kuna vitongoji kibao vinaachwa. Ukija makandarasi wako wanasema wao wamepewa kilometa kumi, sasa kilometa kumi ndiyo mtagua vitongoji vyote, haiwezekani! Pengine mtoe maelekezo mapya kwamba, umeme usiende kitongoji kwa kitongoji uishie kilometa 10. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine Mheshimiwa Waziri tunaomba ufafanuzi, hebu tupe tofauti ya umeme wa *REA* na umeme wa *backbone.* Maana *backbone* wanasema wana nguzo 80 kila kijiji, kwa hiyo, kuna maeneo mengi hawafanyi, ukiwauliza wanasema huu siyo wa *REA,* sasa tofauti ipi? Hebu Waziri tuambie kwamba, pale utakapowekwa wa *backbone* baadae itakuja *REA* kumalizia au ndiyo biashara itakuwa imekwisha ili wananchi wetu wajue. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine Mheshimiwa Waziri, vipaumbele vinapangwa na wenyewe wenye kata yao, Madiwani, vinapangwa na Wenyeviti. Kwa hiyo, msipowashirikisha mkaanza tu mkandarasi anafanya anavyotaka yeye kutakuwa na matatizo ya kurukwa maeneo mengi sana ambayo ni makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri tumekupongeza sana kwa kusambaza umeme, lakini iwezesheni *TANESCO,* Kitengo chao cha *Emergency* kiwe na uwezo, kwa sababu leo mvua ikinyesha zinaanguka nguzo nyingi, *TANESCO* hawana uwezo wa kuzifikia, wanakijiji pale wanakosa umeme karibu wiki mbili mpaka tatu, inakuwa

haiwezekani! Wapeni uwezo mkubwa wa kutatua matatizo yanapojitokeza. Maana tunapokuwa na umeme katika kila kijiji maana yake na Kitengo cha *Emergency* cha *TANESCO* lazima kiwe na uwezo mkubwa wa kushughulikia matatizo yanapotokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nikushauri sana na niombe kwa ajili ya Jimbo langu, tumeomba umeme Tarafa ya Mpwayungu, tarafa nzima haina umeme na pale Serikali imetupatia pesa tunajenga kituo kikubwa cha afya pale, kile kituo usipofika umeme itakuwa haina maana yoyote. Maana kituo kikubwa, Serikali imetupa shilingi milioni 700, lakini umeme bado hakuna hata programu lini utafika pale Mpwayungu. Tunaomba sana katika Kata za Manda, Ilangali, Kijiji kizima cha Ilangali hakuna nyumba hata moja ya tembe, wanakijiji wamehamasika wamejenga nyumba za bati kijiji kizima kama mfano, lakini umeme hakuna hata programu kwamba utafika lini kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Kata ya Huzi, nimetaja Manda, Ndogoe, hayo ni maeneo ambayo tunataka myakumbuke. Vijiji kama kama Nagulo na Mwitikila pale panahitajika umeme ufik. Kwa hiyo, nakuomba sana Mheshimiwa Waziri wakati utakapokuwa ukitoa majibu utuambie Tarafa ya Mpwayungu lini itapatiwa umeme? Lakini je, mmebadilisha sera ya kupeleka kitongoji kwa kitongoji sasa tunapeleka makao makuu tu ya kijiji, *centre?* Ili tujue wananchi wetu tuweze kuwajibu jamani yale maneno anayosema Waziri ya kijiji kwa kijiji, kaya kwa kaya, nyumba kwa nyumba, hayapo tena bali itakuwa ni *centre* tu ya kijiji, wananchi wakielewa hivyo, sisi itakuwa imetusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo lingine ambalo nataka nishauri, Waziri unafanya kazi vizuri, Naibu Waziri anafanya kazi vizuri, *REA* wanafanya kazi vizuri, lakini tuiombe Wizara ya Fedha mtoe fedha. Hii nchi kila siku mnatuambia inakopesheka, kama inakopesheka basi kopeni kwa mambo makubwa kama haya ili tuweze kumaliza kwa sababu tukiwa na umeme wa viwanda deni hilo tutalipa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya, hivi ndio vitu vya msingi kabisa vya kukopea pesa, ili tuweze kumaliza hili zoezi tuende kwenye mambo mangine. Kwa hiyo, nakuombeni sana, namuona yuko dada yangu hapa Naibu Waziri wa Fedha, tusikilize Waheshimiwa Wabunge toeni fedha kwa hii Wizara ili iweze kufanya kazi, vinginevyo tutambana hapa bure Dkt. Kalemani. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Shangazi wajiandae Mheshimiwa Frank na Mheshimiwa Mkundi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuchangia katika hoja iliyoko mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze Mawaziri wa Wizara hii pamoja na timu nzima ya Wizara ya Nishati kwa namna ambavyo wanatenda kazi. Tumemuona Waziri anakimbia, lakini pia hakumuacha nyuma Naibu wake Waziri kila mahali wapo, japo wana deni kwamba bado hawajafika Lushoto, lakini naamini baada ya Bunge hili wataweza kufika Lushoto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze na suala la *REA* na nitaanzia katika Wizara ya Fedha ambayo ndio inayosababisha matatizo yote haya ambayo tunakumbana nayo. Bunge limeshaazimia na tukaweka pesa maalum kabisa na tukaiwekea zuio kwamba iende kusambaza umeme vijijini, lakini pesa hizi haziendi vile inavyopaswa. Mimi nilizungumza na watu wa *REA* wametuhakikishia kwamba kama Serikali ingekuwa inatoa pesa kwa wakati na pesa kama inavyotakiwa siyo kwamba *REA* itakamilika 2020/2021, lakini walikuwa na uwezo wa kuikamilisha 2019/2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nitoe rai sana Wizara ya Fedha iachie mafungu kwenda kwenye miradi hii ya *REA,* makandarasi wapo wengi wa kutosha na makandarasi wengi wana uwezo, lakini tatizo ni kwamba hawana fedha. *Letter of Credit (LC)* hizi ambazo zimefunguliwa miezi tisa iliyopita zimekuja kuachiwa juzi kwa

hiyo, utaona kwamba ni shinikizo la bajeti ndio wamekuja kusaini *LC.* Kwa hiyo, tuombe sana Wizara ya Fedha iwe *serious* katika jambo hili, ili kufika mwaka 2020/2021 huu mradi wa *REA* uwe umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri nimekwambia mara nyingi kuhusu mkandarasi ambaye anahudumia Mkoa wa Tanga kwamba pamoja na matatizo haya ya *LC* lakini utendaji kazi wake bado haujaturidhisha sana. Anachagua baadhi ya maeneo hasa katika Wilaya hizi za tambarare, kule milimani mpaka sasa hivi ninavyozungumza hapa hakuna hata nguzo moja ambayo wameshaikita na tunakaribia kuingia kwenye *round* ya pili ya *REA* Awamu ya Tatu, Awamu ya Kwanza bado hata nguzo moja hajasimikwa.

Kwa hiyo, nikuombe sana ulisimamie jambo hili na hadi hivi ninavyozungumza hapa nina kata nne ambazo hakuna hata kijiji chenye umeme. Kata ya Shagayu ina vijiji vinne hakuna hata kijiji kimoja chenye umeme, Kata ya Mbaramo vijiji sita hakuna hata kijiji kimoja chenye umeme, Kata ya Hemtoye vijiji sita hakuna hata kijiji chenye umeme na hali kadhalika katika Kata ya Mbaru vijiji vinne hakuna hata kijiji kimoja chenye umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kuhusu suala la *densification* bado maeneo mengi hayajaunganishwa. Niombe sana kwamba mkandarasi huyu asimamiwe, pamoja na kwamba tunawatetea waweze kupewa mafungu, lakini naomba sasa jitihada za makusudi zifanyike na ninyi Wizara mtembelee Wilaya ya Lushoto. Tumeona mara nyingi mnaishia Tanga Mjini hamfiki katika maeneo ya pembezoni, tuna Wilaya ya Mkinga, Wilaya ya Kilindi, tuna Wilaya ya Lushoto na Korogwe zote hizi zinaunda Mkoa wa Tanga. Kwa bahati mbaya sana mimi ninapakana na Mwenyekiti wa Kamati ambayo inaongoza Wizara yako, Mheshimiwa Dunstan Kitandula na yeye hali iko hivyo hivyo. Kwamba na yeye vijiji vyake vingi bado havijafikiwa na *REA* Awamu hii ya Tatu. Kwa hiyo, chonde chonde ninakuomba sana hili liweze kutimia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchangia kidogo katika eneo hili la mradi wa uzalishaji umeme pale katika maporomoko ya *Stieglers'.* Kwamba jambo hili Waheshimiwa Wabunge niwashauri sana kwamba, hakuna mradi mkubwa wowote kama huu ambao umepita salama katika nchi yetu, hata tulivyokuwa na Mradi wa Kihansi kulikuwa na upinzani mkubwa. Tulikuwa tunaambiwa kwamba vyura hawa ni wa kipekee duniani wanaozaa ambao siyo wa kutaga mayai watapotea, lakini tulitumia busara na maandiko makubwa yaliandikwa, vyura wale waliahamishwa baada ya zoezi kukamilika walirudishwa na maisha yanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hata katika hili suala la *environmental impact assessment* ni muhimu lifanyike na ninaamini linafanyika vizuri, lakini mradi huu unapigwa vita kwa sababu kadha wa kadha na sababu mojawapo ni kwamba tutakapokamilisha mradi huu tutakuwa na uwezo mkubwa wa kuzalisha umeme kupitia nishati ya maji. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kw amuda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Frank Mwakajoka wajiandae Mheshimiwa Joseph Mkundi na Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na mimi kwa kupata nafasi hii niweze kuchangia. Ninaomba wakati Mheshimiwa Waziri anakuja kuzungumza hasa Waziri wa Fedha kwa sababu Wizara zote ambazo zimewasilisha bajeti hapa tumeona kila sehemu Wizara ya Fedha haitoi fedha kwenye Wizara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti ya mwaka 2017/2018 fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya kuhakikisha kwamba, umeme wa *REA* unapatikana ilikuwa

karibu shilingi milioni 938, lakini fedha iliyotoka ni karibu shilingi milioni 228.6 ambayo ni asilimia 39 tu. Tunaomba sana, tunakaa humu Bungeni nia na madhumuni ni kuhakikisha kwamba, tunachotenga lazima kiende kikafanye kazi, lakini fedha hazipelekwi na hakuna kazi yoyote inayoenda kufanyika pale. Kila siku tutakuwa tunakuja hapa tunakaa tunapanga bajeti halafu hakuna kinachoendelea, itakuwa haina maana kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tumetekeleza miradi ya maendeleo kwa asilimia 39 tafsiri yake ni kwamba bajeti hii tunayokaa ya mwaka 2018/2019 tunakwenda kutekeleza miradi ile ile ambayo tulikuwa tumepanga katika bajeti iliyopita. Sasa huu siyo mfumo mzuri wa kibajeti ni lazima tunapotengeneza bajeti ni lazima tukatekeleze kile ambacho tumekipanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi haisongi mbele inarudi nyuma, hilo lazima lieleweke namna hiyo. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpango, Waziri wa Fedha pamoja na Wizara yake kwa kweli wanalirudisha nyuma Taifa hili na ndiyo maana hata kwenye bajeti iliyopita nilisema kuna tatizo kwenye Wizara ya Fedha kwa sababu hawaoni umuhimu wa kupeleka fedha kwenye miradi ambayo inakuwa imeshapangwa kwa kipindi hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo jambo lingine ambalo ni lazima tulitazame sana kama nchi. Taifa hili sasa hivi idadi ya wananchi ni karibu milioni 54, lakini huwezi kuamini wananchi ambao, tuseme kaya ambazo zinapata umeme sasa hivi hazizidi kaya 2,700,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado tuko nyuma sana ni lazima Serikali ihakikishe kwamba, inapanga fedha za kutosha na kuhakikisha kwamba, fedha hizo zinakwenda na zinatekeleza miradi. Hiki kiwango ambacho tunacho sasa hivi cha kaya za watumia umeme katika nchi hii kwa kweli tuko nyuma sana na hata wakati unafikiria kwamba nchi itakuwa ni ya viwanda inawezekana tunafikiria jambo ambalo hatuwezi kulitekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni lazima tuangalie kwanza wananchi wetu wanapata umeme kiasi gani halafu ndiyo tutakwenda kwenye hicho ambacho tunakifiria zaidi. Kama hata wananchi wanashindwa kupata umeme leo tunafikiria kwamba nchi hii itakuwa ni ya viwanda, ndugu zangu itakuwa ni mambo ambayo hayatawezekana kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa *REA* ulikuwa ni mkombozi sana kwa wananchi wa vijijini. Lakini umeme huu mpaka sasa hivi, mwaka 2014 wakati tunaanza Awamu ya Kwanza mpaka Awamu ya Tatu tulitegemea kupeleka umeme kwenye vijiji 12,268 lakini mpaka leo tumepeleka umeme kwenye vijiji 4,730 tu. Tafsiri yake ni kwamba malengo ya mwaka 2021 yatafika wakati bado hatujafika malengo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo tunazungumza, tunapanga na tunashangilia ndani ya Bunge humu kwamba Serikali inatekeleza vizuri Ilani yake ya Uchaguzi na inatekeleza miradi mbalimbali lakini ni *zero* kabisa katika utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lazima Serikali sasa ihakikishe kwamba inatenga fedha za kutosha kuhakikisha kwamba miradi hii inakwenda kutekelezwa kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Umeme wa *REA* pia tunaona gharama ni kubwa sana kwa wananchi. Kodi kwa wananchi angalia umeme ambavyo ukinunua umeme wa shilingi 30,000 leo hii unalipa kodi mbalimbali; unalipa *REA* shilingi 737.71, lakini *EWURA* unalipa 245.9 na *VAT* unalipa 4,426.22. Ukijaribu kuangalia unaona kabisa kuna shilingi 5,490.80 unalipa kodi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mkundi, ajiandae Mheshimiwa Goodluck Mlinga.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haraka haraka nianze na suala la *REA. REA* Awamu ya Kwanza na *REA* Awamu ya Pili hazikufanya vizuri sana na matarajio yetu kama wawakilishi na wananchi kwa ujumla ilikuwani *REA* Awamu ya Tatu kwamba itakidhi mahitaji ya nishati ya umeme. Mradi huu wa *REA* Awamu wa Tatu umekuwa unasuasua sana na hasa kwa sababu ya kutokutolewa kwa pesa na wakandarasi maeneo mengi wamesimama na shughuli zimekwama kwa maana hiyo yale matarajio ya wananchi yanakuwa yanapotea.

Kwa hiyo ninaishauri tu Serikali kwa maeneo kama matatu, kwanza niombe Wizara inayohusika itoe fedha ili mradi huu wa *REA* Awamu ya Tatu uweze kukamilika na wananchi wengi waweze kupata nishati hii ya umeme. Kwa sababu nishati hii ya umeme kwa umuhimu wake kama itasambaa kwenye maeneo yote hasa vijijini hata matumizi ya mkaa na kuni ambayo yamekuwa yanaharibu mazingira yatapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa utekelezaji wa *REA* Awamu ya Tatu niombe Wizara, ushirikishwaji liwe jambo la muhimu sana kwa sababu kwenye awamu zilizopita kumekuwa na ushirikishwaji mdogo sana kiasi ambacho kimekuwa kinasababisha maeneo mengi sana umeme unafika lakini kwenye maeneo machache. Kama viongozi wa maeneo husika watashirikishwa basi wataweza kutambua ni maeneo yepi ambayo yanapaswa kupelekewa umeme badala ya mfumo unaotumika sasa ambapo umeme unaenda kwenye makao makuu ya vijiji lakini kwenye vitongoji, nishati hii ya umeme haifiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwenye usambazaji wa umeme kwenye maeneo ambayo yako *off* gridi kwa mfano kwenye maeneo ya visiwani kama ilivyo kwenye Jimbo la Ukerewe, kuna maeneo ambayo tayari wakandarasi wameanza kupeleka umeme lakini wameshindwa kuendelea

kusambaza umeme. Kwenye visiwa kama vya Ukara, *I mean* Bulubi na Ghana tayari walianza kusimika nguzo lakini wakasimama ghafla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe Wizara sasa wakati wa kujibu utueleze nini hasa kilichopelekea wakandarasi hawa wakashindwa kuendelea. Lakini kwenye kisiwa cha Ukara watoaji umeme wanasambaza umeme, lakini gharama ya umeme ule ni kubwa sana. Wananchi wananunua umeme *unit* moja kwa shilingi 2,500 mpaka shilingi 3,000 na *unit* ile inatumika kwa siku moja inakuwa imeisha, kwa wananchi wa kawaida hawawezi kuhimili jambo hili. Nilikuomba Mheshimiwa Waziri uweze kutembelea kwenye visiwa hivi tuweze kuona namna gani tunaweza ku-*solve* suala hili. Nitashukuru sana kama hili litatekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni juu ya uzalishaji wa umeme kwenye nchi yetu. Kumekuwa na *notion* kwamba kuna watu wanapinga mradi wa *Stiegler's Gorge*. Mradi huu hatuupingi kimsingi. Kama alivyosema mchangiaji mmoja hoja ya msingi ni Serikali tu kuelimisha nini athari za mradi huu, yaani watu wanahofu tu, lakini wajibu wa Serikali ni kuondoa hofu kwa wananchi ili tuweze kujua hasa nini kinachoendelea kwenye mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati ambapo tunakuwa tunatumia nguvu kwenye miradi hii vilevile tuangalie njia mbadala za kuzalisha nishati ya umeme. Kwa utafiti uliofanywa na Benki ya Dunia imeonekana Tanzania ni moja kati ya maeneo ambayo yana nguvu kubwa ya upepo na yanaweza yakazalisha umeme mkubwa sana kuliko hata ambavyo tunazalisha sasa kwa kutumia maji. Kwa mujibu wa utafiti huo, nchi kama Spain mpaka mwaka 2015 walikuwa wana uwezo wa kuzalisha megawati 23,000. Kwa mujibu wa utafiti huo Tanzania ina uwezo wa kushalisha umeme mkubwa zaidi kuliko hata Spain. Sasa ni kwa nini basi kama Taifa tusiwekeze kwenye mradi huu tukazalisha umeme kwa kutumia upepo badala ya kutumia nguvu kubwa sana kwenye maeneo mengine na kuzalisha

megawati chache chache wakati ambapo tungewekeza kwenye eneo moja kama hili la umeme wa upepo tukatoa umeme mkubwa sana tukaweza kukidhi mahitaji ya umeme kama ambavyo utafiti wa Benki ya Dunia umeweza kuonesha. Kwa kutumia njia hii tunaweza hata kukabiliana na matatizo tunayoyapata ya uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niombe sana Serikali pamoja na nia njema ya kuongeza nishati ya umeme kwenye Taifa letu, tuangalie njia mbadala nyingine kama hii niliyoisema ambayo itatusaidia kukidhi mahitaji ya umeme kwenye Taifa letu, kukabiliana na uharibifu wa mazingira kama ambavyo tumekuwa tunasema juu ya *Stiegler's Gorge* ule ukataji wa miti kimsingi utakuwa na athari zake.

Niombe vilevile kama alivyosema mchangiaji wa mwanzo, Serikali itutoe tu hofu iwe wazi kama kuna utafiti umefanyika *fine*, lakini sasa taarifa zake ni zipi ili tuweze kujua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mlinga, wajiandae Mheshimiwa Atupele Mwakibete na Mheshimiwa Deo Sanga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza naomba nimpongeze Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, kwa kweli tumtendee haki yake. Tatizo alilonalo tu ni moja upatikanaji wa pesa kwake umekuwa shida sana na miradi mingi ya *REA* imechelewa kwa ajili ya upatikanaji wa pesa. Kwa mfano, Mkoa wa Morogoro mkandarasi mpaka leo hii bado hajaanza kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili naomba niendeleze kwa mchangiaji aliyemaliza kuchangia, lakini mimi naomba nipingane naye. Kidunia na kitakwimu chanzo kikubwa cha umeme ambacho kinachoongoza kwa asilimia kubwa ni makaa ya mawe; ya pili ni gesi na ya tatu ni maji. Kwa nini maji imeshika nafasi ya tatu kwa sababu nchi nyingi

hasa za Ulaya hawana mito ya kutosheleza ya uzalishaji wa maji. Kwa kuwa kipindi kingi sana cha mwaka mito ile inakuwa ni barafu kwa hiyo wanashindwa kuzalisha umeme kwa ajili ya barafu. Kingine nchi nyingi kutokana na maendeleo ya viwanda ile mito imeharibika, kwa hiyo wanashindwa kuzalisha umeme kwa njia ya maji. Siyo kwamba hawapendi, hawana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwape kwa asilimia tu, nchi ya China wanazalisha umeme wa maji kwa asilimia 18, Marekani asilimia sita, Japan asilimia tano, Russia asilimia 16, India 20, Ufaransa asilimia 14 na Brazil asilimia 11; siyo kwamba hawapendi, hawana. Na kwa nini maji, maji kwanza yanapatikana kwa urahisi, kingine hayaharibu mazingira kama mnavyosema hakuna *air pollution,* hamna nini, gharama zake ni nafuu *low operating cost,* kwa hiyo msituchanganye, biashara ya umeme ni ya mataifa makubwa. Kama ninyi wanawahonga sisi hawawezi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe tahadhari kwenye mradi wa *Stiegler's* wengi wanaongea lakini hawajui nini kilichomo ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bonde la Mto Kilombero ambalo ndiyo maji yale yanapita, wakazi wanaondolewa mle wanazidi 100,000; mifugo inayoondolewa inazidi 250,000. Tahadhari yangu sasa ambayo napenda kuipa Serikali yangu, wale watu tunaowaondoa kwenye lile bonde sasa hivi wanaondoka kwenda kwenye vile vijiji ambavyo ile mito sasa inatokea. Tunawaondoa kwenye njia tunawapeleka kwenye vyanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kufanya mpango wa dharura kuhakikisha ile mifugo 200,000 inayoondoka kule tunaiandalia mazingira madhubuti kwa ajili ya kutoharibu mazingira maeneo ambayo wanaenda kuishi. Wale wakulima tunapowaondoa mle tufanye miradi mikubwa ya umwagiliaji katika maeneo yale ambayo wanaenda kuhakikisha hawataharibu mazingira ya mito, vile vyanzo vya mito na vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kushirikiana Wizara hizi, Maliasili, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Uvuvi, Wizara ya Maji na Mazingira, mkae kwa pamoja muangalie suala hili mtalitatuaje, la sivyo kama mnachukua hizo shilingi bilioni 700 mnaenda kuanzisha huo mradi, mtakapomaliza huo mradi huku mtakuta mito tayari imeshakauka. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa nawaomba sana kwa sababu kutoka ulanga peke yake kuna mito zaidi ya 52 ambayo inamwaga maji Mto Kilombero. Sasa hawa watu 100,000 wanaotoka kwenye hili bonde wanaenda kuishi huko kwenye vyanzo vya mito. Kwa hiyo, mradi mnamaliza kujenga mradi na maji hakuna. Kwa hiyo naomba tahadhari kubwa ichukuliwe kwenye mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwakibete atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Sanga halafu Mheshimiwa Joel Mwaka.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa na mimi niweze kuchangia kwenye Wizara hii ya Nishati.

Awali ya yote kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalimani pamoja na Naibu wako mnafanya kazi nzuri sana na ikumbukwe kwamba wewe Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu mmekuja mara nyingi sana katika Jimbo langu la Busokelo, kwa hiyo, nawashukuruni sana kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Busokelo na Mkoa wa Mbeya na Rungwe kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba wamekuja kule Mheshimiwa Waziri uliona shida na changamoto za wananchi wa Jimbo langu la Busokelo hasa vijiji vyote ambavyo vivyokuwa katika mpango wa Awamu ya Tatu ya *REA* kwa maana ya vijiji 50. Katika hivyo vijiji 50 kuna vijiji nane ambavyo Mkandarasi aliviacha ama aliruka kwa sababu tu hakupewa ama hakupata *instruction* za

Wizara kwa maana ya kusema vijiji ambavyo vina nyumba ya tope ama za nyasi hawezi kupeleka umeme. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri kwamba jambo hili najua ulilitolea kauli pale lakini bado hawajaenda kufanya *survey,* hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kwamba katika vijiji 42 vilivyobaki kuna kilometa kwa mfano kijiji kimoja mnaweza kupewa labda kilometa mbili na hizo kilometa mbili kwa maana ya *preliminary survey* walikwenda kuangalia na kuhakiki lakini anapokwenda kufanya *detailed design* zinazidi kupungua zaidi Mheshimiwa Waziri. Kwa hiyo, tuombe Wizara yako kwamba vijiji vyote ambavyo viko *scope of work* ya *REA III* viweze kufanyiwa *detailed design* na viweze kupelekewa umeme na si vinapelekewa baadhi vitongoji hii inatuletea shida sana sisi kama wawakilishi wa wananchi kwamba Serikali inasema ni vijiji vyote maanake ni pamoja na vitongoji vyake kwa ujumla lakini vinavyokwenda kupelekewa umeme ni vitongoji vichache, hilo la pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu Mheshimiwa Waziri napenda kuzungumzia hawa wakandarasi wa Awamu ya Pili. Kuna mkandarasi ambaye alikuwa anafanya Mikoa ya Mbeya pamoja na Songwe. Kuna baadhi ya vijiji amevitelekeza na hivi ninavyosema kuna baadhi ya maeneo ambayo kuna nguzo tu na nyaya zinaning'inia maana yke ni hasara kwa Serikali na hajachukuliwa hatua yoyote. Kuna baadhi ya maeneo ambapo transfoma zina zaidi ya miezi minne hadi mitano zimeungua ama zimepigwa radi na bado huyo mkandarasi hajaweza kuzi-*replace* ama kuleta nyingine na wananchi wako gizani. Nikuombe sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa wewe ni msikivu na bado unafuatilia haya mambo kwa karibu na Naibu wako ninaamini haya mambo mtayafanyia kazi na mtaweza kuyatolea majibu mtakapokuja ku-*wind up* hotuba yako hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri pia nikuombe kuna jambo lingine hasa hizi transfoma zinazoungua ningefikiri ingekuwa jambo jema sana kama *TANESCO* ama *REA* hata kabla ya hawajakabidhi mradi wowote ule kuwe na akiba ya hizo transfoma kwamba inapoungua basi iwepo nyingine ya ku-

*replace* kwa sababu inaleta shida sana hasa katika huduma za jamii kwa hospitali na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna huu umeme wa joto *(geothermal).* Mara nyingi nimekuwa nikizungumza katika bajeti ya Wizara yako lakini naamini mwaka huu nimeona katika kitabu chako cha bajeti umesema mmetenga shilingi bilioni 80 kwa ajili ya kuchoronga lakini pia kuajiri baadhi ya wakandarasi ambao watafanya kazi hii ya utafiti katika Ziwa Ngosi na humu limeandikwa Ziwa Ngozi lakini linaitwa Ziwa Ngosi katika Mkoa wa Mbeya Wilaya ya Rungwe na maeneo mengine Wilaya ya Mbeya vijijini eneo la Songwe.

Sasa ninaamini *geothermal* inapatikana maeneo mengi katika nchi hii na kwa mujibu wa takwimu ambazo umeleta katika kitabu hiki ziko zaidi ya megawati 5000 kama tutaweza kuifanyia joto ardhi pia iwe sehemu ya umeme *mix* katika nchi hii ya Tanzania. Naamini mtaifanyia kazi na mtaweza kupeleka na wataalam wengine na maeneo mengine katika nchi hii ikiwemo kwangu kule Busokelo eneo la Ntaba na Mpaka ili tuweze kupata pia umeme wa *geothermal* badala tu ya ku-*rely* kwenye umeme wa *hydro* pamoja na umeme wa gesi. Ikizingatiwa kuwa umeme wa gesi ni gharama kubwa zaidi ukilinganisha na umeme huu wa *geothermal* na ukilinganisha kwamba pia umeme wa *geothermal* ni umeme wa joto ardhi ambao ni *renewable* maana yake ni endelevu tofauti na umeme wa gesi ambao baada ya miaka kadhaa na tafiti zinaonesha pengine miaka 100 huo umeme unakuwa tayari ile tunasema *rocks* tayari zinakuwa haziwezi kutoa tena gesi na inakuwa inakwisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Mheshimiwa Waziri niweze pia kukushauri kwa suala zima la *EWURA* kwamba *mobile fuel stations* ni muhimu kwa maeneo ya vijiji kama Majimboni kwetu kule Busekelo. Hatuna *petrol station* kule, kama zitakuwepo ambazo ni *mobile* zitasaidia, na kuna utafiti ulifanyika na wameshaleta ripoti naamini utazitolea maamuzi hapa kwamba ziwepo sasa kama nchi nyingine walivyofanya kwamba kuwepo *mobile fuel station* kwa ajili

ya maeneo ambayo hakuna mafuta ama vituo vya mafuta.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kukatika katika kwa umeme katika Mkoa wa Mbeya... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEO K. SANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa na mimi nafasi hii niweze kuchangia. Kwanza niishukuru Serikali, nimshukuru Waziri, Naibu Waziri na watendaji kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya juu ya kusimamia Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana Waziri kuna ule umeme ambao unatoka Makambako kwenda Songea hasa katika Kijiji kile cha Kiumba, pale Makatani Kilabuni unajua vizuri ulifika bado hatujapata umeme katika eneo hilo, nikuombe sana watu wako waweze kutuwekea umeme katika eneo ambalo ulikuwa umeagiza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili niombe katika Awamu hii ya Tatu ya *REA* pale Kijiji cha Kifumbe ambapo Mkandarasi anaishia pale kuna ukanda ule Kijiji kitakachokuwa kimebaki ni kimoja kinaitwa Mtanga niombe sana kiweze kuingizwa katika Awamu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu akiwa Waziri na Mbunge alikaa ndani hapa miaka 20; akiwa hapa alikuwa anasikiliza hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge. Mojawapo walizungumzia sana tatizo la umeme kwamba tatizo la umeme ni miaka nenda megawati zaidi ya elfu moja na kitu. Sasa baada ya kusikiliza anakwenda kutekeleza mradi mkubwa wa Bonde la Rufiji ambalo litazaa anakwenda zaidi ya 2 100 kwa ajili ya kuongeza tija ya umeme ili kufanikisha

suala la viwanda nchini kwetu. Bado watu wanasema kwa nini anatengeneza mradi huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili amekaa hapa akisikiliza suala la ndege katika nchi hii. Tumekaa hapa tulikuwa tunazungumzia kwamba ndege kutoka Dara es Salaam kwenda Mbeya ilikuwa zaidi ya shilingi 550,000 na sasa hivi Bombadier ni shilingi 180,000 kutoka Dar es Salaam ilikuwa shilingi 700,000 hadi 800,000 kwenda Mwanza, leo ni shilingi 180,000 kutoka hapa Dodoma kwenda Dar es Salaam vindege vile tumekuwa tukipanda shilingi 500,000 leo ni 180,000, jamani mtu huyu afanye nini? Eeeh! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tumezungumza hapa suala la reli kwamba Kanda ya Kaskazini huku reli ni muhimu sana, leo anakwenda kutekeleza yote hayo ambayo tulikuwa tunazungumzia humu, leo tunaona hakuna anachokifanya, ndugu zangu mtoto huyu, Rais naye amezaliwa kama sisi afanye nini juu ya Watanzania. Leo anakwenda kuwakomboa Watanzania ndege tunasema kwa nini ameleta ndege. Leo ameshughulikia suala la umeme, kwa nini sasa afanye nini? Ninyi Waheshimiwa Wabunge lazima tumuunge mkono na wakati fulani ukikuta watu wakipiga kelele maana yake amepatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri chapa kazi tunahitaji umeme huo ili wananchi wa Tanzania waweze kupata umeme. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua nimewahi kusema hapa Mwalimu Nyerere amewahi kusema mvua ya kwanza ni ya kupandia wote tupande. Sasa inapofika mahali tayari huyu atapanda wakati siyo wakati wake inafika wakati Mungu naye atachoka, maana huyu anaomba mvua huyu haombi mvua.

Sasa Rais wetu anatekeleza yale tuliyokuwa tunasema. Tumezungumzia ndege tumezungumzia nini halafu yuko mtu hapa anasema haoni kitu kinachofanyika, hata hizi barabara na kadhalika huoni?*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joel Mwaka, Mheshimiwa Ezekiel Maige, ajiandae Mheshimiwa Mhagama, ajiandae Mheshimiwa Mary Nagu.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia katika Wizara hii ya Nishati, Wizara muhimu sana. Nianze kwanza kabisa kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano ya Rais John Joseph Pombe Magufuli kwa nia na azma yake nzuri kwa Tanzania kuhakikisha kwamba tunakuwa na umeme wa kujitosheleza angalau tukishughulikia ile *Stiegler's Gorge* kupata zile megawati 2100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake, Katibu Mkuu na watendaji wote katika Wizara ambao wanaifanya kazi nzuri ambayo sote tunaiona hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kwa sababu ya muda naomba nizungumzie jambo moja tu kwamba *REA* Awamu ya Tatu tunaiona inakwenda, lakini mimi niseme kuna maeneo inakwenda kwa taratibu sana, inasuasua. Wengi wamezungumza hapa ama wakandarasi wana matatizo ama wananyimwa fedha. Basi niombe sana kupitia Wizara yako Mheshimiwa Waziri, hebu tuwawezeshe *REA* kufanya kazi yao ili watufikishe pale tunapotaka kwa Tanzania ya viwanda kupitia kuwa na umeme wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema pale kwangu Wilaya ya Chamwino na hasa Jimbo la Chilonwa ndipo mahala ambapo Ikulu ipo, kuna Mji wa Chamwino na Mji wa Buigiri, mji ule hauna umeme wa kutosha. Umeme uko kwenye maeneo machache sana, hebu Mheshimiwa Waziri tupaangalie kwa macho mawili. Mtu akiingia pale ajue ameingia kwenye mji ambao umebeba Ikulu, umeme uwe kila sehemu siyo katikati tu ya kijiji basi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nikuombe sana pamoja na kukushukuru kwamba umeme *REA* Namba Tatu umekwenda maeneo mengi katika vijiji ambavyo nilikuwa

nimeviomba naomba sasa angalia hivyo vijiji hasa vile vilivyokuwa kwenye awamu wa pili vikavushwa kupelekwa Awamu ya Tatu na vimepewa kipaumbele, sasa viweze kuangaliwa na kuhakikisha kwamba vinapata umeme mwanzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa haya machache naomba kutamka kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maige hayupo, Mheshimiwa Mhagama, ajiandae Mheshimiwa Dkt. Nagu.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia leo Wizara hii ambayo kimsingi nai-*appreciate* sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nitaongea kwa sauti ya upole sana kwa sababu ya mambo makuu ambayo Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wamewatendea wananchi wa Madaba na mimi katika ujumla wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Dkt. Kalemani na Dada yangu Naibu Waziri Mheshimiwa Subira Mgalu kwa kuungana na wananchi wa Madaba kutatua tatizo la umeme Madaba Mjini. Nawashukuru sana, katika historia kwa mara ya kwanza wananchi wa Madaba wamepata umeme. Pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ajili ya wananchi wa Kijiji cha Lutukila na Kijiji cha Mbangamawe ambao hawakuwepo kwenye mpango wa awali wa umeme wa *REA* sasa wameingizwa kwa jitihada za Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, nichukue nafasi hii kuwashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeongea sana kuhusu suala la umuhimu wa umeme kwenye kujenga Tanzania ya viwanda na Mheshimiwa Waziri ameeleza hapa vyanzo mbalimbali vya umeme na nimuombe sana Mheshimiwa Waziri wananchi wa Madaba wana imani naye sana

wanaomba sana pamoja na jitihada hizi za kutafuta vyanzo, tunaomba tuendelee kupanua miundombinu ya umeme Madaba kuendelea kusambaza kwenye vijiji vinavyozunguka Madaba, Kijiji cha Kipingo, Mahanje, Mtepa na maeneo mengine ya Madaba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niishauri Serikali ukiangalia hivi vyanzo vya umeme ambavyo kwa pamoja vinatupa megawati 1517 bado havitoshelezi kutupa Tanzania ya viwanda, lakini pale Mchuchuma tuna makaa ya mawe yatatupa megawati 600. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, megawati 600 ni karibu moja ya tatu ya umeme wote ambao tunao sasa. Kwa hiyo, mchango wa makaa ya mawe kwenye hili ni mkubwa sana. Ukiangalia kwenye gharama za umeme ukiondoa umeme wa maji na gesi katika gharama umeme unaofuata ni umeme wa makaa ya mawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napiga hesabu hapa jana, nilibaini kuzalisha *kilowatts hour* moja ya umeme kwa kutumia makaa ya mawe inatugharimu kama shilingi 255 kitu ambacho kimsingi ukilinganisha na umeme wa *fossil diesel* kwa maana ya *diesel* tunazozitumia hizi bado ni nafuu sana. Ninamuomba Mheshimiwa Waziri nina imani kubwa sana naye na ninaamini kama tuta-*exhaust energy* tuliyonayo kwenye eneo la makaa ya mawe tutatatua tatizo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimkumbushe pia Mheshimiwa Waziri kwamba kwenye tafiti zilizofanyika na Benki ya Afrika kwenye masuala ya maji *capacity* ya umeme wa maji yaani vyanzo vyetu vya umeme wa maji nchini haviwezi kutupa umeme unaozidi megawati 4800. Kwa hiyo, megawati zingine ambazo ni muhimu kuipata Tanzania ya viwanda ni lazima zitokane na vyanzo vingine ikiwemo hii ya makaa ya mawe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie nafasi hii pia kumshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa jitihada yake na uthubutu wa kwenda kuzalisha umeme ule wa *Stiegler's*

*Gorge*. Waheshimiwa Wabunge tunajua hatuwezi kuipata Tanzania ya viwanda kwa megawati 5000, ama 10000, ni lazima tufikishe megawati 40000, 64000. Leo Afrika Kusini wanaongelea megawati 64,000 ndiyo Tanzania ya viwanda tunayoitaka. Kwa hiyo, hatutaweza kuipata Tanzania ya viwanda kwa kiwango hiki kidogo. Tumtie moyo Mheshimiwa Waziri, tumtie moyo Mheshimiwa Rais... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Mary tutamalizia na Mheshimiwa Bwanausi.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kunipa nafasi hii kuchangia Wizara hii nyeti ambayo ndio chimbuko la umeme. Na mimi niungane na wenzangu Wabunge kwa kuweza kumpongeza na kumshukuru Waziri kwa kazi nzuri anayofanya yeye pamoja na Naibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kusema kwamba awamu ya kwanza na awamu ya pili Wilaya ya Hanang ilipata vijiji vichache na yeye anajua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana alivyoongeza idadi ya vijiji vikafika 40 lakini naomba vijiji hivyo vipate umeme na ianze sasa hivi awamu ya tatu. Nimesikitika kidogo alivyoenda Mbulu mara mbili, Babati mara mbili, Hanang hajawahi kuja, ninaomba aje ili watu wangu wasifikiri kwamba mimi namzuia yeye kuja huko. Hata akimtuma Naibu wake nitafurahi sana lakini najua kama alivyo msikivu nilishaongea naye atakuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vilevile niseme kwamba ushirikishi ni muhimu sana. Kule Hanang kuna Kata inaitwa Jorodom wamepeleka umeme mahala pamoja tu Darajani wanalalamika, Edang'onyi wanalalamika naomba useme na Meneja pale na *contractor* naye aone kwamba

asipeleke umeme upande mmoja na hilo limeongelewa na Wabunge wengi, kwa hiyo na mimi nisiseme sana maana yake anaelewa ninaongea naye na anasikiliza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya hapo nataka nimpongeze Rais na Waziri kwa S*tiegler's Gorge*. Ule ni umeme ambao wengine tuliupigania muda mrefu sana, sasa Mheshimiwa Magufuli anaukazania na anautekeleza. Nataka niwaambie Waheshimiwa Wabunge kwamba umeme unaotokana na maji ndiyo umeme ambao hauchafui mazingira. Sisi tunatetea mazingira, lakini na ninyi mjue kwamba mazingira hayachafuliwi na umeme unaotokana na maji kwa hiyo tuelewe hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni rahisi, gharama ni ndogo kuliko umeme mwingine jamani. Sasa tusipoanza na gharama ya chini mnataka twende na gharama ya juu haitokuwa sawa. Nampongeza sana Rais na ninaomba kama mlivyokubali sasa imebaki hofu, hofu hiyo tutaiondoa kwa kutoa maelezo zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema vilevile kwamba jamani Tanzania inataka umeme mwingi sana. Sasa hivi tuna umeme megawati 1500 na tunataka zaidi ya megawati 5000. Tusipoanza na gharama nafuu hatutaweza kufika 2025 tuwe na megawati 10000. Kwa hivyo, naomba sana tuondokane na hofu ambayo ipo na wote tusome kwenye mtandao, siku hizi kila kitu kimeandikwa, nashangaa hiyo hofu inatoka wapi, na mimi na hakika kama mama yenu nikisema hivi nisingetaka Tanzania iangamie hata kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisingetaka kabisa Tanzania iangamie ila nataka Tanzania yenye kipato cha juu, wananchi waweze kupata mahitaji yao na namna ya kupata mahitaji ni kuwa na vitu vyenye gharama nafuu na kuwa na uhakika kwamba uchafuzi wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisisitize kwamba *LNG* siyo lazima iende kwenye umeme inaweza kuuzwa nje,

lakini maji ya Mto Rufiji hayawezi kuuzwa nje. Kwa hiyo, naomba tuendelee na *LNG* ili napo tuweze ku-*export LNG* kwenda nje na kama watu watatumia kwa ajili ya gesi au kwa ajili ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa nguvu zote. Ahsanteni sana.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bwanausi. Mchangiaji wetu wa mwisho ajiandae Mheshimiwa Kangi Lugola, halafu Naibu Waziri wa Fedha.

**MHE. JEROME D. BWANAUSI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kukushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii na mimi niwe mchangiaji kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumshukuru kabla sijafika kwa Waziri na Naibu Waziri, kumshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa kuwateua Mheshimiwa Kalemani na dada yangu Mheshimiwa Subira kuwa Mawaziri katika Wizara hii. Hizi sifa ambazo wanazipata wanastahili kupata hizi sifa kwa sababu ni watu ambao wamekuwa wakitusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nielekee moja kwa moja kwenye mradi wetu wa *REA*. Mradi huu unatusaidia sana karibu Mikoa yote, Wilaya zote, Majimbo yote lakini tatizo lililopo lipo kwenye *REA* kupata fedha za kufanyia miradi hii. Mimi nimuombe sana sijamuona Waziri wa Fedha, lakini Naibu Waziri wa Fedha yuko hapa. Ile *flow* ya fedha ikienda vizuri kwa *REA* matokeo ya upatikanaji wa umeme hapa nchini utakuwa ni mzuri sana. Bahati nzuri hizi fedha tulishaamua zitokane kwenye chanzo maalum na chanzo kinacholindwa ili fedha hizi zisitumike kwa kazi nyingine. Kwa hiyo niiombe sana Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *CEO* wa *REA* tutawabadilisha kila siku kama hatuwapi fedha. Hakuna atakaye-*perform* kama fedha haziendi kwenye *REA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, linalofuata lingine ambalo nilitaka niliseme ni kwamba Wabunge wa Kusini wameeleza hasa Mkoa wa Mtwara. Tunalo tatizo kubwa sana, mkandarasi aliyepangwa kwenye Mkoa wa Mtwara hapewi fedha kwa sababu tu kwamba *document* zake zinafanyiwa uhakiki, lakini uhakiki huu ni wa muda mrefu sana. Mimi nimuombe Waziri wa Fedha aendelee kumpa fedha mkandarasi wa Mtwara, Mkoa ambao ni miongoni mwa Mikoa ambayo vijiji vingi havijawashiwa umeme. Kwa hiyo, huo uhakiki pia ufanywe haraka ili tatizo hili liweze kuondoka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kama Wabunge wote walivyosema, amekuwa akitembelea kila eneo na kila Jimbo na bahati nzuri alitembelea kwenye Jimbo langu hivi karibuni na akaja kwenye Kijiji cha Kalipinde na alipata mapokezi mazuri, wananchi wanakukaribisha tena wewe na Naibu Waziri kuja pale Kalipinde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri ulitoa kauli ambayo iliwapa faraja sana wananchi wa Kalipinde kwamba yule mkandarasi atawasha kijiji kizima, lakini matokeo ni kwamba wamewasha nusu kijiji na kijiji nusu yake haijawashwa. Kwa hiyo, ningeomba maelekezo yako unayoyatoa yaheshimiwe na watendaji na wakandarasi ili wasiharibu kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda kwa kumalizia tu niseme, niungane kabisa na wote wanaounga mkono mradi wa umeme wa Bonde la Mto Rufiji. Ni ukombozi mkubwa nami nimeshukuru kwamba wote kwa pamoja wanasema hakuna anayekataa. Hayo maelezo yanayosubiri ya kutolea ufafanuzi yatatolewa tu wala halina tatizo lakini lisiwe kikwazo cha mradi kutoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. HAMOUD A. JUMAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mungu mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kufika mahali hapa na mimi kushiriki katika kikao hiki muhimu cha kujadili hotuba ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2018/2019. Hotuba hii inakwenda kutekeleza na kusimamia miradi mbalimbali na kuhakikisha malengo ya upatikana wa nishati ya umeme inakuwa ya uhakika. Naipongeza Wizara kwa kuandaa bajeti nzuri yenye mlengo chanya kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo mengi yaliyofanyika katika sekta nzima ya nishati na sina budi kuyapongeza ili kuipa ari Serikali kuendelea kuzidisha juhudi zake. Serikali imechukua hatua thabiti kuhakikisha kunakuwepo na umeme wa kutosha na wa uhakiki kwa ajili ya uchumi wa viwanda. Hatua zilizochukuliwa zinalenga kuongeza uzalishaji, kuboresha miundombinu ya usafirishaji wa umeme, kuongeza kasi ya usambazaji wa umeme vijijini na mijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa 2017/2018 imeendelea kutekeleza miradi mikubwa ya *Kinyerezi I (MW 185), Kinyerezi II (MW 240)* na Mradi wa Umeme wa Maji wa Mto Rufiji *(Stiegler's Gorge)* utakaozalisha *MW 2100.* Hizi ni hatua kwa mpango wa Tanzania ya viwanda kwa sababu bila kuwa na nishati ya umeme wa uhakika itapelekea dhana nzima ya viwanda kutofikia malengo. Aidha, Serikali pia imepanua na kuboresha miundombinu ya kusafirisha umeme kwa kutekeleza miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi hiyo ni pamoja na mradi wa Rufiji - Chalinze - Dodoma wenye msongo wa KV400; mradi wa Singida - Arusha - Namanga wenye msongo wa KV400 na mradi wa Makambako - Songea wenye msongo wa KV220. Utekelezaji wa miradi hii umeongeza hali ya upatikanaji umeme nchini kufikia asilimia 67.5. Aidha, uunganishaji umeme kwa watumiaji umefikia asilimia 49. Vilevile Serikali inatekeleza awamu ya tatu ya mradi wa

usambazaji umeme vijijini (*REA*) ambao umepangwa kufikisha huduma ya umeme kwenye vijiji 7,873 ambavyo havijapata umeme nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Kati ya hivyo, vijiji 7,697 vimepangwa kupatiwa umeme wa Gridi ya Taifa na vijiji 176 pamoja na visiwa vitapatiwa umeme nje ya gridi kwani ndiyo njia muafaka ya kuvipatia umeme kwa sasa. Katika mwaka 2018/2019 Serikali itaongeza fedha za mfuko wa *REA* ili kuhakikisha vijiji vilivyosalia pamoja na taasisi zinazotoa huduma za kijamii vijijini zinapata umeme. Jambo lingine ni kwamba Serikali pia itaendeleza miradi ya kuunganisha Gridi ya Taifa na gridi za nchi jirani za Zambia, Kenya, Burundi na Rwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mazuri yote nilishayataja hapo awali, lakini changamoto hazikosekani. Sekta nzima ya nishati bado inakumbana na changamoto mbalimbali, umeme kukatika hovyo bila kutolewa taarifa na hata baada ya tatizo kutokea wananchi wana haki ya kupewa taarifa na kuombwa radhi kwa kukosa huduma hiyo. Hata hivyo hapa kwetu imekuwa ni kawaida kwa wahusika kukaa kimya bila kutoa taarifa na kuomba radhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe nishati hii ni tegemeo la wengi, pindi umeme unapokatika bila taarifa hurudisha nyumba shughuli za kimaendelea na kuzorotesha hali ya uchumi. Ni vema sasa Wizara kuliona hili na kuwakumbusha wahusika kujali watumiaji wa nishati hii ambao ni wananchi na pindi yanapotokea matatizo ya kukatika kwa umeme basi kuwepo na taarifa zitakazowasaidia wadau kujua hali halisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima tutambue kuwa nishati ya umeme kwa sasa ni muhimu sana ikizingatiwa tunakwenda na malengo Tanzania ya viwanda, bila kuwa na umeme wa uhakika kamwe hatutafikia malengo hayo. Ni lazima tuhakikishe umeme unapatikana muda wote na wa uhakika. Tunaipongeza *TANESCO* hasa Idara ya Dharura

kwa kufanya kazi yao ipasavyo, ni vema lakini wakaongeza juhudi kwa kufika kwa wakati zaidi katika maeneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna tatizo la nguzo za umeme chakavu ambazo zinahatarisha maisha ya watu. Baadhi ya nguzo hizo ziko katika hali ya hatari huku zikiwa bado zinapitisha umeme, taarifa hutolewa mara kwa mara kwa wahusika lakini kumekuwa na utekelezaji hafifu kuzibadilisha na kuwaletea hofu wananchi. Naishauri Wizara kuendelea kuwakumbusha wahusika kuchukua hatua kabla ya athari kutokea na kuleta madhara makubwa hapo baadae.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu kuna changamoto kubwa kwenye mradi wa *REA,* wakandarasi hawapati malipo yao kwa wakati, hali inayosababisha mradi kutokukamilika kwa wakati. Naishauri Serikali kuwalipa wakandarasi hawa malipo yao kwa wakati ili miradi hii ikamilike kwa wakati na wananchi waweze kupata umeme. Aidha, hali hii ya ucheleweshaji wa malipo hayo kwa wakandarasi husababisha nguzo kukaa kwenye mradi kwa muda mrefu na kuanza kuharibika kwa kupoteza ubora wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo nguzo hizo zinapoteza ubora hata pindi zikianza kutumika haziwezi kudumu kwa muda mrefu, kwa kuwa zimeshaanza kuharibika na kupoteza ubora wake. Haya yakifanyika kwa wakati wakandarasi wakalipwa kwa wakati basi itasaidia sana mradi huu kukamilika kwa wakati na kuepuka hasara zisizokuwa na sababu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kuna changamtoto nyingine katika mradi huu wa *REA* kwa wananchi kupewa kilometa chache, hali hii hupelekea wananchi wachache kati ya 20 - 40 kupata umeme na walio wengi kukosa nishati hii muhimu. Naiomba Serikali kwa dhamira ya dhati ya kuhakikisha umeme unapatikana vijijini basi iongeze kilometa ili wananchi wangu wote wapate umeme. Aidha, tuna changamoto ya gharama za

kuunganisha umeme, gharama za awali wananchi wanazotangaziwa ni tofauti na pale wanapokwenda kulipa wanakutana na gharama kubwa na kutoweza kuzimudu. Namuomba Waziri atuambie gharama halisi ni zipi za mwananchi kuunganisha umeme? Ikumbukwe mwananchi huyu ni wa kijijini hivyo kumudu gharama kubwa ni ngumu. Gharama hizi za juu zikiendelea kutozwa zitamnyima mwananchi huyu nishati hii muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna vijiji mpaka sasa havina umeme na hatujui ni lini watapata nishati hiyo muhimu. Serikali itueleze ni lini vijiji hivi vitaingizwa katika mradi huu. Ni bahati ya pekee Mkoa wa Pwani umetengwa kwa ajili ya viwanda. Mpango huu ni mzuri na endelevu hivyo basi ni vema tukahakikisha mkoa huu unapata umeme wa uhakika muda wote. Kama nilivyozungumza hapo awali, hakuna viwanda bila umeme wa uhakika, Serikali ihakikishe inatupatia umeme wa uhakika muda wote ili wawekezaji katika sekta ya viwanda waweze kufanya shughuli zao bila shaka yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na timu nzima ya Wizara na taasisi zote zilizo chini ya Wizara yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ni nyingi zingine ziko ndani ya uwezo wao na zingine ziko nje ya uwezo wao hasa za upatikanaji wa pesa za kuendeshea miradi hasa ya umeme vijijini kupitia *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 13/07/2017 Mheshimiwa Waziri alizindua mradi wa umeme wa *REA III* katika Kijiji cha Nyamatala. Niishukuru sana Serikali jana tarehe 23/05/2018 jioni *REA* wamewezesha umeme katika kijiji hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kupitia *REA* kama ambavyo nimekuwa nikikuomba na kushauri

kutokukiacha Kijiji cha Nyambuyi na Kitongoji cha Nyahingi katika kata hiyo ya Ngula kwani ni maeneo mawili tu katika kata hiyo yatakakuwa yameachwa. Si jambo jema kuviacha vijiji hivyo halafu baadae uje urudi tena kwa gharama nyingine, ni vizuri mkavimaliza moja kwa moja ili kupunguza usumbufu na gharama za kurudi katika eneo hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri *REA* wanapoenda katika kata fulani, mfano Mwabomba au Bungulwa ni vizuri vijiji vyote mkavimaliza kuliko kuviwekea umeme katika vijiji vitatu halafu unaacha vijiji viwili au kimoja, halafu uje urudi tena. Hii ni kuongeza gharama na kuichonganisha jamii na vijiji vilivyopata huduma ya umeme na vile ambavyo havikupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana Mheshimiwa Waziri na wataalam wako walizingatie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Ujenzi wa Rufiji *(Hydro Power Project) MW 2100.* Mradi huu hauepukiki, tunauhitaji sana kwa manufaa ya sasa na kesho, achaneni na kelele za wasioitakia mema nchi yetu. Ukiona adui yako anakupinga kwa jambo lako ambalo ni jema kwako na lenye manufaa wewe endelea nalo wala usiwasikilize. Kwani wanajua kuwa endapo utatekeleza jambo hilo ambalo yeye analipigia kelele kwa kukuzomea huyo, huyo huyo, huyo, huyo, wewe songa mbele. Usikatishwe tamaa na makelele hayo, fanya kama vile umeziba masikio songa mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo una manufaa makubwa sana kwa nchi, ni urithi ambao Mungu ametupa, lazima tutumie, hatuwezi kukaa na kulia wakati rasilimali zipo za kuweza kututoa kwenye MW 1500 hadi MW 5000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shime wataalam wetu chapeni kazi hakikisheni mwaka 2021 mradi huo unakamilika. Eneo hilo ni la Tanzania, ni neema kubwa Mungu ametupa, lazima tulitumie bila kusikiliza hizo kelele za huyo, huyo, huyo, tusonge mbele bila kugeuka nyumba hadi tufike tunapotaka kufika kwenye kukamilisha mradi huo wa MW 2100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wote wanaopinga mradi huo hawana uzalendo na nchi hii, ni vibaraka wanaotumika na washindani wetu wa maendeleo. Songeni mbele bila kugeuka nyuma. Aluta kontinua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kuchangia tena eneo hili ambalo mimi naamini nalo ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi wa bomba la mafuta na miundombinu ya barabara, Tanzania tumepata bahati ya mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga, bomba hilo litapita mikoa mbalimbali pamoja na Wilaya takribani 24 ikiwemo Wilaya ya Kilindi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa katika ujenzi wa miundombinu ya bomba hilo kuna umuhimu wa kujenga barabara kwa kiwango cha lami. Eneo ambalo bomba hilo litapita barabara hiyo ni kutoka Handeni – Kibirashi – Kifanga - Kitoto – Nchemba – Singida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii kipindi cha mvua haipitiki kabisa na naamini kutoipa kipaumbele itazorotesha mradi huu ambao ni muhimu sana tena sana. Kwa mfano kwa kipindi cha mwaka huu mpaka sasa mvua ndio zinamalizikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ichukue ushauri kama hatuna fedha za ndani tuone umuhimu wa kupata mkopo nje ya nchi, kwani faida itakayopatikana kupitia mradi ni kubwa na hata kama ikijengwa kwa mkopo faida itapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. RUKIA AHMED KASSIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Chananja Kalemani pamoja na Naibu Waziri wake kwa kazi nzuri wanayoifanya. Ila tatizo kubwa linalowakwamisha ni fedha za bajeti

tunazozipitisha kutokupelekwa kwa wakati au kupewa asilimia ndogo ambayo ilipitishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano inasema ni Serikali ya viwanda, lakini bado hatujawa na umeme wa uhakika. Mwekezaji yeyote hawezi kujenga kiwanda kama hatuna umeme wa uhakika, atapata hasara. Hata wafanyabiashara ndogo ndogo wanashindwa kufanya baadhi ya biashara zao kutokana na ukosefu wa umeme wa uhakika. Jambo hili linaathiri sana uchumi wa nchi, hivyo ni vyema Serikali ikajipanga kueneza umeme katika sehemu zote hasa ukizingatia tuna vyanzo vingi vya kupatia umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* na *ZECO* bado hawajafikia muafaka katika suala la ununuzi wa umeme. Zanzibar inanunua umeme ghali sana tofauti na huku Tanzania Bara. Naiomba Serikali jambo hili walipatie muafaka ili Wazanzibar tujisikie kuwa ni miongoni mwa Watanzania.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri na utekelezaji mzuri wa ilani. Nawapongeza pia Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu Mkuu kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba miradi ya *REA II* ambayo haikutekelezwa ipewe kipaumbele katika *REA III*. Wananchi ambao miradi yao haikutekelezwa wana unyonge sana. Kijiji cha Kondo ambacho kilikuwa katika *REA II*, mradi wao haukutekelezwa. Namuomba Mheshimiwa Waziri amuelekeze mkandarasi Jimbo la Bagamoyo atoe kipaumbele kwa Kijiji cha Kondo katika utekelezaji wa miradi yake katika Awamu hii ya Tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuzingatia mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge kuhusu miradi ya umeme vijijini, kwa ajili ya *REA III* niliwasilisha miradi *REA* kwa kufuata taratibu zilizowekwa na baada ya kujadiliana na Waheshimiwa Madiwani wa jimbo langu. Kitu cha kushangaza ni kuwa mapendekezo hayo hayakuzingatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, orodha ya miradi iliyoletwa ilijumuisha Kata ya Dunda ambayo haihitaji miradi hiyo na wala hatukupendekeza. Ni Kata ya Mjini na maeneo yaliyotajwa ya umeme. Namuomba Mheshimiwa Waziri awaagize *REA* wazingatie mapendekezo ya Wabunge na hasa pale wanapowasilisha mapendekezo hayo katika utaratibu uliowekwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa Miradi ya *REA III*, namuomba Mheshimiwa Waziri ahakikishe Miradi ya Awamu ya Tatu inatekelezwa kwa ukamilifu. Wananchi ni wahitaji sana wa umeme. Baada ya kuahidiwa, wasipotekelezewa wanakuwa wanyonge sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya umeme ambayo imepewa jina la *Peri – Urban* bado hatujaielewa. Ni miradi ya mwaka gani wa fedha? Utekelezaji utaanza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuthubutu kuanzisha mradi mkubwa wa umeme wa maji wa *Stiegler's Gorge*. Bila umeme mwingi wa gharama nafuu, juhudi zote za kusambaza umeme hazitokuwa na tija. Tunahitaji umeme mwingi na wa uhakika kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Serikali isonge mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga hoja mkono.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa naunga mkono hoja hii. Pia nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri sana kwa sababu inaleta matumaini makubwa sana kwa kauli mbiu ya Tanzania ya viwanda na kwa kila kijiji kupata umeme. Napenda kutoa masikitiko yangu kama Mbunge wa Nyang'hwale uzinduzi wa *REA* Awamu ya Tatu tulizindua Kimkoa, Wilayani Nyang'hwale Kata ya Nyinjundu na kupewa majina ya vijiji 35 kupatiwa umeme kwa Awamu ya Tatu. Cha kushangaza hadi leo hii ni kijiji kimoja tu kimewashwa umeme, Kijiji cha Izunya ambapo uzinduzi ulifanyika pale Nyijundu umeme bado kuwashwa hata nguzo kusimikwa.

Naomba Mheshimiwa Waziri kumbuka ahadi yako uliyoitoa pale Nyijundu ya siku ya uzinduzi, wananchi wanauliza ni lini sasa Nyijundu utawaka umeme. Mheshimiwa Waziri nakuomba sana wasiliana na Meneja wa *REA* Mkoa wa Geita ili Nyijundu uwake umeme. Hata Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni mwaka 2015 pale Nyijundu aliwaahidi kuwapatia umeme. Wewe pia uliahidi hivyo hivyo, mimi kama Mbunge naogopa hata kwenda kufanya mkutano wa hadhara Nyijundu, najua maswali yatakuwa magumu kujibu kuhusu umeme lakini naomba pia vijiji ambavyo tuliahidiwa vipelekewe nguzo haraka kuondoa sintofahamu jimboni Nyang'hwale.

Mungu awabariki sana Mheshimiwa Waziri na wataalam wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kuwapongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu wake kwa kazi nzuri sana wanayoifanya kwenye eneo hili la nishati kwa maendeleo ya nchi yetu. Hongereni sana kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa *Rufiji Hydro Power*, naipongeza sana Serikali chini ya Mheshimiwa Rais John Magufuli kwa kuifufua ndoto ya mradi huu iliyootwa na Rais wa Awamu ya Kwanza Mwalimu Julius K. Nyerere. Ninachoishauri Serikali ihakikishe suala la mazingira limewekwa sawa ili kupunguza madhara yatakayotokana na kuanzishwa kwa mradi huu hasa kwa Mbuga ya Wanyama ya Selous na mkondo wa maji yanayoingia baharini. Naamini Serikali ina wataalam wenye uwezo watakaoishauri Wizara vizuri ili tuwe na mradi endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme wa *REA* Awamu ya Tatu, naipongeza Serikali kwa jitihada ya kupeleka umeme vijijini. Ninaiomba Wizara, transfoma inazotumia ziimarishwe kwa maana transfoma nyingi zinazofungwa kijijini hususani kwenye Jimbo langu la Maswa Magharibi zinalipuka

mara kwa mara na kusababisha kutokuwepo kwa umeme vijijini. Licha ya hivyo, transfoma hizo zinapolipuka inawachukua muda mrefu sana *TANESCO* kuleta na kuweka nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kurukwa kwa vijiji na vitongoji ndani ya vijiji. mkandarasi anaweza kuanza kazi kijiji hiki akaruka kingine na sababu *either* hazitolewi au kisingizio cha kijiji hakipo kwenye orodha ya mkandarasi. Naomba wakandarasi na Mameneja wa *TANESCO* wawashirikishe viongozi wa wananchi na wananchi kwa ujumla ili kuepuka shida hii ya kuruka kijiji au vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Kituo cha Kupozea Umeme Maswa/Simiyu, Simiyu na Wilaya ya Maswa hakuna kituo cha kupoozea umeme na hivyo kufanya umeme unaotoka baada na Shinyanga kutokuwa wa uhakika sana na kukatikakatika sana kila mara hasa wakati wa masika. Naiomba Wizara ifanye juu chini kuhakikisha kwamba Mkoa mzima wa Simiyu unapata kituo cha kupozea ili umeme huo uwe *stable*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na naunga mkono hoja.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nishati ya uhakika ni chachu muhimu sana katika kujenga Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kuja na mpango kabambe wa kuifanya Tanzania kujitegemea katika nishati. Tanzania inavyo vyanzo vingi vya uhakika vya umeme kama vile gesi, jua, joto ardhi na kadhaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni dhahiri kwamba uzalishaji wa umeme wa uhakika utasaidia sana usambazaji wa umeme katika miradi ya *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati Mheshimiwa Medard Matogolo Kalemani kwa kufanya ziara ya kikazi Jimboni Mbogwe tarehe 14 Mei, 2018 na kuwasha umeme katika Kijiji cha Shinyanga B kuashiria uzinduzi wa mradi wa *REA* katika Wilaya yetu ya Mbogwe. Aidha, naipongeza sana Serikali kwa jitihada zake za kusambaza umeme katika maeneo mbalimbali wilayani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali ione utaratibu mzuri wa kuhakikisha kata na vijiji ambavyo havijapata huduma hii muhimu ya umeme katika Kata za Bunigonzi, Vijiji vya Bunigonzi, Nyandekwa, Shibutwe na Mwabukwalule; Kata ya Ikobe Vijiji vya Ikobe, Busabaga na Kagongo; Kata ya Ilolangulu Kijiji cha Kakola Mbogwe; Kata ya Ngemo Vijiji vya Ivumwa, Isenengeja, Lwazeze na Mjitundu; Kata ya Ikunguigazi Vijiji vya Kagera, Mwingiro, Bugigizigo; Kata ya Mbogwe Vijiji vya Mwanza, Iboya, Kasosobe, Bwenda Nseko; Kata ya Bukandwe Vijiji vya Maguta Nhung'wiza na Njia Panda ya Nyerere; Kata ya Masumbwe Vijiji vya Budoda, Ilangale, Bugegele Nyakasaluma na Kata ya Isebya Vijiji vya Mgelele, Mjashinge na Kiseke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu Serikali yetu itachukua hatua kuhakikisha wakandarasi wote waliopewa kazi katika *REA* Awamu ya Tatu wanakamilisha miradi yote kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri kwa kuja na mpango kabambe wa kuanza ujenzi wa bwawa la kuzalisha umeme wa *Stiegler's Gorge*. Mradi huu utakuwa ni mwarobaini wa kukatika kwa umeme kwani megawati 2100 zitaingizwa katika Gridi ya Taifa na kusaidia katika kuijenga Tanzania ya viwanda. Kwa vile kutakuwa na umeme wa uhakika na kuwawezesha wawekezaji katika sekta muhimu ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa uhakika ni suala zima la ulinzi wa Taifa letu kwa vile uwekezaji katika sekta ya viwanda utasaidia pia katika uwekezaji wa viwanda vya zana za kivita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyenzi Mungu kwa kuweza kuwepo kwenye bajeti ya mwaka huu 2018/2019 na pia kuwa kwenye mfungo wa mwezi huu mtukufu wa Ramadhani, tujaaliwe Ramadhani njema kwetu sote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayofanya. Naanza kwenye suala la umeme hasa kwenye mkoa wangu wa Pwani. Mkoa una viwanda vingi sana na hitaji la umeme viwandani ni kubwa ni vyema Serikali ikaongeza nguvu ya umeme huo kwenye viwanda ili uzalishaji uwe wa kutosha na hiyo itasaidia kukuza uchumi wa viwanda nchini na kuongeza ajira kutokana na hilo nini mkakati wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la fidia kwa wananchi ambao ama wamejenga au kuwa na mashamba yao na kuwa sehemu ambayo itapita ujenzi wa miradi ya umeme hadi leo hawajalipwa ni zaidi ya miaka mitano sasa. Maeneo hayo hasa Wilaya ya Mkuranga mfano Dundani, Makele, Lukanga, Mwanambaya na kwingine. Nini hatma yao na Serikali ina mkakati gani katika hili ili kuweka twasira nzuri kwa jamii ya eneo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, juhudi za Serikali katika suala la *REA* tunaziona na kuzipongeza sana. Hoja yangu hapa ni kutaka kujua ni lini umeme utafika kwenye vijiji ambavyo havijafikiwa? Kwa mfano Wilaya ya Kisarawe Tarafa ya Chole, Tarafa ya Manerumango - Palaka, Kitonga, Mfula na Tarafa ya Mzenga Dololo, Vihingo, Mtakayo, Tarafa ya Sungwi, Chakenge na Turini, hivyo ni baadhi ya vijiji tu lakini vipo vingi. Pamoja na maeneo ya visiwa vilivyopo Mkoani Pwani kama Jibondo, Juani na vinginevyo ni vipi umeme utafika maeneo hayo kwani unahitajika kwa ajili ya huduma mbalimbali ikiwemo kuongeza kipato cha jamii na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapongeza ujio wa mradi wa *Rufiji Hydro Power* ambao unatarajiwa kuzalisha umeme jumla ya MW 2100*.* Hii ni hatua kubwa kwani lengo la kukuza uchumi wa viwanda litafikiwa na gharama za umeme zitapungua na hivyo kumpunguzia mzigo mwananchi wa kuwa na unafuu wa gharama mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme unatokana na maji na tija kwa Taifa, ili kuendelea kutunza mazingira kwenye maeneo mbalimbali, kuna haja ya matumizi ya gesi asilia majumbani, ungeanza kwenye maeneo ambayo bomba linapita. Je, ni lini Mkoa wa Pwani utafaidika na matumizi ya gesi asilia kwa matumizi ya nyumbani? Naomba jibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafiti ambazo zinafanywa juu ya upatikanaji wa mafuta au gesi huongezeka, nchi yetu tumepata neema na hiyo itasaidia kuongeza pato, maendeleo na kumpunguzia gharama mwananchi. Ucheleweshwaji wa fedha za miradi na pia ulipwaji wa wakandarasi utazorotosha kasi ya azima ya miradi iliyokusudiwa. Hivyo fedha zitoke mapema ili kazi ifanyike kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ZAINAB M. AMIR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nawapongeza Mheshimiwa Dkt. Medard Matogolo Chananja Kalemani, pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Subira K. Mgalu, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ili kuondoa tatizo la wataalam katika Wizara hii ya Nishati iongeze fani (kozi) ya gesi na mafuta katika vyuo vyetu vikuu Tanzania kwa sababu vijana wengi wanaenda kusomea fani hii nje ya nchi na gharama zake ni kubwa sana. Serikali kupitia Shirika la Umeme *(TANESCO),* itoe elimu ya kutosha kwa wananchi ambao hufanya shughuli zao mfano biashara

chini ya transfoma (mashine humba) pia wengine hujenga chini ya nyaya za umeme ili kujua madhara yake kwa binadamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ipunguze bei ya nishati ya gesi kwa matumizi ya majumbani ili kila mwananchi aweze kumudu kununua nishati hiyo na kuondokana na uharibifu wa mazingira unaofanywa na wananchi kwa kukata miti hiyo kwa matumizi ya mkaa na kuni. Naishauri Serikali njia ambayo itasaidia gharama za kuzalisha umeme ziwe za kiwango cha chini, ili kusaidia bei ya umeme kupungua ambapo itamsaidia mwananchi kuweza kuitunza nishati hiyo kwa kupikia, pia kupungua kwa bei ya umeme kutasaidia wananchi kujiunganishia umeme kiholela kwa kuwatumia vishoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ihakikishe *TANESCO* inatoa taarifa mapema kwa wateja kuhusu kukatika kwa umeme eneo husika ili kutokana na nishati hiyo kupata hasara mara tu umeme ukatikapo bila taarifa. Serikali iboreshe miundombinu katika vituo vinavyozalisha umeme ili kuepuka tatizo la kukatika kati kwa umeme mara kwa mara.Vilevile Serikali ili kutekeleza miradi yake kama ilivyopangwa katika Wizara ipeleke fedha kwa wakati ili Wizara iweze kutekeleza miradi yake kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho namuomba Mungu awape afya njema na umri mrefu Mheshimiwa. Dkt. M.M.C. Kalemani na Mheshimiwa. Subira K. Mgalu ili waweze kuyatekeleza majukumu yao ya kuwatumikia Watanzania.

**MHE. ENG. GERSON H. LWENGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja na nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti naunga mkono Mradi wa Umeme wa Rufiji utakaozalisha MW 2100. Naomba katika kupata wakandarasi *due diligence* ifanyike kwa kina ili tupate mkandarasi mwenye uwezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nishukuru sana kwa Waziri kwa kunipa transfoma kubwa ya 500 KW kwa ajili ya viwanda viwili jimboni kwangu Wanging'ombe katika Kijiji cha Dulamu kama kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti na pale Igwachanya kuna kiwanda cha kusaga sembe. Nilikuomba Mheshimiwa Waziri na nashukuru niliambiwa ipo njiani inaletwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri afanye uchunguzi wa kitaalam kwa kazi zilizofanywa na Kampuni ya *Lucky-Export* aliyesambaza umeme wa *REA II* Mkoa wa Njombe. Mpaka sasa taarifa nilizo nazo transfoma 30 zimeingia katika Wilaya ya Wanging'ombe pekee. Sina taarifa ya ngapi maeneo mengine. Inaelekezwa kuwa mkandarasi huyo aliagiza transfoma na vifaa vingine vya mradi na *REA II* kutoka India na ninahisi vilikuwa havina ubora au ujengaji wa miundombinu uko chini ya kiwango; uchunguzi ufanyike. Wakati Mheshimiwa Waziri anazindua Mradi wa *REA III* aliagiza vijiji vilivyoomba na kugharimu viingizwe kwenye *scope* ya mkandarasi aliyeshinda *tender*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuletea orodha ya vijiji na vilikuwa kama ifuatavyo; Masambwa, Idunda, Imalilo, Mungelenge, Hanjawanu, Egando, Ikwavila, Malangali, Mpanga, Wanjamilo na Eyayi. Mkandarasi anaendelea na awamu hii bado hajapewe *additional scope* kama nilivyokueleza. Eneo lingine ninaloomba lifanyie kazi ni kuhusu kupeleka umeme kwenye vitongoji, mpaka sasa Wilaya yangu imepeleka umeme kwa wastani wa kitongoji kimoja kila kijiji wakati vijiji vina wastani wa vitongoji vitano na Wilaya nzima ina vitongoji 550. Je, upo mpango wa kupeleka umeme vitongoji vyote utawezekana *by 2021?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimuomba Mheshimiwa Waziri transfoma 14 kwa Vijiji vya Ng'nda Maloga, Samaria, Uhalinde, Utelene, Mdasi, Masilu, Mlevela, Nyumbamtu Kanamaluga, Wangutwa, Kidungala na Nyuhosei. Nashukuru mmeniletea transfoma nane, bado sita na vijiji hivi vilivyoingizwa ni tangu Desemba, 2017. Naomba Mheshimwia Waziri utusandie hivyo vilivyobaki kwani wanashindwa hata

kusaga unga kwa ajili ya chakula. Pia baadhi ya vijiji vinapelekewa transfoma ndogo za 25 KVA badala ya zile za 50 KVA naomba urekebishwe.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hoja ya hotuba ya Waziri wa Nishati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *REA*, utekelezaji wa miradi ya *REA* unasuasua katika maeneo ya Jimbo la Tunduru Kusini, hamna hata nguzo moja iliyopelekwa katika vijiji vilivyofanyiwa *survey* na mkandarasi. Hata vijiji vilivyopata umeme wa *REA II*, Vijiji vya Azimio Chiwana, Mkandu na Mbesa umeme umepita barabarani tu nguzo hazikuingia ndani kwenye mitaa ambayo wananchi wapo jambo ambalo limeleta malalamiko mengi. Kijiji cha Chiwana kuna vijiji viwili, Chiwana na Umoja. Kijiji cha Chiwana wana umeme wakati Kijiji cha Umoja hawana umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika Kijiji cha Mbesa na Kijiji cha *Mbesa Airport.* Kijiji cha *Airport* hawana umeme jambo ambalo linaleta mtafaruku mkubwa sana wakati waungana nyumba. Katika jimbo la Tunduru Kusini lina vijiji 65 kati ya hivyo vijiji vinne tu ndiyo vimevipitiwa na umeme wa *REA*. Hivyo naomba *REA* kuzingatia maombi yangu ya vijiji vya nyongeza ili vipate umeme kwani jimbo la Tunduru kaskazini vijiji vyake. Ninaomba jimbo la Tunduru Kusini ipewe kipaumbe ili kuondoa chana mbaya iliyotawala kwa wananchi wa jimbo la Tunduru Kusini kuwa wanaonewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi ya *solar* kwenye vijiji na maeneo ya hudumu za jamii, baadhi ya maeneo ya shule za sekandari na zahanati mkandarasi amefunga vifaa pungufu hivyo kufanya umeme usiwake kama vile shule za sekondari za Semeni, Namasakata, Lulumbule na Ligoma ambako mpaka leo wamefunga *panel* lakini betri hamna na sehemu nyingine wamefanya *wiring* bila kufunga vifaa vingine. Baadhi ya vijiji vya Jimbo la Tunduru Kusini havina nguzo za taa za *solar* hazijapewa kama

vijiji cha Naikula, Chinunje havina nguzo za *solar* kama ilivyo katika vijiji vingine na mkandarasi ana zaidi ya miezi sita haonekani Tunduru; hivyo tunaomba mkandarasi arudi *site* akamalizie kazi yake pamoja na kupeleka vifaa vilivyosalia katika ujenzi wa umeme wa *solar.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la upatikanaji wa umeme Tunduru, kumekuwa na tatizo kubwa la umeme katika Wilaya ya Tunduru kutokana na ubovu wa mitambo inayotumika kuzalisha umeme mara nyingi zimekuwa zikizimika zimika bila taarifa. Hivyo tunaomba Tunduru kuunganishwe na umeme kutoka Mtwara au waongeze mashine zingine mpya ili kuongeza nguvu kwa vile vijiji vilivyopata umeme wa *REA* hiyo unahitajika umeme mwingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kipaumbele cha kuongeza mashine za kuzalisha umeme wa gesi, kwa kuwa upatikanaji wa gesi umekuwa mkubwa na kwa kuwa gesi ni nyingi na tunatumia kidogo sana, ninaiomba Serikali iongeze mashine za kuzalisha umeme kwa kutumia gesi hata kama kwa kutumia wafanyabiashara binafsi *(PPP)* ili kuongeza matumizi ya gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashauri Serikali kuchukua na kulipa gharama za bomba la gesi badala ya kuiachia *TPDC,* walipe na Serikali iongeze mitaji *TPDC* na *TANESCO* ili makampuni hayo yajitegemee kibiashara na kuleta tija kwa nchi kwa kutumia gesi asilia. *TPDC* wanategemea sana ruzuku kutoka Serikalini, kama Shirika la Taifa la Mafuta na Gesi *(NOC).* Ninashauri *TPDC* wapewe mtaji wa kutosha ili ishiriki katika Tato la Taifa na kukuza uzalishaji wa gesi na usambazaji wa gesi katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

**MHE. JANETH M. MASABURI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Waziri wa Nishati, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote walioko katika sekta ya nishati, bila kuwasahau *TANESCO* na *REA* kwa kazi kubwa na njema waliyofanya hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri na Naibu Waziri ni watu wasikivu na wanyenyekevu sana. Hali hiyo husaidia kupunguza malalamiko na lawama nyingi kwa Serikali na taasisi zake, tunashukuru sana kwa usikivu wao. Naomba kuchangia machache kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na uzinduzi wa utumiaji wa gesi majumbani na kwa kutambua kwamba mpango huo utasaidia kupunguza matumizi ya kuni na mkaa pia kuzuia uharibifu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ingalie utaratibu wa kupunguza gharama za bei ya gesi za matumizi ya nyumbani ili wananchi wengi waweze kuacha kutumia mkaa na badala yake watumie gesi kwa ajili ya kupikia. *TANESCO* itatue changamoto ya umeme kukatika mara kwa mara na kwa makini kuangalia maeneo nyeti, pia wakati wa hafla au matukio yanayooneshwa katika *tv* (mubashara) kuwa kunakatika umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho narudia kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na naunga mkono hoja asilimia mia moja.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na umeme wa *REA,* kuna maeneo ambayo hayakupata umeme wa *REA I* na *REA II,* hivyo katika mpango wa *REA III* yameorodheshwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa angalizo, Kata ya Iragua ina wakazi wengi sana lakini imezungukwa na misitu ya mbao ya makampuni binafsi ambao wanaleta vikwazo kwa nguzo za umeme kupita (kuwekwa) kwenye mashamba yao na hatimaye umeme kufika kwenye VVijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengi umeme wa *REA I* na *REA II* umefika lakini *TANESCO* hawataki kuwaunganisha wateja kwa mpango wa *REA* kwa bei nafuu, wanawatoza kama wateja wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo umeme umepita tu lakini vijiji unapopita hawanufaiki na umeme huo. Naomba liangaliwe kwa umakini wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukatikaji wa umeme hovyo ni tatizo kubwa sana hivyo kufanya wananchi wanaojiajiri kwenye fani ambazo zinahusisha matumizi ya umeme ku-*fail.*

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu fidia ya wananchi watakaopisha mradi wa 400 *KV* Singida – Arusha – Namanga, naomba kujua ni lini Serikali itawalipa wananchi wa Monduli wanaopisha mradi huu ambao wamesubiri kwa zaidi wa miaka mitatu na wamezuia kuendeleza maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Serikali haina hela basi iruhusu wananchi waendelee na shughuli zao. Wananchi wapewe kipaumbele cha ajira katika kazi wanaweza kufanya kuliko kuwaleta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini Serikali itawaunganishia umeme wananchi ambao walirukwa katika *REA I* na *REA II* katika maeneo ya Vijiji vya Mti Moja, Naalarami, Nafao, Nanja, Selela, Arkatan na Losimingoni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mpango wa Serikali kuwapatia umeme wa *REA III* Vijiji vya Lashaine, Lepurko, Emairete, Mswakini, Mbuyuni, Mbaash, Arkaria, Mfereji, Ndonyonaadu, Baraka, Munjere, Naitulia, Engarooji na Lemooti.

**MHE. OMAR A. KIGODA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa juhudi kubwa za kuleta umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *REA* una changamoto kwa baadhi ya maeneo. Kwa mfano katika Kijiji changu cha Kwamagome umeme umepita pale kwenda kijiji kinachofuata wakati kijiji kile ni moja ya vijiji vyenye wakazi

wengi sana na pia eneo lile Mbunge namalizia kujenga zahanati kubwa ambayo itakuwa mbadala wa Hospitali ya Handeni iliyozidiwa na wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri kwenye majumuisho yake nipate jibu la Kijiji cha Kwamagome. Nimeongea na Naibu Waziri, nimeongea na Msofe na wameniambia itatekelezwa. Naomba Mheshimiwa Waziri tupate majibu kwa niaba ya wananchi wa Handeni wenye shauku kubwa ya kupata umeme Kwamagome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kufanya ziara katika Wilaya na Jimbo la Mbulu Vijijini, Kata ya Maretadu Juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji vyangu 70 havina umeme, umenikubalia kutupa vijiji vya ziada 21 na vile vya kabla ni 11 hivyo kufanya jumla 32. Naomba sana usaidie, ipangwe na *REA* ianze kazi katika mwaka huu, *REA II* sikubahatika. Ombi langu wasibadilishe orodha niliyompa Meneja wa Mkoa na Msofe maana tumeshakubaliana wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Mheshimiwa Dkt. Kalemani akumbuke alisema mbele ya wananchi wa Maretadu kuwa atawasha umeme tarehe 16Juni, 2018. Naomba asimamie ahadi yake.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani pamoja na Naibu wake. Nawapongeza timu yote ya watendaji wa Wizara chini ya Katibu Mkuu, Dkt. Mwinyimvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru *REA* wameanza kufanya kazi katika Jimbo langu, lakini ningeshauri, kuna vifaa vilivyobaki kwenye *REA* iliyopita vipo tu pale Songea wapewe wafanye kazi hiyo kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, genge moja tu kwa kijiji nilivyoahidiwa nadhani italeta shida kidogo. Jimbo langu ni kubwa, kata 20, vijiji 84, hivi watamaliza lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia mkandarasi huyu namfahamu ana uwezo wa kiufundi lakini inaonekana anadai fedha nyingi na hivyo kukwama kikazi. Jamani hata mimi mwenzenu niliyepigana nanyi kutetea Shirika la umeme *(TANESCO)* na mikakati mingine ya kuunga mkono taasisi hii mnaniweka kitanzi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, *please! please!* Jimbo langu ni giza.

**MHE. DKT. HADJI H. MPONDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara kwa masharti ya ufafanuzi wa mambo mawili yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia, Serikali kupitia *TPDC* imeingia ubia na Kampuni ya Swala *Oil na Gas (Tz)* ambapo tayari imeshawekezwa jumla ya *USD* 20.7 *million* katika utafiti na uchimbaji wa mafuta na 2018 kazi ya kuanza kuchimba ingeanza. Katika matayarisho ya kazi hii ya kuchimba (kuchoronga) kisima imekuwa inasitasita sasa katika miaka mitatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu wa uchimbaji wa mafuta ilipofika Machi, 2018, umekwamishwa kutokana na kutopata kibali toka *TAWA* kuruhusu uchimbaji wa mafuta , mradi huu wa faida (mapato) ya *US$* 10 bilioni (shilingi 21.9 trilioni) utalikosesha mapato Serikali lakini pia manufaa ya ajira/shughuli za uchumi. Naomba ufafanuzi wa Serikali kwa nini miradi mikubwa kama hii inaipatia hasara Serikali kabla ya uchunguzi/uchambuzi wa kina kufanyika kabla ya uanzishwaji wa mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya Rufiji (*hydro power project*) naunga mkono ujenzi wa mradi huo ili mradi huo uwe endelevu. Naishauri Serikali wawekeze katika ujenzi wa skimu za umwagiliaji katika maeneo ambayo

yanatengeneza maji ya kuendesha mradi huo kwa asilimia 65 toka bonde la Mto Kilombero toka Wilaya za Malinyi, Ulanga, Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa skimu za umwagiliaji katika maeneo haya yatawezesha utunzaji bora wa maji na vyanzo vyake ambazo husababisha kutiririka (uwepo) kwa maji kwa bonde na hatimaye kuingia katika Mto Kilombero. Bila kilimo cha umwagiliaji (skimu) kutasababisha kilimo holela na kufanya uharibifu mkubwa wa vyanzo vya maji na kusababisha upungufu wa maji katika Mto Kilombero na hatimaye kutishia uendelevu wa mradi huo wa umeme Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa nafasi hii, kwanza kabisa nimpongeze Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri wanayoifanya na naomba sana niongeze mambo machache ya kupata ufafanuzi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Mradi wa REA III – pamoja na kwamba Mkandarasi *Grid State,* alipita Jimboni Mikumi na kufanya *survey* lakini bado kazi hii inasuasua sana kwa kile kilichojulikana kuwa hajalipwa hata *advance*, je, Serikali imeshamlipa? Kama ndiyo lini ataendelea na kazi ya kutuletea umeme kwenye vijiji na Kata zifuatazo:-

(a) Kata ya Tindiga – Vijiji vya Malui, Tindiga A, Tindiga B, Kwalukwambe na Malangali;

(b) Kata ya Zombo – Vijiji vya Nyali, Zombo, Nyameni, Kigunga na Madudumizi;

(c) Kata ya Ulaga – Vijiji vya Kibaoni, Ng'ole, Mbuyuni na Nyameni;

(d) Kata ya Mhenda – Vijiji vya Ilakala, Mhenda, Kitunduweta na Nyahanda;

(e) Kata ya Vidunda – Vijiji vya Chonwe Udung'u na Itembe;

(f) Kata ya Ruhembe – Kijiji cha Kielezo;

(g) Kata ya Uleling'ombe – Vijiji vya Uleling'ombe, Mlunga na Ibada;

(h) Kata ya Malolo – Vijiji vya Chabi, Mgogozi, Malolo A na Maholo B;

(i) Kata ya Masanze – Vijiji vya Chabima, Dodoma Isanga na Munisagala;

(j) Kata ya Mabwerebwere – Kijiji cha Muungano;

(k) Kata ya Kisanga – Vijiji vya Kikonga, Madizini, Muhelu na Wedo; na

(l) Kata ya Kilangali – Vijiji vya Mbamba na Kiduhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, umeme kwenye Mji Mdogo wa Kitalii wa Mikumi, kama ambavyo leo nimeuliza Bungeni ni kuwa Mji Mdogo wa Mikumi ni Mji muhimu sana wa Kitalii na wawekezaji wa mahoteli na miundombinu kadhaa ya utalii bado wanatumia gharama kubwa sana za majenerata kwa kuwa hakuna umeme kwenye maeneo ya Msimba. Je, Serikali haioni kama sasa ni muda muafaka wa kuwavutia wawekezaji zaidi wa tasnia hii muhimu kwa uchumi wa nchi, kwa kuwapatia umeme wa uhakika ili kuongeza pato la uchumi na utalii hapa nchini? Je, ni lini sasa watapatiwa umeme huu wa uhakika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, Mkandarasi Kampuni ya *IBB.* Mkandarasi huyu alifanya kazi huko nyuma kwenye mradi wa *REA* I na II na alishafanya kazi ya maana na kufikia mpaka kiwango cha kuunganisha nguzo na kufunga mita kwenye maeneo ya Vikweme, Ihombwe, Mufilisi, Mbegesela

mpaka Kikonga, lakini kazi hiyo ilisimama ghafla kwa kuwa *IBB* hawajalipwa na Serikali mpaka leo na kazi imeishia hapo. Je, lini watalipwa ili wamalize kazi yao au nini kauli ya Serikali?

**MHE. MENDRAD L. KIGOLA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Serikali kwa kusambaza umeme wa *REA* vijijini, hii itasaidia sana wananchi vijijini kupata maendeleo kwa kuanzisha shughuli za kiuchumi kwa mfano; kuwa na viwanda vidogo vidogo, umeme majumbani, *motor* za umeme kwa ajili ya kusukuma maji, umeme katika Taasisi, Zahanati, Vituo vya Afya na Hospitali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto; umeme wa *REA* katika Jimbo la Mufindi Kusini bado kuna vitongoji na shule za msingi, zahanati, bado hazijapata umeme naomba Serikali isambaze umeme katika maeneo hayo yaliyotajwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Stiegler's Gorge*; naipongeza sana Serikali kwa mipango mizuri kwa kuanzisha mradi mkubwa wa kusambaza umeme *Stiegler's Gorge.* Hii itasaidia sana Watanzania kupata umeme wa uhakika, pia itasaidia sana katika kuboresha viwanda katika kuzalisha bidhaa mbalimbali na itasaidia sana kuinua uchumi wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *gas*; naishauri Serikali kupunguza bei ya *gas* kwa matumizi ya majumbani ili wananchi kuacha kutumia mkaa ambao unasababisha kuharibu mazingira yetu. Napendekeza gesi iuzwe kwa bei ya Sh.15,000 tu ili wananchi hasa wa vijijini waweze kutumia gesi kwa kupikia hasa kwa matumizi ya nyumbani kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. ENG. EDWIN A. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kukutaarifu kuwa hoja hii ya Wizara ya Nishati tunaiunga mkono kwa asilimia mia moja kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, Dkt. Medard Chananja Matogolo Kalemani alifika Jimboni na kutuahidi kuwa kwa mara ya kwanza Namtumbo itapata umeme wa *REA III* baada ya Wilaya yetu kukosa umeme katika miradi ya *REA I* na *REA II.* Hakika Waziri huyu ameitambua Wilaya ya Namtumbo kama Wilaya mojawapo ya nchi yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayohitajika huduma ya umeme vijijini kama zilivyo Wilaya nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Waziri asitusahau, awashe umeme katika vijiji 23 kati ya vijiji/mitaa 77 Wilayani Namtumbo mapema iwezekanavyo na nimwombe Mheshimiwa Waziri asiingie katika mtego uliosababisha Wilaya ya Namtumbo kukosa umeme kupitia miradi ya *REA I na REA II.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dkt. Medard Matogolo Chananja Kalemani amefuatilia utekelezaji wa mradi wa umeme wa gridi wa kutoka Makambako – Songea wa kilovoti 220 ambao utavinufaisha vijiji na Mji Mdogo wa Namtumbo. Nimwombe Waziri, aandike historia ya kuufikisha umeme wa gridi ya Taifa Wilayani Namtumbo kabla ya mwaka huu wa 2018 haujafikia mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizo mbili wananchi wa Namtumbo wamenituma nimshukuru Waziri wa Nishati na kupitia kwake tunamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa uongozi wake uliotukuka na dhamira yake ya dhati ya kutaka kutuinua wanyonge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali ya Mheshimiwa Rais Magufuli kwa miradi hii ya kukuza kiasi cha umeme. Mradi wa Umeme wa Rufiji ndiyo mkombozi wa uchumi wa viwanda nampongeza pia Waziri na watendaji wote wa Wizara ya Nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto; Mradi wa *REA* Awamu ya Tatu hauendelei vizuri katika Jimbo langu la Tabora Kaskazini hasa katika Vijiji vya Kasenga, Majengo, Ikongolo, Nzubuka, Kanyenye na katika taasisi za Serikali kama shuleni na zahanati Mkandarasi haonekani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri afuatilie umeme uweze kuonekana unafungwa. Malalamiko ya wananchi ni kuwa mkandarasi haonekani kabisa namwomba afuatilie hasa katika maeneo niliyoyataja ambako pia ndiyo makazi ya Mbunge. Vijiji vya Kanyenye, Majengo Ikongolo, Kanyenye na Nzubuka. Namwomba sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. EDWARD F. MWALONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Njombe Mjini mradi wa umeme wa vijijini vinavyopitiwa na mradi wa Makambako - Songea unasuasua sana ukizingatia umeanza siku nyingi hadi leo hakuna hata kijiji kimoja ambacho umeme umewashwa, naomba majibu ya Serikali ni nini kinachelewesha mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndani ya Jimbo la Njombe Mjini wapo wazalishaji binafsi wa umeme na wamepewa vijiji vya kusambaza umeme lakini hadi sasa hawajaweza kumaliza kazi hiyo na wanasuasua sana, Serikali itoe majibu ni kwa nini au ni nini kinasababisha hali hiyo na kama wameshindwa je, Serikali haiwezi kuwanyang'anya miradi hii. Wazalishaji hao ni Luponde *Hydro* na St. Getrude Sisters of Imiliwaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii ya Nishati ijue ina jukumu kubwa sana inakabiliana nalo. Nishati inayohitajika zaidi ni nishati ya kupikia ambayo Watanzania wote tunahitaji na wataalam wanasema nishati ya kupikia ni asilimia 98 ya nishati yote inayohitajika. Nashauri pamoja na jitihada zote zinazoendelea, Serikali iwekeze sana katika nishati ya kupikia, ikiwemo uundaji wa majiko ya kutumia umeme na uzalishaji

wa *L.P.G,* Hili litasaidia kuipatia Serikali fedha na kusaidia kuokoa na kulinda mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, *TANESCO* Njombe wanafanya kazi nzuri sana ila wana tatizo la mtambo wa kufua umeme kituo cha Uwemba. Mashine yao moja imekufa kwa miaka mingi na hakuna matengenezo naomba sana Serikali isadie ili ufuaji wa umeme katika kituo hiki uwe vizuri.

**MHE. DEO F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mkaa wa makaa ya mawe. Serikali ione sasa namna ya kuanza kutumia umeme wa makaa ya mawe hasa yaliyopo katika ukanda wa Mchuchuma ambao unaweza kuzalisha *megawatt 600.* Umeme huu ukiingia katika *grid* ya Taifa utaongeza tija kubwa kwa Taifa hasa katika kipindi hiki ambacho Sera ya Taifa la viwanda imetamalaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme vijijini *(REA).* Katika miradi ya *REA* inayoendelea katika Jimbo la Ludewa, awamu hii tumepewa vijiji 19 kati ya vijiji 55, lakini mpaka sasa hakuna kijiji kilichowashwa umeme licha ya ahadi iliyotolewa kuwa ifikapo tarehe 30/04/2018 angalau kijiji kimoja kitapewa umeme licha ya Mkandarasi kuwa *site.* Kuna malalamiko mengi toka kwa Wakandarasi mbalimbali juu ya malipo kwa kazi zilizofanyika hadi sasa. Nashauri wakandarasi walipwe mapema ili kazi ziendelee ili tuone tija na ufanisi wa umeme huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa *grid* ya Taifa – Ludewa. Serikali inaendelea na mpango wa umeme wa *grid* ya Taifa wa Makambako – Songea (220*Kv)* ambao ukitokea Mabada kuja Ludewa ambao kimsingi unatarajia kufika Ludewa Septemba, 2018. Niipongeze Wizara na kushauri zoezi liendelee kwani ni ukombozi kwa Taifa na hasa inapita katika miradi kielelezo ya Chuma –Liganga na makaa ya mawe – Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umeme wa mto Rufiji (*Stiegler's Gorge).* Naipongeza Serikali kwa kuanzisha

mradi huu wa *Stigler's Gorge* utakaotoa umeme wa *megawatt* 2100. Hili ni jambo jema na litafungua fursa nyingi mfano, ajira kwa Watanzania, kilimo cha umwagiliaji, kukuza utalii wa ndani na nje, umeme wa uhakika kwa matumizi ya ndani na kumudu Sera ya Viwanda, pia kuuza umeme nje ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, binafsi napongeza hatua hii kwani inatatua tatizo sugu linalokabili nchi la umeme unaokatikakatika na pia uanzishwaji wa viwanda vidogo nchini. Mradi huu unaakisi *vision* 2015.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, Waziri wa Nishati na Mheshimiwa Subira Mgalu, Naibu Waziri wa Nishati pamoja na timu nzima ya Wizara ikiongozwa na Dkt. Hamisi Mwinyimvua, Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, kwa kazi nzuri hasa ya usambazaji umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa kuanzisha mradi wa umeme wa Mto Rufiji ambao ndiyo utakuwa mkombozi kwa mahitaji makubwa ya umeme kwa nchi yetu. Mradi huu upewe uzito wa hali ya juu ili ukamilike ndani ya muda uliopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza Serikali kwa mkakati wa uendelezaji wa jotoridi katika maeneo ya Ngosi (na sio Ngozi) na Kiejo – Mbaka Mkoani Mbeya (na sio Mkoani Songwe) na Luhoi Mkoani Pwani. Naomba Wizara isahihishe hayo majina na pia ikumbukwe eneo la Songwe na Kijiji cha Songwe kipo Mkoa wa Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na jitihada za kusambaza umeme vijijini kwa kasi, naomba Serikali iongeze uwezo wa *TANESCO* ili iwe na uwezo wa kuhudumia wateja na miundombinu inayoongezeka sana. Bila kuwepo kwa *TANESCO* imara, miradi yote hii haitakuwa ya mafanikio yanayotarajiwa na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Waziri na Naibu wake, wanafanya kazi nzuri sana Mungu awatie nguvu. Tunatambua juhudi zao. Fidia ya *KV* 400 Singida – Namanga shilingi bilioni 68 wanatupa lini? Wananchi wanasumbua sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *all the best* kwa Mheshimiwa Waziri*.*

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza kwa kazi kubwa. Wakandarasi wa kusambaza umeme katika Visiwa vya Ukara, Bulubi na Gana wamesimama kufanya kazi kwa muda mrefu, tatizo ni nini? Katika kisiwa cha Ukara tayari wananchi walianza kutumia umeme lakini gharama yake ni kubwa sana. Mfano, *unit* moja kwa Sh.2,500 mpaka Sh.3,000, ni gharama kubwa sana kwa mwanachi wa kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe ziara yenu katika visiwa vya Ukerewe ni muhimu sana hasa katika Kisiwa cha Ukara ambapo wananchi wanaanza kujitoa katika matumizi ya umeme unaozalishwa na JUMEME kwa sababu ya gharama. Ziara yenu ni muhimu sana kwa ajili ya kuweka suala hili la gharama vizuri kwa sababu lengo ni umeme huu kutumiwa na siyo uzalishwe na kutotumika. Hivyo, ni muhimu sana ziara hiyo ifanyike ili tupate fursa ya kukaa na wananchi pamoja na JUMEME ili tuwe na uelewa mmoja wenye ufanisi kwa maslahi ya maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatakia kila la kheri katika utendaji wao.

**MHE. LUCIA M. MLOWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichangie katika Wizara hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Stiegler’s *Gorge.* Mradi wa Stiegler’s *Gorge* ni mradi mkubwa sana. Mradi huu unahusisha uharibifu wa mazingira kwa ajili ya ukataji wa miti mingi sana. Eneo hilo lina uoto wa asili na ni mbuga za wanyama – Selous. Hivyo vyote vitaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali tuliamua kuachana na umeme wa maji tukaenda kwenda matumizi ya gesi. Mradi huu wa gesi tuliaminishwa kuwa mradi huu utasaidia nchi nzima kuwa na umeme, lakini matokeo yake mradi huu wa gesi umeshindikana. Badala yake gesi imeendelea kuwa gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali kutumia pesa hizo za mradi wa *Stiegler's Gorge* zitumike katika kukamilisha mradi wa gesi ambao hauna athari za kimazingira. Nataka kujua iwapo tunaendelea na mradi huu wa Stiegler's *Gorge,* tuna uhakika gani na mabadiliko ya tabianchi ambayo inaweza kusababisha umeme na hatimaye kupunguza uzalishaji wa maji katika bwawa hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gesi asilia. Tuliambiwa muda mrefu kuwa baada ya mchakato wa gesi asilia watu wataunganishiwa gesi majumbani, lakini naomba kujua hii inachukua muda gani? Kwa sababu ahadi hii kwa wananchi ni ya muda mrefu lakini utekelezaji wake unachukua muda mrefu. Naishauri Serikali imalize haraka mchakato huo wa gesi ili wananchi waunganishiwe majumbani kama ilivyo kwenye maji na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa Mkoa wa Njombe. Vijiji vingi vya Mkoa wa Njombe bado hakuna dalili ya kupata umeme. Mfano, Utalingolo, Magodia, Lugenge, Ihalula, Idihani, Makowo, Mamongolo, Sunji, Boyimande, Kitulila, Luponde, Miva, Iwungilo, Igoma, Uliwa, Ludewa, Makete, Wanging'ombe na Lupembe. Naishauri Serikali itekeleze ahadi ya kuwapelekea umeme katika vijiji vyote vya Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha kuchelewa kwenda kwenye miradi. Naomba Serikali kupeleka pesa za miradi kwa wakati. Kutokana na ucheleweshwaji wa upelekaji wa fedha za mradi husababisha miradi kutokamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya Serikali kwa *TANESCO.* Taasisi nyingi zinadaiwa na *TANESCO.* Naiomba Serikali ihakikishe inalipa madeni yake *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. QAMBALO W. QULWI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani kwa namna anavyofanya kazi kwa ushirikishwaji wa hali ya juu, huyu ni Waziri pekee ambaye anapofanya ziara Majimboni mwetu amekuwa anawahusisha Wabunge kikamilifu na kuelekeza Wakandarasi wafanye kazi na Wabunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, nimpongeze Waziri Kalemani kwa kutoa fedha kwa ajili ya kuunganisha umeme kwenye visima vya maji ambavyo vilikuwa vinatumia mashine za *diesel.* Hakika hatua hii itarahisisha na kupunguza gharama za uendeshaji wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kuendelea kusisitiza umeme wa *REA III* unaenda kila kijiji, kitongoji na kila kaya, bado kuna malalamiko mengi sana kuhusu usambazaji huo. Baadhi ya makandarasi wamekuwa hawawashirikishi kabisa viongozi wa maeneo (Vijiji/Kata) na wanaenda kufanya kazi wenyewe, hivyo kufanya zoezi zima kutokuwa shirikishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii inafanya maeneo muhimu ya huduma kama visima vya maji, shule na kadhalika kuachwa, pia kuna malalamiko mengi juu ya usambazaji mdogo kwenye baadhi ya maeneo, hivi mkandarasi amepangiwa kufanya usambazaji wa umeme katika kila kijiji kwa kilometa ngapi na kwa kaya ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila kuwa na malengo haya makandarasi wataiibia Serikali na wananchi. Mfano, katika Vijiji vya Gongali, Endabash, Basodawish, Kansay, Endamaraneck, ni baadhi tu ya vitongoji vimepata umeme na vitongoji vingi bado, pia, vijiji vya *REA III* bado kazi haijaanza, mkandarasi bado kabisa hajaonekana.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* ameonesha katika taarifa yake ya 2016/2017 kuwa Serikali/ *TANESCO* inabeba mzigo wa kesi dhidi ya *Standard Charterd Bank* iliyopo *ICSID.* Kwenye taarifa ya *PAC* Novemba, 2014 Bunge lilieleza kuwa kampuni ya *PAP/IPTL* ilitoa *deed of indemnity* kukabili kesi zote dhidi ya nchi yetu, kwa nini Serikali/ *TANESCO* inabeba kesi ambayo siyo yake? Kwa nini kampuni ya *IPTL* haiendelei na kesi yake? Kwa nini Serikali inalipia gharama za kesi hii? Wanasheria wa Serikali wanafanya kazi gani kushindwa kutafsiri *deed of indemnity?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Septemba, 2016 *ICSID* waliipa tuzo *SCBHK* ya Dola milioni 148.4 ambazo kimsingi ni fedha zilizokuwemo kwenye akaunti ya Tegeta *Escrow BOT.* Kwa nini Serikali haikutumia *deed of indemnity* kuitaka *IPTL/ PAP* kurejesha fedha za Tegeta *Escrow* na kuwalipa hao *SCBHK?*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumeingizwa kwenye kesi isiyo yetu na Serikali imeingia mzima mzima kana kwamba hatuna Wanasheria. Hoja za *CAG* (Uk. 30 – 31) Kitabu cha Mashirika ya Umma kinaonesha kuwa Serikali inafanya uzembe na kuingia gharama kubwa sana za Mawakili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali itumie *deed of indemnity* kuhakikisha Tanzania haipati hasara kubwa huko *ICSID.* Kesi iliyopo Mahakamani haina maana kuwa fedha za Tegeta *Escrow* hazitumiki na kama tutalipishwa fidia ya dola milioni 614 kutokana na kesi huko *ICSID.* Tanzania ipo kwenye kesi ambayo siyo yake, Tanzania haina mkataba na *SCBHK. SCBHK* na *IPTL/PAP* waendelee na mambo yao sisi hatumo. Serikali isiingize nchi kwenye hasara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umeme wa Jua Kigoma. Mwekezaji amemaliza kufunga *5MW* Manispaa ya Kigoma Ujiji kwa ajili ya kuingiza kwenye Gridi ya Kigoma. Mpaka leo *TANESCO* bado hawajaunganisha umeme huu. Gharama za kuzalisha umeme Kigoma ni kubwa mno. Mradi huu ungepunguza japo kidogo gharama hizi. Kwa nini Serikali

inakatisha tamaa uwekezaji? Umeme huu wa jua ungefanya Kigoma kuwa Mji wa kwanza *EAC* kutumia *renewable energy* mchana kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali imalize suala hili ili utekelezaji wa mkataba ufanyike.

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri kwa kazi zao pamoja na jitihada kubwa waliyonayo. Hoja zangu ni zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya umeme kwa *ZECO.* Shirika letu la *TANESCO* linafanya kazi kubwa sana kusambaza umeme, kuhakikisha kwamba, wananchi wengi wanakuza vipato vyao na uchumi wao kupitia nishati ya umeme. Katika kuhakikisha hilo mara nyingine kumekuwa kukitolewa hata *offers* kwa wananchi ili waweze kuunga umeme kwa bei ya chini. Hata hivyo, *TANESCO* imekuwa ikiiuzia *ZECO* umeme kwa bei kubwa mno. Katika lengo hilo *ZECO* imekuwa ikigharamia baadhi ya kazi ili wananchi wa Zanzibar waweze kupata nishati ya umeme na kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa na vikao kadhaa juu ya suala hili, lakini kumekuwa na ugumu juu ya utekelezaji wake. *ZECO* inanunua umeme *(High Voltage)* kwa ajili ya kuusambaza kwa wananchi wa Zanzibar. Katika miaka ya nyuma *ZECO* ilikuwa katika *category* ya *bulk purchaser,* hivyo ikipata *preferential treatment* na kumekuwa na punguzo la umeme. Kwa sasa imeondolewa na kumekuwa na *high increase* ya umeme kwa upande wa *ZECO,* kwa nini? Kuna nini hapa? Hivi kwa nini Wizara imekuwa na kigugumizi kutatua changamoto hii kwa miaka mingi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kero nyingine ya Muungano. Haiwezekani bei ya umeme kwa *ZECO,* ambalo ni Shirika la Serikali ikawa sawa na bei ya umeme kwa kampuni binafsi ya saruji, haiwezekani. *The same goes to* Pemba, ambako *ZECO* inanunua umeme wa *medium voltage,* lakini bado gharama ni kubwa mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, deni la umeme kwa Taasisi za Muungano zilizopo Zanzibar. Taasisi za Muungano kama Jeshi letu la Ulinzi na Polisi zilizopo Zanzibar zinatumia umeme unaogharamiwa na *ZECO,* lakini cha kusikitisha malipo ya umeme yanalipwa kwa *TANESCO* badala ya *portion* ya Zanzibar kulipwa kwa *ZECO,* je, hili nalo litatatuliwa lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana.

**MHE. ALLY S. UNGANDO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani Matogolo Chananja Kalemani, kwa maandishi:

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umeme wa gridi ya Taifa. Sina budi kumpongeza Waziri na Naibu wake kwa kutuunganisha umeme katika Jimbo langu la Kibiti kwenye gridi ya Taifa. Sasa umeme kukatika katika limekuwa jambo la historia kwani zamani umeme maeneo yetu ya Kibiti ulikuwa kama *indicator* ya taa ya gari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kwenye Mamlaka ya Mji Mdogo Kibiti. Kwenye Jimbo langu la Kibiti ambalo lina Kata tatu za Kibiti, Dimani, Mtawanya, ambapo jumla ya vitongoji 42 ambavyo vitongoji vyake vyote havina umeme. Kwa hiyo, Serikali sikivu inayoongozwa na Rais wetu kipenzi cha watu wanyonge tunaomba watuangalie kwa jicho la huruma, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, kutupatia umeme kwenye maeneo hayo kama Makema, Msoro, Bumba, Ugezi, Zimbwini, Mkunama, Magogo Matatu na maeneo mengine kwani, mji mdogo huu unakua kwa kasi, naomba tupatiwe umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umeme vijiji viporo. Katika Jimbo langu la Kibiti kuna kuna vijiji ambavyo mkandarasi ameviteleekeza kwa muda mrefu. Nguzo zipo na waya zipo kwa muda mrefu na kwa kiu ya kutaka umeme tunaendelea kuzilinda nguzo hizo, nataka Kauli ya Serikali, lini kazi hii itakamilika? Vijiji hivyo ni kama Nyamatanga, Ruaruke, Kikale na Mtunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme maeneo ya Delta; Jimbo la Kibiti lina jumla ya Kata 16, vijiji 58 na vitongoji 272. Kati ya Kata hizo, tano zipo maeneo ya Delta kama Kata ya Salale, Mbuchi, Msala, Maparoni, Kiongoroni, ambazo zinafanya jumla ya vijiji 17 sawa na vitongoji 72 ambavyo vijiji hivyo vyote havina umeme. Naiomba Serikali yangu ya ‘Hapa Kazi Tu’ tupate hata umeme jua kwa visiwa hivi katika maeneo ya Delta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijiji ambavyo hadi leo havina umeme Jimboni Kibiti. Katika Jimbo la Kibiti kuna baadhi ya Kata, vijiji vyake havina umeme kama Vijiji vya Nyamwimbe, Machepe, Motomoto, Mtana, Ngondae, Nyakuvyo, Tomoni, Nyambunda, Nyambili, Kingunguli, Mkenda, Kivinja B, Matumbu. Naomba vijiji hivi vipatiwe umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fidia mradi wa Kilwa *Energy Kinyerezi,* wananchi wangu wa maeneo ya Jaribu Mpakani, Nyamwimbe, Bungu, Kibiti, Pagae, naomba Mheshimiwa Waziri nipate kauli ya Serikali lini wananchi hawa watapata fidia yao ili waweze kufanya shughuli za kimaendeleo, kama kupeleka watoto shule kwa kulipia na kununulia vitendea kazi ili mwanafunzi atimize wajibu wake? Tena cha kusikitisha zaidi wapo baadhi wamepewa hadi cheki, lakini benki pesa hakuna.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuweza kuchangia Wizara ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bomba la Mafuta toka Hoima - Uganda hadi Chongoleani, Tanga, Tanzania ni jambo jema kupata mradi tajwa hapo juu na nashukuru kuwa Tanga itakuwa ndiyo kituo kikuu *(last destination)* ambapo patakuwepo na shughuli nyingi za nishati ya mafuta kama vile *refineries, pumping machines, tankers* na kadhalika. Ushauri wangu kwa Serikali katika kila hatua uwepo ushirikishwaji kwa wananchi, viongozi wa ngazi mbalimbali na kila kitu kiwekwe wazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa ajira utakapowadia wakazi wangu (watu wa Tanga) wapewe kipaumbele cha kwanza. Pamoja na kuwa watahitajika wafanyakazi wenye taaluma *(Skilled Labours),* lakini pia, watahitajika wafanyakazi ambao watafanya kazi zisizo za kitaalam *(Unskilled Labours),* naomba katika maeneo yote mawili watu wa Tanga tumejiandaa kufanya kazi katika mradi huu, naomba tupewe kipaumbele cha kwanza *(First Priority).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* kuendeshwa kwa hasara, bila ya umeme wa uhakika Tanzania ya viwanda itakuwa ni hadithi ya paukwa pakawa, kwani ni muda mrefu sasa umeme unakatikakatika na wakati mwingine hata zaidi ya saa tatu hadi tano. Je, mitambo ya kiwanda ikizimwa zaidi ya saa tatu hadi tano hasara ya kulipa mishahara vibarua nani ataweza kufidia?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TANESCO* mara zote linapozuka balaa la ufisadi Tanzania, *TANESCO* lazima inahusika, hili linanitia shaka na Serikali mara zote haina majibu yaliyoshiba. Mfano wa ufisadi uliohusika na *TANESCO* ni kama vile *RICHMOND, IPTL, SONGAS,* inalipwa *US$ 5 million* kwa mwezi kwa miaka 11, itakuwa ni shilingi 1.3 trilioni. Hata katika *CAG Report* ya *Profesa* Assad ameelezea ufisadi uliopo. Inapokuwa fedha hazitumiki vizuri katika miradi hii ya umeme, je, kuna wawekezaji wa viwanda ambao watakuja kujenga viwanda?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, tuige mfano wa Uganda ambayo 1999 walifanya *reform* ambayo baada ya miaka 18 wameweza kupata faida kama mwaka 2017 faida ni bilioni 100 na gawio kwa Serikali ni 57.5 bilioni. Naamini ikiwa Uganda wameweza na Tanzania tunaweza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi zinazodaiwa na *TANESCO* zilipe ili deni lisizidi kuongezeka kwani, hadi Februari, 2018 deni ni shilingi 969 bilioni. Badala ya kuwakatia umeme

wananchi kwa madeni madogo madogo, izikatie hata taasisi za Serikali zenye madeni makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya umeme na gesi Tanzania kuwa ghali mno; katika tafiti mbalimbali zilizofanywa na wataalam wa masuala ya uzalishaji viwandani, wamegundua Tanzania bei ya umeme na gesi ni ghali mno, tofauti na nchi zote duniani hivyo, kusababisha wananchi wa Tanzania hata wale ambao tayari wanatumia umeme hawautumii kwa mapishi majumbani, hali inayosababisha kushamiri kwa biashara ya mkaa mijini na vijijini. Katika nchi zote za *SADC* ni Tanzania tu ndiyo tunaposafiri tunaona biashara ya magunia ya mkaa na kuni pembeni mwa barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwa Serikali, Serikali ipunguze bei ya *unit* ya umeme tulingane na nchi nyingine duniani hali kadhalika gesi ishushwe bei. Shirika la *TANESCO* ligawanywe na zikaribishwe kampuni nyingine kama ilivyo katika huduma za simu, mfano *tiGO, Vodacom, Zantel, TTCL* na *Airtel,* tuondoe *monopoly system.* Pamoja na umeme wa *hydroelectric power, gas,* makaa ya mawe, lakini tutafute vyanzo vipya vya umeme kama vile *solar power system* na umeme wa upepo *(wind electric).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa *REA* – Tanga; nashukuru angalau umefika katika baadhi ya vijiji, lakini bado haujatosheleza. Yapo maeneo nguzo zilikuwa ni chache na wengine hawajapelekewa na mfano ni katika Kata za Kiomoni, Tangasisi, Masiwani Shamba, Tongoni, Mabokweni, Chongoleani, Marungu, Kirare, Mzizima na Maweni.Kata ya Kiomoni majina ya Vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Pande Marembwe, Ndumi, Muheza, Mavumbi, Masai, Kivuleni. Kata ya Kiomoni, majina ya vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Pande Marembwe, Ndumi, Muheza, Mavumbi, Masai, Kivuleni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata ya Tangasisi majina ya vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Machui A & B, Kiwavu, Kivindani, Msengenyeni Kata ya Masiwani Shamba majina ya

vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Masiwani Shamba, Mbugani, Magomeni, Kwaramsingi; Kata ya Tongoni majina ya Vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Sadani, Tongoni, Kivindani, Lumbwa, Amani, Mwarongo, Mondura, Tambarani. Kata ya Mabokweni majina ya Vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Kibafuta, Mikweni, Kiruku, Mchanga Mweupe, Mchanga Mwekundu, Magunduro. Kata ya Chongoleani majina ya Vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Chongoleani, Putini, Mpirani, Ndaoya, Helani, Mvuuni, Bwagamoyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Kata ya Marungu majina ya vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Geza Barabarani, Geza Ndani, Migombani na Mkembe. Kata ya Kirare, majina ya Vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Mapojoni, Mtakuja, Tunda Uwa, Kirare B. Kata ya Mzizima majina ya Vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Kihongwe, Pangarawe, Mleni, Rubawa, Zaire, Kijiji cha Wafugaji. Kata ya Maweni majina ya Vijiji ambavyo *REA* inahitajika ni Kange *Block D,* Kasera, Kange Kijijini, Mzimuni, Songea, Jaributena, Kange Mkurumuzi, Kichangani na Mwisho wa Shamba

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua nafasi hii kushukuru kwa nafasi hii ya kuweza kutoa mchango wangu katika Wizara hii kwa maandishi. Ni imani yangu kuwa, mchango huu utachukuliwa na kufanyiwa kazi, pia pale panapohitaji majibu patajibiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuona umuhimu mkubwa wa Wizara hii na hatimaye kuitoa kwenye Wizara ya Madini na kuiunda hii yenyewe peke yake ili ufanisi zaidi uweze kufanyika na kuleta tija, ahsante sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati Dkt. Kalemani na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Subira Mgalu kwa kazi nzuri sana wanayoifanya. Tangu wamekabidhiwa Wizara hii ilipoundwa wameonesha uwezo mkubwa sana. Mungu awabariki sana na waendelee na juhudi zao hizi katika kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, pongezi zangu nyingi zifike kwa Kaka yangu Dkt. Mwinyimvua ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara hii ya Nishati kwani umakini wake katika kuendesha Wizara hii unaonekana kwa kusimamia vizuri Watendaji wote katika Wizara na vitengo vyake vyote na ndiyo maana mambo yanaenda vizuri. Hongera sana katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ninayotaka kuzungumzia kwa niaba ya wananchi wa Mkoa wa Singida ni pamoja na kutoa shukrani nyingi sana kwa hatua kubwa ambayo Serikali imefikia kuhusu mradi wa umeme wa upepo wa Singida – *Wind East Africa (WEA) Mw 100*, tunashukuru sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Waziri ameahidi kwenye ukurasa wa 33 wa kitabu cha hotuba yake kuwa, utekelezaji au ujenzi wa mradi huu utaanza/unatarajiwa kuanza mwezi Oktoba, 2018 na kukamilika mwezi Disemba, 2020. Ushauri wangu ni kwamba ili tuendane na kauli/ahadi hii kwa wananchi na Bunge ni vema majadiliano ya mkataba wa kibiashara *(PPA)* kati ya *TANESCO* na Kampuni ya *Wind East Africa (WEA)* yafanyike na kukamilika kwa wakati ili kuweza kufikia lengo la kauli ya Waziri hapa Bungeni na kuweza kukamilika kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili naomba Waziri awe makini na watendaji wetu kwani, kuna wakati huwa wanajisahau na matokeo yake atakayebanwa maswali humu ndani ni Waziri. Nisingefurahi Mawaziri wangu wabanwe maswali na kuanza kutafuta majibu ambayo hayapo. Huo ni ushauri tu wa kuwa makini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ni kuhusu mradi wa *Stiegler's Gorge.* Mradi huu siyo mpya ni kama ilivyo tu mradi wa kuhamia Dodoma. Mradi huu ulibuniwa na kusanifiwa tangu wakati wa Mwalimu Nyerere Baba wa Taifa. Kinachofanyika sasa hivi ni utekelezaji tu na kweli hii ni heshima kubwa sana kwa Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere na hii ndiyo dhana halisi ya kumuenzi kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa maji bado ni chanzo kikubwa sana cha umeme duniani hasa kwa nchi zinazoendelea na ni wa gharama nafuu. Pia, huwezi kutegemea chanzo kimoja tu cha umeme ni lazima tuwe na vyanzo vingine. Hakuna nchi yoyote iliyowahi kujenga bwawa kubwa bila kunyoshewa kidole na wana mazingira. Hivyo, tusiogope kwani hata Marekani na China ndiyo nchi zenye mabwawa makubwa sana duniani ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawatia moyo na kuwashauri waendelee na utekelezaji wa kujenga mradi huo kwani utakuwa ni ukombozi mkubwa kwa Taifa hili. Jambo la msingi wawe na uangalifu sana kusiingie dosari ya kifisadi kwani itatutia doa hasa Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uaminifu na uzalendo utangulie na kuweka mbele maslahi ya Taifa. Tumpe heshima na shukrani Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli ambaye amedhamiria kwa dhati kujenga uchumi wa viwanda wa kuliingiza Taifa katika uchumi wa kati, leo hii wanaopinga kesho ndiyo watakaopongeza. Nawatakia kila la heri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ili kuwapa imani ya subira wananchi wa maeneo yote ambayo yametajwa kwenye *REA III* na walioachwa katika *REA II.* Wajitahidi watangulize nguzo za umeme kwa wingi kila eneo husika, huku wakiendelea na ujenzi wa miundombinu ya kufikisha umeme. Ukweli kelele ni nyingi sana vijijini, wanaona kama tumewatenga, hii yote ni kutokana na uelewa, elimu na shughuli za kibiashara na maendeleo ambayo yameshamiri vijijini, tafadhali *REA* ndiyo mwarobaini wa maendeleo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya niipongeze *TPDC* wamekuwa na ufanisi mzuri katika kusimamia utekelezaji wa gesi asilia na kuhakikisha wanaendelea kupata wateja ambao ni viwandani na

majumbani na kwenye taasisi kama magereza na kadhalika. Hongera sana kwa kuanza kusambaza pia majumbani katika Mkoa wa Dar-es-Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, kwa hatua ambayo wanaendelea kuikamilisha ili utekelezaji uanze kwa Mikoa iliyotajwa katika hotuba ya Waziri Ukurasa wa 81. Hii ni hatua nzuri kwani, itasaidia kuokoa mazingira ya utumiaji wa kuni, hasa kwenye taasisi kama za Magereza. Nina ushahidi wa Magereza ya Ushora Ndago, Wilaya ya Iramba, Singida wamemaliza msitu mkubwa ambao ulikuwa unahifadhi tembo, simba, chui na wanyama wengine, hivyo kwa kupeleka nishati hii ya gesi asilia itaokoa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kama unaweza kutekelezeka, uwekwe utaratibu wa kupelekewa mitungi mikubwa ya gesi kwenye taasisi hizo kama magereza na kadhalika, wakati wakisubiri kufunga mabomba ya kupeleka. Hongera *TPDC* na nawatakiwa utekelezaji mwema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kumpongeza Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara hii, watambue kuwa changamoto ndiyo chachu ya maendeleo. Bila changamoto maendeleo husuasua, hivyo wazipokee changamoto zote na maoni yote ya Wabunge ili kwao iwe ni kichocheo cha kusonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuunga mkono hoja kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Nishati kwa mwaka wa fedha 2017/2018, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi, kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya. Hongereni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali na uongozi wa Awamu ya Tano kwa kuwa na nia ya dhati ya

kuhakikisha kuwa sekta ya Nishati inakuwa na mchango mkubwa katika ukuzaji wa sekta ya viwanda ili nchi yetu iweze kupiga hatua za kimaendeleo kufikia uchumi wa kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kufikia malengo hayo kama Taifa tuna wajibu wa kuhakikisha kuwa *TANESCO* inaendeshwa kwa ufanisi mkubwa. Hivyo, kwa kuwa hali ya kifedha ya *TANESCO* ni mbaya kutokana na kuelemewa na mzigo mkubwa wa madeni na kwa kuwa zipo hisia kuwa shirika hili ni kubwa kuliko Wizara nyingi za Serikali na hivyo kama Shirika kongwe la Umma litakuwa na changamoto za kiufanisi siku zote likiendelea kuwa kama lilivyo, nashauri Serikali ione uwezekano wa kufanya *financial and functional unbundling*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kufanya hivi hata kama *TANESCO* itabaki kuwa na *Apex Company* moja, nashauri uzalishaji, usafirishaji na usambazaji viwe na utawala tofauti na *accounts* tofauti. Utekelezaji wa mpango huu utaenda sawia na *ESI roadmap* ya 2014 hata kama siyo vile ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili nchi yetu iweze kuwa na umeme wa kutosha na hivyo kuwa chachu ya kuleta maendeleo ya viwanda na maisha bora kwa wananchi, kama Taifa tunahitaji fedha nyingi sana kutokana na gharama kubwa za uwekezaji kwa ajili ya kujenga miradi ya uzalishaji umeme kufikia 5,000 *MW* ambazo Serikali imeahidi kuzifikia 2020. Ujenzi wa miradi ya usafirishaji wa umeme *(transmission) 132kv, 220kv* na *400kv* zaidi ya kilomita 3000, miradi ya kuunganisha *grid* yetu na zile za nchi jirani na hata usambazaji wa umeme nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri Serikali ione uwezekano wa kuwa na mfumo madhubuti utakaowezesha kukaribisha uwekezaji wa kiushindani toka kwa wawekezaji binafsi kwenye maeneo ya uzalishaji na hata usambazaji ili kuepuka Serikali kuelemewa na madeni ya kukopa kwa ajili ya miradi hiyo. Jambo la msingi hapa ni kuhakikisha wawekezaji hao wanakuja kuwekeza kwa kuzingatia

masharti yetu hususan bei ya kununulia umeme utakaozalishwa na kutokubali *capacity charges* ambazo kimsingi zimeliumiza sana Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi nyingi zinazoendelea mfano Afrika ya Kusini, Thailand, India, Brazil, China, Mexico na kadhalika zimepata maendeleo ya haraka ya viwanda. Chachu ya maendeleo hayo ni uwepo wa umeme wa uhakika kufuatia wawekezaji binafsi ambao wamepatikana kupitia mfumo wa kuendesha tenda au minada ya makampuni ya kuzalisha umeme kwa kuwapa bei elekezi. Aidha, mchakato uliowezesha kupatikana kwa bei elekezi hizi umeandaliwa na vitengo vya usimamizi vya Serikali na *Regulators*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwezekana kwa jambo hili kunategemea sana kuwepo uwazi na weledi katika kuendesha ushindani huo. Tukiweza kufanya hivi naamini tutaweza kupata maendeleo ya haraka zaidi kuliko Serikali kukopa hela na kujenga miradi hiyo na kuipa *TANESCO* kama zawadi bila *TANESCO* kuwekeza yenyewe maana haikopesheki na inachukuliwa miradi hiyo inayokabidhiwa kama mali ya umma tu bila kuwajibika ku-*service* mikopo hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* haipaswi kuwa mzigo wa kila Mtanzania atakayebebeshwa madeni ambayo Serikali inakopa na badala yake *reform* zikifanyika *TANESCO* inapaswa kujiendesha kama ilivyokuwa miaka ya nyuma. Bila kutatua tatizo la kimfumo la *TANESCO* ambalo ndilo tatizo la msingi, tutegemee kuwa hata mradi wa Mto Rufiji ukijengwa na kukabidhiwa *TANESCO* tatizo litaendelea kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mipango yote mizuri ya bajeti hii, ni vema Wizara ikalieleza Bunge lako kinagaubaga imejipanga vipi kushughulikia deni la *TANESCO* ili hata kama *reform* zinafanyika madeni yasiingizwe katika mgawanyo utakaotokea. Katika hili la kumaliza tatizo la madeni ya *TANESCO* nashauri tujifunze kwa wenzetu wa

Ghana ambao kupitia *energy bond* wameweza kupata fedha nyingi ambazo zimeweza kusaidia kuondokana na mzigo wa madeni makubwa kwenye sekta ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hotuba ya Waziri amezungumzia makampuni yanayojenga vyanzo vya uzalishaji na usambazaji umeme kwenye maeneo ambapo *Grid* ya Taifa haitafika. Naishauri Serikali iweke wazi taratibu zinazoongoza uwekezaji huo ili pindi Serikali itakapofikisha *grid* kwenye maeneo hayo, uwekezaji uliofanyika ujulikane unaingizwa kwenye mfumo wa *grid*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe kuwa lengo la kuanzisha hizi *mini grid* ni kuwapatia maisha bora wananchi wetu. Hivyo Wizara ya Nishati kwa kushirikiana na *EWURA* ni vema ikaweka utaratibu wa kueleweka na wa wazi wa kuwavutia watakaotaka kuwekeza katika maeneo haya ya *mini grids*. *EWURA* pia ipitie bei zote za wawekezaji hawa ili kusiwepo na nafasi ya kuwaumiza watumiaji wa umeme huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, lakini nina mchango ufuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani kwa uchapakazi uliotukuka na vilevile Naibu Waziri wake Mgalu wanafanya kazi sana na wanazingatia maeneo yote na wanaenda kuangaza Tanzania. Muda si mrefu matokeo nimeyaona kwa namna miradi inatekelezwa kila Wilaya na ufuatiliaji unafanyika vizuri kabisa na viongozi wa Wizara hii *Meaning* Waziri na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri Kalemani ndio Waziri pekee aliyefika Jimbo la Nkasi Kusini tarafa ya Wampembe ambapo hakuna Waziri wala Naibu Waziri aliyetembelea kuona changamoto mbalimbali zinazotokea kwenye jimbo

hili ambalo lipo pembezoni. Kwa hiyo, wananchi wa jimbo langu wamenituma niwaeleze Watanzania kupitia hotuba yangu Bungeni ili wajue juhudi za Mheshimiwa Waziri huyu kwa juhudi zake yapo maeneo yaliyokuwa yamebaki kwenye orodha ya vjiji vinavyoenda kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilipomwona aliweza kuvipa miradi, Vijiji hivyo ni Katani, Kisura, Malongwe, Nkomolo II, Nchenje, Sintali, Nkana, Mkomachinda, Kilambo, Mlambo, Mpasa, Chiwa Ntemba hadi vijiji vya Kata ya Wampembe na bado anasisitiza miradi hiyo itekelezwe mapema inavyowezekana. Naomba nimpongeze.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maombi; ombi la kwanza, naomba umeme upelekwe Kata ya , Vijjji vya Kisambala Ninde Msamba, Kaanga na Mkivinga vilevile Lyapinda Lupata, Izinga, Mwinza, Lusembwa na Itanga na kufikia hapo Wizara itakuwa imemaliza kupeleka vijiji vyote vya Nkasi Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ombi la pili, Utafiti wa Madini na Mafuta. Kwenye Jimbo la Nkasi Kusini kandokando ya Ziwa Tanganyika na milima ya Lyambalya Mfipa. Serikali itowe fedha bila kuchelewesha hasa zile ambazo zimewekewa zuio na vilevile hazina itowe hela kwa 100% kwenye Wizara hii. Ahsanteni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ianze kuona umuhimu wa kushirikisha sekta binafsi kwa hatua za kufufua umeme, kusafirisha umeme, kutawanya umeme. Ili tuwe na vyanzo vingi vya umeme, *energy mix* ni muhimu sana.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jimbo langu lina vijiji 115, lakini mpaka sasa hivi ni vijiji 15 ndio vimepata umeme. Vijiji 100 havina umeme, je, wananchi wa jimbo hili hawana haki ya kupata umeme? Je, viwanda katika jimbo langu itawezekanaje bila ya umeme? Ukanda wa Ziwa Rukwa ndio

wenye fursa ya kujenga viwanda ila kikwazo ni umeme, wapeleke umeme Ukanda wa Ziwa Rukwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jimbo langu ipo mito mingi yenye maporomoko ya maji yenye sifa ya kufua umeme wa nguvu ya maji. Mfano, ni Mto Nzovwe ulishafanyiwa utafiti wa kufua umeme *watt* 10 naomba mto huu utumike kuongeza umeme katika Mkoa wa Rukwa. Kwa sasa utawanyaji wa umeme unasuasua, tatizo ni ukosefu wa nguzo za umeme, Serikali ilifanyie kazi tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakandarasi kutolipwa fedha, kunawafanya washindwe kufanya kazi kwa haraka. Tunataka Serikali iwapatia fedha ili wakamilishe haraka.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *REA*. Jimbo la Geita Mjini lina vijiji /mitaa 72 na kata 13, karibu asilimia 80 ya vijiji vipo nje ya Kata za Kalanyaka, Nyankumbu na Buholahala ambazo ndizo zipo mjini, lakini kwenye mradi unaoendelea hivi sasa mkandarasi anasema amepewa mitaa isiyozidi 20, matokeo yake mitaa zaidi ya 50 haikupata umeme kwenye awamu ya III ambayo ni ya mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ambayo tayari nimewasilisha kwao maombi ya pitio la mradi unaoendelea hivi sasa ili umeme wa *REA* katika Kata za Ihanamilo, Nyanguku, Kamla, Shilolezi, Mgusu, Ntakuja, Nyankumbu na Bung'akoko. Maeneo haya kuna sehemu wametupatia mtaa mmoja na sehemu zingine hakuna kabisa. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kuwa Mkandarasi yupo *site* marekebisho haya yafanyike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nishati ya Gesi; Tanzania tunapambana na matumizi makubwa ya mkaa na kuni kuokoa mazingira, kazi hii haiwezi kufanikiwa kama taasisi kubwa zitaendelea kutumia kuni na mkaa. Naishauri Wizara kwa kushirikiana na Wizara zingine kuleta marekebisho ya sheria ambayo yatalazimisha taasisi kutumia gesi ili jambo hili liweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, punguzo maalum la kodi kwenye vifaa vya gesi na gesi yenyewe inayokwenda kutumika kwenye taasisi ni suala la lazima. Mfano kama shule, kununua kuni kwa Sh1,000,000/= kwa mwaka iwapo mtumiaji wa kuni ataweza kutumia pesa ileile au pungufu hakuna atakayebaki anatumia mkaa. Naishauri Serikali kuondoa kodi kwenye gesi na vifaa vyake kama majiko makubwa yanayofaa kwa shule na *hotels*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda mrefu wa kusubiri kuunganishiwa umeme; bado tatizo la muda mrefu unaochukuliwa na *TANESCO* kuunganisha umeme kwa mteja mara baada ya kulipa gharama zote halali. Wananchi wengi wamehusika kujenga viwanda lakini malalamiko ya ucheleweshwaji mkubwa wa huduma yanaendelea Mkoani Geita. Naishauri Serikali kuleta utaratibu utakaofanya huduma hii kupatikana na kwa haraka kuondoa usumbufu uliopo hivi sasa.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kijiji cha Malongolo, Kata ya Dumila, Wilayani Kilosa Mkoani Morogoro zaidi ya miaka mitano (5) nguzo zimelala chini na zimeanza kuharibika, lakini wananchi hawana umeme. Serikali kupitia Wizara hii iangalie namna ya kuokoa fedha za nguzo kuoza na zimenunuliwa na kodi za Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa *REA* bado haujawafikia wananchi wengi vijijini na wapo wananchi wanatamani umeme huu hawana uwezo wa kulipia gharama za kuunganishwa. Kwa nini Serikali isije na mpango wa kusaidia wananchi wenye kipato kidogo kuwakopesha umeme na wakaendelea kulipa *indirect way* kwa kupitia mita/au *charge* za matumizi *per unit* ili kuongeza wigo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mtaa wa Lugala, Kata ya Mindu katika Manispaa ya Morogoro wanapitiwa na umeme

wa gridi ya Taifa lakini hawana umeme tangu uhuru na sio hilo eneo la Lugala yapo maeneo mengi nchini yanapitiwa gridi ya Taifa lakini hawana umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tozo la asilimia 2%; *EWURA* asilimia 1% kwenye umeme ziko wapi fedha hizi? Zinafanya kazi gani na ni lini tutapata majibu sahihi juu ya tozo hizi ambazo wananchi wanakatwa na zinarudije kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vyanzo vya umeme Kidatu Mtera; mkakati gani Wizara inasaidia wananchi wanaozunguka vyanzo hivyo kulinda mazingira, mfano, mito inakoanzia wananchi wanasaidiwaje kulinda mazingira ili kuhakikisha upatikanaji wa maji mwaka mzima hata wakati wa kiangazi.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kumpongeza Waziri wa Nishati Mheshimiwa Dkt. Kalemani na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nampongeza Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa juhudi kubwa anayofanya kuongeza umeme wa uhakika katika Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi naomba sasa nichangie hoja ya Wizara ya Nishati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, ili ahadi ya Ilani ya Chama Tawala (CCM) ya 2015 – 2020 iweze kutekelezwa kuhusu kupeleka umeme katika kila kijiji nchini mwetu, Wizara hii ipewe fedha zote walizoomba ili ahadi hiyo iweze kutekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa ni vijiji 19 tu kati ya vijiji 49 vya Wilaya ya Longido ndio zimeshafikiwa na umeme wa *REA* tangu mpango huu uanze hadi sasa, naomba Serikali iongeze kasi ya utekelezaji wa Mradi wa *REA* na ihakikishe kuwa vijiji 30 vilivyosalia Wilayani Longido

vinajumuishwa katika orodha ya vijiji vitakavyopata umeme katika awamu ya *REA III* inayoanza mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuishauri Serikali iwekeze katika miradi mingine ya umeme jadidifu *(Renewable energy)* kama vile nguvu za jua *(Solar power)*, na upepo *(wind power)* ili ku-*supplement* vyanzo vya umeme wa *REA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naomba kuunga mkono maoni yaliyotolewa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini kupitia Taarifa yao kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Nishati. Aidha, naungana nao katika kuishauri Serikali ihakikishe kuwa utekelezaji wa miradi ya umeme vijijini awamu hii ya III uzingatie sana ushirikishwaji wa wananchi pamoja na viongozi wa jamii katika kila eneo husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Serikali iwasimamie wakandarasi wa miradi ya *REA* kwa karibu ili wafanye kazi kwa weledi na ubora ili Watanzania waweze kupata *value for their money.* Sambamba na hili naomba Serikali ipeleke malipo kwa Wakandarasi kwa wakati ili nao waweze ku-*deliver* miradi husika kikamilifu na kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maeneo ambayo miradi ya umeme nchini inahusisha haja ya kufidia watu waishio kwenye njia itakayopitishwa umeme, wafidiwe kwa haraka ili waweze kupisha mradi utekelezwe pasipo vikwazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache, naomba nitamke kuwa naunga mkono hoja.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Wataalam wote wa Wizara kwa juhudi na kazi ya kuwapatia Watanzania umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Waziri kuzindua mradi wa *REA III* Mkoa wa Tabora na wakandarasi kuanza kazi tangu Januari, 2018 kazi yao inakwenda taratibu sana.

Kaliua tulipangiwa vijiji 25 katika *phase I, REA III* lakini mpaka leo hii ni kijiji kimoja tu kimewashwa umeme tena kwa msukumo wa ziara ya Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani mwezi wa Aprili, 2018 Serikali iwafuatilie kwa karibu wakandarasi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, gharama za *TANESCO* kuwapatia wananchi umeme kwa maeneo ambayo hakuna mradi wa *REA* ni kubwa sana kiasi cha wananchi kushindwa kumudu gharama hizo. Nguzo moja wanaambiwa watoe Sh.700,000 mpaka Sh.1,000,000 bado gharama nyingine na *wiring* katika nyumba zao. Nini mpango wa *TANESCO* kuhakikisha umeme unawafikia wananchi vijijini kwa gharama nafuu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha ya *REA* imewekewa uzio itumike kwa kazi ya kupeleka umeme vijijini kwa mpango wa *REA*, lengo la Bunge lilikuwa kusaidia wananchi maskini wa vijijini wapate huduma ya nishati ya umeme kwa haraka. Leo fedha inayotengwa haitolewi kwa wakati pia haitolewi yote kwa ajili ya *REA*. Tunaomba ufafanuzi kwa nini fedha hii inatumika kwenye mambo tofauti na mradi wa *REA*?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na matukio mengi ya moto, nyumba za wananchi kuungua, vyombo vya ndani kuungua, hasara kubwa kwa wananchi kutokana na uwepo wa vifaa bandia/feki vya umeme madukani. Wananchi wengi hatuna uwezo wa kutambua vifaa halisi na vifaa feki, hili ni tatizo kubwa. Serikali inachukua hatua gani kuhakikisha vifaa vyote vya umeme madukani vinakuwa ni *original*. Pia Serikali inasaidiaje wananchi kutambua vifaa *original* na vifaa feki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kuja na mpango wa kujenga *sub-station* kati ya Urambo na Kaliua na nyingine kati ya Kaliua na Uvinza ili kuondoa kero kubwa ya kukatika kwa umeme Kaliua na Urambo. Serikali iharakishe ujenzi wa mradi huu wa *sub-station* hizi mbili ili twende na *speed* ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nguzo za umeme kutoka Tabora kwenda Kaliua zimekuwa zinaanguka mara kwa mara na kusababisha umeme kukatika. Pamoja na Mheshimiwa Waziri kufika Kaliua mara mbili na kutoa maelekezo kwa uongozi wa *TANESCO* Mkoa kubadilisha zile nguzo, bado zoezi hilo halijafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mita za LUKU nyingi zimekuwa zinaharibika mara kwa mara na wananchi kulipa/kununua umeme mara kwa mara huku matumaini yao ni madogo. Serikali ifanye utafiti wa kina katika upatikanaji/uagizaji wa mita za LUKU ambazo hazina usumbufu.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kumpongeza sana Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Medard M. C. Kalemani kwa kazi nzuri sana inayofanyika katika Wizara ya Nishati. Napenda pia nimpongeze sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Subira H. Mgalu kwa juhudi kubwa na kazi nzuri. Kwa dhamira hiyo hiyo niwasifu wafanyakazi wa Wizara, *REA* na *TANESCO* kwa usikivu, kazi nzuri na kuwaomba waendelee na moyo huo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya yangu ya Mwanga iko katika mpango wa *REA* awamu ya I, II na III. Katika awamu ya kwanza, umeme ulipelekwa Kata ya Kwakoa, Kigonigoni na Toloha. Katika Kata ya Toloha, waliomba wananchi 248 waunganishwe na umeme. Pamoja kuwa wengi wao wamepitiwa na nyaya za kusambaza umeme, ni wateja 50 tu ambao wamepewa umeme wengine 198 bado wanalia hawajapatiwa umeme. Katika Kata ya Kigonigoni, wananchi 349 waliomba wapewe umeme, ni waombaji 29 peke yao waliopewa umeme, wananchi 320 bado wanalia. Hatua ilichukuliwa katika ziara ya Naibu Waziri lakini katika kata hii hali haijabadilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *REA* II, lengo ilikuwa kutoa umeme kwa Kata za Kivisini na Jipe. Katika hatua hii kazi iliyofanywa ni chini ya 20%, Mkandarasi aliteuliwa kuifanya kazi hiyo iliyoachwa. Mkandarasi huyo amefanya kidogo tu

kumwonyesha Naibu Waziri katika ziara yake, baada ya Naibu Waziri kuondoka, huyo Mkandarasi naye kaondoka. Hakuna kinachoendelea kwa ahadi tulizopewa, kilichopo Jipe ni aibu kubwa, watusaidie kuondoa aibu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuchagua Wilaya yangu ya Mwanga iwe kituo cha kuzindulia awamu ya III ya Mradi wa *REA*, Mkoa wa Kilimanjaro. Hata hivyo, tangu mradi uzinduliwe ili utekelezaji uanze, hadi leo mkandarasi hajaonekana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wakati anazindua miradi iliyokamilika katika wilaya za wapinzani Mkoa wa Kilimanjaro achukue hatua angalau mradi uanze ujenzi katika Wilaya ya Mwanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii wakati nikiomba Wizara itupie jicho lake katika Wilaya ya Mwanga.

**MHE. PROF. NORMAN A. S. KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza sana Waziri na Naibu Waziri kwa unyenyekevu wao, ni wasikivu na wanampa heshima sana Mheshimiwa Rais, hongera sana. Sasa naomba kuchangia maeneo machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Makete ina vijiji 98, mpaka sasa ni vijiji 28 tu vyenye umeme. Naomba sana Wizara iitazame Wilaya ya Makete kwa jicho la huruma. Tarafa nzima ya Ukwama hakuna umeme, Kata za Lupila, Mbalache, Mang'oto, Ipepo na Ukwama hakuna umeme. Wilaya ya Makete ndiyo inayotoa mchango mkubwa kwenye Mtera, Kidatu, Kihansi – yanatoka Makete. Naomba Serikali itambue hilo na kuenzi jitihada za wananchi kwa kuwapa umeme. Naomba vijiji vilivyobaki vipewe umeme kwenye *REA* Awamu hii ya III.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umeme kwenye Mto Lumakali ulioko Tarafa za Balongwa na Magoma unahitaji bilioni 900 ili tuweze kupata zaidi ya *MW* 340 na 640. Fedha hizi naamini ziko ndani ya uwezo wetu. Usanifu

ulishakamilika na wananchi wa Makete wanasubiri tu bwawa lianze kujengwa ili tuwe na chanzo cha umeme na ajira. Waziri alipokuwa Naibu swali langu mwaka jana 2016/ 2017 alisema bwawa linaanza kujengwa mwaka huu wa fedha, tafadhali sana watimize ahadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ajira na uchumi kutokana na umeme wa Lumakali ni zaidi ya 30,000. Hii ni muhimu ili wananchi wa Makete wapunguze kilimo kwenye vyanzo vya miti ili kudumisha mtiririko kwenye Mto Rufiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme wa upepo, naipongeza Serikali kwa kupeleka nguvu kwenye kuzalisha umeme wa upepo na hasa pale Singida, Makambako na Same. Utekelezaji wa mradi wa umeme kwa kutumia upepo ni faida kubwa sana kwetu na hasa kwa kuwa makampuni yako tayari kutekeleza mradi huu bila kutegemea Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa umeme wa Liganga na Mchuchuma si wa kupuuza hata kidogo. Ni mradi ambao unatupa sisi Watanzania chanzo cha fedha mkaa na chuma. Kwa hiyo, tutapata mkaa, chuma na umeme, pia miradi kama hii ni ya kukimbilia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitoe ushauri kwa Serikali wakati tunawekeza kwenye umeme, tuangalie kiwango tunachozalisha maana tukiwekeza kupita kiasi tutakosa wa kumuuzia maana Kenya, Uganda, Rwanda, DRC na Zambia nchi hizi kwa sasa zinajiimarisha kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Stieglers Gorge*; jitihada zifanyike ili kuimarisha maeneo ambayo ni chanzo cha miti inayochangia maji kwenye Mto Rufiji. Maana ukubwa wa eneo linalokusanya maji kupeleka Mto Rufiji kunaakisi nguvu kubwa kutunza maeneo yanayochangia maji. Hivyo basi Wilaya kama za Makete, Mbarali, Kilombero zipewe kipaumbele katika kutunza mazingira yao ili vyanzo vya maji katika maeneo hayo visiharibiwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kujali shida za Watanzania na kuhakikisha umeme unapatikana katika Tanzania. Mungu ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. JORAM I. HONGOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Serikali hususan Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kumteua Dkt. Medard Kalemani kuwa Waziri wa Nishati na kumteua Mheshimiwa Subira Mgalu kuwa Naibu Waziri. Viongozi hawa wote wawili wamekuwa wasikivu na wafuatiliaji wazuri wa maendeleo ya sekta hii ya nishati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Katibu Mkuu Dkt. Hamis Mwinyimvua pamoja na watendaji wote kwa kazi nzuri wanayoifanya kuhakikisha kwamba Watanzania wote wanapata umeme. Mungu awabariki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa Umeme Vijijini *(REA III)*; mradi wa *REA* unaendelea vizuri lakini kuna baadhi ya maeneo wakandarasi wamekuwa wakiruka mitaa na maeneo muhimu ya kupeleka umeme kama hospitali, vituo vya afya, zahanati, shule, ofisi za Serikali, makanisa na maeneo mengine muhimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano katika Jimbo la Lupembe (Njombe *DC*) kuna mitaa ya Ikoritho, Kata ya Mtwango, Kivitu, Kata ya Igongolo na maeneo mengine ni muhimu Wizara wawasisitize wakandarasi kuhakikisha kwamba maeneo haya muhimu ambako wananchi wanapo na wanahitaji huduma wapeleke umeme kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Makambako – Songea; mradi huu unapitia kwenye Jimbo la Lupembe (Njombe *DC*) umepita katika vijiji vya Kata za Igongolo, Kichiwa na Ikuna. Umeme huu haujapelekwa kwenye shule,

vituo vya afya na ofisi mbalimbali za Serikali. Tuiombe Serikali iwaagize wakandarasi hawa kupeleka umeme kwenye maeneo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la *TANESCO* limekuwa na changamoto nyingi sana hasa madeni makubwa. Pamoja na kukabiliwa na madeni hayo kwa miaka hii miwili ya karibuni, utendaji wa shirika hili umeanza kwenda vizuri. Katika Mkoa wetu wa Njombe nampongeza sana Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa, anajitahidi sana katika kusimamia shughuli za usambazaji wa umeme katika Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkoa wetu ni miongoni mwa mikoa inayopata mvua nyingi zinazoambatana na radi. Mvua hizi zimekuwa zikisababisha kuungua kwa transfoma na kuwa na katizo la umeme. Hivi karibuni mwaka jana na mwaka huu maeneo mengi yamekuwa yakikosa umeme katika Mkoa wa Njombe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa inaonekana transfoma nyingi za *KV* 25 na zinapoharibika inachukua muda mrefu ikiathiri sana uchumi wa Jimbo la Lupembe na Mkoa wa Njombe, ikizingatiwa kwamba shughuli za viwanda zote zinategemea umeme. Niishauri Serikali yangu kuwa na utaratibu wa kuwa na transfoma za kutosha za ziada hasa kwenye maeneo yenye vipindi virefu vya mvua inayoambatana na radi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa uzalishaji wa umeme wa Rufiji (Rufiji *Hydro Power Project*) *MW* 2100. Naipongeza sana Serikali kwa uamuzi wa kizalendo wa kuanzisha huu mradi. Mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya viwanda vya nchi yetu. Uchumi wa viwanda unategemea sana uwepo wa umeme wa kutosha na wa uhakika. Hivyo mradi huu utatupeleka kwenye uchumi wa kati. Hata hivyo, tukikamilisha mradi huu utatusaidia katika kupunguza gharama za umeme na wananchi wa kipato cha chini wataanza kutumia umeme kama nishati ya kupikia. Hivyo utapunguza uharibifu wa mazingira unaofanywa na wanachi ili kupata nishati ya kupikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili mradi huu uwe endelevu ni muhimu kuangalia namna ya kuisaidia Mikoa ya Nyanda za Juu Iringa, Njombe, Morogoro, Mbeya na Songwe katika kuhifadhi mazingira. Wananchi wengi wa mikoa hii wanakata sana miti kwa ajili ya kilimo na kupata nishati. Hivyo ni muhimu vijiji vyote vipelekewe umeme ili wapunguze matumizi ya nishati kuni. Pia tukipeleka umeme utasaidia katika kusambaza maji ya bomba na wananchi watalima bustani zao maeneo ya nyumbani kupitia kilimo cha umwagiliaji na wataondokana na kilimo cha vinyungu na maeneo ya vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Makaa ya Mawe Mchuchuma. Mradi huu ni muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. Makaa ya mawe yatakuwa na faida kuu mbili kwanza mkaa utatumika kwenye viwanda vikubwa kama vile viwanda vya *cement*, viwanda vya mbolea na matumizi ya nishati ya kupikia majumbani. Lakini mradi huu utasaidia kuongeza umeme kwenye *grid* ya Taifa na hatimaye kuwa na uhakika wa kupata umeme hasa pale kunapokuwa na hitilafu kwenye chanzo kimojawapo. Hivyo mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma ni muhimu sana kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho narudia kumpongeza sana Waziri wa Nishati, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii na Watendaji wote na Mwenyezi Mungu aendelee kuwajalia afya njema katika kutekeleza majukumu yao.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri wanayoifanya pamoja na watendaji wote wa Wizara hii. Mchango wangu utajikita kwenye mambo mawili

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, deni la umeme kwa ajili ya Taasisi za Muungano kutakiwa kulipwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Wote tunafahamu kwamba Taasisi zote zilizo chini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mapato yake yote, mishahara, *Administrative*

*process* zote zinafanywa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano. Ni utaratibu upi unaotumika kuhalalisha madeni ya taasisi hizo kuwa ni madeni ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar? Nitaomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake anieleze kwa kina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, utofauti wa bei inayopangwa na *EWURA* na ile inayokubaliwa na *ZECO*. Ukakasi mkubwa unaoletwa na utofauti huu uliopo. Kwa mawazo yangu nilifikiria *EWURA* wangesitisha kupandisha bei ya umeme hadi watakapokubaliana na *ZECO* juu ya hilo. Nafahamu kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inalipa deni la nyuma na la *current* pia, ila sio suluhisho la tatizo hili lililopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ngumu sana kuweza kutatua tatizo bila ya kusitisha chanzo cha tatizo hilo na kwa jinsi inavyoonekana suala hili limekuwa gumu kumalizika kwa vile makubaliano yanayofikiwa ndani ya vikao hayatekelezwi. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja kuhitimisha hoja yake atueleze wapi wamefikia na ni kwa namna gani tunaweza kuliweka sawa hili.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote, nianze kwa kuunga mkono hoja na nimpongeze Mheshimiwa Waziri sanjari na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa hotuba yao nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya *Maurel and Prom* iliingia Mkataba wa kuchimba visima vya gesi Wilayani Mafia mwaka 2004. Kwa maelezo ya watalaam tafiti zilionesha kuna gesi ya kutosha katika kisima cha Ndagoni Mafia. Baada ya kufanya uchimbaji na kufanya majaribio gesi haikuonekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti,Jambo hili watalaam wanaeleza ni jambo la kawaida kwenye tasnia hii. Wakati wanajipanga ili wachimbe tena leseni yao ikawa imeisha na wakawa katika mchakato wa kuhuisha leseni yao, ikaja

sheria mpya ya madini. Nimwombe Mheshimiwa Waziri atakapokuja kujibu atueleze watu wa Mafia, je, gesi ipo na lini itaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni sera ya Serikali ya kupeleka umeme wa nguvu za jua *solar* katika visima vyote nchini. Sera hii ni nzuri naona kwa upande wa Mafia bado visima vya Jibondo, Chole, Juan na Bwejuu hatujaona dalili zozote za kupatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni uzalishaji wa umeme katika Kisiwa cha Mafia. Mafia kwa sasa tunapata umeme unaozalishwa kwa majenereta ya *diesel*. Hizi jenereta zimezeeka na zimekuwa zinaharibika mara kwa mara lakini kubwa zaidi uwezo wake wote jenereta nne ni kuzalisha *megawatt* mbili na kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wa umeme. Umefika wakati sasa Serikali na *TANESCO* waanze mchakato wa kupitisha nyaya chini ya bahari (*submarine cables*) kutoka Nyamisati hadi Kilindoni. Hii ndio njia ya uhakika na kuondokana na kadhia ya kukatika katika kwa umeme Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni tafiti za mafuta na gesi katika kina kikubwa cha maji baharini kwenye mpaka wa Wilaya ya Mafia na Kilwa baharini kimipaka baadhi ya visima vimo ndani ya mipaka ya Mafia lakini kutokana na urahisi wa kufanya kazi tafiti hizi zinafanyika kutoka Wilaya ya Kilwa. Nitumie nafasi hii kumuomba Mheshimiwa Waziri kuagiza watalaam wake walifanyie kazi hili jambo ili tujue ukweli wa kadhia hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawasilisa na naunga mkono hoja.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na uongozi mzima wa Wizara kwa kazi kubwa wanayofanya lakini pia kupongeza hotuba nzuri iliyojaa matumaini makubwa ya kutatua changamoto ya umeme nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichangie katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa jitihada za kusambaza umeme vijijini kwa awamu ya II na III, hili ni jambo kubwa sana kwani lina dhamira ya kuleta maendeleo kwa wananchi wetu walio wengi, wananchi wa vijijini. Pamoja na dhamira hii nzuri ya Serikali zipo changamoto chache ambazo nashauri Serikali lifanyie kazi nazo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, Vijiji na Vitongoji vingi kurukwa. Katika mpango wa kusambaza umeme vijijini wakandarasi wanaruka maeneo mengi sana, hili sijui ni tatizo la wakandarasi au Mameneja wetu wa Wilaya kutosimamia, zoezi hili limeleta malalamiko makubwa sana kwa wananchi wetu. Niombe Wizara iwe na utaratibu wa kuwasiliana kwa karibu na Waheshimiwa Wabunge ambao ndio wanayajua maeneo yao ya uchaguzi pamoja na changamoto mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilindi ina vijiji 102 lakini kwa mujibu wa vijiji vitakavyopata huduma hii ya umeme wa *REA III* ni vijiji takribani 14 ukijumlisha na vile vya awamu ya II *(REA II)* 22, jumla ni vijiji 36, niombe sana tena bado vijiji takribani 66 havijapata umeme, niombe Wizara yako kupitia *REA,* wapite Wilaya ya Kilindi kupata tathmini ya kina, lakini pia tuna vitongoji takribani 680 ni vichache sana vilivyopata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha Kata ya Kikunde imepata umeme kupitia Wilaya ya Mvomero, tunashukuru kupata umeme, hata hivyo, niombe kata za jirani za Tanga na vijiji vyake umeme kwa sababu vipo kabisa na Kata hii ya Kikunde, kwani kuna takribani vijiji nane havijapata umeme wakati tayari umeshafika karibu, niombe sana Wizara ifanye jitihada za kuwapatia umeme wananchi hawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, changamoto ya umeme dhaifu na kukatikakatika kwa umeme. Ni ukweli

usiopingika wananchi wa Kilindi wana kero kubwa sana ya kukatikakatika kwa umeme na hili imetokana na uhitaji mkubwa wa umeme. Kilindi tunapata umeme kupitia Handeni na utaona kwamba umbali kwa sasa ni mkubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sasa Wizara ione ni namna gani Serikali inaweza kuja na mpango mkakati wa kutatua changamoto hii. Naamini kuwapatia wananchi umeme wa uhakika ni kuongeza mapato ya Shirika letu la *TANESCO,* lakini pia kuliongezea pato Taifa. Imetokea wakati mwingine umeme unakatika takribani wiki sasa unategemea Shirika la Umeme litapataje mapato kwa hali hii?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwa idadi ya wananchi waliopo katika Kata za Sango, Kwadiboma, Negoro, Kibirashi, Kikude na mengine yangeweza kuongeza mapato kama umeme ungekuwa wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. EMMANUEL P. JOHN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja. Tatizo tulilonalo ni kwamba Mkandarasi amelipwa lakini kwa jinsi anavyoonekana hana timu ya kutosha ya watendaji kwa kazi ya kuweka vijiji 30 katika Wilaya. Mfano, alizindua umeme Kijiji cha Resoiti, nguzo nne zilizobaki alitaka kuondoka nazo kwenda Babati sasa tunaomba jicho mbadala ili huyu Mkandarasi aambiwe ripoti ya utendaji wake kila mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Naibu Waziri, Mheshimiwa Subira kwa kukubali vijiji 10 vilivyorukwa katika vijiji vilivyo kwenye mpango wa *REA* III. Mwisho niombe Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani kutembelea Kiteto ajionee mwenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. SHAABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimpongeze Waziri pamoja na timu yake yote kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na kuwakilisha Bungeni makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia umeme, unazungumzia maisha ya watu ambao wanapata mahitaji yao makubwa kupitia umeme. Maana utakuwa unazungumzia maji, viwanda pamoja na ajira kubwa. Hivyo basi katika Jimbo la Lushoto ambalo lina vijiji zaidi ya 50 lakini kati ya hivyo vijiji vilivyopata umeme havifiki 10 na hii *REA III* Mkandarasi amepewa vitongoji 10 tu, lakini navyo vina changamoto, toka mkandarasi huyu apewe kazi toka mwezi wa Nne alikuja kwa wiki moja tu mpaka leo hajaonekana *site* na wala hajamaliza hata kupima hata hivyo vitongoji 10 alivyopewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili la mkandarasi kutoonekana kwa muda mrefu limezua maswali mengi sana kwa mimi Mbunge wa Jimbo, maswali hayo nashindwa kuyajibu. Hivyo basi, niombe Serikali yangu imsukume au isimamie suala hili kwa haraka ili Mkandarasi huyo aweze kwenda na kuweka umeme kwenye maeneo hayo. Kama Mkandarasi huyo hana uwezo asimamishwe kazi apewe mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sana Serikali yangu ipeleke umeme katika Jimbo la Lushoto kwani wananchi wana matumaini makubwa sana ya kupata umeme katika Awamu hii ya Tano chini ya Rais wao ambaye ni kipenzi cha Watanzania na mtetezi wa wanyonge akishirikiana na mimi Mbunge wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi hawa kwa matumaini makubwa waliokuwa nayo wanajitoa kikweli kweli kujenga vituo vya afya, zahanati pamoja na mashule. Kwa mfano, katika kipindi cha miaka miwili na nusu wananchi wamefanikiwa kujenga vituo vya afya viwili; cha kwanza kipo Gare na cha pili kipo Gwelo pamoja na hayo

pia wamefanikiwa kujenga zahanati kumi na nne (14), zote hizi zinahitaji umeme ili kuzikamilisha. Wananchi wakati wa kujenga kama Mbunge wao niliwahakikishia kuwa kila kituo cha afya na kila zahanati pamoja na mashule vitapata umeme kabla ya 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, cha kushangaza hakuna hata kituo cha afya, zahanati wala shule iliyopata umeme. Kwa hiyo, nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri, mimi kama Mbunge suala hili la kutopeleka umeme katika maeneo hayo linaniweka vibaya kisiasa na ananipelekea anguko la 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo wananchi wengi wameshafanya *wiring* katika nyumba zao kwa kuwa na matumaini makubwa ya kupata umeme. Nimwombe sana tena sana Mheshimiwa Waziri na nipo chini ya miguu yake anipelekee umeme katika maeneo haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vijiji ambavyo havina umeme kabisa ni Gare 2, Yamba, Kongei, Boheloi, Masange, Kwemashai, Ngulu, Ubiri-Kizara, Miegeo, Handei, Ngulwi-Nyangei, Ihumba Geni-Madala, Lushoto-Yogoi, Dochi, Maguzoi, Magamba, Kwembago, Kwesimu, Irente, Migambo-Mkuzi, Milungui, Kwabo-Kwefingo, Kwai-Dindira Bandi, Kireti, Kwemakame, Malibwi, Ntambwe, Mazumbai, Kilole, Mbelei, Makole, Kwekanga, Mategho, Bombakomghobole, Mzilagembe-Kigumbe, Ngwelo-Kigulunde, Mazashai, Mlola-Mheza na Mbula, Ungo-Hondelo, Mavului, Mbwei-Kidandi, Mhezi, Kweulasi, Bombo, Mdando, Kwetango na Kwemshazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo ndiyo vijiji ambavyo havina umeme na tumeshawaahidi. Mheshimiwa Waziri ili aamini hili naomba afanye ziara katika Jimbo la Lushoto kwanza, hataona hata nyumba moja ya nyasi, hapo ndio atakapojua wananchi wa Lushoto wamejipanga na wanataka umeme kwa hali yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa umeme ni biashara, basi niiombe Serikali yangu Tukufu ipeleke umeme

Lushoto. Kwani ni imani yangu kubwa kuwa umeme utakaowekwa Lushoto utalipa haraka kuliko maeneo yote ya vijijini katika nchi hii. Serikali itarudisha pesa kwa haraka kuliko maeneo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja, lakini nisisitize vijiji vyangu vya Lushoto vipewe kipaumbele kwa maslahi ya nchi yetu pamoja na wananchi wetu. Mwenyezi Mungu ambariki Rais wetu na ampe umri mrefu. Amina.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Nishati ni nyeti hususan katika kukuza uchumi wa viwanda na shughuli za kibiashara. Hivyo, kwa Wizara hii kuendelea kuzalisha umeme wa ndani kwa uwezo mdogo, katika ukurasa wa 106 Mheshimiwa Waziri amesema Mpanda *(Mw)* uwezo wake ni 5.68 yenye chanzo cha uzalishaji ambao ni *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uzalishaji huu mpaka sasa bado ni changamoto kubwa na *TANESCO* bado haina uwezo wa kuzalisha umeme wa kutosha, Mkoa wa Katavi kuelekea Serikali ya Viwanda ambavyo wanasema. Mpanda Mjini leo wananchi wanakosa umeme kila wiki, umeme unakatika na wananchi bila kujulishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atueleze ni kwa nini bado kero ya umeme Mpanda haiishi na ukizingatia Mpanda ndiyo Makao Makuu ya Mkoa? Kuna Hospitali ya Wilaya, wanakosa umeme na matokeo yake hospitali hii kwa kukosa umeme wanatumia jenereta bovu walilopewa na *UN* Mpanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inapelekea hospitali kukosa umeme na ni aibu na inahatarisha maisha ya wagonjwa. Pia ubovu wa *transforma* na *Mpanda Town Clinic* kila siku Kata ya Kawajense Mpanda Hoteli kwenye viwanda vingi, Makanyagio, Majengo na Madukani, Shanwe kila siku *transforma* mbovu na hupelekea wananchi kukosa umeme.

Tueleze ni lini *transforma* hizi mbovu zitaondolewa na kuletwa mpya ili kuondoa usumbufu huu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni lini mtapeleka umeme wa *REA* katika vijiji hivi ambavyo vina shughuli nyingi za kiuchumi? Ni kwa nini Kata hizi za Ikola, Isengule, Kapala, Msenga, Karema, Kasekese, Ikuba Mwese, Mishemo zilizopewa kipaumbele hazijapewa umeme? Je, ni lini mtagusa maeneo hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kata zilizopo pembezoni, je, kiasi cha Sh.500,000/= na gharama nyingine za kununua vifaa, ndiyo maana wananchi wanalalamika kutokana na gharama kuwa juu? Ni lini watapunguza ununuzi wa nguzo za umeme ili hata Mtanzania wa kawaida aweze kumudu kuweka umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kata mpya Magamba, Kilimahewa Jimbo la Mpanda Mjini na fidia kwa wananchi wanaopitiwa na mradi huu wa umeme *Kv* 400 unaoanzia Sumbawanga Mpanda - Kigoma - Nyakanazi yenye urefu kilometa 760, jumla ya Shilingi bilioni 25.5 zitatumika kulipa fidia. Naomba fidia hizi na tathmini zao zifanyike bila uonevu na kuwalipa bila usumbufu.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJABU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Wakurugenzi wa *REA* kwa jitihada kubwa ambazo wanazifanya kuhakikisha nchi hii inapata umeme kote hususan vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo la Muheza lina Vijiji 135, Kata 37 na Vitongoji 522, lakini pamoja na ukubwa wake ni nusu tu ya Vijiji vyenye umeme. Nawashukuru sana kwa kuruhusu *survey* kufanyika katika vijiji vingi ila naomba Kampuni hii ya *RADI* inayofanya kazi taratibu sana, hadi sasa hakuna hata kijiji kimoja kilichowasha umeme. Pamoja na

*LC's* kutofunguliwa mapema lakini ni vizuri fedha za awamu ya *REA III* awamu ya pili zikatolewa mapema ili pasiwe na *gap* kumfanya Mkandarasi aendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba huyu Mkandarasi aunge vikundi viwe viwili au vitatu maana kwa sasa ana kikundi kimoja na *speed* siyo nzuri. Nimeambiwa lakini hajafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa *Densification* umefanyika kijiji kimoja tu na hao Wakandarasi hawajaonekana tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu mradi wa bomba la mafuta Hoima Tanga. Napongeza sana mradi huu ambao tunategemea utainua sana uchumi wa Tanga. Naomba fidia zilipwe mapema. Kazi ambazo hazina utaalam zifanyike na wanakijiji husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, angalizo; kufuatana na makubaliano ya mkataba sisi Tanzania tupo zaidi ya 90% ukilinganisha na wenzetu waliopo Uganda siyo zaidi ya 20%. Hakuna miradi mikubwa inayoanzishwa bila kupingwa. Kwa mfano, *Stiegler's Gorge*, Mahoteli Rufiji, Bombadier na *SGR*.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukurani kwako kwa kunipatia nafasi hii ya kuchangia katika hotuba ya Waziri wa Nishati. Pili, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Wizara hii pamoja na Watendaji wake wote kwa kuandika na kuwasilisha hotuba hii kwa umakini na kwa ujuzi mkubwa. Katika kuchangia hotuba hii, napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwezo wa Wakandarasi katika miradi ya umeme vijijini *(REA);* napenda kuipongeza Wizara hii kwa juhudi kubwa ya kusambaza umeme vijijini. Hii ni hatua nzuri ya kuhakikisha kuwa wananchi wote wanafaidika na nishati ya umeme. Ushauri wangu katika mradi huu ni kwamba Wizara iwe na umakini mkubwa katika kuchagua Mkandarasi wa ujenzi na ununuzi wa vifaa vya

kazi hii. Tumekuwa na utaratibu wa kuchagua *(select)* Wakandarasi wa bei ya chini. Tumeweka vigezo kuwa katika kupata Mkandarasi kuwa ni yule mwenye bei ya chini *(last bidder)*. Kigezo hicho siyo sahihi sana. Katika mazingira fulani unaweza kumchagua Mkandarasi wa bei ya chini lakini vifaa anavyoleta ni hafifu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano, *transforma* inayotoka China ni rahisi kuliko ile inayotoka katika kiwanda chetu cha *TANELEC* Arusha. *Transforma* za Arusha ni nzuri na *best quality* katika Afrika, lakini wanaposhindana na tranfoma kutoka China, kwa vigezo vya bei rahisi, za China zimeshinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika hili, Wizara iweke utaratibu wa kuzikagua *transforma* hizi. Zilikuwa bado kiwandani kabla ya kupewa Mkandarasi zabuni hiyo. Lazima *transforma* zikaguliwe, *material* inayotengenezewa. Mfano, *windings* zake ni za *aluminium* au *copper? Copper* ni *best* kuliko *aluminium.* Hivyo ni vyema kulazimisha Wakandarasi kutumia *copper* katika kutengeneza *transforma* zetu kama zile za kiwanda chetu cha *TANELEC* Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba kuipongeza Wizara hii ya Nishati kwa kuzindua mradi wa *REA III* katika Jimbo la Same Mashariki. Pia nashukuru kwamba katika hotuba yake Bungeni mwaka huu ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka 2018/2019, ukurasa wa 65 Wilaya ya Same iko kwenye mpango wa kukamilisha upembuzi yakinifu wa nguvu za jua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mradi huu kama utaonekana unafaa, Jimbo la Same Mashariki liingizwe kwenye mpango hasa maeneo ya wafugaji. Hii itasaidia sana wafugaji hawa, wengi wao wakiwa Wamasai waache kuwa wachungi kwa kuhamahama na kupunguza idadi ya mifugo.

Pia ikimpendeza Mheshimiwa Waziri, miradi ya bayogesi ikianzishwa kwa wafugaji itasaidia sana kubadilisha maisha ya wafugaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri ukurasa wa 67 anazungumzia uzalishaji wa umeme kupitia maporomoko madogo ya maji. Naomba Wizara hii ilipe kipaumbele Jimbo la Same Mashariki katika mpango huu. Napenda kumfahamisha Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii ya Nishati kwamba Jimbo la Same Mashariki na mito mikubwa minne yenye maji mengi sana. Kati ya mito hiyo, Mto wa Yongoma una maporomoko makubwa sana. Mto huu maporomoko hayo yako katika Kata ya Lugulu na hutiririsha maji yake kuelekea Kata ya Ndungu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia Wizara hii ifahamu kwamba kuna maporomoko mengine makubwa kwenye Mto wa Hingilili. Mto huu pia una maji mengi, ambao chanzo chake kama ilivyo Mto wa Yongoma ni msitu wa Shengena kupitia Kata ya Bombo na kumwaga maji yake kwenye Kata ya Maore.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo miaka ya nyuma maporomoko yote mawili yalishawekwa kwenye orodha ya kuzalisha umeme ambao ungepunguza upungufu wa umeme katika gridi ya Taifa. Uhaba wa fedha za Serikali kwa wakati huo ulisababisha mradi huo usitekelezwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumwomba Mheshimiwa Waziri wa Nishati aweke kipaumbele katika kuufanyia upembuzi yakinifu mradi huu wa maji ambao utaweza kuzalisha umeme wa kuwezesha kuanzisha viwanda vidogo katika maeneo ya Kata ya Ndungu na Kata ya Maore Jimboni Same Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

**MHE. SILAFU J. MAUFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa watumishi wapendao maendeleo ya

wananchi wetu, kwa kazi nzuri waifanyayo kwa uzalendo uliotukuka. Isipokuwa wanakosa fedha za maendeleo kwa asilimia ya kutosha kwa kukidhi angalau utekelezaji wa asilimia 65 katika miradi ya maendeleo, kwani mwaka wa 2017/2018 walipata fedha za miradi ya maendeleo kwa asilimia 32.6, ni fedha chache ambazo zinapunguza kasi na kupelekea malalamiko makubwa kwa washiriki ya ukamilishaji wa miradi ya umeme kusambazwa vijijini, kwani umeme ni chachu kubwa kwa wananchi wetu kujiajiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2018/2019 ambazo ni asilimia 98.4 ya bajeti yote ya Wizara kwa Sh.1,665,141,000,000/=, Wizara ya Fedha kuona umuhimu wa kutoa fedha hizi ili Wizara ikamilishe ndoto ya vijiji kupata umeme, ukizingatia Mkoa wa Rukwa ambako ni pembezoni uko nyuma kimaendeleo. Hivyo vijiji vya Mkoa wa Rukwa vimo ndani ya vijiji 7,538 vilivyo bado kufikiwa na miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa tuna mahitaji makubwa ya umeme vijijini, hivi Serikali ina mpango upi kuhusu kuwatumia wataalam wake na kuangalia uwezekano wa kutumia maporomoko ya *Kalambo falls* na kuzalisha umeme na kuusambaza kwenye maeneo yanayozunguka na kukaribia kwa hiki chanzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Singida walivyopewa utaratibu wa kutumia upepo na kuzalisha umeme na baadhi ya wananchi wanatumia teknolojia hiyo. Nashukuru kwa Wizara katika bajeti hii tumeweza kukubalika kufikisha umeme wa gridi ya Taifa kupitia mradi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa *Kv* 400 *(North West Grid)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuanzia ukurasa wa 37 hadi 39, huu mradi utaweza kutoa ucheleweshо wa kupatikana kwa umeme wa *REA* awamu ya tatu unaosuasua kukamilika kwenye maeneo yetu na hata usumbufu wa kukatika umeme na matumizi makubwa ya mafuta na wakati mwingine kukosekana na umeme kukosekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu ni mzuri kwetu, Serikali ijipange katika utekelezaji wake na kujiepusha kabisa na changamoto za ulipaji fidia kwa wananchi kwani wanaandaa maeneo kwa mradi, hivyo ichukuliwe kipaumbele kabisa. Bajeti ya Nishati ipewe kipaumbele zaidi katika utekelezaji wa Wizara ya Fedha kama kweli tuna dhamira ya uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme kwa maendeleo yetu. Naunga mkono hoja.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo kupata fursa na afya. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya na kwa maamuzi mazuri ya kuanzisha mchakato wa kufua umeme Bonde la Rufiji maarufu kwa *Stiegler's Gorge.* Umeme huu utakuwa mkombozi wa suala la umeme nchini wenye bei nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na Watendaji wa Wizara, Viongozi wa *REA* wote pamoja na Watumishi wa *TANESCO* kwa jitihada kubwa na nzuri ya kuweka mipango, kutekeleza miradi na kushirikiana na viongozi wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshauri Mheshimiwa Waziri na timu yake kuhusiana na masuala machache ili kuboresha na kuleta ufanisi katika kazi ya kuongeza nishati kwa matumizi ya umeme na matumizi ya majumbani, viwandani na katika Taasisi zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashauri Wizara ingeangalia namna ya kuongeza nishati mbadala zaidi kama hiyo ya *Stiegler's Gorge (hydro)* pamoja na *solar,* upepo na *geothermal* ili kuleta ufanisi na kuwa na *energy mix* nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri Wizara iangalie upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya vifaa vya kutengeneza mradi wa *REA III.* Mfano, nguzo za miti na madawa ya

kuzisindika *(treat), transformers* na mafuta yake pamoja na nyaya na *insulators.* Kuna hofu vifaa hivi havipatikani kwa muda muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nashauri katika maeneo ya kutekeleza mradi wa *REA III,* Mkoa wa Manyara uwe katika mpango wa kupata mradi wa awamu hii wa *densification* kwa sababu kwa sasa umeme unaopozwa katika Vituo vya Afya Babati, Mbulu na Karatu ni asilimia 15 hadi 18 tu hutumika. Naishauri *REA III* ingepeleka umeme katika vijiji vyote pamoja na kwenye sekta binafsi kama mahoteli na *lodges, campsites,* geti la Tarangire na viwandani ili kuongeza mapato ya Shirika (*TANESCO)* na matumizi ya nishati inayopotea bure.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nashauri *TANESCO* itoe viwango na muundo *(specifications* na *design)* ya nguzo za *(cement)* zege ili tuweze kuzalisha kwa wingi pamoja na kupeleka mradi wa umeme wa *REA III* katika maeneo muhimu yaliyoachwa na yaliyokuwepo katika mpango kama Dabil, Kazaroho, Maganjwa, Ufana, Seheda, Darwedica, Diffir, Saydods, Gafal, Gidingwar, Gidewari, Bacho, Donom, Kero Ndogo, Kero Six-Zahanati, Kero Dini, Hamir Estate, Kimasa, Magereza, *TANAPA Gate Sangaiwe* na Kefifi cha Sangaiwe, Kahoi na hoteli na *lodges* zilizopo. Pia Agamango na Tsanasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia baadhi ya maeneo tuboreshe upimaji ili *line* ipitie watu wengi zaidi.

**MHE. JAMES F. MBATIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naambatanisha maeneo ambayo hayana umeme katika Jimbo la Vunjo kama ifuatavyo:-

(i) Kata ya Kirua Vunjo Magharibi katika Vijiji vya Marua - Mkonja na Manaenaeni na Kijiji cha Manu.

(ii) Kata ya Kirua Vunjo Mashariki Vijiji vya Mero, Kileuo-Kileuo Kusini, Mrumeni - Mfirieni, Lashaku na Kijiji cha Nganjoni - Nganjoni Chini, Urenga.

(iii) Kata ya Kirua Vunjo Kusini Vijiji vya Yamu - Masia na Kiraracha, Mabungo - Kilindini na Kiriche Juu na Kijiji cha Uparo - Mandageni, Sumi Kombera.

(iv) Kata ya Kahe Magharibi kwa Vijiji vya Oia-Reli A, Reli B, Stesheni, Kwa Ginja na Mwisho wa shamba; Ngasinyi - Upuurun, Malilo, Mbeu na Mwaru; Rau River - Mkonja na Rau Kati; Miwaleni – Madukani; Ngasinyi B - King'aroni, Longoni, Lengisia, Kisengheni, Lowira; Kisangesangeni - Kisangesangeni A; Mawala na Mwangaria.

(v) Kata ya Kahe Mashariki kwa Vijiji vya Kichakindo; Soko na Mikameni.

(vi) Kata ya Kilema Kaskazini kwa Vijiji vya Makami Juu - Kilowa, Mamrecha, Ngumeni, Mamboyeni na Sango na Ruwa - Kilai na Kirumuni.

(vii) Kata ya Kilema Kusini kwa Vijiji vya Legho Mulo – Ngororomini na Masaera - Masaera Kusini na Maembeni.

(viii) Kata ya Marangu Magharibi kwa Vijiji vya Komalyangoe – Majengo na Mbahe-Mbahe Kaskazini yote haina umeme.

(ix) Kata ya Mwika Kusini kwa Vijiji vya Matala – Kyaronga; Wamanjeni; na Kiruweni – Matala.

(x) Kata ya Makuyuni kwa Vijiji vya Lotima – Kifula na Kiriche.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kupata nafasi hii ya kuchangia. Kwanza nianze kuchangia kuhusu umeme wa *REA.* Wananchi zaidi ya asilimia 80 wanaishi vijijini na wengi wao ni wakulima, lakini umeme unaopelekwa vijijini *voltage* zake ni ndogo sana hata kuwasha *bulb* peke yake ni tatizo. Hapo hapo Serikali inatangaza Tanzania ya viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo wangu, viwanda vya kuwasaidia Watanzania ni viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao, hivyo ukipelekwa umeme wa uhakika na siyo wa kisiasa na wananchi, wakulima wakaweza kusindika mazao yao kule, wataweza kuchangia mapato Serikalini na vijana wetu watakuwa na uhakika wa kujiajiri na kupata ajira kule vijijini na hawatakimbilia mijini kutafuta kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni umeme wa upepo. Je, ni kwa nini sijaona jitihada za Serikali za kuwekeza katika kuzalisha aina hii ya umeme? Nchi nyingi zilizoendelea zina aina ya umeme unaotumia upepo na hapa kwetu mahali kama Singida, Kilimanjaro kule, Same kuna upepo wa kutosha wa kuzalisha umeme. Serikali ingeweza kutafuta wataalam kutoka nchi kama Uholanzi wakaja kufundisha wataalam wetu hapa tukaanza kutumia njia hii ya umeme ambayo haichafui mazingira kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaweza kuzalisha umeme wa taka, ukizingatia kuna takataka nyingi lakini hazitumiki, badala ya Serikali kung'ang'ania umeme wa maji ambao baadhi ya miradi hiyo itapelekea miti mingi kukatwa na kuharibu mazingira na kupelekea kukosekana kwa mvua kama hakuna miti.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia Wizara hii nikiwa na wasiwasi mkubwa na iwapo nisipopata majibu ya Serikali kuhusu wasiwasi niliokuwa nao kwa niaba ya wananchi wa Mlimba, kwa kero kuu tatu zinazopelekea kuwa na mashaka, hatutaelewana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa mradi wa *low cost* uliotekelezwa Jimbo la Mlimba, Kata za Mchombe, Igima, Mbingu, Namwawala na Idete ambao hadi sasa wananchi wengi hawajaunganishwa na nguzo kupitishwa mbali na makazi ya watu. Rushwa iliyokithiri na Wizara inajua kwani walituma Mwakilishi kuongea na wananchi na kutoa ushuhuda. Aliahidi Mkandarasi haongezewi muda na kuleta Mkandarasi mwingine toka

mwezi Januari hadi leo hakuna kinachoendelea. Siyo vizuri unapopeleka taarifa kwa Naibu Waziri, unaambiwa uandike barua. Huu utaratibu haukubaliki, waendeni wakatatue hayo matatizo huko huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mradi mkubwa wa umeme wa Bwawa la Rufiji ni ukweli kwamba Serikali ina mpango wa kuchukua kilomita zisizopungua 239 katika vijiji vya Jimbo la Mlimba. Maeneo hayo yanayopendekezwa kutwaliwa na Wizara ya Maliasili ni maeneo ya kilimo na mifugo na makazi na kwa kufanya hivyo, kumeleta taharuki kwa jamii. Hakuna mtu anayepinga huo mradi, tatizo ni namna gani waathirika hao hawapewi taarifa za kutosha na Serikali ina mpango gani na maisha ya hao watakaoathirika? Serikali iseme hatma ya wananchi hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kilombero sasa ina vyanzo vingi vya upatikanaji wa umeme, mfano; Kidatu, Kihansi, maji ya kutosha kulisha Bwawa la Rufiji lakini vijiji vingi vya Jimbo la Mlimba havina umeme. Pia Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero haifaidiki na chochote kinachopatikana kwenye miradi hiyo kama inavyotokea kwenye madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ilete mabadiliko ya Sheria ili maeneo yanayotunza mazingira na kusababisha uzalishaji mkubwa wa umeme yawe yanapata gawio kwa kuwa umeme ni biashara na siyo huduma.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa napenda kuongelea kuhusu fidia kwa wananchi wanaopisha miradi ya umeme kutokana na ahadi za Serikali za malipo ambazo zimekuwa hazitekelezwi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi ambao unapitia katika maeneo ya Kiluvya, Kibaha na Chalinze sasa hivi ni miaka mitatu tangu wananchi waambiwe wasiendeleze maeneo hayo kwa madai ya kuwalipa, kitu ambacho

hakijafanyika mpaka sasa. Tathmini ilishafanyika lakini Serikali haijarudi kwa wananchi kuwaeleza kinachoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wameshindwa kuendelea kujenga hata vyoo ambavyo vimebomoka. Hata hivyo, wameshindwa kupangisha nyumba zao kwa kuwa zina alama ya 'X' hivyo kuwapa umaskini mkubwa na kutoona faida ya mradi huo wakati wao wangekuwa walinzi wa miradi hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba wananchi walifurahia sana kupatikana kwa gesi na matumaini waliyopewa na Serikali yao kuwa matumizi ya gesi kufua umeme, bei ya umeme huo itapungua, kitu ambacho kimekuwa kinyume na matarajio yao. Wananchi wanakata tamaa na kuona rasilimali za Taifa hazina faida ya moja kwa moja kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama tulitoka kwenye umeme wa maji tukasema kutokana na tabianchi tutumie umeme wa gesi: Je, tunaporudi kwenye maji tunajihakikishiaje kuwa hatutakumbana na tabianchi maji yakipungua? Kama suala ni fedha za kuwekeza kwenye gesi, imekuaje tunaweza kuanza mradi wa maji kwenye maporomoko ya Mto Rufiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali kulipa madeni ambayo inadaiwa na *TANESCO* hivyo kusababisha Shirika hili kuyumba na kushindwa kujiendesha. Nashauri kwamba Taasisi za Serikali zilipe madeni hayo ili *TANESCO* iweze kufanya kazi yake kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile naishauri Serikali kupeleka fedha zote kwa wakati ili Wizara iweze kufanya kazi yake kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na kuwalipa Wakandarasi kwa wakati ili kuepuka *variation* zinazopelekea miradi kujengwa kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na Serikali kuona ni vyema kulinda madini yetu kwa faida ya wananchi wa Tanzania, imeweza kujenga ukuta huko Mererani. Napenda

kujua, hivi madini katika uchimbaji hauwezi kutokea kuruka ukuta huo huo chini kwa chini? Ni mkakati gani wa kuhakikisha wachimbaji hao hawatokezi mbali, nje ya ukuta huo? Kama ulinzi huo wa *Tanzanite* unafaa: Je, Serikali ina mpango gani kuhusu migodi mingine ya dhahabu, mfano Buzwagi na kwingineko?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujua, Serikali ina mpango gani juu ya kuwa na mitambo ya uchenjuaji wa madini yetu hapa hapa nchini kuliko ambavyo iko sasa hivi, kuchenjuliwa nje na kushindwa kupata faida halisi ya madini yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea juu ya madini ya kokoto, michanga ambayo ina matumizi makubwa ya kila siku katika kuboresha makazi ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini haya kodi zake ni za juu kiasi cha kupelekea wananchi kushindwa kugharamia ununuzi wa madini hayo, kuyapata kwa ajili ya ujenzi wa makazi bora na salama kwa wananchi. Napenda kuishauri Serikali kuliangalia hilo kwa ajili ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuhusu madini ya Liganga na Mchuchuma. Napenda kushauri Serikali kuharakisha mchakato wa uchimbaji kwani chuma au nondo tunazojengea sasa hivi siyo imara, zinatokana na vipande vipande chakavu vinavyookotwa na kuyeyushwa inayopelekea nyumba nyingi za kawaida kuporomoka na magorofa pia. Naishauri Serikali kuliona kwa ukaribu kwani nondo za nje ni ghali sana na za hapa ni dhaifu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni fidia kwa wananchi wanaopisha wawekezaji. Natambua madini mengi huvumbuliwa na wananchi, hivyo badala ya kuwaondoa wazawa, wangeongezewa uwezo kwa kukopeshwa vifaa vya uchimbaji ili wachimbaji wadogo wadogo, wazawa waweze kujiongezea pato kwani wawekezaji wanapopewa uwekezaji hawataki kuwashirikisha wazawa, wanawafanya

vibarua na kuwanyanyasa. Naishauri Serikali iliangalie kwa faida ya wachimbaji wadogo wadogo kwani wanasaidia mzunguko wa fedha hapa nchini na kukuza uchumi wa nchi tofauti na wawekezaji ambao wanatorosha fedha hii kwa manufaa ya nchi zao.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na kuipongeza *REA* na Wizara kwa ujumla kwa ushirikiano wa kikazi. Kila nikibisha hodi mnatufungulia mlango na tayari tumewasha katika Kijiji cha Lumwago. Hata hivyo niliwasilisha maombi kwa ajili ya kupanua wigo *(scope)* na pia kwa ajili ya *densification* kwenye Kijiji cha Kitelewasi ambapo kuna Shule ya Sekondari ya Mnyigumba na haikufikiwa na *REA III.* Hivyo nilizungumza na *REA* mnamo tarehe 27 Februari, 2018 na kuwaandikia barua tarehe 28 Februari, 2018. Hivyo naomba kukumbusha kwa kuwapa tena nakala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Mafinga kuwa na *sub-station.* Nashukuru kwa timu ya wataalam kutoka *TANESCO* walifika Mafinga kuona hali halisi. Mafinga inakua kwa kasi hasa katika sekta ya mazao ya misitu, viwanda vikubwa na vya kati zaidi ya 40 vipo Mafinga Mjini, achilia mbali Kiwanda cha Pareto na Chai Bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu hizi zote na ukuaji wa mji nimezipeleka kwenye barua yangu ya tarehe 3 Novemba, 2017. Ombi langu ni kwamba jitihada zilizoanza, *speed* iwe kubwa kwa sababu kuna *potential* kubwa sana ya mahitaji ya umeme, hivyo hata kibiashara ni fursa kwa *TANESCO.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambatanisha barua husika. Ahsante.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchangia hoja hii kwa maandishi. Naomba kushauri Wizara ifungue milango ili *TANESCO* iwe na pande mbili; ya kusambaza umeme na upande mwingine kuwekeza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia kuishauri Wizara ya Nishati ifungue milango kwa sekta binafsi ili kuwe na ushindani na hatimaye bei ya umeme itapungua na umeme utapatikana kwa wingi. Naishauri Wizara kuangalia bei ya umeme wa *TANESCO* kwa watu wa mijini na vijijini. Kuna dhana kwamba watu wa mijini wana pesa ndiyo maana wanalipa Sh.321,000/= wakati vijijini wanalipa Sh.177,000/=. Hii dhana siyo sawa kwa sababu wapo watu mijini wana hali mbaya kuliko wa vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujua kama maeneo ya Jimbo la Ukonga ambayo yaliainishwa mwanzo na Mheshimiwa Naibu Waziri alifanya ziara kwenye Kata za Msongola, Chanika, Buyuni, Zingiziwa na Kivule na mitaa iliyotajwa itapata umeme wa *peri-urban.* Naomba kuishauri Wizara kwamba suala la umeme wa *REA* na miradi yote ya umeme iwe ya kufa na kupona ili Watanzania wapate umeme na twende kwenye masuala mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali ihakikishe kwamba tuhuma za kufuja pesa katika miradi mbalimbali ya umeme inashughulikiwa ili kuokoa pesa za umma ambazo zingetumika kuwaletea Watanzania maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha kwa matarajio ya kupata majibu ya hoja zangu.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze hoja yangu kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani, Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa utendaji mzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la umeme ni injini ya maendeleo katika Taifa letu. Napongeza mpango wa Serikali wa umeme wa *REA III* wa miaka mitano wa kupeleka umeme kwenye vijiji vyote vya Tanzania. Wananchi wa Tanzania wanayo matumaini makubwa sana juu ya umeme huu. Ninachoomba sana, vile vijiji 30 vya nyongeza nilivyopeleka ofisini kwa Mheshimiwa Waziri, viwepo katika Mpango wa *REA III,* awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia kuleta mapinduzi ya kiuchumi katika Jimbo la Busanda kutokana na uwekezaji katika viwanda. Wananchi wengi wanajishughulisha na shughuli za uchimbaji wa madini na umeme unahitajika sana. Vilevile, Serikali itoe kipaumbele katika kupeleka umeme katika huduma za kijamii mfano Shule, Zahanati, Vituo vya Afya na Makanisa au Misikiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba Serikali itoe kipaumbele kwenye umeme vijijini kwa kutenga na kutoa fedha ili kutekeleza mipango muhimu tuliyojipangia. Wizara ione umuhimu wa kuwa na mpango kabambe wa nishati mbadala kwa ajili ya kupikia ili kunusuru mazingira katika Taifa letu. Miaka ya hivi karibuni miti mingi inakatwa kwa ajili ya kutengeneza mkaa katika maeneo mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara kwa kushirikiana na Wizara inayoshughulikia mazingira, waone umuhimu wa kutafutia ufumbuzi tatizo hili la mazingira kwa kupata nishati mbadala ya kupikia kutusaidia kutunza uoto wa asili kwa ajili ya uendelevu wa utunzaji wa mazingira na kupunguza changamoto za mabadiliko ya tabianchi. Naomba Serikali iangalie kwa uzito jambo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kalemani; Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayofanya kuhakikisha Watanzania wanafikiwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta hii ni muhimu sana katika maendeleo ya jamii na maendeleo ya kiuchumi. Ni ukweli usiopingika kuwa kama Taifa tumebarikiwa na vyanzo vingi vya kuzalisha umeme, lakini bado tuna changamoto kubwa ya umeme siyo tu vijijini, hata kwenye miji yetu, bado hatuna umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali yetu kwa kuthubutu na kuanza kutekeleza Mradi wa *Stiegler's.* Hata busara inaagiza huwezi kuweka mayai kwenye chombo kimoja. Kwa hiyo, kuanzishwa kwa mradi huu kutatuhakikishia kuwa na chanzo kingine cha umeme badala ya kutegemea umeme wa gesi pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napongeza juhudi zilizofanywa na *REA* kuhakikisha umeme unafika kwenye vijiji vya Mkoa wa Iringa. Ila napenda kushauri kuwa wakati tunasambaza umeme huu lazima tufanye jitihada za makusudi kuhakikisha maeneo muhimu kama shule zetu na vituo vya afya vinafanikiwa kupata umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* wamekuwa na mzigo mkubwa sana. Hii inaleta changamoto nyingi kwa wananchi. Ushauri wangu ni kuwa tuache wenzetu wa *REA* waweze kusambaza na kusimamia miradi hii kwa sababu wameonesha kuwa wana uwezo mkubwa wa kufanya kazi hii. Badala ya kuanzisha kampuni nyingine, *REA* na *TANESCO* wanaweza wakashirikiana kwa sababu lengo ni kuhakikisha tunawafikia Watanzania wote hasa waliopo vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni muhimu sana kwa Serikali kuhakikisha inapeleka pesa za maendeleo kwa wakati. Miradi mingi ya maendeleo imekuwa ikizorota, siyo kwa sababu watendaji ni wazembe, bali kwa sababu hawapati pesa, hata hizo kidogo hazifiki kwa wakati. Mpaka sasa tumeweza kufikia vijiji 4,730, kati ya vijiji 12,268. Kwa hiyo, utaona kabisa bado tuna kazi kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. DKT. DAMAS D. NDUMBARO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara ya Nishati kwa kazi nzuri sana ya kuwapa mwanga Watanzania. Pongezi nyingi zaidi kwa kuwa chachu ya kuendeleza Sera ya Viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nzuri zaidi mmeifanya katika mradi wa Makambako – Songea (220) ambao utaondoa kabisa tatizo la umeme wa kuaminika katika Mikoa ya Njombe na Ruvuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuhakikisha tunakuwa na vyanzo vya umeme wa kuaminika ni lazima kutumia makaa ya mawe yaliyopo Kata ya Luanda, Wilaya ya Mbinga ili kuzalisha umeme mwingi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mradi wa *REA* ikumbukwe kuwa kuna vijiji ambavyo vipo katika Majimbo ya Majiji. Katika Jimbo la Songea Mjini kuna Kata ambazo zina mazingira ya vijijini kama vile Lilambo, Tanga, Mletele, Ndilimalitembo na Subira. Utekelezaji wa Mradi wa *REA* katika Kata hizi umekuwa ni changamoto kwa sababu tu zipo katika Jimbo la Mjini. Tunaomba sana vijiji hivyo vipatiwe umeme wa *REA* kwa sababu mazingira yao na kipato chao ni chini sana.

**MHE. ALFREDINA A. KAHIGI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wake kwa hotuba yao nzuri na ya kutia matumaini. Napongeza Kamati ya Nishati kwa maoni yao, naomba yazingatiwe kwani ni ya maana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu katika Wizara, naomba nami katika Mkoa wangu Wilaya ya Bukoba Vijijini katika Tarafa ya Bugabo, Kata ya Rubafu, Kijiji cha Kyamalange; Kata ya Kishanje, Kijiji cha Bushasha, Buhendagabo, Kijiji cha Kashozi Nyakato – Kijiji cha Ibosa, Kata ya Kagya Kijiji cha Buzi na Tarafa Katerero; baadhi ya Kata nyingi za Vijiji vingi sambamba na Tarafa ya Kyamutwala, Tarafa ya Rubale Kata na Vijiji vingi sana. Je, ni lini Mheshimiwa Waziri Tarafa, Kata na vijiji hivyo vitapatiwa umeme ili nao waepukane na taa za mafuta na vibatari?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, kwa haya machache naomba niliyoandika yafanyiwe kazi na nawatakia kila la heri, wachape kazi.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu kwenye bajeti ya Wizara hii kwa kumshukuru sana Meshimiwa Waziri pamoja na Serikali kwa ujumla kwa kuingiza Mkoa wa Lindi kwenye Gridi ya Taifa kwani hii sasa ni dalili ya kumaliza matatizo ya umeme kwenye Mikoa ya Lindi na Mtwara. Jambo hili kama likikamilika, sasa Mkoa wa Lindi na Mtwara kunaweza kuvutia wawekezaji na kujenga viwanda, kwani hakuna uwekezaji bila umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na juhudi hizi, naomba kuishauri Serikali katika kuimarisha miundombinu ya umeme kwa upande wa nguzo imara, *transformer* imara na ukaguzi wa mara kwa mara kwenye njia za umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matumizi ya gesi majumbani ni muhimu sana hasa kwenye kusaidia kulinda mazingira kwa kupunguza matumizi ya mkaa. Mradi huu ni lazima uharakishwe hasa kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara kwa kuzingatia kuwa mikoa hiyo ndiyo chimbuko la nishati hii ya gesi. Hivyo, kupelekea gesi Dar es Salaam ukaacha Mtwara kutatuongezea manung'uniko kwa Mikoa ya Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa *REA* awamu ya *I* na *II* haikuzingatia kuzipatia umeme Taasisi za Umma kama mashule, hospitali, vituo vya afya na zahanati. Hivyo hadi leo taasisi hizo hazina umeme. Je, ni utaratibu gani sasa wa kuzipatia taasisi hizi umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Awamu ya *III* imeanza vizuri sasa, lakini tatizo kubwa ni kuwa na Wakandarasi wenye uwezo mdogo na ni wachache. Mfano, Mkoa wa Lindi, hadi Halmashauri ya Liwale haina Mkandarasi aliyepangiwa, bado yuko Ruangwa. Hivyo *REA III* awamu ya pili itaanza kabla ya Liwale kuanza awamu ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, vijiji vichache vilivyowekwa kwenye *REA III* awamu ya kwanza, kuna vijiji vya Lilombe, Ndapata, Kikulyungu, Mpigamiti, Mtungunyu, Miruwi, Kimambi na Mlembwe. Vijiji hivi viko mbali sana toka

Makao Makuu ya Wilaya, hivyo kuwa vigumu kupata umeme toka kwenye chanzo hiki. Hivyo kuhitaji umeme jua. Je, ni lini vijiji nilivyovitaja vitapata umeme?

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kushangaza, kijiji kilicho karibu na chanzo cha umeme kimepewa umeme jua vikaachwa vijiji vya mbali. Kijiji cha Mbaya kiko kilomita 16 toka Liwale Mjini kikaachwa Kijiji cha Kikulyungu ambacho kiko kilometa 42 toka Liwale Mjini. Ni kigezo gani kilitumika kufikia maamuzi haya? Ni kwa nini hapakuwa na ushirikishwaji wa Watendaji katika Halmashauri zetu? Naomba kuongezewa vijiji vya umeme jua, kwani vijiji vingi viko mbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliaminishwa hapo mwanzo kuwa mradi wa gesi asili kuwa ndiyo ungekuwa kama mwarobaini wa gharama za umeme hapa nchini, lakini kinyume chake hadi leo gharama za umeme bado ni za juu sana ukilinganisha na nchi jirani pamoja na kuwa na vyanzo vingi vya umeme nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili linafanya viwanda vyetu kuzalisha bidhaa ambazo zinashindwa kuingia kwenye soko la ushindani Kimataifa kwa bidhaa zetu ni ghali sana. Hivyo, naishauri Serikali kuangalia gharama za uzalishaji wa umeme nchini. Pamoja na usambazaji wake ikichangiwa na ubovu na uchakavu wa miundombinu ya umeme.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia Wizara ya Nishati kimaandishi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, malipo ya fidia mlimopita bomba la gesi (Mashamba ya Mzee Edarusi Liwelu); wakati bomba la gesi linajengwa lilipita kwenye mashamba ya wananchi Mtwara na Lindi. Wapo waliolipwa fidia na wengine hawajalipwa au wamepunjwa kinyume na sheria na taratibu za fidia katika mradi huu wa bomba la gesi kutoka Mtwara mpaka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wananchi wengi Mtwara mjini ambao hawajalipwa na bomba la gasi limechukua mashamba yao, miongoni mwao ni Mzee Edarusi eneo la Lwelu, Tarafa ya Mikindani, kila siku analalamika sana. Naitaka Serikali itoe kauli hapa hapa juu ya fidia za wazee hawa waliochukuliwa mashamba yao, watawalipa lini fedha zao za fidia? Huyu Mzee Edarusi mkazi wa Mtwara Mjini analia sana kila siku na wengine wengi wanalia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku tatu zilizopita tumezindua gridi ya Taifa, lakini cha ajabu nguzo zilizobeba umeme huo ni zile za *REA* vijijini ambazo ni ndogo sana. Nguzo hizi haziwezi kubeba umeme mkubwa kwa sababu zinatumika kupeleka umeme majumbani na siyo kubeba umeme mkubwa wa *grid* ya Taifa kutoka Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naitaka Serikali wakati wa kuhitimisha watueleze mpango wa kuweka nguzo za chuma kwenye *Grid* ya Taifa Kusini upoje? Nguzo ndogo zitadondoka muda wowote. Pia Mheshimiwa Waziri atuambie, nguzo zile za *REA* zilizounganishwa *grid* ya Taifa kusini zinaweza kubeba ngapi? Mbona mikoa yote iliyopelekwa *grid* ya Taifa umesafirishwa kwa nguzo kubwa za chuma? Kwa nini Kusini kunadharaulika? Naomba majibu ya Serikali tafadhali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafanyakazi wengi wa *TANESCO* Kusini wanafanya kazi kimazoea, hawasikilizi wananchi hasa Mainjinia. Wanamshauri Mheshimiwa Waziri mambo ya uongo hasa kuhusu maeneo ya kupeleka umeme. Wanadanganya kuwa wameweka, kumbe uongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengi ya Mtwara Mjini nguzo hazijapelekwa. Maeneo mengine nguzo zimesimama kwa miaka mitatu hivi sasa, hazijawekwa *wire.* Mfano, Kata ya Mitengo – Kilimahewa, Mtwara Mjini, nguzo zimesimama kwa miaka mitatu, hivi sasa hakuna *wire,* Mheshimiwa Waziri anaambiwa tayari tumeweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri aje Mtwara Mjini nimwoneshe maeneo yote na asije kimya kimya, wana Mtwara wanamhitaji sana.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia upande wa Serikali na tunaanza na Mheshimiwa Kangi Lugola, Mheshimiwa Ashatu na Mheshimiwa *Attorney General* ajiandae.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hoja hii muhimu sana ya Nishati. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwa kazi nzuri sana ambazo wanazifanya za kuhakikisha kwamba nchi nzima, vijiji vyote, vitongoji na mitaa yote, inakuwa na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesimama hapa kwa jambo moja tu na jambo lenyewe ni kuhusu mradi mkubwa wa umeme ambao Serikali inatarajia kuutekeleza kwenye Bonde la Mto Rufiji ambao ni maarufu kwa *Stiegler's Gorge*. Umeme ambao utakuwa ni wa *megawatt* 2,100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pengine nianze na maneno haya: *come what may, come rain come shine, by hook and crook,* piga ua garagaza, Serikali itatekeleza ujenzi wa mradi wa kufua umeme wa *Stiegler's Gorge*. Tunajua kwamba huwa chura wanapiga kelele lakini Waswahili wanasema kelele za chura hazimzuii ng'ombe kunywa maji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza vizuri sana Mheshimiwa Joseph Mkundi pamoja na wengine pengine nitumie hoja ya Mheshimiwa Mkundi kwamba wao hawana hofu, hawapingi mradi huu wa *Stiegler's Gorge* lakini wanachotaka ni kuelimishwa ili kuwaondolea hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapata taabu sana. Kazi ya Mpinzani kuanzia tarehe Mosi Januari mpaka tarehe 30 Desemba ni kupinga mambo yote ya Serikali. Ni kwa jinsi

gani tutaweza kumuelimisha Mpinzani ambaye yeye kazi yake ni kutupinga mpaka atuelewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali hatutachoka kutoa elimu na kuwaelimisha hao wanaopinga mradi huu lakini pia na kuwaondolea hofu Watanzania juu ya mradi huu. Sasa naomba Mheshimiwa Mkundi kwa kuwa ameomba Serikali iwaelimishe, kuwaondolea hofu sasa naomba wakae vizuri nianze kuwaelimisha na kuwaondolea hofu, juu ya mradi huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa ambapo Bunge limejengwa, hapa ambapo Wabunge sasa hivi wamekaa ni eneo ambalo lilikuwa na mazingira sawa na mazingira ya maeneo mengine, lakini tuliamua kujenga hapa Bunge hili tukaharibu mazingira. Hawa unaowaona hawa Waheshimiwa wana makazi yao nimeona niwape mifano rahisi sana na makazi yao hata kama ni *medium* au *low density* waliharibu mazingira ili waweze kujenga nyumba zao. Wananchi hawa ambao tunawaongoza kule vijijini nasi Wabunge, tunayo mashamba tunayolima, tukitaka kulima tunafyeka, tunachoma moto na tunaharibu mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, elimu ya uharibifu wa mazingira ambayo inaleta athari baada ya mazingira kuharibika ndipo linakuja suala la kisheria. Sheria Na. 20 ya mwaka 2004, ukienda ukasoma Kifungu cha 81, ukaenda kusoma na Jedwali Namba 3, Kifungu cha 2(8) kinachozungumzia matakwa ya anayetaka kufanya mradi wa miundombinu ya umeme anatakiwa afanye kitu kinaitwa tathmini ya athari kwa mazingira, lugha ya Kiingereza ndio hiyo, *environmental impact assessment*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tathmini hii ya athari kwa mazingira ambayo imefanywa pia kwenye mradi wa *Stiegler's Gorge*, taarifa yake ni ya kitaalam. Taarifa ile ambayo ni ya kitaalam imesheheni wataalam waliobobea kwenye mazingira, ikolojia, wadudu, mimea, wanyamapori pamoja na maji. Pamoja na hayo, mwenye mradi ambaye sasa ni *TANESCO* baada ya kumpa Mshauri Mwelekezi Chuo

Kikuu cha Dar es Salaam, wale wamefanya mambo yote ya kutathmini mazingira yaliyopo pale kwenye Bonde la Mto Rufiji ambapo mradi utajengwa ili kuona ni athari gani za mazingira zitakazotokea. Athari zote zile zimeorodheshwa iwe ndogo au kubwa, baada ya kuorodhesha athari zote hizo…

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** wataalam ambao nimewataja wanachambua ili kuona…

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Kuona athari hizi zitakuwa *mitigated* vipi, yaani athari hizi ambazo zitatokea namna gani zitakabiliwa na mwenye mradi. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu na iwe utaratibu usitafute njia, kona kona ili uingie katika taarifa.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mzungumzaji anayeendelea kuzungumza wakati anachangia alivunja Kanuni ya 64 kwamba Mbunge hatatoa lugha ya kuudhi Wabunge wengine pale anapochangia. Mzungumzaji alisema kwamba wanaopiga kelele ni vyura na hapa hakuna chura kila mmoja anashauri Serikali kwa nafasi yake. Mradi huo kama Serikali inatekeleza siyo vitisho, wanaopitisha ni sisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa nini anawaita Wabunge ambao wanatoa mawazo mbadala kwamba ni vyura.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa nimekuelewa, nitakujibu baadaye, Mheshimiwa Naibu Waziri endelea. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, methali hizi huwa zinaanzia darasa la tano kwamba kelele za chura hazimzuii ng'ombe kunywa maji, pamoja na mbinu wanazosema, sasa nashangaa ameikosa elimu ya darasa la tano. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri endelea na mchango wako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti...

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lugola endelea na mchango wako.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya wataalam hawa niliowasema kwenye *EIA* kutoa taarifa yao ambayo inaitwa *Environmental Impact Assessment Report,* taarifa ile ndiyo ambayo baada ya kuifanyia uchambuzi wakihusisha pamoja na kitu kinaitwa *Technical Advisory Committee* inakuwa imechukua mawazo ya wadau. Baada ya hapo, kile cheti mnachokisikia ambacho ni cha tathmini ya athari kwa mazingira kinatoa masharti ya namna mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, masharti ya kwanza tunaita *general conditions* na pili ni *specific conditions,* yale masharti ndiyo yanayozalisha kitu kinachoitwa *environmental*

*management plan* yaani kwamba mwenye mradi kwa athari zote alizoziona atakwenda kukabiliana nazo vipi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, naomba Waheshimiwa Wabunge masuala haya ni ya kitaalam, masuala haya Watanzania wasiwe na hofu kwamba mradi ule athari zitakazotokea zitakabiliwa kama kawaida kwa sababu masuala ya kitaalam yamefanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwaambie Wabunge, hawa ambao wanapinga mradi huu ukiwatazama wanahitaji umeme ufike katika vijijini vyao, wengine ni wachumi, unajiuliza hivi hawa wanaopinga mradi huu, wanaotaka umeme na kweli kama ni wasomi wanajua uchambuzi wa mambo haya umefanyika, lakini bado wanapinga, maana yake ni moja tu. Maana yake ni kwamba mradi huu wanaona Serikali ikiutekeleza tutakuwa na umeme mwingi wa kumwaga, tutakuwa na viwanda na yale Mataifa ambayo yalizoea tusiwe na umeme mwingi, tutakuwa tumewapiga bao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Zitto, wewe ni Mchumi uliyebobea, nilitarajia pamoja na kwamba uko peke yako humu Bungeni lakini kwa elimu uliyonayo hebu isaidie Serikali kuwaelimisha wenzako hawa kwa sababu ni wapinzani mnaweza kuelewana kwa sababu sisi tukiwaelewesha hawataki kutusikia.

**MHE. KABWE Z. R. ZITTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nimeshasema taarifa sitoi, Mheshimiwa Lugola nenda kwenye hoja yako muda wako umebaki dakika moja tu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali baada ya kuwa tumewaelimisha Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuelimisha Watanzania na kuwaondolea hofu, Serikali itaendelea kujenga mradi huu

na wale wote ambao wanapinga mradi huu kwa kutumwa, narudia kama Serikali, Serikali itawachukulia hatua. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Tumetumwa na nani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Na kama ni kuwapeleka jela tutawapeleka jela kwa sababu mnatumwa kuja...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU WAZIRI OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):** Kwa sababu mnatumwa kuja... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia kidogo katika bajeti hii ya Nishati. Kwanza kabisa nianze kwa kuwapongeza Mheshimiwa Kalemani na Mheshimiwa Subira kwa kazi nzuri wanayoifanya katika sekta hii muhimu sana kwa maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi wanazozipata Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu wake zisingewezekana kama Wizara ya Fedha isingefanya kazi yake. Hili napenda tulielewe vizuri, hawezi kufanya kazi Waziri wa Nishati kama hapelekewi fedha. Kwa hivyo hili ni jambo la msingi Bunge lako Tukufu lifahamu hiki ambacho tunakifanya;, tumeaminiwa, tunatenda kazi na tutaendelea kutenda kwa ajili ya Watanzania maskini wa Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kusema jambo moja ambalo limesemwa kwamba Serikali sasa inakwenda kuchukua *service levy* kwenye gesi na ikusanywe na Mamlaka ya Mapato ije kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. Nimeomba niletewe hizo barua zilizoandikwa na Mamlaka ya Mapato

kwa sababu hatuna hizo barua, tunaosimamia Mamlaka ya Mapato hatuna hizo barua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifahamu *service levy* zozote zile zinakusanywa na *Local Government.* Hiki ndicho kilichopo na ndicho tulichopitisha kwenye Sheria ya Fedha tunayoitekeleza mwaka huu na miaka yote iliyopita. Kwa hiyo, niwatoe wasiwasi wananchi wa Mtwara na Lindi wote kwenye gesi, *service levy* ni ya Halmashauri. Serikali haina haja ya kuchukua hii *service levy* ya gesi kuileta Mfuko Mkuu wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mabadiliko yote ya sheria kwenye kodi, tozo na ushuru huletwa kwenye Sheria ya Fedha ya kila mwaka, wao wameipata wapi kusema hiyo barua iliyoandikwa. Tuseme ukweli na mtutendee haki, hili napenda kuliomba kabisa mtutendee haki, tunasimamia sheria, hatuwezi kutenda kile kitu ambacho kipo nje ya sheria ambazo zinapitishwa na Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kusema kwamba mbele ya Bunge lako Tukufu, Sheria ya Bajeti Kifungu cha 12 na 68 pia na Sheria ya Fedha za Umma, kifungu cha tano ya mwaka 2001 na marekebisho yake ya mwaka 2004 yamempa dhamana Waziri wa Fedha kusimamia mapato na matumizi ya fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili lieleweke wazi na ndiyo maana imesemwa hapa kwamba *LC* za makampuni haya yanayotekeleza umeme vijijini zimetolewa baada ya msukumo wa Kamati ya Bajeti. Napenda kusema hapana, zimetolewa *LC* hizi zote 36 baada ya kujiridhisha na haya ambayo yametendeka kutekeleza vifungu hivi vya sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuko tayari Waheshimiwa Wabunge unawasikia wenyewe wakisema kwamba pesa za Serikali zinatumika ndivyo sivyo, hatuko tayari Serikali ya Awamu ya Tano kuona pesa za Serikali zinaendelea kutumika ndivyo sivyo. Tutajiridhisha kuanzia mwanzo wa mchakato mpaka mwisho wa mchakato na *value added* ionekane kwa

maisha ya Watanzania. Hilo ndiyo lengo tulilonalo, tutaendelea kusimama hivyo na tuweze kutekeleza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, yamesemwa mengi kuhusu Wizara ya Fedha imeshindwa kufanya kazi, hatupeleki fedha. Naomba niliambie Bunge lako tukufu kwa takwimu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitisha bajeti hapa kwa ajili ya Mfuko wa Umeme Vijijini, tulichopitisha mwezi wa Saba tulitakiwa kukusanya shilingi bilioni 31.06. Serikali kwa sababu hiki ni chanzo mahsusi kwa ajili ya kazi mahsusi, tukakusanya shilingi bilioni 21.5 na tukazipeleka fedha hizi zote kwenye Mfuko wa *REA. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi Agosti tulitakiwa kukusanya shilingi bilioni 37.5, tumekusanya shilingi bilioni 36.7 na tumepeleka shilingi bilioni 36.7 asilimia 100. Tutendeeni haki basi pale mnapoongea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwezi wa Tisa tulitakiwa kukusanya bilioni 36, tumekusanya bilioni 25, tukapeleka bilioni 35 kwa sababu kulikuwa na pesa nyingine zilizotakiwa kupelekwa zaidi ya asilimia 141 ya fedha iliyotakiwa kupelekwa kwenye Mfuko wa *REA,* ilipelekwa na Wizara ya Fedha. Ndiyo maana nasema ndugu zangu mnapotaka kumuua mbwa, tumezoea kumpa jina baya, tusifikishane huko, hapana. Mpaka hapa ninapoongea tumeshapeleka fedha zilizokusanywa kuanzia Julai mpaka Aprili asilimia 99.9, asilimia 0.1 hii ni *plus or minus* ya kimahesabu… *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuwe na taarifa sahihi…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima *please* kaa chini, muda wetu umekwisha, mmeuliza sasa anajibu, mwacheni ajibu.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** *No*, mtakuja baadaye kwenye vifungu mtazungumza hoja zenu, mwacheni ajibu, Mheshimiwa Halima *please* kaa chini mwacheni ajibu. Ni kipindi cha Serikali kutoa majibu, endelea Mheshimiwa Waziri.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Huo ni uwongo hapo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana na tufike sehemu tujitendee haki nafsi zetu kuzingatia huu ni mwezi Mtukufu wa Ramadhan, sipo tayari kusema uwongo, nimefunga nailinda swaumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana Watanzania waelewe dhamira njema ya Serikali ya Awamu ya Tano. Dhamira njema ya Serikali ya Awamu ya Tano ni kufikisha umeme kwenye kila Kijiji na tutafikisha. Tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na tutaitekeleza kwa nguvu zetu zote kuhakikisha haya yote yanatendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme jambo la mwisho, nasema tunatekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Yamesemwa malipo ya fidia, napenda kuliambia Bunge lako Tukufu, ndani ya mwezi huu wa Tano tunakwenda kulipa shilingi bilioni 34.079 baada ya kuhakikisha, kifungu cha 44 cha Sheria ya Bajeti kimezingatiwa. Hatuwezi kulipa bila kuhakikisha, sheria tulizokabidhiwa tunazisimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaenda kulipa bilioni 34 kwa ajili ya miradi ifuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa kwanza ni mradi wa umeme kutoka Singida kwenda Babati mpaka Arusha, tunakwenda kuilipa mwezi huu wa Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi wa pili ni mradi wa umeme wa kutoka Rusumo mpaka Nyakanazi, tunalipa mwezi huu wa Tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi wa Tatu ni mradi wa kutoka Bulyanhulu mpaka Geita tunakwenda kulipa kwa sababu tu tumeshajiridhisha kinacholipwa ni sahihi na Watanzania watapata thamani ya fedha yao ambayo imekusanywa kupitia kodi zao*. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusema naunga mkono hoja, nawapongeza Mheshimiwa Kalemani, tupo tayari kuhakikisha kwamba Tanzania nzima inawaka umeme.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG.*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Uwongo!

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Bilioni 64 kati ya 68, huo ni uwongo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja iliyopo mezani...

*(Hapa Mhe. Halima Mdee alizungumza bila utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Halima!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nitajielekeza kwenye masuala mawili, suala la *SONGAS* na suala la *Shell* na kwa sababu kuna masuala ya kisheria katika masuala haya mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na suala la *SONGAS* ambalo liliibuliwa na Mheshimiwa Jesca Kishoa, aliyeeleza kwamba kuna tatizo katika mradi ule kwa sababu Serikali katika *investment* iliwekeza kiasi kikubwa lakini katika *shares* ina kiasi kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kama tunavyofahamu ule ni mradi ulio katika mpango wa *PPP* na ndani ya ule mkataba iko mikataba midogo midogo kama 42 na kwa hiyo, kwa *nature* yake ni mkataba ambao upo *complex.* Sasa nataka kulitaarifu Bunge lako kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imechukua hatua kuhusiana na suala la *SONGAS* na hatua ilizochukua ni kuiitisha hii mikataba yote na kuifanyia rejea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo linafanyika chini ya sheria hii mpya ya *The Natural Wealth and Resources Contracts Review and Renegotiation of Unconscionable Terms Act, 2017.* Kwa hiyo, matokeo yatakayotokana na *review* ile Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataishauri Serikali nini cha kufanya na sasa tuna nafasi hata ya kurekebisha baadhi ya mikataba ile au *terms* za mikataba ile tunapewa uwezo sasa na sheria mpya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala pili ni suala la *Shell* kuinunua *BG* na suala la *capital gains tax* ambalo liliibuliwa katika mchango wa Mheshimiwa David Silinde. Kwanza ni kweli kwamba kumekuwa na huu ununuzi wa *Shell* kuinunua *BG* lakini napenda nilifahamishe Bunge lako Tukufu kwamba huu ununuzi nao ni *complex* kwa sababu ulifanyika *globally* yaani hapa ni *Royal Dutch Shell PLC* ambayo ni *global* ikainunua *British Gas Group (BG) PLC* ambayo nayo ni *global.* Kwa hiyo, katika *global level, Shell* ikainunua *BG*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ununuzi huu pia ulifanyika kwa asilimia 81 tu ya *shares* za *BG*, sasa hiyo ni katika *global level.* Tunaifahamu kwamba *BG* Tanzania ni sehemu ya ile *BG Group PLC.* Sasa yapo mambo mengi ambayo yamefanyika hapo katikati lakini la msingi kabisa ni ile hoja kwamba *capital gains tax* haikulipwa wala haikudaiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba *TRA* wameidai hiyo *capital gains tax.* Wamewadai *BG* wailipe na hiyo ni kwa mujibu wa kifungu cha 86(1) na kifungu... *(Makofi)*

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kifungu cha 86(1) na (3) cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015. Sasa tatizo lililopo ni ubishani, kama nilivyoeleza kilichonunuliwa ni *BG Global* sasa *issue* ikawa *BG* Tanzania *asset* zake zina thamani kiasi gani ndani ya ule ununuzi wote wa *BG Global.* Sasa *TRA* waliwafanyia *assessment* na wakawataka walipe ile *capital gains tax,* lakini *BG Tanzania, Shell* tuseme hawakukubaliana na ile *assessment* iliyofanywa na *TRA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa maana ya kwamba *Shell* wanalalamika kwamba *TRA assessment* yao waliyofanya ni kubwa kuliko ambayo wao *Shell* wanasema inatakiwa kuwa *assessment* halisi. Kama nilivyoeleza ni kwa sababu ya hiyo *complex situation* kwamba hao *Shell* wameinunua *BG Global* na kwa hiyo asilimia ngapi ya hiyo *BG Global* inaangukia katika *Shells* za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa kusema kwamba *Shell* kwa kuwa hawakuridhika na hiyo *assessment* ya *TRA* basi wamelipeleka kwenye *Tax Tribunal* na kwa hiyo kama tunavyozungumza sasa hivi, tunasubiri maamuzi ya *Tax Tribunal* na nadhani hayo ndiyo yatatu- *bind* na ambaye hataridhika basi atapeleka kwenye *Appeals Tax Tribunal.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, jioni tunaanza na Naibu Waziri halafu ataingia mtoa hoja. Nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa Kumi. *(Makofi)*

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa Mpaka saa 10.00 Jioni)*

*(Saa 10.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, sasa namwita Mheshimiwa Naibu Waziri, una dakika 25.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nakushukuru kwa kunipa fursa jioni ya leo nami kuchangia hotuba ya Wizara yetu ya Nishati, nianze moja kwa moja kwa kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba nimshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kuniwezesha kusimama katika mimbali hii katika kumi la kwanza la Mwezi wa Ramadhani, kumi la rehema na naomba pia niwatakie Waislamu wote ulimwenguni *Ramadhan Kareem. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza naomba sana nimshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli, kwa imani yake kwangu na kuniteua kuwa Naibu Waziri wa Nishati. Hakika sina neno zaidi la kusema zaidi ya kumshukuru sana na kumuomba Mwenyezi Mungu anilindie kiapo changu nilichokula mbele yake na namuahidi kufanya kazi kwa weledi na uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, naomba nimshukuru sana Waziri wangu, Mheshimiwa Dkt. Medard Kalemani, kwa uongozi wake, kwa uchapakazi

wake, kwa kufanya kazi kwa weledi na kwa ubunifu ambao kwa kweli umetusaidia Wizara yetu kufanya majukumu mbalimbali na kwa kweli namshukuru sana Mungu kwa kunipa fursa ya kufanya kazi kama msaidizi chini yake na ninamtakia kila la kheri katika majukumu yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nimshukuru sana Katibu Mkuu wetu, Dkt. Hamisi Mwinyimvua, Makamishna, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara yetu, Wenyeviti wa Bodi, Watumishi wote wa Wizara na Taasisi zilizokuwa chini yetu kwa namna ambavyo wamekuwa wakinipa ushirikiano tangu nimeteuliwa kuwa Naibu Waziri na kutimiza majukumu yangu kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda sana sasa niishukuru sana familia yangu, mume wangu, Juma Mtemvu na watoto wetu, wazazi wangu, ndugu, jamaa na marafiki. Pamoja na hayo, kipekee niwashukuru sana Viongozi wa UWT, viongozi ambao wamenileta ndani ya Bunge kwa mara ya pili ambao leo pia walikuwepo hapa kushuhudia namna ambavyo Wizara yetu inawasilisha bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana na Wenyeviti wenzako, niwashukuru sana Mheshimiwa Spika na Naibu Spika kwa malezi yao, niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ushirikiano wenu kwa namna ambavyo mmekuwa mkituunga mkono na kwa ambavyo mjadala umeendelea leo, tangu jana, nawashukuru sana. Kipekee, nimshukuru *Chief Whip* kwa namna ambavyo anatuongoza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini siyo kwa umuhimu, naomba niishukuru sana Kamati ya Nishati na Madini kwa namna ambavyo tumefanya nayo kazi kwa kipindi chote cha kujadili utekelezaji wa bajeti yetu ya mwaka 2017/2018, lakini hata bajeti inayoendelea ya 2018/2019 na kwa ushirikiano, naishukuru sana Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizowasilishwa ndani ya siku mbili ni nyingi na dakika zangu ni 20, naamini sitaweza

kuzizungumzia zote na pia kwa kuwa Waziri wangu yupo. Niwashukuru wachangiaji 120 wa bajeti yetu, waliochangia kwa kuzungumza ni 51 na waliochangia kwa maandishi ni 69. Napenda kuwaahidi yale yote ambayo wameyachangia kwanza tumeyajibu kimaandishi, tutawasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa siyo rahisi kujibu hoja ya kila mmoja, kwa hiyo naomba niwashukuru kwa ujumla wao kwa namna ambavyo wamechangia bajeti yetu, ushauri wote walioutoa tutautekeleza, hata yale ambayo yalionesha ukinzani tumeyapokea tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze kuchangia kwa hoja ya namna ya uzalishaji wa umeme. Nachangia hoja hii nikirejea Ilani ya Chama chetu cha Mapinduzi ukurasa wa 72 ambayo imeainisha namna ambavyo tumewaahidi Watanzania kuongeza uzalishaji wa umeme kwa kutumia vyanzo mbalimbali ambavyo Ilani ukurasa wa 74 imetaja vyanzo hivyo na kwa kipaumbele chake ni makaa ya mawe, maji, gesi asilia, nishati jadidifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mjadala wa ndani ya siku mbili, ulijielekeza kwenye mradi mpya ambao upo ndani ya bajeti yetu, Mradi wa *Rufiji Hydro Power* ambako tumetenga zaidi ya bilioni 700 na naliomba Bunge lako leo baada ya majumuisho haya liipitishe bajeti yetu ili tukautekeleze ule mradi. Kwa nini tunautekeleza sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mjadala wapo Waheshimiwa Wabunge walisema pengine Serikali yetu haisikilizi, haifuati Ripoti ya *CAG.* Nataka niwarejeshe kwenye Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2015/2016, ukurasa wa 36, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali alisema yafuatayo:-

Kuchelewa kuendeleza miradi ya kuzalisha umeme kwa njia ya maji (a) ujenzi wa mradi wa maji ya kuzalisha umeme katika Korongo la *Stiegler's.* Serikali ya Awamu ya Tano imesikiliza na ndiyo maana imekuja na huu mradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelezo ya *CAG* ukurasa wa 37, baada ya kupitia nyaraka mbalimbali na hata pale *RUBADA* mwaka 2012 walipoingia *MoU* na Kampuni ya Odrich ya Brazil ya kutekeleza mradi huu, *CAG* alisema yafuatayo:-

Kwanza, mradi una manufaa zaidi ya kiuchumi ukilinganisha na mingine na *CAG* katika mlolongo wa ushauri wake alisisitiza umuhimu wa mradi huu kutekelezeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nataka niseme tunapoutekeleza leo mradi wa *Rufiji Hydro Power* na nimepata kusema ndani ya Bunge mradi huu ni wa muda mrefu, nyakati zote ulifanyiwa tathmini za mazingira, nyakati mbalimbali. Kipindi cha baada ya uhuru mapema tu, miaka ya 1980, miaka ya 2012, kinachofanyika sasa stadi inayoendelea sasa ni baada ya kupitia stadi zote za awali na ndiyo maana ikatupa nguvu, ikampa nguvu Mheshimiwa Rais wetu, Dkt. John Pombe Magufuli, kupata uthubutu kwamba mradi sasa kwa kuwa tunatekeleza uchumi wa viwanda, lazima tuutekeleze sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge na kama ambavyo amechangia Naibu Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira, huu mradi ukiuangalia na kwa kuwa tunataka *energy mix* na nimepata kusema nchi yoyote lazima wazalishe umeme kwa vyanzo mbalimbali, iwe gesi, maji, makaa ya mawe, upepo, jua, hapa kwenye maji tunatarajia megawati 2,100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi mlijielekeza kwa nini tunahama kwenye gesi, hatujahama kwenye gesi, gesi ina matumizi mengi, tumegundua gesi trilioni 57 *cubic feet* lakini ina matumizi. Viwanda vinategemea gesi trilioni 3.5 *cubic feet,* majumbani tumeanza kusambaza inategemea gesi trilioni zaidi ya 0.6. Sambamba na hilo, Mikoa ya Kusini tunatarajia kujenga viwanda vya mbolea ambapo makadirio wanahitaji gesi trilioni 3.5 *cubic feet*, umeme wenyewe unahitaji gesi ya trilioni 8.8.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niseme umuhimu wa mradi huu siyo kwamba miradi ya gesi tumeiacha kama tulivyopata kusema, upo Mradi wa Mtwara megawati 300, Somanga Fungu megawati 330, Kinyerezi I *Extension* megawati 185, Kinyerezi II megawati 240 na tulishaingiza 168, kuna Kinyerezi III megawati 600.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nilithibitishie Bunge lako na niwatoe wasiwasi, kwa kweli kwa umuhimu wa *energy mix* lazima tuzalishe umeme wa maji, lakini umeme huu ni wa bei nafuu kama nilivyopata kusema. Nimepata kusema ndani ya Bunge kwamba kuna miradi ya Rumakali, Luhuji, Songwe, Mpango, Rusumo, Kakono. Mimi sikusoma uchumi, lakini kwa wale Wachumi watajua kuna kitu kinaitwa *economies of scale,* unatumia *input* kidogo kuzalisha zaidi kwa hiyo, miradi mingine yote ni midogomidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tumewaalika sekta binafsi na ndiyo maana miradi hii ipo kwenye kitabu chetu kwa sababu sekta binafsi itafanya, *Stiegler's* itafanywa. Niliona niliweke hilo vizuri, faida zake zimeelezwa, naomba mtuunge mkono, mumuunge mkono Mheshimiwa Rais wetu, uchumi wetu wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo pekee kwa mfano Bagamoyo, eneo la *EPZ* vitajengwa viwanda 190 vinahitaji zaidi ya megawati 900 likikamilika lile eneo. Ni njia pekee ambayo ni kuongeza uzalishaji huu wa umeme. Tutakapozalisha *Stiegler's* na miradi mingine, 2020 tunatarajia kufika megawati 5,000. Tunapozalisha tunataka tuusambaze. Kwa hiyo, baada ya uzalishaji tunasambaza umeme kupitia miradi ya R*EA* - Umeme Vijijini na Waheshimiwa Wabunge wote mliochangia leo asilimia 70 mmezungumzia masuala ya umeme vijijini na kwa nini, kwa sababu ya umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kama Viongozi wa Wizara hii tumepokea hoja mbalimbali, ushauri mbalimbali, tumepokea changamoto zilizojitokeza *REA I, REA II,* wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge mmesema, yapo baadhi ya maeneo *REA II* haikukamilika, tumepokea. Pia

wapo baadhi ya Waheshimiwa Wabunge mmesema *REA III* vijiji vimerukwa, vitongoji vingine havijaainishwa, taasisi za Umma hazijaunganishwa, nataka niseme kwa ujumla wake yote tumeyapokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwathibitishie kwamba mpaka sasa Serikali kupitia Benki Kuu na naishukuru sana Wizara ya Fedha, imeshafungua *letters of credit* za bilioni 268 kwa makampuni 18 na dola milioni 52. Kwa hiyo nataka kulithibitishia Bunge lako kuanzia sasa na tunavyoendelea miradi hii itaendelea kwa kasi mpya, ari mpya na nguvu mpya. Namna ambavyo Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake amesema, pamoja na Wakandarasi kusuasua lakini mpaka sasa tumewasha vijiji 545. Sambamba na hivyo, vijiji 502 vipo na miundombinu imeendelea kujengwa. Kwa hiyo nataka niseme vijiji vilivyosalia vitaendelea kufanyiwa kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niwashukuru Waheshimiwa Wabunge, mmeleza vijiji vingi vilirukwa, tumepokea maombi yenu. Mapokezi ya maombi yenu tumekuja na orodha ya vijiji vipya 1,541 ambavyo vinatakiwa vifanyiwe kazi, lakini kwa kuwa Bunge ndiyo mnaoidhinisha vijiji vile tukiongeza na 3,559 *REA* mzunguko wa kwanza tunaweza tukavifikia vijiji 5,200 vikabaki vijiji 2,227.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vijiji hivi vitakavyoongezeka pana gharama zinaongezeka, hivi vijiji 3,559 gharama yake mradi mzima ni bilioni 908, lakini vitakavyoongezeka gharama itakuwa trilioni moja na bilioni 300 lakini siyo neno kwa sababu Bunge lenyewe, wawakilishi wa wananchi ndiyo wanaohitaji na wanaohitaji zaidi ni wananchi, lakini siyo neno pia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mheshimiwa Rais anaweka jiwe la msingi katika uzinduzi wa Reli ya *Standard Gauge* alisema mpango wake yeye mpaka 2020 ahakikishe vijiji vyote 7,200 vinapatiwa umeme. Kwa kutambua dhamira hiyo ndiyo maana tunafanya kazi kwa bidii zote kuhakikisha hatumuangushi Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, nataka nilifahamishe Bunge lako, tunaposema miradi ya umeme vijijini, ipo ya aina nyingi, tunayo *densification* awamu ya kwanza mikoa nane, vijiji 305, tulikuwa tunalenga kuwaunganisha wananchi 53,000. Nataka nilitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa mradi huu ambao unakamilika Mei tulishawasha vijiji 300.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hizo, upo Mradi wa *Peri-Urban,* huu tunakuja nao mpya baada ya kuona mahitaji ni makubwa miji inakuwa, huu *peri-urban* utahusisha vijiji zaidi ya 252, mitaa, vijiji. Tunaanza Mkoa wa Dar es Salaam maeneo ya Ukonga, maeneo ya Kigamboni, na zimetengwa bilioni 83. Sambamba na hilo, Benki ya Maendeleo ya Afrika imeonesha nia ya usambazaji wa umeme katika Miji Mikuu, Majiji ya Mwanza, Arusha, Dodoma yenyewe na upembuzi yakinifu unaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia upo mradi unaoendelea wa Mkuza wa *Kv* 400 unaotoka Iringa – Shinyanga, vipo vijiji 121 tunaendelea kupelekea umeme. Kwa hiyo nataka niseme hata haya maeneo Wabunge wengi mmeeleza vitongoji mbalimbali vilivyorukwa, *densification* awamu ya pili inakuja kwa mikoa 11, Mikoa ambayo itahusisha Shinyanga, Morogoro, Dodoma, Tabora, Singida na Geita, kwa hiyo Mikoa 11 tunaanza 2018/2019. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kwamba wafadhili wetu wanaiamini Serikali ya Awamu ya Tano, wameendelea kuipa *support* katika miradi ya umeme. Tunao ufadhili wa Serikali ya *Sweden,* tunao wafadhili wa Serikali ya Norway, tunao wafadhili wa Serikali ya Uingereza katika maeneo ambayo yako *off grid* ambayo tutapeleka umeme katika visiwa mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge wengi kwa kweli, kama nilivyosema, asilimia 80 wote mmehitaji umeme vijijini, lakini mmehitaji ushirikishwaji. Nataka nitoe wito kwa Wakandarasi na pia kwa Wasimamizi wetu,

tumewateua wasimamizi saba kwa Kanda kutoka Wizara ya Nishati, tumeteua wasimamizi kila Mkoa kutoka Ofisi ya *TANESCO,* tumeteua wasimamizi wa miradi hii kila Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe wito tunaendelea kusema tuaomba washirikishe viongozi wa Serikali za Mitaa, washirikishe Wabunge, washirikishe Wakuu wa Wilaya kuainisha mahitaji ili hata wale wananchi waone kwamba mradi huu ni wa kwao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge pia walionesha wasiwasi kuna baadhi ya maeneo uunganishwaji unavyoenda pengine unaashiria rushwa, nataka niseme Wizara yetu tunakemea uwepo wa vishoka katika miradi hii na tunaendelea kusisitiza gharama ni ileile 27,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja nyingine ambayo ilijitokeza ni uendeshaji wa Shirika la *TANESCO.* Lazima nikiri, ni kweli Shirika letu la *TANESCO* linadaiwa, linadai, lakini tunao mpango kupitia *Electricity Supply Industry Roadmap* ambayo iliandaliwa 2014, mle ndani kwenye kile kitabu ukikipitia kuna vipindi mbalimbali vya namna ya ku-*reform* Shirika letu la *TANESCO* na tuko ndani ya muda huo, muda uliwekwa mpaka 2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, ni lazima tukiri haya madeni inayodaiwa *TANESCO* ni madeni ya muda mrefu. Nimeona Waheshimiwa Wabunge wengine wakijaribu kulinganisha kipindi cha tangu Serikali ya Awamu ya Tano imeingia madarakani na kusema kwamba ufisadi na nini, siyo kweli, madeni yalikuwa ya muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, hata katika ripoti ambayo nime-*refer* ya Mdhibiti, mwaka 2015/2016 alitushauri namna gani gharama za kuzalisha umeme kwa *TANESCO* kwa kutumia wazalishaji binafsi na mitambo binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ukiangalia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali tulichofanya Awamu hii ya Tano ni kujitahidi kuachana na mitambo hii ya kuzalisha umeme, kuachana na wazalishaji binafsi wa umeme, kuipunguzia gharama *TANESCO.* Kwa sababu kwa mujibu wa ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kipindi kile 2015/2016, *TANESCO* ilikuwa inapata hasara ya shilingi 265 kwa *unit* moja lakini kwa kupunguza kutumia umeme unaozalishwa na mitambo wa Aggreko, *IPTL, Symbion*, tumelipa uhai mpya Shirika letu la *TANESCO. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kwa kutumia ubunifu wa kuunganisha Mikoa kwenye Gridi ya Taifa kama tulivyofanya Mtwara na Lindi, kama tulivyofanya Wilaya za Kibiti na maeneo ya Ikwiriri, Biharamulo na Ngara, hotuba ya Mheshimiwa Waziri imeonesha hapa. Tumepunguza matumizi, kwa mfano kwa kuunganisha tu gridi katika maeneo hayo bilioni 11.34 kwa mwezi ambazo zingenunulia mafuta mazito kwa ajili ya kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulipotoa maelekezo ya kuagiza vifaa vinavyotumika kwenye kusambaza miundombinu ya umeme ndani ya nchi, tumeisaidia *TANESCO* ku-*save* zaidi ya bilioni 162 zilizokuwa zinatumika kwa kununua vifaa nje ya nchi. Hizo zote huwezi ukafanya *unbundling* sasa bila kufanya *reforms* za namna hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo zipo *reforms* mbalimbali ambazo zinaendelea. Kwanza, kuzuia upotevu wa umeme; pili, kuwaunganisha wateja wengi ili kulifanya shirika lipate mapato; tatu, kukusanya madeni yetu kama *TANESCO* kama ambavyo Mheshimiwa Rais ametupa baraka kupitia ‘KATA’. Yote hayo leo utakapotaka kuigawa *TANESCO* wakati bado inadaiwa, hujafanya *asset valuation,* hujaitengenezea miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Serikali inaisaidia *TANESCO* kuwekeza kwenye miradi ya kimkakati

maana utakapoigawa wakati miradi hiyo haijakamilika, mfano kama nilivyosema Rufiji, kuna Rusumo unaendelea, kuna ujenzi pia wa *transmission line,* umeme unapotea kwa sababu ya ubovu wa miundombinu, lakini Serikali ya Awamu ya Tano imejielekeza kwenye ujenzi wa *transmission lines* hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tumejenga Makambako - Songea, tuna matarajio mwezi Septemba mwaka huu Mkoa wa Ruvuma utaacha kutumia majenereta kuzalisha umeme, tuta-*save* kiwango kikubwa. *(Makofi)*

Sambamba na hilo mimi nasema mnyonge mnyongeeni haki yake mpeni, pamoja na changamoto zote lakini *TANESCO* yako mambo pia amefanya, ubunifu huo mdogo mdogo leo tusingetegea gridi ifike Mtwara na Lindi hatujajenga hata laini mpya, lakini kwa kutumia utalaam wao wa *synchronization* leo Maumbika, kituo cha Mtwara na kituo cha Mbagala vinaonana na umeme unawafikia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kwa kusema kwamba yote ambayo kwa kweli yamezungumzwa sisi tumeyapokea. Tunawaomba Waheshimiwa Wabunge na mimi niwahaidi kwamba pamoja na changamoto zote hizo, lakini tutakuwa tunalisimamia Shirika letu la *TANESCO,* watendaji wamekuwa na wao wakijitahidi kufanya vizuri. Pia tumepunguza kwa kiwango kikubwa upotevu wa umeme, lakini pia tunatambua changamoto iliyokuwepo ya uunganishaji, wananchi wanalipia inachukua muda mrefu hilo tunalishughulia. Sambamba na hilo pia tumewaelekeza TANESCO kufunga mita hizi za *Automatic* ili kuweza kuzuia upotevu wa umeme, sitarajii kengere inigongee tena, lakini nataka nishukuru...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Muda wako umekwisha.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI**: ...kwa kunipa fursa, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge UWT Pwani mmeona mambo hayo? Kwa lugha ya mjini inaitwa habari ndo hiyo, Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kabla sijafika mbele nianze kwanza kuunga mkono hoja. Nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa mara nyingine kwa kunipa uhai, lakini pia kwa kupata fursa ya kuzungumza na kuhitimisha hoja yangu ambayo nimeileta katika Bunge lako tukufu. Pia namshukuru sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kuniteua kusimamiwa Wizara hii muhimu katika ujenzi wa uchumi wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie, Mheshimiwa Rais na Watanzania wote kwamba nitasimamia shughuli za Wizara hii kwa nguvu zangu zote, kwa akili zangu zote na kwa weledi mkubwa ili tufikie malengo ya Tanzania kuwa nchi ya viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Makamu wa Rais mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa ushauri anaotupa na kwa ushirikiano katika kutekeleza miradi hii. Pia nampongeza na kumshukuru sana Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) ambaye ndiye msimamizi wa shughuli kubwa za Serikali ndani na nje ya Bunge, Mwenyezi Mungu amjalie sana na ampe maisha marefu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, wewe Mwenyekiti na Wenyeviti wengine, lakini na Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Bunge akiwemo kaka yangu Mheshimiwa Dunstan Luka Kitandula, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini pamoja na Makamu wake Mheshimiwa Mariam Ditopile Mzuzuri. *(Makofi)*

Niwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge wote wa Kamati zote na hasa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini. Niwashukuru sana Waheshimiwa, Wabunge wote bila kujali itikadi mmetupa ushirikiano wa kutosha ni hakika tukienda namna hii tunajenga uchumi wa nchi yetu, hongereni sana Wahehimiwa Wabunge na sisi tuko tayari sana katika kuwasikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar kwa ushirikiano wanaotupa katika masuala ya Muungano kati ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Tanzania Bara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze sasa katika hoja za Wizara yetu; Mheshimiwa Naibu Waziri alipokuja hapa alisema tumepokea jumla ya hoja na maswali pamoja na ushauri 120, wakati akiwa anasoma hapa tu zimeongezeka hoja nyingine 18, kwa hiyo, tunazo hoja 138 na kati ya hizo hoja za maandishi ambazo Waheshimiwa Wabunge mmetoa ni 69, hoja za kuzungumza ni 51 pamoja na hoja za Kamati ya Kudumu ya Bunge kwa ujumla wake hoja tisa, tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa hoja zenu na ushauri wenu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote kwa niaba ya Wizara yangu naahidi kwamba mawazo yote mliyoyatoa yale kwa maandishi, yawe kwa kuzungumza yawe kwa kupenyeza kwa namna yoyote sisi tutayazingatia kwa weledi mkubwa na yote tutayafanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu si rahisi kutoa majibu yote hapa, niahidi tu kwamba hoja zote zilizotolewa kwanza tutazijibu kwa maandishi, lakini pamoja na maandishi zile ambazo zinahitaji kutolewa ufafanuzi tutaendelea kuzitolea ufafanuzi ndani hata nje ya Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nitachukua nafasi kwa sababu muda ni mfupi ya kufafanua

hoja chache sana ambazo kimsingi zinazungumza mawazo ya ujumla. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya kwanza ya msingi ni juu ya Mradi wa Rufiji wa megawati 2100. Jambo la msingi hapa, nawapongeza Wahehimiwa Wabunge na sisi kama Serikali tumetoka tumefarijika kwamba Wabunge wote kimsingi wameunga mkono hoja ya kutekeleza mradi huu. Isipokuwa walichoshauri ni kwamba lazima tuzingatie masuala ya mazingira na hilo ni kweli tutazingatia, tuzingatie masuala ya *CSR* ni kweli tutazingatia pamoja na *mitigation* ya masuala ya utekelezaji wa mradi. Niwaahaidi Waheshimiwa Wabunge yote hayo tutayazingatia kabla na wakati wa utekelezaji wa mradi hatua zote hizo zitazingatiwa ili mradi huu uwe na tija zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme machache tu na hasa katika *mitigation measures.* Shirika la *TANESCO* halianzi kutekeleza miradi ya aina hii leo kwa sasa, limetekeleza miradi ya Kihansi ambayo inawanyama na viumbe hai adimu. Kwa hiyo huwa inatenga fedha kwa ajili ya kuendeleza mazingira na katika kila mwaka *TANESCO* huwa inatenga jumla ya shilingi milioni 150 kwa ajili ya *CSR* katika maeneo ambako shughuli za miradi zinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya hizo shilingi milioni 64 huwa ni kwa ajili ya miradi ambayo imejengwa kuzalisha umeme wa maji. Kwa hiyo ni matumaini yetu kadiri hii *EIA* itakavyoelekeza ambayo hivi karibuni inakamilishwa; na kwa taarifa tulizopata kwamba ni wakati wowote zitasainiwa ili ianze kutumika; ni matumaini yetu kwamba taratibu zote hizo zitazingatiwa. Kwa hiyo, suala la *CSR* kwa mradi huu muhimu itazingatiwa kwa kiwango cha juu sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumze suala la pili la *Environment Management Plan* ambapo kila mradi unatakiwa utengewe fedha kwa ajili ya utunzaji wa mazingira, kadhalika katika miradi ya namna hii na katika kila mwaka Shirika letu la Umeme nchini hutenga shilingi

milioni 436 kwa ajili ya ku-*mitigate* mazingira kutokana na shughuli zinazoendelea.

Kwa hiyo, ni matumaini yetu katika mradi huu tutaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuchunguza athari mazingira mahala ambapo mradi huu unatekelezwa, ili usiwe na athari zaidi na badala yake mradi uwe na tija. Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge taratibu zote zitazingatiwa na mradi huu utatekelezwa kwa kweli kwa nguvu zote kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mmeunga mkono hoja, na kwa hili nawashukuru ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunao mradi wetu *LNG;* Mradi wa *LNG* zipo hisia kwamba wawekezaji katika mradi huu wanakimbia na kwenda Msumbiji, si kweli. Kinachoendelea ni kwamba maandalizi ya Mradi wa *LNG* hapa nchini umeanza mwaka 2013, wakati Msumbiji umeanza mwaka 2009, kwa hiyo, umeanza mapena kabla yetu na kingine mtekelezaji mmoja wapo katika mradi huu *Exzone Mobile* ana miradi mitatu kule Msumbiji, kwa hiyo ameanza muda mrefu kule. Hata hivyo hakumaanishi kwamba anapotekeleza miradi mingine nje ya nchi huku hawezi kutekeleza, makampuni mengi yanatekeleza miradi katika nchi mbalimbali na zaidi ya miradi moja katika baadhi ya nchi na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ni matumaini yetu mradi huu, niwathibitishie Watanzania mradi wa *LNG* uko pale pale na tunautekeleza kwa *speed* kubwa. Hatua tuliyofikia kwa sasa, mradi huu tulishapa eneo la jumla ya hekta 2071. Tulishafanya tathimini ya fidia kwa wananchi wanaopisha mradi ambapo tatribani shilingi bilioni 50 zinatarajiwa kufidia wananchi watakaopisha maeneo yale baada ya uhakiki kukamilika. Kwa sasa tunafanya majadiliano kati ya wawekezaji na Serikali kwa ajili ya kuenedelea na hatua nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nichukue nafasi hii kuwaambia wananchi na Waheshimiwa Wabunge kwamba

mradi huu unakwenda kama ambavyo imepanga. Mwezi uliopita tulikaa Kamati pamoja na wawekezaji na tarehe 22 mwezi ujao tunakaa pia na timu nyingine kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo. Kwa hiyo, nilitaka kuliambia Bunge lako tukufu kwamba mradi utatekelezwa na utakuwa na tija kubwa sana. Mradi huu katika mwaka huu wa fedha kama ambavyo mmeona tumeutengea shilingi bilioni 6.5 ; hii ni *commitment* kubwa sana ya Serikali na ninaomba tuipongeze Serikali ya Awamu ya Tano kwa juhudi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi mwingine ni wa bomba la mafuta la kutoka Hoima nchini Uganda kuja Tanzania, huu ni mradi mkubwa. Napenda niwapongeze Wahesimiwa mwaka jana mli-*ratify* mkataba wa *Intergovernmental Agreement (IGA)* ambapo tunakwenda kuutekeleza, haikuwa kazi rahisi hongereni sana Waheshimiwa Wabunge kazi kwetu ni kuutekeleza sasa kwa *speed* kubwa. Mradi huu kwa mwaka wa fedha kama ambavyo nimeeleza kwenye taarifa yangu ya bajeti kwamba tumeutengea jumla ya shilingi bilioni 54.2 kwa ajili ya maandalizi ya utekelezaji wa mradi huu. Utekelezaji wa mradi utaanza rasmi ifikapo mwezi Julai, 2018. kwa bahati nzuri kwa upande wa Tanzania tumepiga hatua mbele zaidi ya asilimia 80 dhidi ya wenzetu wa Uganda. Kwa hiyo, tuipongeze Serikali kwa *speed* kubwa ya kutekeleza mradi huu. Mradi huu kama mnavyojua utakamilika baada ya miaka mitatu tangu kuanza kwake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, madeni ya *TANESCO;* ameeleza kidogo Mheshimiwa Naibu Waziri lakini niseme kidogo, madeni ya *TANESCO* ambayo kwa sasa yanafikia shilingi bilioni 938 mengi ni ya zaidi ya miaka 20 na kuendelea, na baadhi ya maeneo ambayo yamechangia sana kuwa na madeni ni pamoja na uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta mazito.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitendo ambacho Serikali ya Awamu ya Tano inataka iondokane nacho kutokana sasa na kuzalisha umeme mkubwa huu tunaouita wa *Stiegler's*

*Gorge* kwa maana ya kuzalisha megawati 2100. Hiyo sasa ndiyo itakuwa chachu ya maenedeo na kuachana na umeme mwingine wa gharama. Kwa hiyo, umeme wa gharama nafuu tunaokwenda kuutengeneza maana yake utaepusha madeni makubwa, vilevile utaondoa gharama kubwa ya uendeshaji wa shirika letu nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kidogo juu ya hatua ambazo tumejipanga kuondokana na tatizo hili. Mikakati gani Serikali inachukua kuondokana na deni hili, la kwanza tunafanya uhakiki ili tujihakikishie kama hilo deni kweli ni sahihi. Kwa sababu linatokana na shughuli za miaka mingi na wakati mwingine shughuli ambazo zimefanya kuwa na deni lazima tuzihakiki. Mara baada ya kuzihakiki tutajua deni ni halisi na namna gani na hatua gani tuendane nalo. Hata hivyo kwa sasa juhudi za makusudi ni zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja, tumeachana na mitambo mikubwa ya *IPTL,* katika mitambo hiyo, kwa *IPTL* na *Aggreko* tulikuwa tunatumia shilingi bilioni 6.9 kwa mwezi kulipa gharama za kununua umeme kitendo ambacho sasa shirika litakwenda kuokoa ambapo sasa tutakuwa na uwezo wa kuwahudumia wateja wetu vizuri. Katika hilo haya madeni mengine yametokana pia na mikataba ambayo mmezungumza Waheshimiwa Wabunge Kama ambavyo tumeeleza, Serikali imeshaanza kuchukua hatua na tayari Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameshaanza kuyafanyia kazi. Ni matumaini yetu kwamba baada ya maoni na ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali mikataba itakayofuata itakuwa ni bora zaidi kwa ajili maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *reform* ya *TANESCO;* Waheshimiwa Wabunge *TANESCO* ilianzishwa mwaka 1931 wakati wa ukoloni wa Mwingereza. Sasa ukihesabu baada ya miaka kama 30 tangu kuanzishwa na kulikuwa ni mashirika mawili ilikuwa na *TANESCO* ya Tanga pamoja na *DARESCO* ya Dar es Salam. Mwaka 1964 yakaunganishwa na Serikali ikayatwaa mwaka 1975 na sasa likawa ndilo Shirika la Serikali. Sasa ukitoka miaka hiyo ninayoizungumza mpaka leo ni shirika kongwe. Kwa hiyo ni dhahili kwamba linahitaji

maboresho. Katika hilo Waheshimiwa Wabunge niwapongeze sana, linahitaji maboresho lazima tuji-*reform. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge cha msingi nani ai-*reform* TANESCO na tui-*reform* kwa namna gani na kwa *interest* ya nani, hayo ndiyo mambo ya msingi. Waheshimiwa Wabunge tunachotakiwa kufanya tukitazama shirika letu ili liwe na tija, tuliboreshe liwe na tija, lakini tusiliboreshe likatuponyoka likasimamiwa na watu wengine. Umeme ni usalama, umeme kweli ni siasa lakini umeme ni uchumi. Ukilibinafsisha shirika hovyo hovyo matokeo yake tunaweza tukapata shida mbeleni. Ni kweli tunauzingatia ushauri, ushauri wote tumeuchukua; lakini tunawaomba Waheshimiwa Wabunge tutekeleze suala hili kwa umakini na kwa uangalifu mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu baada hayo katika hilo, nipende tu kusema shirika letu ya *TANESCO* kwa sasa hivi kwa kweli linaimarika. Kuanzia mwaka jana shirika letu likiwa ingiza vifaa kutoka nje, tulikuwa tunaingiza nguzo kutoka nje, transfoma kutoka nje na mita za umeme kutoka nje. Hivi sasa baada ya kusitisha ni kweli kabisa shirika linaanza kufanya kazi sasa kwa tija, mapato ya shirika yanaanza kuimarika; mapato ya shirika yalikuwa yanaishia shilingi bilioni 29 kwa wiki sasa hivi yanafika shilingi bilioni 32.5 kwa wiki, hii ni kutokana na kuboreka kwa shirika letu.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, nichukue nafasi hii na kuwapongeza sana Wenyeviti wa Bodi na Menejimenti ya Shirika letu la *TANESCO* kwa kazi kubwa wanayoifanya pamoja na mapungufu waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu deni la Serikali, napenda nipongeze Serikali, niwapongeze sana Waheshimiwa Wabunge, lakini nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais katika hili. Kweli deni la Serikali lilikuwa limefika shilingi bilioni 277, lakini mashirika mengi na taasisi zake zimeanza kulipa hivi sasa limepungua limekuwa sasa shilingi bilioni 200 na mashirika mengi na Taasisi

zinaendelea kulipa. Nichukue nafasi hii kuwapongeza sana mashirika ambayo pia mlikuwa mnadaiwa. Hata hivyo, pamoja na kuwapongeza niendelee kusisitiza ndugu zangu msipolipa tutaendelea kukata umeme. Kwa hiyo, niwaombe na kuwashauri tuziwezeshe taasisi zetu ziweze kulipa ili tulijengee uwezo shirika letu liweze kutuhudumia kwa nguvu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengine lipo suala pia limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge, suala la kuingiza mafuta. Ni kweli kabisa mafuta yanayoingia hivi sasa kwa sasa hivi tunaingiza kwa utaratibu wa kununua kwa jumla, lakini hatuna *single storage facility.* Ni kweli kama Serikali ili tuwe na uhakika wa mafuta ni lazima tuwe na *single receiving facility*. Taasisi tuliyonayo kwa sasahivi ni *TIPER,* lakini tunafanya majadiliano na wadau wote. *TAOMAC* nawapongeza sana kwa ushauri wanaotupa, ni kwamba tunataka tufanye utarabu ambao Serikali hata siku moja isije ikaingia kwenye janga la kupungukiwa au kuishiwa mafuta. Ni dhamira ya Serikali kwamba lazima tuwe na mafuta ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa mafuta yanayoingia *reserve* tuliyonayo tuna lita milioni 180 za petroli zinazotutosha kwa siku 35 na lita milioni 132 za dizeli zinazotosha pia kwa mwezi na mafuta ya ndege pamoja na mafuta ya taa yanaweza kututosha kwa mwezi, hayo ni ya ziada. Tunataka tuwe na *storage* ambayo ni ya kudumu ambayo itatusaidia sana kuwa na uhakika wa mafuta. Waheshimiwa Wabunge niwapongeze pia, tumeongeza bandari za kushusha mafuta badala ya kuwa na bandari moja mwaka juzi tuliongeza pia bandari ya Tanga mwaka jana, na mwaka huu ninaipongeza sana Serikali, tumeongeza bandari ya Mtwara ambayo itaendelea kushusha mafuta. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yetu kwamba bei za mafuta katika maeneo ambako yanashushwa itakuwa ni ya bei ya chini na wananchi wataendelea kunufaika na upatikanaji wa mafuta hayo. Niipongeze sana Serikali katika

hatua hizo na *Mwenyezi aiweke mahala pema peponi* Serikali *yetu. (Kicheko)*

Ndugu zangu, ahsante, baada ya kusema hayo, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa ushirikiano mnaotupa; nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge naitakia kila la kheri Serikali yetu kwa utekelezaji wa majukumu yake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nizungumze kidogo kuhusiana na bei za umeme kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamesema,ni kweli kabisa bei za umeme kwa sasa kwa nchi yetu inaendelea vizuri…

**MWENYEKITI:** *Order please*.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukilinganisha...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa utulivu ndani ya Bunge, Waheshimiwa naomba utulivu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bei za umeme, napenda kuchukua nafasi hii pia kuishukuru sana Serikali yetu na kuipongeza. Ukilinganisha na nchi nyingine hivi sasa bei za umeme hapa nchini kwa kweli zimeboreka sana ukilinganisha na nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitoe mfano mzuri tu kwamba bei za umeme linganifu kwa nchi ya Tanzania kwa sasa ni bei ambayo imeimarika sana kutoka kwa sasa hivi sent 4.6 ukilinganisha na wenzetu wa Uganda na Kenya ambao wanazidi senti 5.9…

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri subiri kidogo. Waheshimiwa naomba utulivu ndani ya Bunge. Hoja

zinazojibiwa ni muhimu, naomba tuzisikilize, tuzielewe, tumalize siku yetu leo salama, salmini.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani nilisema vizuri kwamba Mwenyezi Mungu aibariki Serikali yetu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nilikuwa nazungumza suala la bei za umeme, ni kwamba napenda pia kuipongeza serikali, kwa kweli bei za umeme zinaendelea kuimarika na ndiyo maana tunawaomba waheshimiwa Wabunge waridhie bajeti yetu. Baada ya bajeti kupita ni matumaini yetu kwamba bei za umeme zitaendelea kushuka kadiri ya gharama za uzakishaji zinavyoendelea kupungua. Kwa hiyo ni matumaini yetu Waheshimiwa Wabunge mkiridhia bajeti yetu bei za umeme zitaendela kushuka ingawa hata sasa ukilinganisha na nchi nyingine bei ya umeme kwa nchi yetu ni bora kwa sababu ni dola senti 4.6 ukilinganisha nan chi zingine ambazo ni zaidi ya dola senti 5.9.

Mheshimiwa Mwenyekityi, suala lingine ambalo ningependa kuzungumza kwa upande wa Tanzania, ni kwamba tunajenga miundombinu ya kuzalisha umeme mwingi. Matumizi ya gesi kwa sasa kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge mlipenda sana kujua, napenda nitoe sababu ya kwa nini tumevuka kidogo. Maelezo yanayotolewa na Waheshimiwa Wabunge kwamba tuko chini ya asilimia sita ya kuitumia gesi ukweli si huo , ukweli ni kwamba mwaka 2014 tulikuwa tunatumia gesi kwa kweli kwa asilimia sita, lakini mwaka 2016/2017 tulifikia kwa asilimia 23 na hivi sasa 2017/2018 mpaka mwakani tutakuwa na asilimia 39.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo matumizi ya gesi yanaendelea kupanda kadiri uwekezaji unavyokwenda kwenye kuzalisha umeme wa gesi. Niwaombe Waheshimiwa Wabunge, hivi sasa tunatekeleza miradi ya Somangafungu megawati 330 pamoja *na* megawati za Mtwara pamoja na megawati nyingine 300 na 300 mara mbili kwa jumla 600 za *Kinyerezi IV.* Ni matumaini yetu asilimia itapanda ya kutumia

gesi asilia na kwa hiyo, si kweli kwamba tunaacha kutumia gesi na badala yake tunatumia umeme wa maji. Tunakwenda na *energy mixing* kwa ajili ya kujihakikishia usalama wa uzalishaji wa umeme katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niliondolee wasiwasi Bunge lako tukufu kwamba njia za kuzalisha umeme zote tutazizingatia. Bahati nzuri sana *reserve* tuliyonayo kwa sasa ya maji ni nyingi. Tunayo *reserve* ya kuzalisha megawati 4700 na kwa sasa hivi uwezo tunaoweza kuzalisha kwenye hiyo *reserve* tuliyonayo ni asilimia 12 tu, kwa hiyo, ni chini hata ya asilimia ya umeme tunaozalisha kwa njia ya gesi. Kwa hiyo lazima tuendelee kutumia rasilimali ya maji ili tufikie kiwango cha juu cha kuitumia kwa sababu ndiyo *resource* tuliyonayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo tutaendelea pia kuzalisha umeme kutokana na makaa ya mawe. *Potential* tuliyonayo na ya makaa ya mawe kwa sasa hivi ni *five billions tonnes* na hatujaanza kuitumia. Kwa hiyo ni lazima tulitumie kwa sababu ni *resource* kubwa, lakini pia itakuwa na tija sana kwenye kuendesha uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kadhalika tutaendelea kutumia *renewables* nyingine kama ambavyo tumesema ikiwemo *geothermal* ambayo tuna *potential* ya kuzalisha megawati 5000 na hatujaanza kuzalisha hata megawati moja. Kwa hiyo, niwaombe Waheshimiwa Wabunge waridhie haya tunayoyasema ili uzalishaji wa umeme uongezeke na baadae gharama za umeme ziweze kupungua kadri uwekezaji unavyopunguza gharama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, miradi ya *REA,* nizungumze kidogo, lipo jambo limezungumzwa suala la mahusiano na ushirikishwaji wa wadau. Nitumie nafasi hii, yako maboresho makubwa. Wakati natekeleza mradi wa *REA* Awamu ya Kwanza ni kweli kabisa ushirikishwaji haukulingana na tunavyofanya sasa, lakini tumechukua hatua gani, kwa heshima ya Wabunge kutokana na ushauri wao, mlitushauri sana Waheshimiwa Wabunge kuwashirikisha ninyi, lakini

Madiwani na viongozi mpaka ngazi za vijiji na kwa kweli tunafanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya kwanza tunayoifanya, mara nyingi Waheshimiwa Wabunge pamoja na mkandarasi kwenda *site* lakini tunakwenda kila mkoa na kuwaalika Waheshimiwa Wabunge, Madiwani, Wakuu wa Mikoa na Wenyeviti wa Vijiji ili kuwashirikisha na kuwakabidhi mkandarasi, hiyo ni hatua kubwa sana ya ushirikishwaji. Pamoja na hayo bado tunaendelea kuwashirikisha wananchi kulingana na mahali mradi unapofanyika na kwa ngazi mpaka za chini. Ushirikishwaji huu utaendelea ili kuboresha upelekaji wa mradi na kuhakikisha kwamba vijiji vyote ifikapo mwaka 2021 viwe vimeshafikishiwa miundombinu ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali, mwaka 2008 tulikuwa na asilimia nane tu ya umeme vijiji, lakini mwaka 2015 ilipanda na kufika asilimia 20.2. Kwa sasa ndani ya miaka hii miwili, umeme umetapakaa katika maeneo ya vijijini na kufikia asilimia 49.5, hizi ni juhudi kubwa sana. Naomba tuipongeze sana Serikali yetu katika hilo na katika nchi za Afrika zinazozunguka, Tanzania tunaongoza kwa asilimia ya tofauti asilimia 22. Hili ni fanikio kubwa na kwa kweli Serikali yetu hatuna budi kuipoongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika suala ya kupeleka umeme vijijini, nawaomba niwaombe Wenyeviti wa Halmashauri kupitia kwenu Waheshimiwa Wabunge muanze sasa kutenga fedha ili taasisi zote za umma zote zipelekewe umeme. Limekuwa ni jambo la kusikitisha ambalo kwa kweli halina tija kama umeme ukienda namna hiyo bila kuziunganishia umeme taasisi zetu. Kwa hiyo, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge kwa kuwatumia wenzetu Madiwani na Wenyeviti wa Serikali za Vijiji waanze kutenga fedha ili taasisi za umma zikiwemo shule, zahanati, hospitali, ofisi pamoja *dispensary* nazo zipelekewe umeme na tukifannya hivyo umeme utakuwa na tija na utatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambio lingine la msingi ambalo ningependa kulizungumza kwenye mradi huu; ni kweli

yako maeneo yaliyorukwa, tulichofanya Waheshimiwa kama kijiji "A" kimeenda kwenye kijiji "C"; kijiji "B" kikarukwa, tunachokifanya nu kurudi nyuma na kuanza kuvihakiki vijiji vyote ili vijiji vyote vilivyorukwa navyo viingie kwenye utekelezaji wa mara moja. Itakuwa ni jambo la kusikitisha, tunakubali endapo Kijiji kitarukwa na kurudi tena kwa gharama kubwa na kwa kumtafuta mkandarasi mwingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ili kuepuka hilo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, vijiji vyote vilivyobaki 7,873 vyote vitaunganishiwa umeme ndani ya muda tuliojiwekea. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, niwahakikishie kwamba umeme tunaoupeleka unelanga kujenga viwanda. Hivi sasa nchi yetu tumeambiwa na wenzetu wa viwanda tuna jumla ya viwanda 53,000 tu lakini baada ya miaka mitano wanatuambia itakuwa ni mara nne ya viwanda vilivyopo, kwa hiyo sisi lazima tutangulie kupeleka umeme vijijijni ili viwanda viukute umeme vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huu tunaousema wa *REA* unaweza ukawa na changamoto zake, lakini ukitekelezwa vizuri utakuwa na tija kubwa. Niwaambie Waheshimiwa Wabunge, nchi nyingi zinajifunza kwetu kutokana na mradi huu. Kwa hiyo, tuipongeze sana Serikali katika kuutekeleza mradi huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la ushirikishwaji, katika miradi ya *Stiegler's,* bomba na mafuta, pamoja na mradi wa *LNG* hatua tunazofanya sasa ni kuwashirikisha wadau wote. Tumefanya vikao mkoa kwa mkoa, tumefanya vikao na Kamati zetu na tunafanya vikao na jamii zinazozunguka ili kuwapa uelewa wa utekelezaji wa miradi hii. Naungana na Waheshimiwa Wabunge kwamba inawezekana kuna hofu baadhi ya miradi inapotekelezwa. Sasa namna ya kuondoa hofu ni kuwashirikisha Waheshimiwa Wabunge, kuwashirikisha wananchi kabla na wakati wa utekelezaji, kitendo ambacho tunakifanya sasa. Tunafanya hivyo katika *Stiegler's.*

Niwakumbushe Waheshimiwa Wabunge, wiki mbili zilizopita tuliwaita Wabunge wanaozunguka miradi ile, tukafanya kikao, tumeshakwenda Rufiji, tumeshakwenda Kibiti, tumeshakwenda Malinyi na maeneo mengine tumefanya vikao. Lengo ni kuondoa hofu kwa wananchi juu ya utekelezaji wa miradi hii kabla ya miradi haijatekelezwa.

Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge na wananchi kwamba tutaendelea kuwashirikisha wananchi, tutaendelea kuwapa uelewa wananchi ili hofu hiyo inayotanda iweze kuondoka na miradi itekelezeke kwa tija kubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kukaimu, ni kweli kabisa ziko nafasi za kukaimu. Niseme tu kidogo kwamba Wizaa yetu kwa kiasi kikubwa bado mpya lakini pamoja na upya kuna nafasi ambazo kwa kweli bado watalaama wetu wanakaimu lakini zipo sababu za msingi. Baadhi ya maeneo ni kwamba baada ya watalaama wengine kuondolewa kwa taratibu za kikanuni, taratibu za kiuchunguzi zinaendelea sasa taratibu za kiuchunguzi zinapoendelea ni lazima u-*buy time* kwa ajili ya kuangalia *finding* ya uchunguzi itakuwa ni nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo ni matumaini yetu si muda mrefu nafasi hizo zitajazwa ili kusudi watalaama hawa waweze kufanyakazi kwa uhakika zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nitoe taarifa kwamba baadhi ya nafasi tumeshatoa matangazo, nafasi kwa mfano, ya Mtendaji Mkuu wa *PURA* tumeshaitangaza tangu mwezi uliopita, ni matumaini yetu itajazwa kwa haraka zaidi na nafasi zingine tunaendelea kutumia utaratibu wa Kanuni za Utumishi wa Umma ili kupata watalaam na taratibu za *vetting* ambazo pia ni muhimu kuzizingatia. Niseme tu nimepokea ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea kuyafanyiakazi haya ili baadae kusiwe na nafasi nyingi za ukaimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda suala la mwisho ambalo ningependa kulizungumza kidogo ni miradi ya kusafirisha umeme. Hivi sasa eneo pekee lililobaki bila kuwa na Gridi ya Taifa ni lile la upande wa *North West grid,* ni lile la kutoka Mbeya, Sumbawanga, Mpanda, Nyakanazi hadi Kigoma lakini mradi na usanifu wake umeshaanza. Ni matumaini yetu mwaka ujao tutaanza kutekeleza miradi hii ili wananchi wa kule nao baada ya miaka miwili waweze kupata Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo kwa Mkoa wetu wa Kigoma tumeanza hatua za kuingiza katika Gridi ya Taifa baada ya kukamilisha mradi wa Mtwara na Lindi. Tutajenga *sub-station* pale Kijiji cha Uhuru-Urambo na *sub-station* nyingine katika eneo la Uvinza na Kaliua ili kuunganisha Gridi ya Taifa Tabora pamoja na Kigoma. Matayarisho ya mradi yameshaanza na ni matumaini yetu kuja kufika mwezi Machi mwakani *In Shaa Allah* wenzetu wa Kigoma nao wataweza kuwa wameunganishwa na Gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Mradi wa Mto Malagarasi wa megawati 45; kwa kweli mradi huu umekuwa ni wa miaka mingi sana. lakini niipongeze sana Serikali mwaka huu tumepata shilingi dola milioni 149.5 ambazo tumeji-*commit* kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi huu. Ni matumaini yetu mradi huu ukikamilika kwa wananchi wa Kigoma na maeneo jirani utakuwa na tija kubwa na tumejipangia kuukamilisha mwaka 2021. Kwa hiyo, niwaombe wananchi wa Kigoma na maeneo ya jirani wavute subira wakati wa ukamilishaji wa mradi huu unaendelea.

Mheshimiwa Mwenykiti, kwasababu hoja za Wabunge zilikuwa ni nyingi, nyingi tumeziandika na tutawapatia Waheshimiwa Wabunge mzipitie lakini tungependa sana yale ambayo tumeyaeleza kwa Waheshimiwa Wabunge muendelee kutushauri, kutupa ushirikiano ili miradi yote ya Serikali ambayo tumeiomba iweze kutekelezwa kwa tija tuweze sasa kujenga uchumi wa viwanda wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja na naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imeungwa mkono. Katibu.

**NDG. BAKARI KISHOMA - KATIBU MEZANI:**

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**Fungu 58 – Wizara ya Nishati**

Kif.1001-*Admin. and HR Management*......Sh. 2,205,750,000/=

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa nina majina tayari ya vyama, Mheshimiwa Profesa Norman.

**MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri ya Mradi wa *Stiegler's* ninaomba sana Serikali iseme neno kwenye *up stream,* kwa maana ya Mto Lumakali kwa sababu Waziri wakati anajibu maswali kama haya mwaka jana alielekeza kwamba Mradi wa Lumakali wa kuzalisha umeme wa zaidi ya megawati 640 utatekelezwa mwaka huu, lakini kwenye kitabu chake hajasema chochote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nipewe majibu vinginevyo nitashika shilingi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kabisa Mheshimiwa King alivyosema, Mradi wa Lumakali una uwezo wa kuzalisha megawati 222 na umefanyiwa tafiti kwa miaka mingi na ulianza pamoja na Mradi wa Luhuji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nitumie nafasi hii kusema hii miradi inakwenda kwa tathmini. Bahati mbaya katika kukamilisha tathmini za mapitio za mradi huu zilichelewa kwa wataalam ambao walipewa kazi, kwa hiyo, tukaona twende na miradi ambayo tunaweza kuitekeleza mwaka huu halafu mwakani mradi huu nao tuuingize kwa sababu tathmini zake bado zinaendelea. Kwa hiyo, kwa kweli naungana mkono na Mheshimiwa Mbunge avute subira ili tukamilishe taratibu za kufanya tathmini ili na mradi huu nao tuuingize na uweze kutekelezwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Profesa Norman.

**MHE. PROF. NORMAN A. SIGALLA KING:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme ninamshukuru Waziri. Naomba sana tekelezeni mradi huu sawa sawa na ahadi yako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudisha shilingi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Saada Mkuya.

**MHE. SAADA SALIM MKUYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mimi kabla sijakwenda kwenye hoja yangu nataka tu nimwambie Mheshimiwa Waziri kwamba kule Zanzibar, Rais anaitwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi si Rais wa Baraza la Mapinduzi wala si Rais wa Serikali ya Mapinduzi ni Rais wa Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu kwamba katika muendelezo huu tuna-*recognise* kazi nzuri ambayo anaifanya Mheshimiwa Waziri pamoja na *performance* nzuri ya *TANESCO* lakini *performance* ya *TANESCO* yaani inainyima fursa hata *ZECO* kule Zanzibar ku-*perform* vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bei ya umeme ambayo *ZECO* inanunua ni ghali sana, ni kubwa *in such a way* kwamba hata wananchi kule hawawezi ku-*afford* na haya mazungumzo yamekuwa yaliendelea muda mrefu sana. Wakikaa kwenye meza wanakubaliana kimantiki lakini wakiondoka mwezi unaofuata *invoice* inayokuja bei ni ile ile.

Nimemweleza Mheshimiwa Waziri, nilitegemea sana ataweza kutoa majibu ili wananchi wapate kusikia lakini sikusikia kitu chochote. Haya mazungumzo yataisha lini ili utekelezaji wa hili jambo ambalo tunakubaliana kwenye meza halafu tukiondojka halitekelezwi, lini litaanza kuletekelezwa?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru pia Mheshimiwa Mbunge. Kweli Zanzibar inanunua *bulk* na huwa tunaipelekea jumla ya megawati 65 kutoka *Mainland* lakini wananunua kama wanunuzi wa jumla sawa na ambavyo wananunua wanunuzi wa jumla hapa Tanzania Bara. Kwa hiyo, ni kweli gharama ambayo wanakuwa-*charged* kwa sababu wananunua *bulk* haitofautiani na wengine wanaonunua *bulk,* hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, kutokana na hivyo sasa wenzetu *ZECO* walikuwa na sababu za msingi pengine za kusema wao wapunguziwe kwa sababu wao hawafanyi biashara, wanakwenda kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwaka 2016 Sheria yetu ya Kodi baada ya kufanyiwa marekebisho, kulikuwa pia na *argument* kwamba ile bei ambayo wanatozwa na *VAT* kule kwa *ZECO* isi-*apply VAT* kwa sababu ile sheria inasema zile *goods* ambazo zinatoka *Mainland* zimesamehewa kwa upande wa Zanzibar. Kwa hiyo ile *VAT* wenzetu wanasema indolewe kwa sababu ya ile sheria na nadhani Mwanasheria Mkuu wa Serikali baadaye atatoa ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo niseme tu kwamba, hili deni la sasa hivi ambalo kwa kweli *ZECO* wanadaiwa, kwanza niwapongeze Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kulipa, wanalipa kila mwezi, wanalipa *outstanding* na wanalipa *current. Outstanding* ilikuwa shilingi bilioni 60.2 na *current* ambayo imebaki sasa hivi ni shilingi bilioni 27 lakini mwezi tu waliolipa Mheshimiwa Mbunge nikupongeze sana kwa Serikali ya Zanzibar imelipa 4.4 *billion*

*outstanding*, tunawashukuru sana lakini na *current* mmelipa *2.5 billion.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nizungumze sasa limefika wapi, mwaka jana wakati tuko hapa lilipojitiokeza tuliunda Kamati inayowahusisha wenzetu wa Zanzibar pamoja na *Mainland*, na mwezi mwaka wa tatu mwaka huu, tarehe 18 walikaa tena kwa *level* ya Makatibu Wakuu, tukakubaliana kwamba awekwe mtaalam (mshauri) aangalie *low cost design* aje na mapendekezo kitu gani kiondolewe na kitu gani kibaki na akapewa jukumu hilo mwenzetu *EWURA* ili amu-*assign.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nitoe taarifa kwamba mwezi uliopita yule Mkandarasi alishapewa *award* na anaweza akaanza kazi mwezi huu na anamaliza kazi mwezi Julai. Mara bada ya kazi kukamilika atakuja na mapendekezo ya kitu gani kiondolewe kwa upande wa umeme tunaoiuzia Zanzibar na kitu gani kibaki. Lile deni lililobaki ambalo ni *31 billion* ambayo wenzetu wanaibishania nani alilipe. Kwa hiyo, niseme kwa sababu jitihada ni za pamoja suala hili litaletwa tena kwenye Kamati ya Muungano kusudi suala hilo liweze kupatiwa ufumbuzi. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saada hukutoa shilingi, Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi, na nisema hapa mwanzoni tu kabisa kama sitoridhika na maelezo ya Serikali ninakusudia kutoa shilingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania wanatumia umeme wa *TANESCO* kwa gharama kubwa na huduma

haturidhika nayo lakini hatua *options*. Bunge hili lilipitisha sheria hapa ya kuruhusu makampuni mengine yawaweze kuzalisha umeme, lakini pia yaweze kusambaza umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* amekuwa dalali ananunua umeme kutoka kwa wazalishaji wengine halafu yeye ndiye anayeusambaza kwa mlaji wa mwisho. Kitendo hiki kinafanya bei ya umeme nchini kuwa kubwa sana. Hata huu mfano aliomalizia hapa wa Zanzibar, kama *ZECO* pengine ingekuwa inanunua umeme pengine kwa mzalishalishaji moja kwa moja pengine bei ingekuwa nafuu kule Zanzibar, lakini hata huku haturidhiki na bei kubwa ya umeme tunayoitaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kujua Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba *soon TANESCO* haitouza umeme ambao haiuzalishi. Wao wauze umeme ambao wanauzalisha wao na wazalishaji wengine wauze moja kwa moja kwa mlaji ili tuwe na *competition* kwenye soko la umeme na pengine tutapata nafuu ya bei na lakini tutapata huduma iliyo bora na watu tutakuwa na *option* za kuchagua. Naomba majibu ya Serikali. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kadhalika nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, wazo lake kwanza ni nzuri kwamba tuuze umeme tunaozalisha wenyewe. Mheshimiwa Mbunge nikupongeze kwa sababu Bunge hili mwaka jana tulipoazimia kuachana na umeme wa mafuta mazito tulidhamilia kuachana nao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo niseme tu kwamba kwa sasa hatuna umeme wa mafuta mazito tunautumia ambao ulikuwa na gharama kubwa na tunakwenda kwenye miradi ambayo Serikali inaimiliki. Ndiyo maana natumia nafasi hii kuwaambia tu Waheshimiwa Wabunge kwamba miradi mingi ambayo sasa hivi tunazalisha mingi Serikali inamilikiwa kwa asilimia 100 na ndiyo maana ule mradi wa Kinyerezi Namba I na Namba II inamilikiwa na Serikali kwa asilimia

mia moja, lengo ni kupunguza gharama badala ya kutumia umeme wa kukodi ambao ilikuwa ni gharama kubwa. Kwa hiyo tunauchukua ushauri huo ambao kwa kweli msingi. Ndiyo maana tunataka twende kwenye miradi yenye gharama nafuu kama ya mradi wa mto Rufiji na ninawapongeza Wabunge kwa kuliunga mkono hilo. Kwa hiyo tunazingatia ushauri na Mheshimiwa Mbunge kuhakikisha kwamba hatufanyi hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na kwa *ZECO* kwa sababu watakuwa wananunua huku, tukizalisha kwa gharama nafuu huku kwa vyoyote vile na *ZECO* hata wakinunua huku watanunua kwa gharama nafuu. Kwa hiyo, niombe kwamba wakati tunajipanga na mambo hayo tukubaliane na mawazo ya Mheshimiwa Mbunge kwamba tuendelee kutumia umeme ambao tunamiliki Serikali, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea, una mengine ya ziada?

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli ni kwamba Serikali haioneshi nia ya dhati ya *TANESCO* ya kuachana na udalali wa kuuza umeme wa wazalishaji wengine. Sisi tungependa wazalishaji wengine waendelee kuzalisha lakini waende wakauze wenyewe kwa mlaji. Pengine kwa sababu hawana miundombinu ya kusambaza labda *TANESCO* ingekuwa inapata faida ya kupata *capacity charge,* pengine hayo makapuni mengine yangetumia miundombinu ya *TANESCO* kuusambaza umeme kwa walaji. Kwa hiyo, *TANESCO* yenyewe ingekuwa inapata faida badala ya wao kununua kutoka kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi siridhiriki na majibu haya ya Mheshimiwa Waziri na kwa sababu gharama ya umeme na hizi kero ambazo tunazipata ziko nchi nzima ningependa Waheshimiwa Wabunge tulijadili hili kidogo. Kwa hiyo, mimi naomba kutoa hoja.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** *Any way* kwa mujibu wa Kanuni unaruhusiwa lakini Waziri alieleza vizuri sana. Nakuruhusu kwa sababu zinaruhusu, lakini vilevile sioni ile mantiki ya kutaka kuli-*prolong for no reasons*. Mheshimiwa Masoud, Mheshimiwa Heche, Mheshimiwa Keissy na Mheshimiwa Deo. Tuanze na Mheshimiwa Masoud.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Mtolea. *TANESCO* inanunua umeme mwingi kutoka kwa Songas na hoja iliyopo ni kwamba kama kungekuwa na *competition* basi mlaji wa mwisho angepata unafuu. Lakini Serikali haioneshi nia kabisa wanaendelea kung'ang'ania pale pale tu kwamba watuachie baada ya muda hili jambo litakaa vizuri. Hii pia imeathiri pia mpaka tutasema suala la *ZECO*, ingawa Mheshimiwa Waziri amesema suala la *ZECO*, lakini kama ingekuwa *TANESCO* haina udalali huo *ZECO* ingepata umeme nafuu zaidi kuliko wakati mwingine wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hasa katika hali hii, mimi nafikiri Mheshimiwa Waziri ukae ukubali kwamba kwa vyovyote iwavyo hili jambo ukae ulipe mantiki yake, ulipe nafasi yake, uione basi kwamba hili jambo bado anayeumia ni mlaji wa mwisho na ndiye tunayemlalamikia sio mtu mwingine. Baada ya hayo machache bado naendelea kung'ang'ania kwamba bado Serikali haina nia nzuri na kuona mlaji wa mwisho anaendelea kuumia.

**MWENYEKITI:** Ahsante, lakini Mheshimiwa Masoud na Mheshimiwa Mtolea, Serikali ime-*spell out very clearly* na sasa hivi *TANESCO* inaanza kupata faida. Hasara ambayo ilikuwa inapatikana ilikuwa kwenye *capacity charge*. Serikali imeachana na *IPTL*, imeachana na *Symbion* na wanaendelea na mikakati ya kupunguza hizi gharama, kwa hiyo mnaposema Serikali haioneshi nia hamuitendei haki. Mheshimiwa Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi siungi mkono hoja ya Mheshimiwa Mtolea kwa sababu haya mashirika ambayo anasema yazalishe umeme ndio yaliyotufikisha hapa tulipo; *IPTL*, Songas, *Aggreko* walikuwa wanatuuzia umeme senti 50 wakati *TANESCO* wanauzi senti 11. Haya mashirika ndiyo yametunyonya tumefikia hapa kwa hiyo, siungi mkono hoja, naunga mkono Serikali.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Heche.

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namuunga mkono Bwana Mtolea, nafikiri Keissy hajaelewa. Iko hivi, *TANESCO* wame-*monopolies* kila kitu kwenye umeme. Wao wamekuwa shirika moja tu ambalo halina mshindani mwingine yoyote anayezalisha umeme. Sasa kwa matokeo hayo *demand* yote ya nchi hii inakwenda *TANESCO* na *TANESCO* wanajipangia na kutokana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa sababu hiyo uendeshaji wa *TANESCO* kuwa mbovu, na mwenyekiti umesema hapa kwamba, hapa *TANESCO* wameanza kupata faida. Kamwe mpaka dunia hii iishe *TANESCO* hawatapata faida kwa sababu mkataba walioingia na *Songas,* mkataba wa kihuni na wa wizi , ndio unaosababisha shirika hili kuendelea kuwa na madeni na hata dunia hii ikiisha kama mkataba wa aina ya Songas utaendelea kuwepo madeni ya *TANESCO* yataendelea kuwa makubwa na makubwa.  Leo *TANESCO* ina mzigo wa deni zaidi ya bilioni 900…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *AG*, wakati tuna *wind up* mchana ulitoa maelezo mazuri sana kuhusu Songas, na kwa bahati mbaya Mheshimiwa Heche alikuwa ana dharura, hakuwepo. Hebu jaribu dakika moja mbili umuelezee kitu gani Serikali mnafanya kuhusu ku-*revisit* mikataba.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hiyo. Kwa kifupi kabisa nilieleza kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inatambua juu ya tatizo lililopo katika mikataba ya Songas na kwa sababu si mkataba mmoja iko mikataba 42.

Kwa hiyo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali ameitisha mikataba hiyo yote na kuifanyia rejea tukiongozwa na sheria iliyotungwa mwaka jana na Bunge hili Tukufu inayoturuhusu kurejea mikataba yote na kama kuna haja ya kufanyia mabadiliko tutafanya mabadiliko na hiyo ndio hatua tuliyopo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Deo.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naunga mkono hoja ya Serikali kwamba Shirika hili la *TANESCO* sasa hivi limeshaweka mkakati mkubwa wa kuweza kujikwamua. Nazungumza hivyo kwa sababu moja tu, sasa hivi *TANESCO* inadaiwa shilingi bilioni 900 wakati yenyewe inadai taasisi mbalimbali shilingi bilioni 700. Hatua ambazo tayari zimeshachukuliwa sasa hivi inaonesha kuna ongezeko la mapato. Kwa hiyo ukijaribu kuweka hesabu tu zile za kawaida *its is automatic* kwamba itafika mwisho wa safari *TANESCO* itaanza kupata faida yake yenyewe.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Waheshimiwa Wabunge, hebu tuwe, Mheshimiwa Heche umezungumza hakuna aliyekuingilia kwanini tusiwe na *policy* tui-*civilize* humu ndani? Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakubaliana na baadhi ya maoni ya Waheshimiwa Wabunge lakini niseme tu neno moja, bei zetu kwa sasa ukilinganisha na nchi nyingine hasa za jirani za kwetu ziko chini sisi na Warundi. Sisi kwa sasa hivi kwa wateja wa kawaida kabisa wa chini watanunua umeme kwa dola senti, kwa sababu tunalinganisha na maana ya nchi nyingi 4.6; Burundi tu ndio 4.1, lakini nyingine zote ziko zaidi ya 6.8 na hasa Uganda mfano na Kenya ambapo mpaka senti 11, kwa hiyo ziko chini. Hata hivyo maombi ya Waheshimiwa Wabunge ni ya msingi kwamba lazima tuendelee kutaza bei zetu. Tunachoweza

kusema tu ni kwamba kadiri tutakavyokuwa tunazalisha umeme wa bei nafuu kama ambavyo tunaelekea, Serikali itaendelea kulifanyia kazi jambo hili.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mtolea.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza baadhi ya Wabunge hawajaelewa, Mheshimiwa Keissy hakuelewa hoja...

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nani hajaelewa,nini wewe?

**MWENYEKITI** Mheshimiwa Mtolea wewe elezea tuhoja yako.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Elezea hoja yako tu.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja hapa ni kutaka kuipunguzia mzigo *TANESCO*. Kwa sababu yako maeneo *TANESCO* wananunua umeme bei kubwa kuliko bei anayoenda kuiuza kwa mlaji. *TANESCO* pia anaziuzia umeme taasisi nyingine za Serikali ambazo si walipaji wa hizo gharama, ambavyo haya makampuni mengine yanayozalisha umeme yangekuwa yanauza kuna watu wengekuwa wanakimbia kuziuzia hizi taasisi hizi za Serikali ambazo hazilipi.

**MWENYEKITI:** Sawa

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kwa sababu kwa sasa hivi hakuna *option* ni lazima tu *TANESCO* ndio wasambaze ndiyo maana unakopwa sana na mzigo wake unakuwa mkubwa, hii kampuni itakufa. Lakini nashukuru Mheshimiwa Waziri ameelewa ninachokisema. Kwa hiyo, uweke mikakati ya kuachana na kufanya kazi ya udalali wa umeme, kila anayezalisha auze mwenyewe, chukua shilingi yako. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Ahsante, tunataka Bunge *matured* kama hivi ukielezwa vizuri unaelewa, na haitaki makura kura haya,

hayasaidii chochote. Nakushukuru sana bwana kwa kuelewa na namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kueleza na *AG*. Mheshimiwa Mama Kafulila, Mheshimiwa Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante jana wakati nachangia hapa niligusia suala la namna ambavyo mikataba mibovu inapelekea hasara kubwa Taifa letu, na nikawa *specifically* kwenye mkataba wa Songas. Nisiporidhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri nakusudia kushika shilingi. Ninashukuru Mheshimiwa *AG* hapa amekiri kwamba kuna wizi mkubwa sana kwenye Songas na naomba atakapokuja hapa kujibu awe *specific* kwamba ni lini sasa huu mkataba unaenda kufanyiwa *review?* Kwa sababu Serikali yetu imeibiwa kwa miaka kumi na nne mfululizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba Mheshimiwa Waziri alichukulie hili kwa uzito wa kipekee, asimbatanishe na mikataba mingine mingi, kwa sababu Songas mkataba wake ni wa miaka 20, mpaka sasa hivi miaka 14 imekwisha tumebakiza miaka sita tu. Ninaomba Mheshimiwa Waziri awe *specific* ni lini huu mkataba unaenda kupitiwa upya na kufanyiwa marekebisho kwa haraka kwa sababu kila  mwezi tunapoteza dola milioni tano?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa *AG*

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri jambo hili nimelieleza vizuri sana mchana. Kwanza tunazungumzia mikataba na si mkataba. Halafu cha pili sikutamka kwamba kuna wizi mkubwa, nilisema kuna *complications* katika ile mikataba na cha tatu zoezi la ku-*review* mikabata hii lilishaanza, lakini mikataba ni mingi na kama nilivyosema, iko kama 42 na labda ndani ya miezi miwili ijayo tutakuwa tumemaliza hili zoezi, naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kishoa, Mheshimiwa Silinde vipi mbona mdadi hivyo? Mwachie mwenyewe labda anamaliza sasa hivi hapa. Mheshimiwa Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe shilingi kwa Mheshimiwa Waziri kwa sababu suala hili limezungumzwa na mamlaka juu ya tofauti kubwa kwa miaka mingi na ahadi zimekuwa za namna hii. Kwa bahati mbaya tena Mheshimiwa *AG* amebadilisha tu neno kutoka kwamba mkataba huu sio wa wizi ila uko *complicated*, kwamba amebadilisha tu lugha, lakini pia ametaka kui-*soft.* Kwa umuhimu, hapa anaposema ndani ya miezi miwili akumbuke kwamba kwa kila mwezi katika hiyo miezi miwili bado tutapoteza dola milioni tano kwenye hiyo miezi miwili anayosema.

Naomba kutoa shilingi ili tuweze kujadili. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mimi ndiye naendesha Bunge hapa sio Ndassa wala sio nani.

Mheshimiwa Selasini, Mheshimiwa Silinde, Mheshimiwa Makamba pamoja na Mheshimiwa Gekul. Tuanze na Mheshimiwa Selasini.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, katika jambo...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Bashe ulisimama? Mheshimiwa Bashe.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jambo ambalo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania amelisimamia kidete ni pamoja na mikataba mibovu ambayo inaliingizia Raifa hili hasara kubwa; na ndio maana tuliona jinsi Rais alivyosimama kidete dhidi ya mikabata iliyokuwa inahusu madini. Suala hili tunalolizungumza linapoteza pesa za nchi hii dola milioni tano kila mwezi, hili si jambo la kuvumilika. Kuna miradi mikubwa sana ambayo inahitaji fedha, Watanzania katika maeneo mbalimbali sasa hivi wanasukumwa kulipwa kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwa nini *AG* asituambie ni lini hasa jambo hili litashughulikiwa ili kuweza kuokoa fedha za watanzania zinazopotea bure? Maana yake kutolishughulikiwa ni kusema kwamba, kuna *double standard* ambayo Serikali inatumia katika kushughulikia mambo haya. Kwamba lile la Makinikia lilikuwa na *interest* nyingine sasa hili la Songas Serikali hamtaki kulishughulikia kwa sababu inawezekana mna mkono wenu ndani ya jambo hili. *AG* ni lini jambo hili litashughulikiwa limalizike?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Silinde.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Jesca Kishoa kwa maslahi ya Taifa hili. Kuna mambo ya msingi Serikali inapaswa kujua na *AG* lazima ulifahamu hili jambo. Jambo la kwanza, Songas mimi naweza kuisema kwa mujibu wa mkataba ni mali ya *TPDC* kwa *percentage*, hela iliyowekwa mle ndani na *TPDC.* Lakini jambo la pili, ukipitia huu mkataba wenyewe huu pale kuna *share* za aina mbili. Kuna *preferred shares* na kuna *redeemable shares.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo kampuni ya Songas ikipata hasara wao *share* zao haziathiriki vyoyote ila *shares* za Serikali zinaathirika kabisa. Mimi bahati nzuri nilikuwepo kwenye Kamati ya Mheshimiwa Makamba kupitia hii mikataba ya gesi wizi waliokuwa wameufanya *Pan Africa Energy*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipowaita wale wamiliki wa haya makamuni hususani *PAET* wao kwanza walikataa kuleta ile mikataba kwetu, wakasema hii mikataba *is like a bible* ndio walitumia hilo neno *is like a bible*, yaani huwezi kubadilisha jambo lolote, *you can change anything*…

**MWENYEKITI:** Ahsante umeeleweka vizuri.

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunahitaji Serikali itoe majibu juu ya hili jambo, tunahitaji haraka ukamilke.

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Makamba.

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru mimi naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kishoa kuhusiana na mkataba wa Songas kwa sababu kuu mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitegemea *Attorney General*, kama mwanasheria anayeshauri Bunge hili atueleze pamoja na mazungumzo waliyonayo juu ya mkataba huu, je, wamechukua hatua gani kuweka zuio pesa zisiendelee kulipwa mpaka tutakapokubaliana?

Jambo la pili nilitegemea Mwanasheria Mkuu wa Serikali ataueleze ni hatua gani shughuli hii imefikia ili tuweze kupata imani na *commitment* ya Serikali juu ya kutatua huu mgogoro. *Attorney General* aje na *commitment* iliyo *full* kwa sababu pesa za wananchi zinapotea na mwisho wa siku tutakwenda kwenye madai ya kuomba kurudishiwa fedha na wakati tuna nafasi ya kusema zisilipwe fedha mpaka mkataba utakapoeleweka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hoja ya Mheshimiwa Kishoa Serikali haina *commitment* juu ya mkataba wa Songas. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, dola milioni tano ni fedha za kutosha ambazo zingesaidia wananchi wetu, lakini mwanahisa (Serikali) ambaye ana hisa katika mkataba huo, zaidi ya asilimia 70 wanakubali kuendelea kupoteza hizi fedha bila kutuambia kwa *interest* ya nani. Sasa Mwanasheria Mkuu wa Serikali angetuambia hapa kwamba kuanzia leo tuna *stop* hizi fedha zisiendelee kupelekwa huko tungemuelewa, sasa asituambie kuna *complication*. Ni Serikali ya ajabu ambayo inahubiri majukwaani kwamba wao wanapambana na ufisadi, huu tumeusema muda mrefu sana. Kwa hiyo hoja ya Mheshimiwa Kishoa ni kwamba Mwanasheria Mkuu wa Serikali atuambie ni *interest* ya nani hizi fdha zinaendelea kupotea wakati ninyi

mnasema kwamba mnapambana na ufisadi kwa hiyo hatujibu kuanzia leo wa- *stop* kupeleka hizi fedha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Bashe.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme jambo moja, hakuna mtu anayepinga kwamba nchi yetu ilikabiliwa kwa muda mrefu kuwa na mikataba mibovu hasa katika sekta ya umeme. Tumesikia kauli ya Mheshimiwa *Attorney General.*

Mimi nadhani ni busara kwamba Mheshimiwa Kishoa akarudisha shilingi kwa sababu *AG* amesema wanapitia mikataba yote ya umeme na amesema ndani ya kipindi cha miezi miwili watakuwa katika hatua bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, d*ecision* yoyote ambayo tutafanya hapa ya kusema aidha malipo yasilipwe na nini ita-*attract legal issues* na kutuingiza kama nchi katika kesi ambazo hazina sababu. *On top of that* Mheshimiwa Spika ameunda Kamati Maalum na miongoni mwa *terms of reference* wanayopitia mojawapo ni *issue* ya Songas. Kwa hiyo mimi nadhani *let us give benefit of doubt* waweze kufanyia kazi. Wote tunakubaliana kwamba mikataba hii ni ya kinyonyaji, tuyaachie Serikali iweze kuchukua hatua. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa *Attorney General,* Mheshimiwa *AG*.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na changamoto mbili kuhusiana na haya msuala ya mikataba. Changamoto ya kwanza ambayo inatokea katika sheria za kimataifa za uwekezaji ni kuhusu *confidentiality* ya hii mikataba. Hata hivyo sheria tuliyotunga mwaka 2015 ya *Extractive Industries Transparency and Accountability Act* imetufungulia mlango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo la pili ilikuwa pia hatuwezi tukaanza ku-*review* hii mikataba bila ya kuwa na

*legal bases.* Mwaka jana tumetunga tena sheria nyingine *The Natural Wealth and Resource Contract Review and Renegotiation of Unconscionable Terms Act*. Nimeeleza vizuri kabisa, ni *on the basis* ya sheria hii ndiyo hata Mwanasheria Mkuu wa Serikali amepata nguvu na mamlaka kwa sheria inayomuongoza na iliyoanzisha ofisi hii kuweza kupitia mikataba hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hicho ndicho tumekifanya, na kazi hii ni *technical.* Nimesema kwamba tuna makisio ya miezi miwili tutakuwa tumeimaliza na kama kuna vipengele vyovyote ambavyo vilitupeleka katika hali ile hatutasita kutoa mapendekezo ya kuvibadilisha katika mkataba huo. Hii ndiyo *commitment* ambayo ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kwa niaba ya Serikali inatoa, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kishoa nafikiri AG amejieleza vya kutosha. *Process* ipo mbioni, *road map* ndio hiyo Halima wewe Mwanasheria unajua maswali kisheria hayasemwi hadharani mnaweza mkasema hadharani *strategy* za Serikali wakazidaka. Haya Mheshimiwa Kishoa.

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, *AG* anazungumzia *legal basis, 14 years? Who is behind this,* nani yuko nyuma ya pazia kwenye mkataba huu ambaye anashindwa kuhusika? Leo mimi ningetamani kuona ni nani anaunga mkono wizi huu na nani ambaye analinda rasilimali za taifa letu. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kishoa dakika moja kuna Kamati inashughulikia hoja yako hiyo ya msingi na sasa hivi tunasubiri tu tarehe ya Spika kutangaza matokeo ya Kamati Maalum ambayo ipo na anajua kuna Wabunge wa upande wako wamo kwenye Kamati, tutoe *benefit of doubt* mrudishie shilingi Mheshimiwa Waziri tusubiri Kamati.*(Makofi)*

**MHE. JESCA D. KISHOA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hata makinikia kile tuliambiwa imekwisha, lakini tunaona mambo hayaeleweki ni hivi nilitegemea basi hata kwamba

wanaweka zuio watafanya utaratibu wa kuweka zuio ili fedha zisiendelee kuibiwa mimi naomba tupige kura kwa ajili ya suala hili ili tuweze kujitathimini tuangalie pia mnafaidika nini na mkataba huu wa Songasi badala ya kutetea Serikali ambayo inaibiwa kila mwezi? *(Makofi)*

**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Jesca kura ni haki yako ndio ulichokitaka na utakipata na matokeo yake utayaona. Wale wanaokubali...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKTI:** Subirini basi ni hoji au niingie *guillotine* saa hizi?

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa Kukataliwa)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, *order* nafikiri Serikali/*AG* umejieleza vizuri sana mtu yoyote mwenye kutaka kujua ukweli, ukweli umeueleza njia ambazo mikataba mibovu hatua zinachokuliwa zinaonekana na zitakuja kuibua mambo mengi sana kwa siku za mbele. Mheshimiwa Mlata.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Mimi ninaomba tu ufafanuzi kidogo kwa Mheshimiwa Waziri kutokana na gesi asilia. Ameeleza vizuri katika kitabu chake juu ya utekelezaji unavyoendelea, lakini bado nilikuwa naona hatua zile jinsi wanavyoendelea hauna *speed* ambayo tulikuwa tunaitegemea kama ilivyoanza mwanzo. Kwa sababu usambazaji wa gesi majumbani kwanza kuna ile ya majumbani na kuna ile ya viwandani, na *TPDC*/Waziri amesema kwamba wamepata wateja wa kutosha lakini bado hawajawapelekea wenye viwanda na akasema kwamba wanaleta mpaka hapa Dodoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nilikuwa naomba ufafanuzi ni jambo gani ambalo linazuia kufanya kasi ambayo tulikuwa tunaitegemea tangu mwanzo

kuchelewesha ili kuusambaza kwanza majumbani lakini na kwenye viwanda vingi ambavyo vimeomba. Kama hatajibu vizuri na mimi nitashika mshahara wake ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mlata kwa hoja yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwneyekiti, ni kweli kwamba upo mpango wa kusambaza gesi majumbani na viwandani lakini hata katika magari yetu. Labda nimsahihishe kidogo si kwamba mradi umechelewa, ila mradi unakwenda hatua kwa hatua. Ni kweli kabisa mpango wa Serikali ni kusambaza gesi kwa ajili ya matumizi ya majumbani katika mikoa yote, lakini tunaanza hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mikoa ambayo ni nje ya Dar es Salaam na Mtwara pamoja na Lindi kazi inayofanyika sasa hivi ni kufanya *study.* Kama mnavyojua Waheshimiwa Wabunge miradi mikuba kama hii ni lazima kwanza ufanye *study,* uifanyie *review,* uilkamilishe ndipo uje kwenye utekelezaji. Kwa hiyo, nimuambie Mheshimiwa Mbunge kwamba ni kweli tunatekeleza maeneo yote na kwamba hatujachelewa isipokuwa tunakwenda hatua kwa hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba tumeshaanza, mwezi uliopita tumeanza kusambaza gesi kwa mradi mpya katika Jiji la Dar es Salaam ambao utakwenda kwa wananchi zaidi ya 1000; lakini kadhalika tunakwenda sambamba pamoja na wananchi wa mikoa ya Mtwara.

Kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge ukienda katika ameneo ya Ubungo, Chuo Kikuu, Makongo juu, Mlalakuwa, Mwenge, Sinza, *Ocean Road* tutapeleka gesi hii na tumeshaanza. Kwa hiyo, kwa kweli tunajitahidi sana kama Serikali kupeleka miradi hii haraka lakini tutakwenda hatua kwa hatua baada ya kukamilisha taarifa zote. Mheshimiwa

Mbunge nakushukuru uendeleee kutupa ushirikiano ili tukamilishe taratibu hizo ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Martha Mlata.

**MHE. MARTHA M MLATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, nakushukuru Mheshimiwa Waziri kwa maelezo yako mazuri mimi nilikuwa ninaomba sana hizo hatua kwa hatua angalau ziongeze kasi kwa sababu hivi tunavyoongea ukienda kwa mfano kwenye mkoa wa Singida na mikoa mingine hasa kwenye magereza yetu wamemaliza ile miti kwa sababu wanakata yale magogo, wapelekeeni basi hata ile mitungi mikubwa wakaanze kutumia gesi ili tuokoe misitu yetu.

Mimi ninapongeza hatua hiyo, lakini hebu kueni na ubunifu, kwenye mikoa ambayo bado hamjafika basi bebeni mitungu muwapelekee, hasa kwenye taasisi zinazotumia kuni au magogo kwa wingi au mkaa kwa wingi. Ahsante mimi naomba nirudishe shilingi yako. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mhshimiwa Jitu Soni.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa naomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri. Huu mpango wa *REA III* ambao unaenda vizuri sana, na karibu makampuni yote sasa wameshaanza kufanya mchakato wa kuanza kazi rasmi baada ya kupata malipo; tulitaka kujua uhakika wa upatikanaji wa vifaa vya kufanyia kazi; kwa mfano transfoma pamoja na nguzo kutokana na kazi hii ni kubwa na karibu vijiji zaidi ya 4000 na zitapatiwa umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, idadi ya nguzo ambayo inatakiwa zipatikane pamoja na transfoma na bidhaa zingine ambao watatoa nje tunataka uhakika kutoka Serikalini kwamba kampuni ambayo tunasema kwamba zizalishe hapa nchini hizo nguzo uwezo huo wanao? na *TANELEC,* je, wataweza ku-*supply* kwa muda muafaka ndani ya hii miezi michache transfoma hizo zaidi ya 4000 au 6000? Kwa sababu

kama kuna vijiji vyenye transfoma zaidi ya moja *transformer* karibu 600, je, uwezo wa upatikanaji wa vitu hivyo ndani ya nchi upo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Jitu na ninapenda kuthibitisha kwamba kutokana na miradi inavyoendelea ya awamu ya tatu tumeshakaa vikao zaidi ya mara tatu na wazalishaji wa vifaa vya umeme wa ndani. Tumekaa na wazalishaji wa nguzo, tumakaa na wazalishaji wa transfoma na vifaa mbalimbali. Naomba nimthibitishie kwamba katika mkutano ule ambao na wakandarasi walihudhuria tulijiridhisha kwamba viwanda vyetu vya ndani vina uwezo. Changamoto iliyokuwepo ni kwamba kulikuwa na masuala ya *letter of credit* na zishafunguliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa kwa vifaa vinavyotakiwa nguzo, kampuni zilikuwepo ikiwemo *Saw Mill* kutoka Iringa lakini pia *TANELEC* yenyewe na kampuni ya Kilimanjaro pia ambayo inatengeneza transfoma. Kwa hiyo nimthibitishie, hata hivi karibuni kuna viwanda viwili vimefunguliwa ambavyo vinatengeneza mita na ndiyo maana Mheshimiwa Waziri ametoa maelekezo kwamba ndani baada ya miezi mitatu hata mita zitakuwa zinatengenezwa ndani ya nchi badala ya kuagiza nje ya nchi. Kwa hiyo, nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa kweli kwa wakandarasi hakutakuwa na shida na viwanda viko tayari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa nafasi hii. Kwanza niseme tu sina kusudio la kushika mshahara wa Mheshimiwa Waziri, lakini nitapenda maelezo ya kina na ikinilazimu basi tutashika mshahara wa Waziri lakini sio kwa matakwa yangu ni kulingana na majibu ambayo nitapata kwa upande wa Serikali. Napenda

kuwapongeza Wizara kwa sababu kimsingi mimi nitaongelea kuhusu masuala ya *REA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama alivyoongelea Mheshimiwa Naibu Waziri hapo, ni kweli Serikali imeweza kufungua *letter of credit* na Serikali imeweze kulipa kiasi cha takribani bilioni 200 kwa wakandarasi wote waliokuwa na mahitaji ya vifaa kwa ajili ya kuendeleza sekta hii ya umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaporejea *Finance Act* ya mwaka 2012 Bunge hili lilipitisha kusudio la Serikali kutoza shilingi 100 kwa kila lita ya mafuta na pesa hii iweze kupelekwa kwenye mfuko wa *REA* kwa ajili ya kusaidia mchakato mzima wa maendeleo ya umeme vijijini. Lakini sambamba na hilo *Finance Act* ya mwaka 2012 ilieleza kusudio la Serikali kuweza kuona kwamba fedha hizi zinakuwa *reinforced.* Hata hivyo ukisiliza michango ya Wabunge wote waliochangia wengi wao waliochangia walioneshwa kusikitika kwa kuona kwamba fedha hizi zinazokusanywa na *TRA* na kupelekwa *central bank (Treasury)* pengine hazifii kwa wakati na hata zikifika kwa wakati zinafika chini ya kiwango kusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie majibu ya kina na anieleze ni mikakati gani mipya Wizara imekuja nayo ya kuhakikisha kwamba taasisi hizi zinazohusika na ukataji wa tozo hili inasimama katika misingi ya kisheria kusudiwa vinginevyo nitashika mshahara wa Mheshimiwa Waziri. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mmasi mbona una *double,* umesema huna haja ya shilingi, sasa unashikaje shilingi, kwa hiyo mimi nachukua kauli yako ya mwanzo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha majibu.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Mmasi kwa kuhoji jambo hili na mimi naomba niliambie Bunge lako tukufu kwamba fedha hizi kumekuwa na sintofahamu ambayo sielewi chanzo chake ni kipi. Fedha hizi za Mfuko wa *REA* pamoja na mifuko mingine kama Mfuko wa Barabara pamoja na Mfuko Reli,

Mfuko wa Maji kisheria jinsi ilivyo na utaratibu jinsi ulivyo fedha nyingine za makusanyo hukusanywa na kupelekwa kwenye akaunti ya makusanyo ya mamlaka ya mapato, baada ya kuwa imeshakusanywa hii ambayo si fedha ambayo maalum kwa ajili ya matumizi ndio inakwenda katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha hizi za mifuko maalum haziingizwi kwenye *TRA Collection Account,* fedha hizi zimefunguliwa *account* yake *special* ambayo inaitwa *Fuel TRA Deposit Account* fedha inayotokana na *charge* ya mafuta tu ina *account* yake *separate* na inapokusanywa ile pesa haina *connection* yoyote na *Consolidated Account* ambayo ni Mfuko wetu wa Hazina. Fedha hii inakusanywa kisheria na kama nilivyosema wakati nachangia mchana hoja hii fedha hii yote kama Serikali tunaipeleka katika *account* maalum ambayo ni *REA Deposit Account,* haiingii katika mfuko wetu wa Hazina.

Kwa hiyo nimuombe tu Mheshimiwa Mmasi pamoja na Waheshimiwa Wabunge wengine na Bunge lako tukufu wafahamu dhamira njema ya Serikali yetu. Fedha yote tunaikusanya na tuna-*deposit* katika *account* ya *REA* haiingii kwenye Mfuko mkubwa wa Hazina ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Sannda. Mheshimiwa Mmasi kaa huna hoja.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, na kabla sijasema hoja yangu napenda nitangulize kusema kwamba kama sitaridhika na majibu ya Mheshimiwa Waziri nakusudia kushika shilingi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika letu la *TANESCO* linadai sana na linadai taasisi za Serikali zikiwemo taasisi za umma zote pamoja na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, takribani zaidi ya shilingi bilioni 700; wakati huo lenyewe linadaiwa zaidi ya shilingi bilioni 900.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi hili shirika pamoja na kuendelea kufanya faida ambapo kumeonekana sasa hivi kuna kwenda, tunaona vipi, litaendaje hili? Kuna suala tunaita *going concern;* nikiliangalia pamoja na kwamba inaanza kuleta faida nina wasiwasi shirika hili tunaenda kuliua. Sijaona mkakati madhubuti wa Serikali kuhakikisha fedha hizi zinazodaiwa za Serikali Jamhuri ya Muungano na Mapinduzi Zanzibar zinalipwa. Mheshimiwa Waziri hebu naomba tuelezee tupate *comfort level* kidogo ya kuona kama shirika hili litakuwepo; nakushururu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nakumbuka ulilijibu lakini labda alikuwa hayupo lijibu *for his benefit*.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Sannda kwa swali zuri. Nilieleza kidogo wakati natoa majumuisho, lakini vizuri nikareja tu. Ni kweli kwanza nimeeleza hapo nyuma kwamba madeni mengi ni ya miaka mingi, hilo la kwanza, lakini madeni mengi yametokana pia na uzalishaji wa mitambo ya kukodi wa miaka mingi pia. Sasa hatua na mikakati ambayo tumeanza kuchukua kama ambavyo ulianza kwanza tumeachana na hiyo mikataba hiyo ni hatua muhimu sana na ndiyo maana nikaipongeza Serikali, lakini hatua ya pili kama Serikali na kupitia shirika tumeanza kuchukua hatua nyingine za muda mrefu nyingine za muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua za muda mfupi ambazo tunaweza kuchukua ni pamoja na kusitisha Kuleta vifaa kutoka nje kwa sababu vilikuwa vinaingiza mzigo mkubwa. Vinaponunuliwa hapa ndani kwanza tunajenga uwezo wa viwanda, kuzalisha nguzo na vifaa vingine na kununuliwa kwa bei ya nafuu. *TANESCO* mitambo wanaponunua kwa ya bei nafuu maana yake wanazalisha pia faida ambayo itatumika sehemu yake ya kulipa madeni; kwa hiyo ni mkakati mmoja wapo wa kuanza kulipa madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine kama ambavyo umesema, ni kweli Waheshimiwa Wabunge, Shirika letu imeelezwa la muda mrefu na yale madeni ni ya muda

mrefu, lakini mkakati mwengine wa makusudi kabisa, mikataba iliyokuwa inaingiwa ambapo umezungumza Mheshimiwa Mbunge; nimpongeze sana Mheshimiwa Spika na Wabunge wenyewe, ulipounda Kamati ya kupitia mikataba hii. Naamini nitakuja na mapendekezo mazuri sana hiyo Kamati Maalum. Yale mapendekezo yatakapotoka yakiielekeza na kuishauri Serikali sisi tutayachukua ili tuyatumie kuboresha ufanisi wa Shirika letu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sannda.

**MHE. EDWIN M. SANNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshuru Mheshimiwa Waziri. Nilichotegemea ni kwamba walau tungeanza kuona *trend* ya namna ya kulipa, na upande wa pili *trend* ya namna ya tunavyolipwa ndipo tungeweza kulilipa. Mimi nafikiri hili jambo linafaa kujadiliwa kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Sannda ngoja kidogo, hebu kaa kwanza. Sidhani kama kuna jibu jipya, Zanzibar wameanza kulipa madeni, Serikali ya Tanzania inalipa madeni, *TANESCO* hawanunui vitu kutoka nje. Mheshimiwa Sannda huna hoja.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 1002- *Finance and Account* ...............Sh. 911,577,000/=
Kif. 1003 - *Policy and Planning*...................Sh. 1,122,598,000=
Kif. 1004 - *Internal Audit Unit*..................Sh. 470,444,000,000=
Kif. 1005 - *Legal Service Unit*........................Sh. 556,790,000=
Kif. 1006 - *Government Communication Unit*...Sh. 494,456,000=
Kif. 1007 - *Procurement Management Unit* ......Sh. 468,474,000=
Kif.1008 - *Environmental Managemental Unit*...Sh. 330,283,000=
Kif 1009 - *Management Information System* .....Sh. 554,190,000=
Kif 2001 - *Mineral* ..........................................Sh. 0/=
Kif. 2002 - *Madini Institute* ...................................Sh. 0/=
Kif 2004 - *Tanzania Diamond Sorting Agency* .............Sh. 0/=
Kif 2005 - *Eastern Zone* ........................................Sh. 0/=
Kif. 2006 - *Western Zone* ......................................Sh. 0/=

Kif 2007 - *Lake Zone* ........................................Sh.0/=
Kif 2008 - *Northern Zone* ..................................Sh. 0/=
Kif 2009 - *Southern Zone*......................................Sh. 0/=
Kif 2010 - *Central Western Zone*............................Sh. 0/=
Kif 2011 - *Central Zone* .......................................Sh. 0/=
Kif 2012 - *Sothern Western Zone* ...........................Sh. 0/=
Kif 2013 - *Lake Victoria Eastern Zone* ......................Sh. 0/=
Kif 2014 - *Lake Nyasa Zone* ..................................Sh. 0/=
Kif 3001 - *Electricity and Renewable Energy*..........................................Sh. 2,534,716,000/=
Kif 3002 - *Petroleum and Gas*............... Sh.17,495,736,000/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa mtaona kuna vifungu kama sita havikutengewa fedha kwa sababu vilikuwa vinahusikana na madini, na madini imehama kwenye Wizara hii wana Wizara yao maalum na wiki ijayo wataleta bajeti yao.

**MATUMIZI YA MAENDELEO**

Kif. 1003 - *Policy and Planning* ...............Sh.1, 658,000,000/=
Kif 2001- *Minerals* ...........................................................Sh. 0/=

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif 3001 *Electricity and Renewable Energy*...................................Sh.1,561,613,000,000/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaomba ufafanuzi katika kifungu hiki ambapo fedha zote za miradi nategemea ziko hapa. Hata hivyo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha wakati anajibu kuhusu malipo ya fidia, ya KV 400 Kutoka Singida mpaka Namanga alisema watalipa shilingi bilioni 34 kati ya shilingi bilioni 68. Wananchi wa Babati

wanadai shilingi bilioni 68 katika mradi huu na mradi mzima kutoka Singida mpaka Namanga zaidi ya shilingi bilioni 68. Sasa naomba nifahamu ni wananchi wangapi mnakwenda kuwalipa katika jimbo la Babati Mjini? Kwa sababu Mheshimiwa Waziri ulitoka juzi pale ukawaambia unawalipa kila siku unawaahidi tarehe kama mama mjamzito ambaye anatakiwa kujifungua wamechoka, tuambie leo unawalipa wananchi wangapi na shilingi ngapi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Gekul tumia lugha za Kibunge hamna mjamzito humu, Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nishukuru kwa swali hili bahati nzuri nilishamaliza kuzaa siku nyingi kwa hiyo hamna mjamzito hapa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilisema wazi wakati nachangia hapa kwamba mwezi huu wa tano tunakwenda kulipa shilingi bilioni 34, mwezi wa sita tunamalizia shilingi bilioni 34 na kwa hesabu tu ya darasa la pili jumla yake ni shilingi bilioni 68 anayoisema Mheshimiwa Gekul.

**MWENYEKITI:** Ahsante, tatizo mkikaa ndani hamsikilizi majibu, hamtaki kujazwa majibu.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kif. 3002 - *Petroleum and Gas* ……….….Sh. 101,870,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**NDG. BAKARI KISHOMA – KATIBU MEZANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Matumizi imemaliza kutoa kazi yake.

*(Bunge Lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Tukae, mtoa hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Kuhusu Utaratibu Mwenyekiti

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther kaa chini nitakupa nafasi baadae, Mheshimiwa mtoa hoja.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Inahusu sasa hivi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther sasa unabishana na Kiti? Mheshimiwa kaa chini nitakupa nafasi baadae. Mheshimiwa mtoa hoja.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa kanuni za kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 kanuni ya 104(3)(a) na (b). Kwamba Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na imekamilisha kazi zake za kupitia kifungu kwa kifungu, naomba taarifa hiyo ya Kamati ya Matumzi ikubaliwe na Bunge lako. Naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu kabla ya hoja kuamuliwa.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Esther nikisimama wewe unakaa, ndiyo *regulations,* hata kule kwenye *netball* kuna sheria zenu.

Mheshimiwa nikisimama unakaa hakuna kanuni, nikisimama hakuna kanuni, *period*.

Waheshimiwa Wabunge sasa nitawahoji, kuwa sasa Bunge likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa mwaka 2018/2019.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*
*(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 – Wizara ya Nishati yalipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri nikupongeze sana wewe na Naibu wako na timu yenu ambayo iko hapa kwakweli mnafanya kazi nzuri na Wabunge wote humu ndani wamewasifia. Pale ambapo mtakapopata kuongezewa pesa, tunahakika mtafikia *target* zenu kabla ya mwaka 2020. Kwa hiyo, muendelee na kazi nzuri, niwashukuru Wabunge kwa ushirikiano wenu.

Sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka siku ya Jumatatu saa 3:00 asubuhi.

*(Saa 11:50 Jioni Bunge liliahirishwa hadi siku ya Jumatatu, Tarehe 28 Mei, 2018 Saa Tatu Asubuhi)*